



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI**



ISO 9001:2015 Certified

# **RIPOTI KUU YA MWAKA YA UKAGUZI WA SERIKALI KUU KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23**



**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU  
WA HESABU ZA SERIKALI  
MACHI 2024**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI**



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Audit House, 4 Barabara ya Ukaguzi, S.L.P. 950, 41104 Tambukareli, Dodoma. Simu ya upepo "Ukaguzi" Simu: +255 (026) 2161200 Nukushi: +255 (026) 2117527; Barua pepe: ocag@nao.go.tz Tovuti: www.nao.go.tz.

**Kumb. Na. No.CGA.319/421/01B**

**28 Machi 2024**

Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan,  
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,  
Ikulu,  
S.L.P. 1102,  
1 Barabara ya Julius Nyerere,  
11400 Chamwino  
40400 DODOMA.

**YAH: RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA SERIKALI KUU KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23**

Ninayo furaha kuwasilisha ripoti yangu ya mwaka ya ukaguzi wa Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha 2022/23 kwa mujibu wa Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, na Kifungu cha 34 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418.

Ripoti hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi na mapendekezo ya hatua za kuchukua ambazo zinalenga kukuza uwajibikaji katika ukusanyaji wa mapato na matumizi ya rasilimali za umma.


Nawasilisha kwa unyenyekevu,

**Charles E. Kichere**  
**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**  
**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

# KUHUSU OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

## Mamlaka

Mamlaka na majukumu ya kisheria ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yameainishwa chini ya Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ikisomwa pamoja na Kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418.



### Kufanya kazi kwa uhuru na bila upendeleo

Sisi ni taasisi ya umma isiyo na upendeleo, inayotoa huduma za ukaguzi wa hali ya juu kwa wateja wetu kwa njia isiyo na upendeleo.

### Kufanya kazi kwa ushirikiano

Tunathamini na kufanya kazi kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje.

### Kufanya kazi kwa kuzingatia matokeo

Tunazingatia katika kufikia malengo muhimu yenye kuaminika kwa wakati, usahihi na utumizi stahiki.



### Kufanya kazi kwa utaalum

Tunatoa huduma za ukaguzi za hali ya juu kwa kuzingatia maarifa ya kitaaluma, ujuzi na mbinu bora.

### Kufanya kazi kwa uadilifu

Tunazingatia na kudumisha viwango vya juu vya maadili na sheria katika utoaji wa huduma za ukaguzi.

### Kufanya kazi kwa ubunifu na uvumbuzi

Tunahimiza, kuvumbua, na kubuni mawazo ya kuongeza thamani kwa ajili ya kuboresha huduma za ukaguzi

# YALIYOMO

KUHUSU OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI .....	i
YALIYOMO .....	ii
ORODHA YA MAJEDWALI .....	iv
ORODHA YA VIELELEZO .....	vii
ORODHA YA VIAMBATISHO .....	viii
ORODHA YA VIFUPISHO .....	ix
SALAMU KUTOKA KWA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ..	xi
MUHTASARI .....	xii
SURA YA KWANZA .....	1
MAELEZO YA AWALI .....	1
SURA YA PILI .....	3
HATI ZA UKAGUZI .....	3
SURA YA TATU .....	10
UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA MIAKA ILIYOPITA .....	10
SURA YA NNE .....	13
MAANDALIZI NA UTEKELEZAJI WA BAJETI .....	13
SURA YA TANO .....	23
USIMAMIZI WA UKUSANYAJI WA MAPATO YA KODI, MAPATO YASİYOTOKANA NA KODI, NA DENI LA TAIFA .....	23
SURA YA SITA .....	54
USIMAMIZI WA MATUMIZI .....	54
SURA YA SABA .....	59
USIMAMIZI WA UNUNUZI .....	59
SURA YA NANE .....	105
USIMAMIZI WA MALI NA MADENI .....	105
SURA YA TISA .....	122
USIMAMIZI WA RASILIMALIWATU, MISHAHARA, NA MAFAO YA WASTAAFU ....	122
SURA YA KUMI .....	129

UFANISI KATIKA UTENDAJI .....	129
SURA YA KUMI NA MOJA .....	187
UTAWALA, UDHIBITI WA MIFUMO YA NDANI NA USIMAMIZI WA VIHATARISHI .	187
VIAMBATISHO.....	202

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 1: Hati za Ukaguzi Zilizotolewa kwa Kipindi cha Miaka Mitano ....	5
Jedwali Na. 2: Sababu za Hati Zilizotolewa .....	5
Jedwali Na. 3: Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kaguzi Zilizopita (Mwenendo wa Miaka Mitano) .....	11
Jedwali Na. 4: Mwenendo wa asilimia za Makusanyo kutoka kila chanzo kilichoainishwa .....	15
Jedwali Na. 5: Usuluhishi wa Mapato yaliyokusanywa na Mapato yaliyowasilishwa Mfuko Mkuu (Kiasi katika Sh. Trilioni) .....	17
Jedwali Na. 6: Makusanyo na Matumizi yaliyofanyika katika Akaunti ya Mfuko Mkuu .....	19
Jedwali Na. 7: Matumizi Yaliyofanyika Zaidi ya Bajeti Sh. bilioni 10.20 .....	21
Jedwali Na. 8: Mchanganuo wa Makusanyo ya Mapato (Tanzania Bara) .....	23
Jedwali Na. 9: Mchanganuo wa Makusanyo ya Mapato (Zanzibar) .....	24
Jedwali Na. 10: Mwenendo wa Ukusanyaji wa Mapato Jamhuri ya Muungano wa Tanzania .....	27
Jedwali Na. 11: Uwiano wa Kodi kwa Pato la Taifa la Tanzania na Nchi Zingine za Afrika Mashariki kwa Miaka Mitano .....	28
Jedwali Na. 12: Mwenendo wa Mashauri ya Kikodi .....	30
Jedwali Na. 13: Mashauri ya Kikodi Yaliyobaki Tanzania Bara .....	30
Jedwali Na. 14: Mashauri ya Kikodi Yaliyopo katika Mahakama ya Rufaa ya Mapato ya Kodi (Zanzibar) .....	31
Jedwali Na. 15: Taasisi Zilizokuwa na Mapato ambayo Hayakukusanywa .....	44
Jedwali Na. 16: Taasisi Zilizokuwa na Fedha Zilizoachwa kwa Muda Mrefu bila Kutumiwa .....	46
Jedwali Na. 17: Mapato Yasiyolipwa kutoka kwa Kampuni Zingine za Bima za Afya na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi .....	47
Jedwali Na. 18: Hospitali na Kiasi cha Fedha za Misamaha Zilizotolewa kwa Wagonjwa Wasiostahili .....	48
Jedwali Na. 19: Mwenendo wa Deni la Ndani (Deni Halisi) .....	50
Jedwali Na. 20: Mwenendo wa Ukopaji wa Ndani (Thamani Halisi) .....	51
Jedwali Na. 21: Mwenendo wa Deni la Nje .....	51

Jedwali Na. 22: Taasisi Zilizofanya Malipo bila Kudai Stakabadhi za Kielektroniki .....	54
Jedwali Na. 23: Orodha ya Taasisi Zilizokuwa na Bakaa ya Fedha katika Akaunti za Matumizi za Masurufu .....	55
Jedwali Na. 24: Taasisi Zilizofanya Ununuzi bila Kuidhinishwa na Bodi za Zabuni .....	61
Jedwali Na. 25: Taasisi Zilizofanya Ununuzi Nje ya Mfumo wa Kielektroniki ..	63
Jedwali Na. 26: Tasisi Zilizofanya Ununuzi bila Kutumia Njia za Ushindani wa Bei.....	65
Jedwali Na. 27: Ununuzi wa Bidhaa Uliofanyika bila Mikataba .....	67
Jedwali Na. 28: Taasisi Zilizokuwa na Mikataba Isiyopekuliwa na Wanasheria	68
Jedwali Na. 29: Mikataba Inayotekelezwa bila Dhamana za Utendaji Kazi ...	73
Jedwali Na. 30: Uchelewaji wa Ununuzi na Usambazaji wa Magari na Pikipiki	75
Jedwali Na. 31: Taasisi Zilizopokea Bidhaa bila Kukaguliwa.....	76
Jedwali Na. 32: Vituo vya Afya Vilivyopokea Vifaatiba ambavyo Havikuwamo kwenye Jedwali la Mahitaji .....	93
Jedwali Na. 33: Vituo vya Afya Vilivyopokea Vifaatiba na Kiasi cha Vifaatiba	94
Jedwali Na. 34: Vifaa Vilivyosambazwa zaidi ya Mahitaji .....	95
Jedwali Na. 35: Tofauti kati ya Ripoti za Mauzo za Bohari Kuu ya Dawa na Uwasilishaji Halisi .....	97
Jedwali Na. 36: Uchambuzi wa Fedha Zilizopokelewa Bohari Kuu ya Dawa...	98
Jedwali Na. 37: Orodha ya Bidhaa Zilizotozwa Bei Kubwa .....	103
Jedwali Na. 38: Taasisi Zilizokuwa na Mali Zilizotelekezwa kwa Muda Mrefu bila Matengenezo au Kuuzwa .....	108
Jedwali Na. 39: Taasisi Zilizo na Majengo Yaliyochaa na Kutelekezwa.....	110
Jedwali Na. 40: Ofisi za Balozizi Zilizo na Viwanja ambavyo Havijaendelezwa	111
Jedwali Na. 41: Taasisi ambazo Hazikuwa na Hatimiliki za Ardhi Inayomilikiwa na Serikali .....	113
Jedwali Na. 42: Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Zilizofungwa .....	115
Jedwali Na. 43: Taasisi Zenye Madeni Tarajiwa .....	121
Jedwali Na. 44: Taasisi ambazo Hazikuwasilisha Makato ya Mishahara .....	123
Jedwali Na. 45: Majalada ya Wastaafu Yaliyokaguliwa katika Mwaka 2022/2023 .....	125
Jedwali Na. 46: Majalada ya Mafao Yaliyokokotolewa Kimakosa .....	126

Jedwali Na. 47: Majalada Yaliyochelewa Kuandaliwa na Kuwasilishwa .....	127
Jedwali Na. 48: Majalada yenye Hoja ambayo Hayakurejeshwa kwa Ukaguzi wa Awali .....	128
Jedwali Na. 49: Migodi Iliyoidhinishwa Kufungwa Inayosubiri Malipo ya Dhamana za Ukarabati .....	134
Jedwali Na. 50: Upotevu wa Mapato Unaotokana na Maji Yanayopotea .....	135
Jedwali Na. 51: Kucheleweshwa kwa Malipo ya Madai ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa Hospitali Maalumu na za Rufaa za Mikoa .....	138
Jedwali Na. 52: Fedha Zinazoshikiliwa na Bohari Kuu ya Dawa bila Kusambaza Dawa na Vifaatiba .....	139
Jedwali Na. 53: Gharama za Ziada Zilizotokana na Ununuzi wa Dawa na Vifaatiba kutoka kwa Wasambazaji Binafsi .....	140
Jedwali Na. 54: Bodi, Idadi ya Vibali Vilivyoisha Muda Wake, na Kiasi cha Fedha ambacho Hakikusanywa .....	145
Jedwali Na. 55: Hospitali na Thamani ya Dawa ambazo Muda Wake wa Matumizi Ulikuwa Umeisha lakini Hazikuteketewa .....	151
Jedwali Na. 56: Bodi za Mabonde ambazo Hazikuwekewa Mita Jumuiifu .....	162
Jedwali Na. 57: Mamlaka za Maji Zilizokuwa na Wateja ambao Hawakufungiwa Mita za Maji .....	162
Jedwali Na. 58: Miradi ya Ujenzi wa Barabara Chini ya Mikataba ya EPC+F .	164
Jedwali Na. 59: Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira Zilizokuwa na Uwezo Mdogo wa Kukidhi Mahitaji ya Maji .....	170
Jedwali Na. 60: Vyama vya Siasa ambavyo Havikuwasilisha kwenye Akaunti za Benki Michango ya Wanachama Wake .....	183
Jedwali Na. 61: Vyama vya Siasa Vilivyoshindwa Kukusanya Mapato .....	184
Jedwali Na. 62: Taasisi zenye Bodi za Uongozi zenye Mapungufu .....	188
Jedwali Na. 63: Taasisi ambazo Hazikuwa na Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani	192
Jedwali Na. 64: Taasisi ambazo Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani Vilikuwa na Upungufu .....	193
Jedwali Na. 65: Taasisi ambazo Hazikutumia Mfumo MUSE .....	198
Jedwali Na. 66: Taasisi ambazo Hazikuwa na Mipango ya Urejeshaji wa Huduma za TEHAMA baada ya Kutokea Majanga .....	200



## ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo Na. 1: Mwenendo wa Ufadhili wa Bajeti .....	16
Kielelezo Na. 2: Ulinganifu wa Uchangiaji wa Makusanyo Halisi Kiidara 2022/23 na 2021/22 (Tanzania Bara).....	25
Kielelezo Na. 3: Ulinganifu wa Uchangiaji wa Makusanyo Halisi Kiidara 2022/2023 na 2021/2022 (Zanzibar).....	26
Kielelezo Na. 4: Mwenendo wa Uwiano wa Kodi kwa Pato la Taifa kwa Miaka Mitano .....	28
Kielelezo Na. 5: Mwenendo wa Ukuaji wa Deni la Serikali .....	50

## ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatisho Na. I: Hati za Ukaguzi Zilizotolewa.....	202
Kiambatisho Na. II: Orodha ya Taasisi Zilizofanya Ununuzi bila Kuzingatia Mipango ya Ununuzi ya Mwaka .....	220
Kiambatisho Na. III: Miradi Iliyotekelezwa bila ya kuwa na Cheti cha Tathmini ya Athari za Kimazingira na Kijamii .....	221
Kiambatisho Na. IV: Taasisi Zilizochelewa Kulipa Madeni Kinyume na Masharti ya Mikataba.....	222
Kiambatisho Na. V: Orodha ya Taasisi Zilizokuwa na Majengo ambayo Hayakukamilika kwa Wakati .....	223
Kiambatisho Na. VI: Taasisi ambazo Hazikurekodi Mali Zake katika Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Mali za Serikali.....	225
Kiambatisho Na. VII: Majengo Chakavu katika Vyuho vya Mafunzo ya Maendeleo ya Jamii, na Makazi ya Wazee na Watoto Wenye Mahitaji Maalumu .....	226
Kiambatisho Na. VIII: Taasisi Zilizokuwa na Madeni ya Muda Mrefu .....	227
Kiambatisho Na. IX: Uptevu wa Mapato kutokana na Kukataliwa kwa Madai ya Bima ya Afya .....	229
Kiambatisho Na. X: Vifaa Vilivyonunuliwa lakini Vilikuwa Havitumiki.....	231
Kiambatisho Na. XI: Idadi Pungufu ya Wataalamu wa Afya na Vifaatiba .....	234
Kiambatisho Na. XII: Ankara za Maji ambazo Hazikukusanywa.....	234
Kiambatisho Na. XIII: Vyombo vya Kijamii vya Utoaji wa Huduma za Maji ambavyo Havikufikia Lengo la Kusambaza Maji Vijijini .....	235
Kiambatisho Na. XIV: Vyombo vya Kijamii vya Utoaji wa Huduma za Maji ambavyo Mita Zake za Maji Hazikuhakikiwa na Wakala wa Vipimo.....	236
Kiambatisho Na. XV: Vyombo vya Kijamii vya Utoaji wa Huduma za Maji ambavyo Havikufikia Lengo la Ukusanyaji wa Mapato .....	237
Kiambatisho Na. XVI: Vyombo vya Kijamii vya Utoaji wa Huduma za Maji Vilivyokuwa na Upungufu wa Watumishi Wenye Sifa Muhimu za Kitaaluma ..	238
Kiambatisho Na. XVII: Taasisi Zilizokuwa na Upungufu katika Utendaji wa Kamati za Ukaguzi.....	239
Kiambatisho Na. XVIII: Taasisi Zisizo na Ufanisi katika Usimamizi wa Vihatarishi .....	240

## ORODHA YA VIFUPISHO

AGITF	Mfuko wa Pembejeo wa Taifa
ASA	Wakala wa Mbegu za Kilimo
ATCL	Shirika la Ndege Tanzania
BADEA	Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Kiuchumi Barani Afrika
BRELA	Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni
BUWSSA	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Biharamulo
BWB	Bodi ya Maji ya Bonde
CBWSO	Chombo cha Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii
DAWASA	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Dar es Salaam
EFD	Mashine ya Kutoa Risiti za Kielektroniki
eHMIS	Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Afya za wagonjwa
EWURA	Mamlaka ya Udhhibiti wa Matumizi ya Nishati na Maji
FETA	Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi
GAMIS	Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Mali za Serikali
GePG	Mfumo wa Serikali wa Kukusanya Mapato
GOT	Serikali ya Tanzania
GPSA	Wakala wa Ununuzi wa Umma
GST	Utafiti wa Jiolojia wa Tanzania
HCMIS	Mfumo wa Taarifa Shirikishi za Kiutumishi na Mishahara
ICU	Kitengo cha Uangalizi Maalumu wa Wagonjwa
IPSAS	Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu Katika Sekta ya Umma
ISCF	Mfuko wa Ushirika wa Ukaguzi na Usimamizi
JKT	Jeshi la Kujenga Taifa
JNIA	Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere
KFD	Mfuko wa Kuwait kwa Maendeleo ya Uchumi wa Kiarabu
LITA	Wakala wa Mafunzo ya Mifugo
LTBWB	Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Tanganyika
MDAs	Wizara, Idara na Wakala
MoEST	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia
MoF	Wizara ya Fedha
MOHA	Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi
MoU	Mkataba wa Maelewano
MPWSSA	Mamlaka ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Makonde Plateau
MSD	Bohari ya Dawa

Na.	Namba
NEMC	Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira
NFRA	Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula
NHIF	Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya
NIDA	Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa
NRW	Maji Yasiyo na Mapato
NSSF	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Taifa
OFID	Mfuko wa OPEC kwa Maendeleo ya Kimataifa
OI	Taasisi Nyingine
OSHA	Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi
PFR	Kanuni za Fedha za Umma
PPA	Sheria ya Ununuzi ya Umma
PPRA	Mamlaka ya Udhhibiti wa Ununuzi wa Umma
PSSSF	Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma
RBWB	Bodi ya Maji ya Bonde la Rufiji
REA	Wakala wa Nishati Vijijini
RRH	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa
RSCBWB	Bodi ya Maji ya Bonde la Ruvuma Kusini mwa Pwani
RUWASA	Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini
Sh.	Shilingi
TAA	Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania
TANePS	Mfumo wa Ununuzi kwa Njia ya Mtandao
TANESCO	Shirika la Umeme Tanzania
TANROADS	Wakala wa Bararaba Tanzania
TATC	Shirika la Nyumbu
TBA	Wakala wa Majengo Tanzania
TEMESA	Wakala wa Ufundi na Umeme
TIA	Taasisi ya Uhasibu Tanzania
TPSC	Chuo cha Utumishi wa Umma
TRA	Mamlaka ya Mapato Tanzania
UNESCO	Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni
UNICEF	Shirika la Watoto la Umoja wa Mataifa
USD	Dola ya Marekani
VAT	Kodi ya Ongezeko la Thamani
WMA	Wakala wa Vipimo
WSSAs	Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira



## SALAMU KUTOKA KWA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI


Ninayo furaha kuwasilisha ripoti ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023 ambayo inajumuisha Wizara, Idara Zinazojitegemea, na Wakala za Serikali. Napenda kutambua mipango ya serikali inayoongozwa na Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuendeleza uwajibikaji na uwazi katika usimamizi wa rasilimali za umma. Pia nashukuru ushirikiano wa menejimenti za taasisi katika kutoa taarifa na ufafanuzi muhimu kwa ajili ya kuandaa ripoti ya ukaguzi.

Matokeo ya ukaguzi yanadhihirisha nyanja mbalimbali za usimamizi wa fedha katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, na Wakala wa Serikali. Ingawa baadhi wameonesha usimamizi mzuri wa fedha, wengine wamekabiliwa na changamoto katika kudumisha ustahimilivu wa kifedha na utendaji. Ni muhimu kwa serikali kuingilia kati na kuhakikisha taasisi zinafanya kazi kwa ufanisi, kuchangia kukuza uchumi, na kutoa huduma za hali ya juu kwa wananchi.

Ripoti hii ina sura 11, kila moja ikizingatia vipengele tofauti, ikiwa ni pamoja na usimamizi wa ununuzi, usimamizi wa mapato na fedha, usimamizi wa matumizi, usimamizi wa bajeti na kufuata sheria za kodi. Ripoti hii pia inabainisha maeneo ambayo taasisi hizi zinahitaji kuboresha utendaji kazi na kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

Katika ripoti hii, nimetoa mapendekezo ya jinsi ya kuimarisha utendaji kazi wa taasisi zilizoripotiwa, kuongeza uwazi na uwajibikaji, na kuimarisha utawala bora. Ninaamini mapendekezo haya yatakuwa na manufaa kwa serikali, na wadau wengine katika kuhakikisha utoaji wa huduma bora.

Mwisho, natoa shukrani zangu za dhati kwa wafanyakazi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa juhudi zao za dhati katika kufanya ukaguzi na kuandaa ripoti hii. Kujitolea kwao na bidii yao imekuwa muhimu katika utayarishaji wa ripoti hii, na ninashukuru kwa mchango wao.

  
**Charles E. Kichere**  
**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**  
**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

## MUHTASARI

Taarifa hii inachambua matokeo na mapendekezo yaliyopatikana kutokana na ukaguzi wa taarifa za fedha na uzingatiaji wa sheria katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, na Wakala za Serikali kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023. Ukaguzi ulihusisha taasisi 475 zikiwemo mafungu 64, ofisi za Balozi 43, Wakala za Serikali 30, mifuko maalumu 19, vyama vya siasa 19, hospitali za rufaa na maalumu 34, na taasisi nyingine 266.

### (i) Bajeti

Katika mwaka wa fedha wa 2022/23, Serikali ilikusanya Sh. trilioni 41.880, zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa ya Sh. trilioni 41.480, ikiwa ni ongezeko la makusanyo kwa Sh. bilioni 400. Aidha, nilibaini ongezeko la makusanyo la Sh. trilioni 3.582, sawa na asilimia tisa ikilinganishwa na Sh. trilioni 38.298 zilizokusanywa katika mwaka wa fedha uliopita wa 2021/22.

Makusanyo ya ndani yanayotokana na kodi, mapato yasiyotokana na kodi, na makusanyo ya Halmashauri yalifadhili bajeti kwa Sh. trilioni 26.515 (63%), wakati Sh. trilioni 15.365 (37%) zilitokana na misaada na mikopo (Sh. bilioni 759 za Misaada na Sh. trilioni 14.606 za Mikopo).

### (ii) Hati za Ukaguzi

Kwa mwaka wa fedha wa 2022/23, nimetoa hati za ukaguzi kwa taasisi 475 zilizowasilisha taarifa za fedha kwa ajili ya ukaguzi. Hati 471 zilikuwa zinarithisha, moja ilikuwa hati yenye shaka, moja ilikuwa hati mbaya, na nilishindwa kutoa maoni kwa taasisi mbili. Aidha, nilifanya ukaguzi wa hesabu jumuiifu za serikali ambapo nilitoa hati yenye shaka.

### (iii) Utekelezaji wa Mapendekezo ya kaguzi za miaka ya nyuma pamoja na Maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC).

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023, kulikuwa na mapendekezo 7,342 ya ukaguzi yaliyotolewa miaka iliyopita. Tathmini yangu imebaini kuwa mapendekezo 2,946 (40.1%) yametekelezwa, mapendekezo 2,725 (37.1%) yalikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji, mapendekezo 617 (8.4%) hayakutekelezwa, mapendekezo 366 (5%) yamepitwa na wakati, na mapendekezo 688 (9.4%) yamerudiwa kutokana na kuendelea kuonekana.

Vilevile, uhakiki wa utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ulionyesha kuwa, kati ya maagizo 96 ya kamati kutoka katika ripoti zangu za miaka iliyopita, maagizo 38 (39.6%) yalitekelezwa

kikamilifu, maagizo 43 (44.8%) yalikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji, maagizo matano (5.2%) hayakutekelezwa, wakati agizo moja (1%) limerudiwa, na maagizo tisa (9.4%) yamepitwa na wakati.

#### **(iv) Kodi, Mapato yasiyotokana na Kodi, Deni la Taifa na Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali**

##### **(a) Usimamizi wa Kodi**

Tathmini ya utendaji na ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya kodi katika mwaka wa fedha 2022/23, ilitambua kesi 967 za kodi kwenye Mahakama za Rufani zenye thamani ya Sh. trilioni 10.48, ikiwa ni ongezeko la Sh. trilioni 5.65 sawa na 117% ikilinganishwa na Sh. trilioni 4.83 za mwaka uliopita, ongezeko hili lilichangiwa na kuchelewa kwa uteuzi wa wajumbe muhimu wa kusikiliza kesi za rufani za kodi pamoja na ufinyu wa bajeti.

Pia ukaguzi ulitambua uwepo wa lita 1,105,466 za mafuta yaliyopitiliza muda wa kukaa nchini zaidi ya siku 30 za kisheria ambayo yalipaswa kwenda nchi jirani yenye ushuru wa forodha unaokadiriwa kuwa Sh. milioni 929.6 hivyo kuna hatari ya kutumika nchini bila malipo ya kodi.

##### **(b) Makusanyo yasiyotokana na Kodi**

Ukaguzi ulitambua taasisi mbili za serikali kampuni ya ulinzi ya SUMA JKT na Jeshi la Uokoaji na Zimamoto (Fungu 14) hazikukusanya jumla ya Sh bilioni 1.86 baada ya kushindwa kutoa huduma, vituo vinne vya ukaguzi wa afya katika mipaka, bandari na viwanja vya ndege vilishindwa kukusanya tozo za ukaguzi Sh. milioni 879.11 baada ya ukaguzi na Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi (PHAB) haikukusanya kiasi cha Sh. milioni 768 kutoka kwenye vituo 2,640 vya Afya vilivyosajiliwa upya.

Nilitambua Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ulitoa mikopo ya Sh. bilioni 1.13 kwa vikundi vya wanawake na watu binafsi bila kuikatia bima. Pia, nilitambua kati ya mikopo hiyo iliyotolewa ya Sh. milioni 664.50 zimeshindwa kurejeshwa kwa muda wa miaka saba hadi 20, huku Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ikishindwa kukusanya Sh. bilioni 32.43 zilizotolewa kwa Halmashauri ili kutekeleza mipango ya upimaji na umilikishwaji wa hati miliki za ardhi baada ya kumalizika kwa muda wa urejeshwaji wa fedha hizo tarehe 30 Juni 2022. Katika Hospitali za rufaa, nilitambua kuwa Hospitali nne za rufaa zilishindwa kukusanya Sh. milioni 452 kwa kushindwa kufuatilia fedha za matibabu ya wagonjwa wanaotumia bima za mifuko mingine, wakati Sh. milioni 111.76

hazikukusanywa baada ya hospitali tatu za rufaa kutoa misamaha ya gharama za matibabu kwa wagonjwa wasio na sifa za kupata misamaha ya matibabu.

Aidha, nilibaini kuwa Sh. bilioni 61.09 hazikukusanywa na Taasisi 29 licha ya kutoa huduma, fedha hizo zimeripotiwa kama madai, nilibaini uwepo wa Sh bilioni 4.058 katika akaunti za taasisi tano za serikali zilizokaa muda mrefu bila kutumiwa na Sh. bilioni 7.73 zilikusanywa na taasisi tatu nje ya mifumo ya ukusanyaji.

Katika hali nyingine, nilibaini Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) iliingia makubaliano ya upangishaji eneo la ardhi lenye mita za mraba 11,000 katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam kwa shughuli za kibiashara kwa masharti nafuu yanayopelekea ukusanywaji mdogo wa mapato ya serikali, malipo ya pango kwa mita mraba yalikuwa dola za Marekani 4.36 tangu mwaka 1995 hadi mwaka 2018, ambayo yalipunguzwa hadi dola za Marekani 4.09 kwa mita mraba.

#### **(c) Usimamizi wa Deni la Serikali**

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023, deni la serikali lilikuwa Sh. trilioni 82.25 likijumuisha deni la ndani na nje Sh. trilioni 28.92 na Sh. trilioni 53.32 mtawalia ikiwa ni ongezeko ikilinganishwa na deni la mwaka 2021/22 la Sh. trillioni 71.31. Ongezeko hilo limesababishwa na mikopo halisi (Mapokezi ya mikopo mipya dhidi ya ulipaji wa mikopo).

Deni la Serikali ni himilivu, kwani uwiano wa thamani ya sasa ya deni la Serikali (deni la nje na deni la ndani) kwa Pato la Taifa (GDP) umebaki kuwa chini ya kiwango ukomo/elekezi. Hata hivyo, nilibaini kuwa vihatarishi vya deni la nje bado vipo kiwango cha wastani kama ilivyokuwa mwaka uliopita. Hii ilichangiwa na uhafifu wa mauzo ya nje (exports).

#### **(v) Usimamizi wa Matumizi**

Nimebaini kuwa taasisi saba zimekiuka kanuni za fedha kwa kuwa na bakaa ya fedha kiasi cha Sh. bilioni 2.45 katika akaunti zao za matumizi za masurufu. Pia, taasisi 13 zilifanya malipo ya Sh. bilioni 2.87 bila kudai stakabadhi za kielekitroniki kutoka kwa wauzaji wa bidhaa na watoa huduma.

Pia, ukarabati wa jengo la ofisi ya Balozi Kampala, Uganda haujaanza licha ya kuwa na bakaa ya fedha Sh. bilioni 1.78 tangu mwaka 2018. Kumekuwa na gharama kubwa za kodi ya pango ya kiasi cha Sh. bilioni 18.46 kwa majengo ya



ofisi na makazi katika balozi 39 za Tanzania nje ya nchi kwa mwaka wa fedha 2022/23.

#### **(vi) Usimamizi wa Ununuzi**

Nilibaini, taasisi 25 hazikutekeleza mipango yake ya ununuzi yenye thamani ya Sh. bilioni 565.49, mamlaka nne za maji zilifanya ununuzi wa jumla ya Sh. milioni 537.93 bila kuwa na mipango ya ununuzi ya mwaka; na taasisi sita zilifanya ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 1.82 bila kujumuishwa katika mipango yao ya ununuzi ya mwaka. Nilibaini miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 635.12 ilianza bila kuwa na cheti cha tathmini ya athari kwa mazingira na kijamii, wakati ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 7.12 kwa taasisi 15 ulifanyika bila kuidhinishwa na bodi za zabuni.

Pia nilibaini upungufu kwenye michakato ya utoaji wa zabuni, ambapo taasisi 16 zilifanya ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 149.56 bila kutumia mfumo wa kielekitroniki. Taasisi sita zilifanya ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 77.67 bila kutumia njia za ushindani wa bei. Ununuzi wa bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni 2.16 ulifanyika bila kutumia mikataba na mikataba yenye thamani ya Sh. bilioni 4.78 haikupekuliwa na Wanasheria.

Aidha, nilibaini mapungufu katika kutimiza majukumu ya kimkataba ambapo taasisi 11 zilichelewa kulipa madai ya Sh. bilioni 38.73 na kutolipa madai ya Sh. bilioni 19.37 ndani ya muda uliokubaliwa. Wizara ya ujenzi haijalipa riba ya Sh. bilioni 17.48 iliyotokana na uamuzi wa usuluhishi uliofikiwa tangu mwaka 2014, pamoja na riba ya Sh. bilioni 34.82 iliyotozwa kwa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kwa kuchelewa kulipa wakandarasi. Pia, mikataba 46 ya ujenzi ilikosa dhamana za utendaji kazi zenye thamani ya Sh. bilioni 383.76.

Nilibaini kuwa, Tume ya Madini na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) hazikudai dhamana ya utendaji kazi na malipo ya awali yenye thamani ya jumla Sh. milioni 675.90 kwenye mikataba iliyositishwa. Zaidi ya hayo, nilibaini miradi iliyotelekezwa yenye thamani ya Sh. bilioni 7.12 na kasi ndogo ya utekelezaji wa miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 200.01.

Ukarabati wa jengo la zamani la ubalozi wa Tanzania, lililoko kwenye Barabara ya 2139 R-Street, NW Washington, DC 20008, USA yalikuwa na dosari zifuatazo: gharama ya mkataba iliyonukuliwa ilizidi gharama iliyokadiriwa na mshauri elekezi kwa asilimia 94, ukarabati haukujumuishwa katika mpango wa ununuzi wa mwaka. Aidha, kiwango cha kodi ya ongezeko la thamani cha asilimia 20 kilichotajwa katika mchanganuo wa gharama za kazi na ambacho kililipwa

katika malipo ya awali hakikuwa na uhalisia kwa kuzingatia kiwango cha kodi ya ongezeko la thamani ya Washington ambayo ni asilimia sita. Kulikuwa na hatari ya kulipa riba kwa mkandarasi kutokana na kucheleweshwa kwa malipo ya hati za madai (IPCs) Na. 1 na 2 ambazo zilitolewa tarehe 15 Machi 2023 na 05 Mei 2023, mtawalia, na hazijalipwa mpaka sasa. Mkandarasi alikuwa anawasiliana moja kwa moja na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki pasipo kumtumia Meneja Mradi.

Nilibaini kuwa Bohari Kuu ya Dawa ilinunua mashine 10 za kuondoa maumivu, ukakamavu na mkazo wa misuli (Diathermy) kwa bei ya Sh. milioni 136.7 na kuacha kununua vifaa hivi kwa mzabuni aliyebainika kuwa na bei ndogo wakati wa ushindani ya Sh. Milioni 103.2 hivyo kupelekea gharama za ziada ambazo zingeweza kuepukika za kiasi cha Sh. milioni 33.5. Vilevile nilibaini ununuzi wa vifaatiba kwa wazabuni 32 waliopewa zabuni zenye thamani ya Sh. bilioni 4.14 bila kufanyiwa uchambuzi wa awali na kuidhinishwa na bodi ya zabuni. Pia vifaatiba vyenye thamani ya Sh. bilioni 13.37 ambavyo ununuzi wake haukuwa umeanza.

Pia, nilibaini uchelewaji wa ununuzi na usambazaji wa vifaatiba katika vituo vya afya kwa siku zinazoanzia 23 hadi 1,458 tangu fedha zilipopokelewa na Bohari Kuu ya Dawa hadi vifaatiba vilipofika kwenye vituo vya afya, pia vituo 21 vya afya vilipokea vifaa vyenye thamani ya Sh. bilioni 1.68 ambavyo vilikuwa havijaanza kutumika.

#### **(vii) Usimamizi wa Mali na Madeni**

Ukaguzi wangu ulibaini uwepo wa mali 522 ambazo ni vifaa na magari, vilivyoachwa kwa muda mrefu bila kutumika. Nilibaini pia majengo chakavu na yaliyotelekezwa katika wizara, idara na wakala za serikali tano, ofisi za balozi tano, pamoja na uwepo wa viwanja ambavyo havijaendelezwa katika ofisi tatu za Balozi.

Katika ukaguzi wa Mfuko wa Mikopo kwa Watumishi wa Umma, nilibaini hasara ya Sh. bilioni 5.73 ambayo ilitokana na kutokurejeshwa kwa mikopo iliyotolewa kwa wafanyakazi kutokana na sababu mbalimbali kama vile vifo, kufukuzwa kazi, kujiuzulu, au kuachishwa kazi. Zaidi, mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 2.10 ilitolewa kwa wafanyakazi, lakini haijaanza kufanyiwa marejesho.

Katika Mfuko wa Pembejeo za Kilimo, nilibaini hasara inayotarajiwa kutokana na uwepo wa mikopo chechefu yenye thamani ya Sh. bilioni 20.43, ambayo ni

sawa na 80% ya mikopo yote ambayo bado haijalipwa hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023.

Kuhusu usimamizi wa madeni, nilibaini malimbikizo ya riba ya Sh. bilioni 103.22 kwa kushindwa kulipa madai ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) yanayohusiana na ujenzi wa Daraja la Nyerere (Kigamboni). Katika Ubalozzi wa Tanzania New York, kodi ya majengo na riba ilifikia jumla ya dola za Marekani 847,888.40 (sawa na Sh. bilioni 2.16) kwa majengo mawili. Kodi hii na riba imetokana na kuondolewa kwa kinga ya kidiplomasia katika majengo hayo kutokana na uchakavu na kutokukarabatiwa kwa muda mrefu. Pia nilibaini kwamba, deni la Jeshi la Polisi la Tanzania linalodaiwa katika Dola za Marekani limeongezeka kwa Sh. bilioni 24.10 kutokana na kuchelewesha malipo. Ongezeko hili limetokana na mabadiliko katika viwango vya ubadilishaji wa fedha za kigeni.

Pia, taasisi 97 ziliripoti jumla ya madeni ambayo hayajalipwa kwa zaidi ya miezi 12 yenye thamani ya Sh. trilioni 1.88, sambamba na kuwapo kwa madeni tarajiwa yenye thamani ya Sh. bilioni 626.89 kwenye taasisi 17 yanayosubiri uamuzi wa mahakama juu ya mashauri ya kisheria.

#### **(viii) Ufanisi katika Utendaji**

##### **(a) Usimamizi wa Fedha**

Ukaguzi wangu ulibaini usimamizi usioridhisha wa fedha katika Wizara, Idara na Wakala za serikali. Nilibaini gharama za ziada katika miradi ya miundombinu ya barabara kiasi cha Sh. bilioni 13 zilizosababishwa na makosa ya awali katika usanifu na mapitio ya usanifu ambayo hayakuweza kuonesha mahitaji halisi yanayohitajika katika eneo la ujenzi. Pia, nilibaini kutolipwa kwa tozo ya ucheleweshaji wa ushushaji wa mafuta Sh. bilioni 18.94 kutokana na ufuatiliaji usioridhisha na kutokutekelezwa kwa makubaliano ya mkataba. Zaidi, nilibaini kutowasilishwa kwa dhamana ya fedha kutoka kwa makampuni ya madini yenye jumla ya Sh. bilioni 335.16, na hasara ya upotevu wa mapato ya kiasi cha Sh. bilioni 9.93 kutokana na maji yanayopotea.

Pia, nilibaini usimamizi wa fedha usioridhisha unaohusisha Hospitali Maalumu, Hospitali za Rufaa. Ikihushisha masuala muhimu kama upotevu wa mapato ya Sh. bilioni 8.94 kutokana na kukataliwa kwa madai ya huduma ya bima ya afya na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kutolipa kwa wakati madai ya Sh. bilioni 12.52 ya gharama za matibabu kwa hospitali maalumu na za rufaa. Aidha, Bohari Kuu ya Dawa kukaa na fedha za hospitali

kiasi cha Sh. bilioni 10.13 kwa zaidi ya mwaka mmoja bila kusambaza dawa, vifaatiba na vitendanishi, pia Hospitali za rufaa kuingia gharama za ziada za Sh. milioni 115.50 zilizotokana na ununuzi wa dawa na vifaatiba kutoka kwa wasambazaji binafsi, pamoja na vifaa vyenye thamani ya Sh. bilioni 3.47 vilivyo nunuliwa na Hospitali za Rufaa lakini havitumiki.

#### **(b) Ukiukwaji wa Sheria, Kanuni, na Miongozo**

Nilibaini kutoteketezwa kwa dawa za thamani ya Sh. Bilioni 1.99 zilizokwisha muda wake wa matumizi, pia nilibaini mapungufu katika uendeshaji wa vitengo vya afya mipakani na katika viwanja vya ndege.

#### **(c) Masuala yanayohusu Vyama Vya Siasa**

Nilibaini vyama vitano vya siasa; yaani, Chama cha Kijamii (CCK), National League for Democracy (NLD), NCCR Mageuzi, African Democratic Alliance (ADA) TADEA na Union for Multiparty Democracy (UMD), vilikusanya michango kutoka kwa wanachama mbalimbali jumla ya Sh. milioni 104.08 bila kuziwasilisha katika akaunti za benki za vyama husika. Hii ni kinyume na kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Vyama vya Siasa [Sura ya 258 iliyorekebisha mwaka 2019] kinachotaka kila chama cha siasa, ambacho kimesajiliwa kisheria kufungua akaunti ya benki ya chama, ambayo mapato yote yanayopatikana kuwasilishwa benki.

Kwa kuongezea, nilibaini kuwa vyama vinne vya siasa, yaani; Alliance for Africa Farmers Party (AAFP), Demokrasia Makini (DM), National Reconstruction Alliance (NRA), na National League for Democracy (NLD) havikuwasilisha tamko la kila mwaka la mali zinazomilikiwa na vyama hivyo kwa Msajili wa vyama vya siasa kwa mwaka ulioisha tarehe 30 Juni 2023.

#### **(d) Usimamizi wa Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji (CBWSO)**

Nilibaini upungufu wa upatikanaji wa mtandao wa maji katika vyombo vya watoa huduma ya maji (CBWSO), hivyo kuathiri uendelevu wa miradi ya maji inayosimamiwa na vyombo vya watoa huduma ya maji hali inayochangiwa na ukosefu wa wafanyakazi wenye ujuzi na kushindwa kukusanya mapato ya Sh. bilioni 1.64.

# SURA YA KWANZA



## MAELEZO YA AWALI

### 1.1 Utangulizi

Ripoti hii inatoa matokeo na mapendekezo yaliyobainika wakati wa ukaguzi wa taasisi za Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023.

Ripoti hii inajumuisha maeneo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na hati za ukaguzi, hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya miaka iliyopita, usimamizi wa vihatarishi, udhibiti wa mifumo ya ndani na utawala, maandalizi na utekelezaji wa bajeti, usimamizi wa mapato na matumizi, usimamizi wa rasilimali watu, usimamizi wa mali na madeni na ufanisi katika utendaji kazi. Ripoti hii pia imejumuisha matokeo ya Ukaguzi wa vyama vya siasa kwa mwaka wa fedha 2022/23.

### 1.2 Malengo ya ukaguzi

Ukaguzi ulilenga kutoa hati iwapo taarifa za fedha zilitayarishwa kwa kuzingatia viwango vya uandaaji wa taarifa za fedha. Aidha, ukaguzi ulilenga kupitia na kutathmini ufuataji wa sheria za ununuzi pamoja na sheria ya bajeti, kanuni, na miongozo husika.

### 1.3 Mbinu ya ukaguzi

Ukaguzi ulifanywa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Taasisi za Juu za Ukaguzi wa Serikali (ISSAI) vilivyotolewa na Shirika la Kimataifa la Taasisi za Juu za Ukaguzi wa Serikali (INTOSAI), pamoja na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA).

Mbinu za ukaguzi zilijumuisha hatua mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kukagua nyaraka, kufanya mahojiano, kuchambua taarifa na kutembelea maeneo husika. Ukaguzi pia ulihusisha tathmini ya mifumo ya udhibiti wa ndani na kuangalia kama inazingatia sheria, kanuni, na sera husika.

#### 1.4 Mawanda ya Ukaguzi

Ukaguzi ulijumuisha ukaguzi wa taarifa za fedha na utekelezaji wa sheria katika maeneo ya usimamizi wa mapato, usimamizi wa matumizi, usimamizi wa ununuzi, mishahara na usimamizi wa rasilimali watu, na utendaji kazi. Aidha, ukaguzi ulijumuisha tathmini ya usimamizi wa vihatarishi, udhibiti wa mifumo ya ndani na utawala katika Wizara, Idara na Wakala za serikali. Vilevile, ukaguzi ulihusisha ukaguzi wa awali wa mafao ya watumishi wa serikali walioastaafu ambao mafao yao yanalipwa moja kwa moja kutoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.



### 2.1 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa hati za ukaguzi zilizotolewa kwa taasisi mbalimbali za serikali kuu kwa mwaka wa fedha 2022/23. Hati zilizotolewa zimetokana na uchambuzi na tathmini ya ushahidi na vielelezo vilivyopatikana wakati wa kazi za ukaguzi, kwa lengo la kubaini iwapo taarifa za fedha zimeandaliwa kwa kuzingatia miongozo ya kimataifa ya uandaaji wa taarifa za fedha kama vile IFRS au IPSAS. Tathmini hii inazingatia Viwango vya Kimataifa vya Taasisi za Ukaguzi wa Hesabu (ISSAI) 1200.

### 2.2 Aina za Hati za Ukaguzi

Baada ya kufanya uchambuzi na tathmini ya vielelezo vilivyotumika kuandaa taarifa za fedha, kuna aina nne za hati za ukaguzi ambazo zinaweza kutolewa. Aina hizo za hati zinategemea na kupatikana kwa ushahidi unaojitosheleza kuthibitisha ubora na usahihi wa taarifa inayowasilishwa katika taarifa za fedha. Aina hizo za hati ni kama ifuatavyo:

**Hati inayoridhisha:** aina hii ya hati hutolewa pale ambapo mkaguzi amepata ushahidi na vielelezo vya kutosha, na kuthibitisha kwamba taarifa za fedha ni sahihi na zimeandaliwa kwa kufuata viwango kubalifu vya kimataifa vya uandaaji wa taarifa za fedha. Aina hii ya hati ndio inayotazamiwa zaidi na inaonesha kiwango kikubwa cha kuaminika na usahihi wa taarifa za fedha.

**Hati Yenye Shaka:** aina hii ya hati hutolewa pale taarifa za fedha zinapokuwa zimetayarishwa kwa usahihi isipokuwa kwa dosari moja au zaidi ya moja ambazo kwa ujumla wake ni kubwa lakini hazijaathiri sehemu kubwa ya taarifa za fedha. Pia, aina hii ya hati hutolewa pale ambapo mkaguzi hakupata ushahidi wa kutosha kumwezesha kutoa maoni ya ukaguzi, lakini akahitimisha kwamba dosari zilizotokana na kukosa ushahidi ni kubwa lakini hazijaathiri sehemu kubwa ya taarifa za fedha.

**Hati Mbaya:** aina hii ya hati hutolewa pale ambapo mkaguzi amepata ushahidi wa kutosha kuwa dosari moja au zaidi ya moja au kwa ujumla wake zilizobainika wakati wa ukaguzi ni kubwa na zimeathiri sehemu kubwa ya taarifa za fedha hivyo kupelekea taarifa hizo kutokuwa sahihi.

**Kushindwa Kutoa Maoni:** aina hii ya hati hutolewa pale mkaguzi anaposhindwa kupata ushahidi wa kutosha kumuwezesha kutoa maoni ya ukaguzi. Katika hali hii, mkaguzi atahitimisha kwamba athari zinazoweza kutokea kutokana na dosari zisizogundulika za taarifa za fedha zinaweza kuwa kubwa na zinaweza kuathiri kwa kiasi kikubwa taarifa za fedha. Mkaguzi atashindwa kutoa maoni katika mazingira nadra sana, ambayo yanahusisha shaka kwa kiasi kikubwa hivyo kuhitimisha kwamba, ingawa amepata ushahidi wa kutosha wa ukaguzi kuhusu kila shaka, haitawezekana kutoa maoni juu ya taarifa za fedha kwa sababu ya mwingiliano wa shaka hizo na athari zake kwenye taarifa za fedha.

### 2.3 Hati za Ukaguzi Zilizotolewa kwa Mwaka wa Fedha 2022/23

Katika mwaka wa fedha 2022/23, nilikagua jumla ya taasisi 475<sup>1</sup> za serikali kuu. Kati ya hizo, taasisi 471 zilipata hati inayoridhisha; taasisi moja (Chama cha Wananchi CUF) ilipata hati yenye shaka; taasisi moja (Chama cha National Reconstruction Alliance) ilipata hati mbaya; na nilishindwa kutoa maoni kwa taasisi mbili (Chama cha Alliance for African Farmers, na chombo cha watoa huduma ya maji Utegi). **Jedwali Na. 1 na Kiambatisho Na. I** zinaonesha mtiririko wa hati za ukaguzi na orodha ya taasisi na aina za hati zilizotolewa. Sababu za hati zilizotolewa zimeoneshwa katika **Jedwali Na. 2**.

Aidha, kwa mwaka wa fedha 2022/23, taasisi nne<sup>2</sup> ambazo ziliripotiwa katika ripoti ya mwaka 2021/22 zimeripotiwa katika ripoti ya mashirika ya umma. Vilevile, kuna taasisi 146<sup>3</sup> ambazo zimekaguliwa kwa mara ya kwanza. Pia, mafungu mawili (Fungu 11 na Fungu 60) yaliyokuwa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda, na Biashara yameunganishwa kwenda Fungu 44 na kuunda Wizara ya Viwanda na Biashara.

<sup>1</sup> Hati hizi hazihusishi hati ya Hesabu jumuifu za serikali

<sup>2</sup> Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kibaigwa, Mugumu, Tarime, na Namtumbo

<sup>3</sup> Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani; Deni la Serikali, Mfuko wa Sanaa na Utamaduni Tanzania; Shirika la Uvuvi Tanzania; Ubalozi wa Tanzania Vienna; Ubalozi wa Tanzania Jakarta; Mfuko wa Polisi wa Tuzo na Tozo; Baraza na Taifa la Usalama Barabarani, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, Taasisi ya Utafiti wa Tumbaku Tanzania, na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Makete, na Vyombo 135 vya Watoa Huduma za Maji kwa Jamii.



Zaidi ya hayo, katika mwaka wa fedha 2022/23, nilishindwa kukagua balozi za Tanzania Tel Aviv-Israel na Khartoum-Sudan kutokana na migogoro inayoendelea katika nchi hizo.

**Jedwali Na. 1: Hati za Ukaguzi Zilizotolewa kwa Kipindi cha Miaka Mitano**

Aina ya Hati	2022/23	2021/22	2020/21
Inayoridhisha	471	323	315
Yenye shaka	1	10	5
Mbaya	1	2	5
Kushindwa kutoa maoni	2	1	2
<b>Jumla</b>	<b>475</b>	<b>336</b>	<b>327</b>

Chanzo: Taarifa za Ukaguzi

**Jedwali Na. 2: Sababu za Hati Zilizotolewa**

Chama	Sababu za Hati
<b>Chama cha Alliance for African Farmers</b>	<p><b>Sababu ya Kushindwa Kutoa Maoni</b> Katika ukaguzi wa Taarifa za Fedha kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023, nilibaini kuwa Chama cha Alliance for African Farmers (AAFP) kiliandaa taarifa za fedha kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023.</p> <p>Hata hivyo, taarifa hizo hazikujumuisha taarifa linganifu za mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2022. Kutojumuisha taarifa hizi linganifu kuliathiri kwa kiasi kikubwa mawanda ya ukaguzi wa taarifa za fedha za Chama cha AAFP. Upatikanaji wa taarifa hizi ni muhimu kwa sababu zina mchango wa moja kwa moja kwenye usahihi wa taarifa za fedha za mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2023. Vilevile, kutojumuisha taarifa linganishi kunaathiri kiwango cha kueleweka kwa taarifa hizo na hakumpi mtumiaji taarifa za kutosha ili kumsaidia kufanya maamuzi sahihi. Hii imetokana na kuwa taarifa za msingi katika taarifa za mwaka wa fedha uliopita hazikuwasilishwa kwa ajili ya Ukaguzi.</p>
<b>Chombo cha Watoa Huduma ya Maji kwa Jamii - Utegi</b>	<p><b>Sababu ya Kushindwa Kutoa Maoni</b> Chombo cha Watoa Huduma ya Maji kwa Jamii - Utegi kiliripoti jumla ya matumizi ya Sh. 15,188,518 kama inavyoonekana kwenye Taarifa ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2022/23. Hata hivyo, ukaguzi wangu ulibaini kuwa matumizi ya jumla ya Sh. 14,948,732 (sawa na 98.7% ya matumizi yote) hayakua na nyaraka toshelezi za kuthibitisha usahihi wa matumizi yaliyofanywa.</p>
<b>Chama cha National Reconstruction Alliance (NRA)</b>	<p><b>Sababu ya Hati Mbaya</b> Nilibaini kuwa taarifa za fedha za Chama cha NRA zilijumuisha madeni ya Sh. 2,000,000, ambayo hayakuwa na nyaraka toshelezi za kuthibitisha usahihi wake. Pia, taarifa ya mizania ya Chama ilionyesha kuongezeka kwa wadaiwa wake kwa Sh.</p>

Chama	Sababu za Hati
	<p>3,750,000. Hata hivyo, ongezeko hilo halikuoneshwa katika taarifa ya mapato na matumizi ya chama.</p> <p>Aidha, taarifa ya mtiririko wa fedha haukuwa na taarifa lingalishi za mwaka wa fedha 2021/22. Kulikuwa na kutolingana kwa taarifa za fedha katika sehemu tofauti za taarifa za fedha, kama vile Taarifa ya Ulinganisho wa Bajeti na Fedha Halisi ilionesha jumla ya fedha iliyopokelewa ya Sh. 6,030,000 badala ya Sh. 2,280,000 iliyoonekana katika Taarifa za Mtiririko wa Fedha.</p>
<b>Chama Cha Wananchi (CUF)</b>	<p>Taarifa za Fedha za Chama cha Wananchi (CUF) hazikujumuisha baadhi mali za Chama. Taarifa ilionesha tu kuwa Chama kinamiliki mali lakini thamani ya mali hizo haikujumuishwa katika taarifa za fedha. Jambo hili ni kinyume na matakwa ya aya ya 26 na 27 ya IPSAS 17 (Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu katika Taasisi za Umma) na kanuni ya 22(1) ya Kanuni za Uandaaji wa Taarifa za Fedha za Vyama vya Siasa za Mwaka 2019. Hivyo, thamani ya mali zilizooneshwa katika taarifa za fedha za Chama cha Wananchi (CUF) hazikuonesha uhalisia wa mali zake zote.</p>

## 2.4 Ukaguzi wa Hesabu Jumuifu

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilianza kutumia Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu katika Taasisi za Umma (IPSAS Accrual) tarehe 1 Julai 2012 na kwa mara ya kwanza iliandaa hesabu jumuifu kwa kuzingatia matakwa ya IPSAS 35 katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2013. Hata hivyo, licha ya juhudi zinazoendelea, Serikali inaendelea kukabiliana na changamoto katika kufanikisha kwa ukamilifu uandaaji wa hesabu jumuifu kama ilivyodhihirishwa wakati wa ukaguzi wangu wa taarifa za fedha kwa mwaka wa fedha 2022/23. Hivyo, taarifa za hesabu jumuifu zimepewa hati yenye shaka. Sababu za kupewa hati hii ni kama inavyofanuliwa hapa chini.

### 2.4.1 Kutoondolewa Kikamilifu kwa miamala baina ya Taasisi za Serikali (inter economic entities transactions) katika Hesabu Jumuifu

Mapitio yangu ya hesabu jumuifu na hesabu binafsi za taasisi za Serikali yalibaini kutoondolewa kwa miamala iliyofanyika baina ya taasisi katika hesabu jumuifu. Nilibaini madeni ya kiasi cha Sh. bilioni 135.9 yameripotiwa zaidi katika hesabu jumuifu kutokana na kutoondolewa kikamilifu; mali za Serikali na gharama za matumizi kuripotiwa zaidi kiasi cha Sh. billion 14.59 na Sh. bilioni 17.89 mtawalia kutokana na kutoondolewa kwa miamala baina ya Taasisi. Hii ni

kinyume na Aya ya 40(a-c) ya IPSAS 35 ambayo inataka kuondoshwa kikamilifu kwa miamala baina ya taasisi za serikali ikijumuisha madeni, mali, mtaji, mapato.

Kutoondolewa kwa miamala baina ya taasisi kumesababishwa na mapungufu ya kutowekwa wazi kwa miamala iliyofanyika baina ya taasisi katika taarifa binafsi za hesabu za taasisi na kukosekana kwa mfumo wa uhibitaji mbadala wa Serikali katika kuainisha miamala baina ya taasisi.

Hii inasababisha uwepo wa taarifa zisizo sahihi katika hesabu jumuiifu ambapo kunadhoofisha uhalisia kwa taarifa za kifedha.

#### 2.4.2 Kutokwepo kwa Ulinganifu kati ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu Katika Sekta ya Umma ‘IPSAS’ na Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu ‘IFRS’ na kutokuwepo kwa taarifa ya wazi ya mtazamo tofauti katika Hesabu Jumuiifu

Aya 38 na 41 ya IPSAS 35 inaitaka taasisi inayoandaa Hesabu Jumuiifu kutumia sera za uhasibu moja kwa miamala iliyo sawa na miamala mingine yenye mazingira ya kufanana. Endapo kuna taasisi zinatumia sera za uhasibu tofauti na sera zinazotambuliwa na Hesabu Jumuiifu marekebishi sahihi yanahitajika katika hesabu za taasisi zinazojumuishwa wakati wa kutengeneza Hesabu Jumuiifu ili kuhakikisha kama kuna ulinganifu wa sera za uhasibu za taasisi husika.

Taasisi za Serikali zimekubali kutumia njia ya gharama za awali za ununuzi “*cost model approach*” baada ya utambuzi wa awali juu ya mali za uwekezaji ambazo umilikiwa kwa ajili ya kupata pango/kodi na/au kuongezeka thamani na Mali, Mitambo na Vifaa (PPEs) zinatakiwa kutambuliwa kwa gharama ya manunuzi ukitoa ongezeko la uchakavu na ongezeko la kushuka kwa thamani.

Katika mapitio ya mali za uwekezaji pamoja na mali, mitambo na vifaa (PPEs) zilizoripotiwa katika Hesabu Jumuiifu nimebaini upungufu ufuatayo: -

#### 2.4.3 Kutowiana kwa njia ya Uthamini wa Mali kati ya njia ya Thamani za awali za Ununuzi na Thamani Halisi ya Soko katika Mali za Uwekezaji

Mapitio ya Hesabu Jumuiifu yamebaini kuwa Serikali iliripoti mapato mengineyo kiasi cha Sh. billion 4,223 kwenye Noti Na. 19 ya Hesabu Jumuiifu. Hata hivyo,

kati ya kiasi hicho kilichoripotiwa nilibaini kuwa Sh. bilioni 712.09 kilikuwa ni faida ya thamani halisi kwenye mali na madeni ambapo Sh. bilioni 131.81 zilikuwa ni faida ya thamani halisi ya mali za uwekezaji kilichoripotiwa kwa modeli ya thamani halisi ya soko. Hivyo, faida kutokana na thamani halisi ya mali za uwekezaji imeripotiwa kwenye hesabu jumuiifu pasipo kufanyiwa marekebisho kulingana na sera za uhasibu (Accounting Policy), kinyume na matakwa ya IPSAS yaliyotajwa hapo juu pamoja na sera za uhasibu zilizokubaliwa.

**a) Kutowiana kwa Njia ya Uthamini wa Mali kati ya njia ya Thamani za Awali za Ununuzi na Thamani hasili ya Soko katika Mali, Mitambo na Vifaa ‘PPE’**

Nilibaini kuwa, taarifa ya mchanganuo inayoonesha mabadiliko ya mali Halisi/Mtaji imeripoti thamani ya ziada inayotokana na uthaminishaji wa mali sokoni ‘revaluation surplus’ kiasi cha Sh. bilioni 153.08 inayohusiana na mali za kudumu za taasisi 13 bila kurekebishwa wakati wa utayarishaji wa hesabu Jumuiifu, wakati huo gharama za uchakavu wa vifaa (depreciation expenses) kwa taasisi hizo ziliendelea kuripotiwa kiasi cha Sh. trilioni 3.32. Kuripoti ziada ya uthamini na kushuka kwa thamani ya vifaa (PPE) kunakinzana na matakwa ya Aya 38 ya IPSAS 35.

Kutowiana kwa utumiaji wa miundo ya uhasibu kwa mali za uwekezaji na Mali Mitambo na Vifaa (PPEs) katika hesabu jumuiifu kunachangiwa na kutobainishwa kwa mkakati wa kuzileta taarifa hizo pamoja wakati kunapotofautiana kwa sera za uhasibu na mfumo wa utoaji taarifa ambao una athari kwenye maandalizi ya Hesabu Jumuiifu.

Ukosefu wa usawa katika sera za uhasibu hudhoofisha usahihi wa taarifa’ na ulinganifu wa taarifa za fedha hivyo kuathiri uhalisia wa Hesabu Jumuiifu kwa wadau kufanya maamuzi sahihi.

**b) Kutowekwa wazi kwa miamala baina ya taasisi za serikali kwenye hesabu za taasisi husika**

Mapitio yangu ya zoezi la uondoaji wa miamala baina ya Taasisi za Serikali ili kutengeneza Hesabu Jumuiifu yalibaini kuwa, kati ya sampuli 50 za hesabu binafsi za taasisi za serikali, taasisi 20 ziliripoti madeni na madai jumla ya Sh. bilioni 7,425 pasipo kuwekwa majedwali ya miamala baina ya taasisi. Kutokuwekwa wazi kwa miamala hiyo kumesababishwa na kutokuzingatia miongozo ya uhasibu, mianya katika usimamizi na kukosekana kwa uelewa juu

ya matakwa mahususi kama yalivyoainishwa kwenye Aya ya 3.12 ya Waraka wa Uhasibu Na. 1 wa 2021/2022 kuhusu utayarishaji wa hesabu za taasisi za Serikali.

Kukosekana kwa uwazi wa miamala iliyofanyika baina ya taasisi katika hesabu za taasisi kunaleta changamoto katika kutambua na kuondoa miamala iliyofanyika baina ya taasisi za Serikali wa uandaaji wa Hesabu Jumuiifu kinyume na matakwa ya Aya ya 3.12 ya Waraka wa Uhasibu Na.1 wa 2021/2022 na IPSAS 35. Pia, inaweza kuzuia uwezo wa wasomaji wa taarifa kufanya tathmini ya uhalisi wa taarifa za kifedha na utendaji kazi wa taasisi, hivyo kuathiri ufanyaji wa maamuzi.

# SURA YA TATU



## UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA MIAKA ILİYOPITA

### 3.1 Utangulizi

Kupitia sura hii, nimetoa muhtasari wa hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi niliyoyatoa kwa menejimenti na wale wanaohusika na usimamiaji Utawala Bora katika eneo la Serikali Kuu, pamoja na hatua zilizochukuliwa na Maafisa Masuuli husika katika kujibu na kutekeleza mapendekezo hayo. Sura hii pia imeainisha utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali.

Katika kutekeleza majukumu yangu, nilifanya mapitio ya ufuatiliaji wa mapendekezo ya ukaguzi yanayohusu miaka ya fedha iliyopita ili kutoa tathmini inayoonesha jinsi Maafisa Masuuli walivyochukua hatua za kurekebisha mapungufu yaliyoibuliwa kupitia utekelezaji wa mapendekezo hayo ya miaka ya nyuma.

Nathamini jitihada zinazofanywa na Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) na Maafisa Masuuli katika kujibu hoja za ukaguzi katika ripoti zangu na kutoa mipango kazi ya utekelezaji wa mapendekezo hayo.

### 3.2 Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi wa Miaka Iliyopita Kutoka Kwenye Taarifa za Ukaguzi wa Taasisi za Serikali Kuu

Kanuni ya 38 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2009 inamtaka Waziri mwenye dhamana, kuwasilisha majibu kwa maandishi kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndani ya kipindi cha miezi mitatu tangu tarehe ya kupokea mapendekezo ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuandaa mpango kazi unaoeleza ni kwa kiasi gani, mapendekezo yaliyotolewa yametekelezwa.

Katika mwaka huu wa ukaguzi, nilifuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa mwaka uliopita katika taasisi zipatazo 328 za Serikali Kuu zilizokuwa na jumla ya mapendekezo 7,342.

Tathmini yangu inaonesha kuwa; hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023, kulikuwa na jumla ya mapendekezo 7,342. Kati ya mapendekezo 7,342, mapendekezo 2,946 (40.1%) yalitekelezwa, 2,725 (37.1%) yanaendelea kutekelezwa, 617 (8.4%) hayajatekelezwa, 366 (5%) yalifutwa kutokana na kupitwa na wakati na mapendekezo 688 (9.4%) yalirudiwa.

Uchambuzi wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyopita kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2023 unaoneshwa kwenye Jedwali Na. 3.

**Jedwali Na. 3: Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kaguzi Zilizopita (Mwenendo wa Miaka Mitano)**

Mwaka wa fedha	Mapendekezo yaliyotekelezwa	Utekelezaji wa mapendekezo unaendelea	Mapendekezo hayajatekelezwa	Mapendekezo yamerudiwa	Mapendekezo yamefutwa kutokana na wakati	Jumla
2022/23	2,946	2,725	617	688	366	7,342
2021/22	2,380	2,506	1,104	637	320	6,947
2020/21	5,290	6,032	3,548	1,166	1,143	17,179
2019/20	2,308	2,441	1,257	621	333	6,960
2018/19	1,508	2,003	1,211	259	502	5,483

Chanzo: Taarifa za ukaguzi za mwaka 2022/23

Hivyo, ni muhimu kuendelea kufuatilia na kutathmini maendeleo yaliyofikiwa katika utekelezaji wa mapendekezo ambayo utekelezaji wake haujakamilika na kuchukua hatua stahiki za kurekebisha inapobidi.

### 3.3 Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC)

Tathmini yangu ya hali ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/23 imebaini kuwa maagizo 96 yalitolewa; kati ya maagizo hayo, maagizo 38 (39.6 %) yalitolewa.

yalitekelezwa, 43 (44.8 %) yanaendelea kutekelezwa, maagizo 5 (5.2%) hayakutekelezwa, agizo 1 (1%) lilirudiwa na maagizo 9 (9.4%) yalifutwa kutokana na kupitwa na wakati. Aidha, ufuatiliaji usioridhisha na ucheleweshaji wa utekelezaji wa mapendekezo yangu ya ukaguzi na maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali inatoa taswira kuwa kasoro zilizobainika na kutolewa mapendekezo ya uboreshaji hazishughulikiwi ipasavyo na hivyo kuendelea kuziweka taasisi hizo kuwa kwenye hatari ya ubadhirifu wa rasilimali za serikali na kukosa ufanisi kwenye utendaji na uendeshaji wa taasisi husika.

**Ninapendekeza kuwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Maafisa Masuuli kuweka juhudi zaidi katika kutekeleza kikamilifu mapendekezo ya ukaguzi na maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali ili kusaidia kuboresha utendaji na ufanisi wa Taasisi za umma pamoja na kuchukua hatua za tahadhari na stahiki ili mapungufu hayo yasiendelee kujitokeza.**





MAANDALIZI  
YA BAJETI

### 4.1 Utangulizi

Serikali hupanga bajeti kila mwaka ambayo inaeleza vyanzo vya ukusanyaji wa mapato na matumizi yatakayofanyika. Mkakati huu unairuhusu serikali kutekeleza vipaumbele vya kitaifa kulingana na mgawanyo wa rasilimali zilizopo.

Bajeti ya Serikali ya mwaka 2022/23 ilijikita katika hatua mbalimbali za kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani, ikiwa ni pamoja na kuimarisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT) katika kukadiria kodi, kutumia teknolojia katika kuwasilisha ritani za kodi kwa wakati ili kuhakikisha makusanyo ya kodi yanalipwa kwa wakati, kusimamia matumizi ya mfumo wa malipo (GePG) na matumizi ya nambari za malipo kwa kila malipo yanayofanywa kwa serikali; kuboresha mazingira ya biashara kwa kutoa fursa zaidi kwa sekta binafsi ili kuongeza mchango wake katika uchumi, kuongeza vituo vya huduma za pamoja ili kukuza biashara na uwekezaji na kupunguza matumizi ya serikali yasiyo ya lazima.

Katika sura hii, natoa matokeo ya ukaguzi wa bajeti ya mwaka wa 2022/23 kama ilivyoelezwa hapa chini:

### 4.2 Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/23

Kwa mwaka wa fedha wa 2022/23, Serikali ya Tanzania ilipanga kukusanya na kutumia Sh. trilioni 41.48, sawa na ongezeko la asilimia tisa ikilinganishwa na Sh. trilioni 37.99 za mwaka wa fedha wa 2021/22. Makusanyo yalipangwa kutokana na vyanzo vya makusanyo ya ndani ya Sh. trilioni 28.018, mikopo Sh. trilioni 12.361 na misaada Sh. trilioni 1.101.

### 4.3 Bajeti ya Matumizi ya Serikali

Jumla ya Bajeti ya Sh. trilioni 41.48 zilipangwa kufadhili matumizi ya serikali ya Sh. trilioni 15 (36%) kwa matumizi ya maendeleo na Sh. trilioni 26.48 (64%) kwa matumizi ya kawaida.

### 4.4 Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti

Katika mwaka wa fedha 2022/23, serikali ilikusanya Sh. trilioni 41.880 ikiwa ni zaidi ya bajeti ya Sh. trilioni 41.480 kwa Sh. bilioni 400. Ikilinganishwa na Sh. trilioni 38.298 zilizokusanywa mwaka 2021/22, nilibaini ongezeko la asilimia tisa sawa na Sh. trilioni 3.582. Tathmini na mwenendo wa makusanyo katika kila chanzo kilichoainishwa ni kama ifuatavyo;

#### i. Makusanyo ya Kodi

Makusanyo ya kodi ya Tanzania Bara yalikuwa Sh. trilioni 22.583 sawa na 95.5% ya bajeti ya Sh. trilioni 23.652, hivyo Serikali haikukusanya Sh. bilioni 1.069 ikilinganishwa na makusanyo ya Sh. trilioni 20.945 za mwaka 2021/22, nilibaini ongezeko la makusanyo kwa Sh. trilioni 1.638 sawa na ongezeko la asilimia nane.

#### ii. Makusanyo yasiyotokana na Kodi

Makusanyo yasiyotokana na kodi yaliyokusanywa na Wizara, Idara na sekretarieti za mikoa na taasisi nyinginezo yalikuwa Sh. trilioni 2.7095 sawa na 81% ya bajeti iliyoidhinishwa ya Sh. trilioni 3.352 hivyo makusanyo ya Sh. bilioni 643 hayakukusanywa. Ikilinganishwa na makusanyo ya Sh. trilioni 2.709 ya mwaka 2021/22, nilibaini ongezeko la makusanyo yasiyotokana na kodi ikiwa ni ongezeko dogo.

#### iii. Makusanyo ya Serikali za Mitaa

Makusanyo ya Serikali za Mitaa yalikuwa Sh. trilioni 1.222 ikiwa ni makusanyo Zaidi ya bajeti ya Sh. trilioni 1.012 kwa 21% sawa na ongezeko la Sh. bilioni 21. Ikilinganishwa na makusanyo ya serikali za Mitaa ya Sh. bilioni 892 ya mwaka 2021/22, nilibaini ongezeko la makusanyo kwa Sh. bilioni 330 sawa na 37%.

#### iv. Misaada

Katika mwaka wa fedha misaada iliyopokelewa ni Sh. bilioni 759 sawa na 69% ya bajeti ya Sh. trilioni 1.101 hivyo kiasi cha Sh. bilioni 342 hakikukusanywa. Ikilinganishwa na misaada ya Sh. trilion 1.305 iliyopokelewa mwaka 2021/22, nilibaini kupungua kwa misaada kiasi cha Sh. bilioni 546 sawa na 42%.

**v. Mikopo ya Ndani**

Makusanyo yanayotokana na mikopo ya ndani ni pamoja na Ankara za Hazina, hati fungani na ufadhili wa ndani, jumla ya Sh. trilioni 6.124 zilikusanywa ikiwa ni zaidi ya bajeti ya Sh. trilioni 5.780 sawa na ongezeko la Sh. bilioni 344 (asilimia sita). Ikilinganishwa na mikopo ya Sh. trilioni 6.489 zilizokusanywa mwaka 2021/22 nilibaini kupungua kwa mikopo ya ndani ya Sh. bilioni 365 sawa na asilimia sita.

**vi. Mikopo ya Nje Yenye Masharti Nafuu**

Mikopo ya nje yenye masharti nafuu ya Sh. trilioni 5.523 ilipokelewa katika mwaka wa fedha zaidi ya bajeti ya Sh. trilioni 3.547 kwa Sh. trilioni 1.976 sawa ogezeko la 56%. Ikilinganishwa na mikopo ya Sh. trilioni 4.149 iliyopokelewa mwaka 2021/22 nilibaini ongezeko la mikopo ya nje yenye masharti nafuu kwa Sh. trilioni 1.374 sawa na ongezeko la 33%.

**vii. Mikopo ya Nje Isiyo ya Masharti Nafuu**

Mikopo ya nje isiyo ya masharti nafuu ya Sh. trilioni 2.959 ilipokelewa sawa na 97% ya bajeti ya Sh. trilioni 3.034 hivyo mikopo isiyo ya masharti nafuu ya Sh. bilioni 75 haikupokelewa. Mikopo isiyo na masharti nafuu imeongezeka kwa kwa 64% au Sh. trilioni 1.150 ikilinganishwa na Sh. trilioni 1.809 zilizopokelewa mwaka 2021/22. Mwenendo wa asilimia za makusanyo kutoka katika kila chanzo ni kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 4**.

**Jedwali Na. 4: Mwenendo wa asilimia za Makusanyo kutoka kila chanzo kilichoainishwa**

Maelezo	2022/23 (Sh. Trilioni)	2021/22 (Sh. Trilioni)	2020/21 (Sh. Trilioni)
Bajeti	41.480	37.992	34.879
Makusanyo	41.880	38.298	31.326
Makusanyo katika %			
Kodi	54%	55%	56%
Makusanyo yasiyotokana na Kodi, na makusanyo ya Serikali za Mitaa	9%	9%	9%
Mikopo ya Ndani	15%	17%	16%
Misaada na Mikopo ya Nje	22%	19%	19%

**Chanzo:** Taarifa ya Ukaguzi wa Deni la Taifa na Mfuko Mkuu kwa Mwaka 2020/21 to 2022/23


Katika kipindi cha miaka mitatu kutoka 2020/21 hadi 2022/23, kumekuwa na ukuaji katika mwenendo wa makusanyo. Tathmini ya makusanyo ya jumla dhidi

ya bajeti inaonesha, makusanyo ya mwaka 2022/23 yamekuwa zaidi ya bajeti kwa asilimia moja, ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka 2021/22 yaliyozidi bajeti kwa asilimia 0.8%. Aidha nilibaini ongezeko la misaada na mikopo ya nje kwa asilimia tatu ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

#### 4.5 Mwenendo wa Makusanyo, Misaada na Mikopo

Makusanyo ya ndani yanayotokana na; kodi, makusanyo yasiyotokana na kodi na makusanyo ya serikali za mitaa yalikuwa Sh. trilioni 26.515 (63%), wakati misaada na mikopo ilikuwa Sh. trilioni 15.365 (37%) (Sh. bilioni 759 (asilimia mbili) zilitokana na misaada, na Sh. trilioni 14.606 (35%) zilitokana na mikopo). Mwenendo wa makusanyo, misaada na mikopo kwa kipindi cha miaka mitatu ni kama inavyooneshwa kwenye **Kielelezo Na. 1**.

**Kielelezo Na. 1: Mwenendo wa Makusanyo, Misaada na Mikopo**



**Chanzo:** Ukaguzi wa Deni la Taifa na Mfuko Mkuu kwa Mwaka wa fedha 2020/21 hadi 2022/23

#### 4.6 Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali

##### 4.6.1 Taratibu za Uhasibu katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali

Ibara ya 135 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inataka makusanyo yote ya Serikali yapokelewe kwenye mfuko mkuu wa hazina ya serikali iliyopo Benki Kuu ya Tanzania na kusimamiwa na Mhasibu Mkuu wa

Serikali. Makusanyo yanayotokana na vyanzo vya kigeni, ikiwemo makusanyo ya washirika wa Maendeleo “Development Partners”, yanajumuisha makusanyo ya akaunti za pamoja “Basket funds”, misaada ya kibajeti, Fedha za Miradi zilizopewa idhini ya matumizi “Exchequer”, pamoja na fedha za miradi zilizopelekwa moja kwa moja kwenye miradi (Fedha za Miradi zinazopewa idhini ya matumizi “Exchequer” baada ya kutumiwa) hupokelewa na Taasisi kwa utaratibu wa kupokea idhini ya matumizi “Exchequer” ama kupelekwa moja kwa moja kwenye utekelezaji wa miradi kutoka kwa wadau wa maendeleo.

Kati ya Sh trilioni 41.880 zilizokusanywa, Sh. trilioni 38.447 zilipokelewa mfuko mkuu wa hazina ya serikali, hivyo kupelekea tofauti ya Sh. trilioni 3.433<sup>4</sup>. Tofauti hiyo inatokana na Sh. trilioni 3.656 fedha zilizopelekwa moja kwa moja kwenye miradi kutoka kwa wadau wa maendeleo na makusanyo yaliyopelekwa Zanzibar ambayo hayapitii mfuko mkuu wa hazina ya serikali pamoja na Sh bilioni 223 zinazotokana na bakaa za makusanyo ya kodi za mwaka uliopita na makusanyo mengine yaliyopokelewa mfuko mkuu wa hazina ya serikali nje ya makisio ya bajeti. Maelezo zaidi ni kama yalivyoainishwa katika Jedwali Na. 5.

**Jedwali Na. 5: Usuluhishi wa Mapato yaliyokusanywa na Mapato yaliyowasilishwa Mfuko Mkuu (Kiasi katika Sh. Trilioni)**

Maelezo	Bajeti	Makusanyo	Makusanyo yaliyopokelewa mfuko mkuu wa hazina ya serikali	Tofauti	Sababu za Tofauti
Kodi	23.652	22.583	22.6919	0.108	Makusanyo ya ziada yaliyowasilishwa yanatokana na bakaa ya kodi ya mwaka uliopita, makusanyo ya bandari, fedha zilizorudishwa na ZRA na makusanyo yasiyo na makisio ya TRA
Makusanyo yasiyotokana na Kodi	3.3520	2.7095	2.694	(0.015)	Makusanyo katika akaunti ya makusanyo 14 series ambayo hayajawasilishwa mfuko mkuu wa hazina ya serikali

<sup>4</sup> Tofauti ya Sh. trilioni 3.433 = Sh. trilioni 3.656 - Sh. bilioni 223

Maelezo	Bajeti	Makusanyo	Makusanyo yaliyopokelewa mfuko mkuu wa hazina ya serikali	Tofauti	Sababu za Tofauti
Makusanyo ya Serikali za Mitaa	1.012	1.222	0.840	(0.382)	Makusanyo ya Serikali za Mitaa yaliyotumiwa bila kuwasilishwa Mfuko Mkuu
Misaada	1.101	0.759	0.728	(0.03)	0.01042 zilizopo katika akaunti za miradi na 0.02007 zilizopelekwa Zanzibar.
Mikopo ya Ndani	5.780	6.124	6.124	0	
Mikopo ya Nje isiyo na Masharti nafuu	3.034	2.959	2.927	(0.032)	0.20389 ziliwasilishwa katika akaunti za deni la serikali bila kuwasilishwa Mfuko Mkuu wa hazina ya serikali;0.00021 Faida iliyotokana na mabadiliko ya fedha na 0.17188 zilizopokelewa Mfuko Mkuu wa hazina ya serikali bila kunakiliwa katika deni la serikali.
Mikopo ya Nje nyenye masharti nafuu	3.547	5.523	2.327	(3.197)	Fedha zilizopelekwa moja kwa moja kwenye Miradi
Makusanyo Mengine	-	-	0.115	0.115	Makusanyo mengine yaliyokuwa nje ya Bajeti.
<b>Jumla</b>	<b>41.480</b>	<b>41.880</b>	<b>38.447</b>	<b>3.433</b>	

Chanzo: Ukaguzi wa Mfuko Mkuu

#### 4.6.2 Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali katika Mwaka 2022/23

Jumla ya matumizi yaliyofanywa katika mfuko mkuu wa hazina ya serikali ili kugharamia matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/23 yalikuwa Sh. trilioni 39.523 bila kujumuisha Sh. bilioni 665.80 zilizotolewa kama fedha zilizorejeshwa “*refunds*” na matumizi mengine kwenye jumla ya makusanyo ya Sh trilioni 38.447, hivyo kusababisha nakisi katika benki kuu ya Sh. trilioni 1.742 kufikia tarehe 30 Juni 2023. Maelezo ya mapato na matumizi kutoka kwenye mfuko mkuu wa hazina ya serikali yanapatikana katika **Jedwali Na. 6.**

**Jedwali Na. 6: Makusanyo na Matumizi yaliyofanyika katika Akaunti ya Mfuko Mkuu**

Makusanyo na Fedha zilizotumiwa mfuko mkuu wa hazina ya serikali	Kiasi (Sh. Trilioni)
Kodi	22.6919
Makusanyo yasiyotokana na Kodi	2.694
Makusanyo ya Serikali za Mitaa	0.840
Misaada	0.728
Mikopo ya Ndani	6.124
Mikopo ya Nje	5.254
Makusanyo Mengine	0.115
<b>Jumla ya Makusanyo mfuko mkuu wa hazina ya serikali(A)</b>	<b>38.447</b>
Fedha zilizotolewa kwa Matumizi ya Serikali	39.523
Fedha zilizorudishwa na Matumizi mengine	0.665
<b>Jumla ya Matumizi katika mfuko mkuu wa hazina ya serikali (B)</b>	<b>40.189</b>
<b>Nakisi katika Benki Kuu 2022/23 (A-B)</b>	<b>(1.742)</b>

Chanzo: Ukaguzi wa Mfuko Mkuu

**4.7 Fedha zilizotolewa Mfuko Mkuu wa hazina ya Serikali Kwa Serikali Kuu.**

Jumla ya fedha zilizotolewa Mfuko Mkuu kwa matumizi ya Serikali ni Sh. trilioni 39.523; Fedha zilizotolewa kwa matumizi ya serikali kuu ikijumuisha; Wizara, Wakala, Tume na Idara zilikuwa Sh. trilioni 31.917 wakati Sh. trilioni 7.606 zilitolewa kwa matumizi ofisi ya Rais TAMISEMI pamoja na tawala za mikoa na serikali za mitaa, taarifa za matumizi hayo zimechambuliwa katika Ripoti Kuu ya Mwaka ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Usimamizi wa bajeti, fedha zilizotolewa pamoja na matumizi yaliyofanyika ni kama yanavyoelezwa katika aya zifuatazo:

**4.7.1 Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Fedha**

Ukaguzi wa taarifa za fedha za Wizara, Wakala na Idara ulibaini Sh. trilioni 20.990 sawa na 99% ya bajeti iliyoidhinishwa ya Sh. trilioni 21.280 zilitolewa kwa matumizi ya kawaida, hivyo kiasi ya Sh. billioni 290 hazikutolewa. Ikilinganishwa na fedha za matumizi ya kawaida zilizotolewa mwaka 2021/22 za kiasi cha Sh. trilioni 17.754 hivyo nilibaini ongezeko la fedha za matumizi ya kawaida zilizotolewa kwa Sh trilioni 3.236 sawa na 18%.

#### 4.7.2 Fedha zilizotolewa kwa Matumizi ya Kawaida na Matumizi Yaliyofanyika

Matumizi ya Kawaida yaliyofanywa na Wizara, Wakala na Idara yalikuwa Sh. trilioni 20.927 sawa na 99.7% ya fedha zilizotolewa za Sh. trilioni 20.990, hivyo kiasi cha Sh. bilioni 63 hazikutumiwa na kurejeshwa kwa mlipaji mkuu wa serikali (PMG). Ikilinganishwa na matumizi ya kawaida ya mwaka 2021/22 ya Sh. trilioni 17.541 nilibaini ongezeko la matumizi ya kawaida ya Sh. trilioni 3.386 sawa na asilimia 19%.

Ni maoni yangu kuwa, uwepo wa bakaa ya fedha zisizotumika unamaanisha kutotekelezwa au utekelezaji hafifu wa shughuli zilizokusudiwa, ama uwezo hafifu wa taasisi katika kutumia fedha zilizotolewa kwa wakati.

#### 4.7.3 Bajeti ya Matumizi ya Maendeleo na Fedha zilizotolewa

Ukaguzi wa taarifa za fedha katika wizara, idara na wakala ulibaini kuwa Sh. trilioni 10.927 sawa na 94% zilitolewa kwa matumizi ya maendeleo kati ya bajeti iliyoidhinishwa ya Sh. trilioni 11.686. Ikilinganishwa na fedha zilizotolewa kwa mwaka 2021/22, Sh. trilioni 11.595, nilibaini kupungua kwa fedha za maendeleo zilizotolewa kwa Sh bilioni 668 sawa na asilimia sita.

#### 4.7.4 Fedha zilizotolewa kwa Matumizi ya Maendeleo na Matumizi yaliyofanyika

Matumizi ya fedha za maendeleo katika wizara, Idara na Wakala ilikuwa Sh. trilioni 10.896 sawa na 99% ya fedha zilizotolewa za Sh. trilioni 10.927 zilitumiwa, hivyo kiasi cha Sh. bilioni 31 hakikutumika na kurejeshwa kwa mlipaji mkuu wa serikali (PMG). Ikilinganishwa na matumizi ya Maendeleo ya Sh. trilioni 11.397 ya mwaka 2021/22 nilibaini kupungua kwa matumizi ya maendeleo kwa kiasi cha Sh. bilioni 501 sawa na asilimia nne. Kutokutumia fedha zilizotolewa kunaweza kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizokusudiwa.

### 4.8 Uzingatiwaji wa Sheria na Kanuni za Bajeti

#### 4.8.1 Tofauti kati ya Mabadiliko ya Bajeti iliyoidhinishwa na Mabadiliko ya Bajeti yaliyopitishwa katika Mfumo

Kifungu cha 45 cha Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 Toleo la Mwaka 2020 inahitaji matumizi yanayofanyika katika Mfuko Mkuu chini ya sheria ya bunge kuzingatia



madhumuni yaliyowekwa kisheria na mabadiliko ya bajeti kwa kila fungu utategemea utendaji wa mafungu, bajeti ziliyoidhinishwa, na fedha zilizokusanywa.

Ukaguzi wa taratibu za usimamizi wa bajeti, ikijumuisha ukaguzi wa bajeti iliyoidhinishwa na Sheria ya Bajeti, Taarifa ya mabadiliko ya bajeti (Na. 1 na 2), mfumo wa MUSE na taarifa za fedha kwa kila taasisi, nilibaini utofauti wa taarifa za bajeti zilizoripotiwa kwa Sh. bilioni 524.99 kati ya bajeti iliyorekebisha na kuripotiwa katika mfumo na bajeti iliyoidhinishwa. Mapungufu haya yalichangiwa na kukosekana kwa uwiano wa taarifa za mabadiliko ya Bajeti iliyoidhinishwa na mabadiliko ya bajeti yaliyoripotiwa katika mfumo, jambo linaloashiria mapungufu makubwa katika taratibu za usimamizi wa bajeti.

Ninapendekeza Serikali kupitia Hazina kuimarisha uthibiti dhidi ya usimamizi wa mabadiliko ya bajeti na kuhakikisha, mabadiliko ya bajeti yaliyoidhinishwa hayatofautiani na taarifa za bajeti zilizoripotiwa katika mfumo.

#### 4.8.2 Matumizi yaliyofanyika Nje ya Bajeti

Kifungu cha 27 (4) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 Toleo la Mwaka 2020 kinataka matumizi yaliyoidhinishwa kwa Serikali na taasisi za umma yafanyike kulingana na madhumuni yaliyoelekezwa na kwa mujibu wa mipaka iliyowekwa na makadirio yaliyopo.

Ukaguzi ulibaini taasisi nne za serikali zilitumia jumla ya Sh bilioni 10.20 kama malipo ya matumizi ya kawaida na maendeleo zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa, kwa maelezo zaidi ni katika **Jedwali Na. 7**.

**Jedwali Na. 7: Matumizi Yaliyofanyika Zaidi ya Bajeti Sh. bilioni 10.20**

Taasisi	Maelezo	Kiasi (Sh.)
Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira (RUWASA)	Wakala ilipanga kutumia Sh. 18,885,495,240 kama malipo ya mishahara. Hata hivyo Sh. 22,605,088,700 zilitumika hivyo kupelekea matumizi zaidi ya bajeti ya Sh. 3,719,593,460	3,719,593,460
Fungu 52	Wizara ilifanya malipo kwa TOL Gases Limited kwa ununuzi wa mitungi 4,600 ya oksijeni ya matibabu iliyokuwa nje ya Bajeti	1,143,990,651
Mamlaka ya Mapato-TRA (Matumizi)	Mamlaka ilitumia jumla ya Sh. 2,909,392,371 kwa vitu visivyo na bajeti, wakati Sh. 2,199,301,347 zilikuwa matumizi yaliyofanywa zaidi ya bajeti	5,108,693,718


Taasisi	Maelezo	Kiasi (Sh.)
Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu	Mamlaka ilipanga matumizi ya Sh. 520,812,000 kama gharama za Utawala. Hata hivyo, matumizi halisi yalikuwa Sh. 758,265,606 zaidi ya bajeti kwa Sh. 237,453,606	237,453,606
Jumla		10,209,731,435

Chanzo: Taarifa za Ukaguzi za Mwaka 2022/23

Matumizi ya fedha katika kutekeleza shughuli ambazo hazijapangwa kunaathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa. Aidha, kunaweza kuchangia uwepo wa matumizi yasiyo na tijakwa serikali.

**Napendekeza Serikali na mamlaka zinazohusika kuzingatia Sheria ya Bajeti na kanuni zake ili kuwezesha upatikanaji wa thamani ya fedha. Aidha, taasisi za serikali zinapashwa kuhakikisha zinatenga bajeti ya matumizi yanayopaswa kufanyika.**

# SURA YA TANO



## USIMAMIZI WA UKUSANYAJI WA MAPATO YA KODI, MAPATO YASIYOTOKANA NA KODI, NA DENI LA TAIFA

### 5.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha hoja muhimu za ukaguzi wa hesabu na uendeshaji wa taasisi kuhusu masuala yanayohusiana na usimamizi wa ukusanyaji wa mapato ya kodi, mapato yasiyo ya kodi, hesabu jumuiifu za Serikali na deni la taifa.

### 5.2 Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato ya Kodi Unaofanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania

Mamlaka ya Mapato Tanzania ilianzishwa kupitia Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania Sura ya 399 kama Taasisi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yenye jukumu la kusimamia bila upendeleo makusanyo yote ya kodi za ndani, ushuru wa forodha, na tozo kwa niaba ya Serikali kuu. Mamlaka ya Mapato Tanzania ina jukumu kubwa katika kuhakikisha kunakuwa na ufanisi pamoja na usawa wa ukusanyaji wa mapato, ikichangia shughuli za kifedha za serikali nchini Tanzania.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikusanya jumla ya Sh. trilioni 22.583, chini ya lengo lililowekwa la Sh. trilioni 23.652, ikionesha upungufu wa Sh. trilioni 1.069, sawa na 4.5% ya malengo ya mapato yote katika Tanzania Bara. **Jedwali Na. 8** linaonesha mchanganuo wa ukusanyaji wa mapato kiidara kwa Tanzania Bara.

**Jedwali Na. 8: Mchanganuo wa Makusanyo ya Mapato (Tanzania Bara)**

Idara	Makisio (Sh. Bilioni)	Makusanyo Halisi (Sh. Bilioni)	Makusanyo ziada (Pungufu) Sh. Bilioni	% ya Ziada/ (Upungufu)
Kodi za Ndani	5,024.15	5,287.19	263.04	5.2
Walipakodi Wakubwa	9,801.57	9,032.31	(769.26)	(7.8)
Ushuru na Forodha	9,432.27	9,325.51	(106.77)	(1.1)
Jumla ya Makusanyo	<b>24,257.99</b>	<b>23,645.01</b>	<b>(612.99)</b>	<b>(2.5)</b>
Punguza: Marejesho ya Kodi na Hamisho kwenda Mamlaka ya Kodi Zanzibar	657.83	1,079.05	421.21	64

Idara	Makisio (Sh. Bilioni)	Makusanyo Halisi (Sh. Bilioni)	Makusanyo ziada (Pungufu) Sh. Bilioni	% ya Ziada/ (Upungufu)
Jumla baada ya Marejesho ya kodi na Hamisho	23,600.16	22,565.96	(1,034.20)	(4.4)
Ongeza: Vocha za Hazina (TVC) <sup>5</sup>	52.60	17.58	(35.02)	(66.6)
<b>Jumla</b>	<b>23,652.76</b>	<b>22,583.54</b>	<b>(1,069.22)</b>	<b>(4.5)</b>

Chanzo: Taarifa za Makusanyo za Mapato Zilizokaguliwa Mwaka 2022/23

Mamlaka ya Mapato Zanzibar ilikusanya jumla ya Sh. bilioni 456.19, ikiwa ni zaidi ya lengo lililowekwa la Sh. bilioni 454.06, hivyo kusababisha ukusanyaji wa ziada wa Sh. bilioni 2.14, sawa na 0.5%. **Jedwali Na. 9** linaonesha mchanganuo wa makusanyo ya mapato kiidara Zanzibar.

#### Jedwali Na. 9: Mchanganuo wa Makusanyo ya Mapato (Zanzibar)

Idara	Makisio (Sh. Bilioni)	Makusanyo Halisi (Sh. Bilioni)	Makusanyo Ziada (Pungufu) (Sh. Bilioni)	% ya Ziada/ (upungufu)
Kodi za Ndani	226.02	231.85	5.83	2.6
Ushuru na Forodha	228.04	224.35	(3.69)	(1.6)
<b>Jumla ya Makusanyo</b>	<b>454.06</b>	<b>456.19</b>	<b>2.14</b>	<b>0.5</b>

Chanzo: Taarifa za Makusanyo za Mapato zilizokaguliwa 2022/2023

Katika mwaka wa fedha 2022/23, utendaji wa Idara za Walipakodi Wakubwa na Ushuru na Forodha katika ukusanyaji wa mapato ulikuwa chini ya malengo waliyowekewa, wakati Idara ya Kodi za Ndani ukusanyaji ulikuwa juu ya lengo. Kwa ujumla, utendaji duni wa ukusanyaji ulitokana na kutofikiwa kwa malengo ya ushuru wa bidhaa (excise duty), kodi ya zuio (withholding tax), ushuru wa mafuta (fuel levy), kodi yaongezeko la thamani (VAT), na kodi ya faida (corporate tax).


Aidha, kulikuwa na utendaji mzuri katika marejesho ya kodi (tax refund), uliosababishwa na ongezeko la kasi ya kuhakiki madai yaliyowasilishwa. Hali hii ilisababisha ongezeko la kiasi kilichorudishwa kwa walipakodi ikilinganishwa na kiasi kilichokadiriwa.

Ulinganifu wa idara katika ukusanyaji wa mapato kwa Mamlaka ya Mapato (Tanzania Bara) ulionesha kuwa, Idara ya Ushuru na Forodha ilichangia asilimia

<sup>5</sup> Vocha ya Hazina ni malipo yanayofanywa kupitia mfumo wa kodi kwa ajili ya kulipia ushuru wa uagizaji kwa watumishi wanaostahili, ambao ni pamoja na watumishi wa umma, maofisa wa umma, na mashirika. Katika hali hii, Vocha ya Hazina ziliingizwa kama sehemu ya tathmini ya ukusanyaji kwa idara ya Ushuru na Forodha.


39.4 ikifuatiwa na Idara ya Walipakodi Wakubwa kwa asilimia 38.2, na Idara ya Kodi za Ndani kwa 22.4%. Ulinganisho wa ukusanyaji wa mapato halisi kwa mwaka wa fedha 2022/23 na 2021/22 kiidara unaoneshwa katika **Kielelezo Na. 2.**

**Kielelezo Na. 2: Ulinganifu wa Uchangiaji wa Makusanyo Halisi Kiidara 2022/23 na 2021/22 (Tanzania Bara)**



**Chanzo:** Taarifa za Hesabu za Mapato za Mamlaka Zilizokaguliwa Mwaka 2022/23 na 2021/22

Kwa Zanzibar, ukusanyaji wa mapato ulionyesha kuwa Idara ya Kodi za Ndani ilichangia 50.8% ikifuatiwa na Idara ya Ushuru na Forodha kwa 49.2%. Ukusanyaji wa mapato halisi kwa mwaka wa fedha 2022/23 na 2021/22 kiidara unaoneshwa katika **Kielelezo Na. 3.**

**Kielelezo Na. 3: Ulinganifu wa Uchangiaji wa Makusanyo Halisi Kiidara 2022/23 na 2021/22 (Zanzibari)**

**Chanzo:** Taarifa za Hesabu za Mapato za Mamlaka Zilizokaguliwa Mwaka 2022/23 na 2021/22

Ulinganifu wa ukusanyaji wa mapato halisi kiidara kwa miaka ya fedha 2022/23 na 2021/22 unaonesha kuwa mchango wa ukusanyaji wa mapato umeongezeka kwa 32.9% kwa Idara ya Kodi za Ndani, 6.8% kwa Idara ya Ushuru na Forodha, na umepungua kwa asilimia mbili kwa Idara ya Walipakodi Wakubwa.

Aidha, uchanganuzi unaonesha kuwa Idara ya walipakodi wakubwa na Idara ya Ushuru na Forodha hazikufikia malengo katika ukusanyaji wa mapato, wakati Idara ya Kodi za Ndani ilifanikiwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa kiasi kilichopangwa kwa mwaka wa fedha 2022/23.

### 5.2.1 Mwenendo wa ukusanyaji wa mapato

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, ukusanyaji wa mapato umekua chini ya malengo yaliyowekwa ambapo kiwango cha makusanyo ya chini ya lengo ni kati ya asilimia nne na 14%. Kumekuwa na kupanda na kushuka katika makusanyo halisi ikilinganishwa na malengo, huku makusanyo yakiwa chini ya malengo kwa kiasi kikubwa zaidi katika mwaka wa fedha 2020/21. Mwenendo huu unatia shaka kuhusu ufanisi wa mikakati ya ukusanyaji wa mapato na kuna uhitaji wa uangalizi wa karibu dhidi ya mambo yanayochangia kutofikiwa kwa

malengo ya makusanyo. **Jedwali Na. 10** linaonesha mwenendo wa ukusanyaji wa mapato kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

**Jedwali Na. 10: Mwenendo wa Ukusanyaji wa Mapato Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**


Mwaka wa Fedha	Makisio (Sh. Bilioni)	Makusanyo Halisi (Sh. Bilioni)	Makusanyo Pungufu	% ya Upungufu
2022/2023	24,106.81	23,039.73	(1,067.09)	4.4
2021/2022	22,191.17	21,303.87	(887.30)	4.0
2020/2021	20,709.32	17,897.86	(2,811.46)	13.6
2019/2020	19,451.12	17,930.88	(1,520.25)	7.8
2018/2019	18,332.67	15,764.66	(2,568.00)	14.0

**Chanzo:** Taarifa za Hesabu za Mapato za Mamlaka Zilizokaguliwa Mwaka 2018/19 hadi 2022/23

**Uwiano wa kodi kwa pato la taifa**

Uwiano wa kodi kwa pato la taifa ni kipimo kinachoonesha uhusiano kati ya jumla ya mapato ya kodi ya nchi na pato la taifa. Uwiano huu hutoa taarifa juu ya kiwango cha kodi kulingana na ukubwa wa uchumi. Uwiano mkubwa wa kodi kwa pato la taifa huashiria kuwa sehemu kubwa ya pato la taifa inakusanywa kama kodi. Kinyume chake, uwiano mdogo wa kodi kwa pato la taifa huashiria kuwa sehemu ndogo ya pato la taifa imekusanywa kama kodi.

Katika mwaka wa fedha 2022/23, utendaji wa Mamlaka ya Mapato ulionesha mwelekeo wa kushuka kwa kiwango cha kodi kwa pato la taifa (uwiano wa kodi kwa pato la taifa) ikiwa ni 12.5% ikilinganishwa na 12.8% katika mwaka wa fedha 2021/22. **Kielelezo Na. 4** kinaonesha uwiano wa kodi kwa pato la taifa kwa miaka mitano.

**Kielelezo Na. 4: Mwenendo wa Uwiano wa Kodi kwa Pato la Taifa kwa Miaka Mitano**

**Jedwali Na. 11** linaonesha ulinganisho wa uwiano wa kodi kwa pato la taifa Tanzania na nchi zingine za Afrika Mashariki.

**Jedwali Na. 11: Uwiano wa Kodi kwa Pato la Taifa la Tanzania na Nchi Zingine za Afrika Mashariki kwa Miaka Mitano**

Nchi	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22	2022/23
Kenya	15.50%	14.60%	13.70%	15.00%	14.20%
Rwanda	16.30%	16.20%	16.30%	15.80%	15.00%
Tanzania	12.00%	12.60%	11.70%	12.80%	12.50%
Uganda	15.10%	12.10%	13.00%	13.50%	13.70%
Burundi	15.20%	16.50%	17.00%	17.60%	18.00%

Chanzo: Kamati za Ufundi za Mamlaka za Mapato za Afrika Mashariki

Kutoka kwenye jedwali hapo juu, ninaweza kuhitimisha kwamba takwimu zilizotolewa kuanzia mwaka 2018/19 hadi 2022/23, uwiano wa kodi kwa pato la taifa umenadilika kwa kati ya 11.7% na 12.8%, na kwa mwaka 2022/23 ni 12.5%. Uwiano wa kodi kwa pato la taifa kwa Tanzania kwa ujumla ni mdogo ikilinganishwa na baadhi ya nchi zingine za Afrika Mashariki, jambo linaloonesha kuwa sehemu ndogo ya pato la taifa hokusanywa kama kodi.

Ufanisi wa ukusanyaji wa kodi nchini Tanzania katika kulinganisha mapato halisi na malengo, unahitaji kuboreshwa kupitia juhudi zaidi katika ukusanyaji wa mapato kwa kuongeza wigo wa kodi, kuziba mianya ya uvujaji wa mapato, na kuhamasisha kulipa kodi kwa hiari. Hatua hizi hatimaye



zitapunguza nakisi ya bajeti ya nchi na kupunguza pengo katika ufadhili wa deni.

### 5.2.2 Kushikiliwa kwa Kodi Zinazofikia Sh. trilioni 10.489 kwenye Mahakama za Rufaa za Kodi

Katika ukaguzi wangu wa hesabu za Mamlaka ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2022/23, nilibaini kuwapo kwa mashauri 967 ya kikodi katika mahakama za rufaa za kodi kwa muda mrefu yanayofikia Sh. trilioni 10.489 (inahusisha dola za Marekani 19,261,725 zilizobadilishwa kwa Sh. 2,339.10/dola ya Marekani) kwa Tanzania Bara.

Kiasi hiki kinaashiria ongezeko la Sh. trilioni 5.65 sawa na asilimia 117 ikilinganishwa na Sh. trilioni 4.836 zilizoripotiwa mwaka wa fedha 2021/22. Mambo yanayosababisha uchelewashaji wa maamuzi ya mashauri ya rufaa ni pamoja na kutofanya uteuzi wa wajumbe wa bodi kwa mikoa isiyo na wajumbe, na kutoteua kwa haraka wajumbe, wenyeviti, na makamu wenyeviti, na uhaba wa bajeti za mahakama za rufaa za kodi. **Jedwali Na. 12** linaonesha mwenendo wa mashauri ya kikodi.

**Jedwali Na. 12: Mwenendo wa Mashauri ya Kikodi**

Taarifa	Idadi Ya Mashauri	Mahakama Ya Rufaa		Mahakama Ya Rufaa Ya Mapato Ya Kodi		Bodi Ya Rufaa Za Mapato Ya Kodi		Jumla	
		Sh.	Dola Za Marekani	Sh.	Dola Za Marekani	Sh.	Dola Za Marekani	Sh.	Dola Za Marekani
Idadi ya mashauri mwanzoni mwa mwaka	898	232,905,700,174	12,594,326	491,162,240,828	-	3,699,271,178,162	3,118,906	4,423,339,119,164	15,713,232
Mashauri yaliyofunguliwa ndani ya mwaka	674	23,860,231,891	-	104,289,997,089	2,926,107	7,359,913,504,406	12,159,461	7,488,063,733,387	15,085,568
Jumla Ndogo	1572	256,765,932,066	12,594,326	595,452,237,918	2,926,107	11,059,184,682,568	15,278,367	11,911,402,852,551	30,798,800
Mashauri yaliyoamuliwa	(605)	(51,978,794,894)	(8,610,968)	(311,296,439,597)	(2,926,107)	(1,104,032,613,516)	-	(1,467,307,848,007)	(11,537,075)
Idadi ya mashauri yaliyobaki mwishoni mwa mwaka	967	204,787,137,171	3,983,358	284,155,798,321	-	9,955,152,069,052	15,278,367	10,444,095,004,544	19,261,725

Chanzo: Taarifa za Hesabu za Mamlaka ya Mapato Mwaka 2022/2023

Mchangano wa mashauri ya kikodi umeoneshwa kwenye Jedwali Na. 13.

**Jedwali Na. 13: Mashauri ya Kikodi Yaliyobaki Tanzania Bara**

Mwaka	Idadi Ya Mashauri	Mahakama Ya Rufaa		Mahakama Ya Rufaa Ya Mapato Ya Kodi		Bodi Ya Rufaa Ya Mapato Ya Kodi		Jumla	
		Sh.	Dola Za Marekani	Sh.	Dola Za Marekani	Sh.	Dola Za Marekani	Sh.	Dola Za Marekani
2018	4	-	-	586,364,625	-	8,893,085,680	-	9,479,450,305	-
2019	6	-	-	-	-	7,528,564,872	-	7,528,564,872	-
2020	15	10,495,589,534	-	49,729,889,875	-	82,856,439,100	-	143,081,918,509	-
2021	157	60,655,103,403	-	58,129,654,062	-	417,941,067,045	2,926,107	536,725,824,510	2,926,107
2022	398	124,426,326,016	3,983,358	115,079,098,431	-	2,409,893,268,511	254,761	2,649,398,692,959	4,238,119
2023	387	9,210,118,218	-	60,630,791,328	-	7,028,039,643,845	12,097,500	7,097,880,553,390	12,097,500
JUMLA	967	204,787,137,171	3,983,358	284,155,798,321	-	9,955,152,069,052	15,278,367	10,444,095,004,544	19,261,725

Chanzo: Taarifa za Hesabu za Mamlaka ya Mapato Mwaka 2022/23

Kwa Zanzibar, kulikuwa na mashauri 96 yanayofikia Sh. bilioni 20.753 kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 14.

**Jedwali Na. 14: Mashauri ya Kikodi Yaliyopo katika Mahakama ya Rufaa ya Mapato ya Kodi (Zanzibar)**

Mwaka	Idadi Ya Mashauri	Bodi Ya Rufaa Ya Mapato Ya Kodi	Mahakama Ya Rufaa Ya Mapato Ya Kodi	Jumla
		Sh.	Sh.	Sh.
2019	9	553,356,113	-	553,356,113
2020	1	-	19,696,833	19,696,833
2022	1	-	125,366,562	125,366,562
2023	85	20,054,190,872	-	20,054,190,872
Jumla	96	20,607,546,985	145,063,395	20,752,610,380

Chanzo: Taarifa za Hesabu za Mamlaka ya Mapato Mwaka 2022/23

Ninapendekeza Serikali iongeze kasi ya kusikiliza na kutolea uamuzi mashauri ya kikodi yaliyopo kwenye mahakama za rufaa za kodi kwa; kuongeza bajeti za mahakama za rufaa za kodi, kuhakikisha uteuzi kwa wakati wa wajumbe wa bodi kwa mikoa isiyo na wajumbe, na kuteua kwa haraka wajumbe, wenyeviti, na makamu wenyeviti. Hatua hizi zitasaidia kufanyika kwa vikao vingi zaidi na kurahisisha uamuzi wa haraka wa rufaa za kodi.

### 5.2.3 Upungufu katika Kutambua Makusanyo na Madeni Kwenye Sekta ya Utalii

Mapitio yangu ya taarifa za mapato ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa mwaka wa fedha 2022/23 yalibaini kuwa Sh. bilioni 399.73 ziliripotiwa kama makusanyo ya sekta ya utalii ikiwa ni pamoja na kodi ya ongezeko la thamani kwa huduma zilizotolewa. Kiasi hiki kiliamishwa kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali kupitia akaunti kuu ya Mamlaka ya Mapato.

Wakati huohuo, sekta ya utalii iliendelea kuwasilisha ritani ya kodi ya ongezeko la thamani ya kila mwezi, ikijumuisha mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato, ikiwa pamoja na kodi ya ongezeko la thamani. Katika hali hii, deni la kodi la Sh. bilioni 87.47 linalohusiana na Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) lililotokana na ritani hizo za kodi liliendelea kubaki kwa sababu mapato yaliyotarajiwa kulipa deni hilo yalikusanywa na kuhamishiwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Wakati kiasi kilichokusanywa kwa wateja kama malipo ya awali ya watalii hakikuripotwa kwenye taarifa za kifedha za TANAPA kama deni, mapato yaliyokusanywa yaliripotwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Inapotokea tukio la kufutwa/kuahirishwa kwa safari za kwenda kwenye hifadhi, marejesho ya ada za utalii yaliyokusanywa hayataweza kurudishwa kwa wakati, kwa sababu mapato yanakuwa yameshamishiwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Ninapendekeza Serikali iratibu vizuri uendeshaji wa huduma za utalii na michakato ya ukusanyaji wa mapato yatokanayo na utalii ili kuwezesha uwasilishaji sahihi na utoaji wa huduma kwa watalii. Hata hivyo, taasisi yoyote ambayo mapato yake yanahamishwa moja kwa moja kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali, taasisi husika zinapaswa kuondolewa kuwajibika kupeleka ritani za kodi. Ili pendekezo hili lifanyiike, kuna haja ya kurekebisha sheria.

#### 5.2.4 Upungufu wa Ving'amuzi vya Kieletroniki wakati wa Kuthibitisha bidhaa Zinazopita nchini kwenda Nchi Jirani

Katika mapitio yangu ya miamala ya bidhaa zinazopita nchini kwenda nchi jirani kupitia mipaka ya forodha ya Mutukula, Rusumo, na Tunduma, nilibaini upungufu mbalimbali wa ving'amuzi vya kielekitroni. Mathalani, nilibaini king'amuzi kutoonekana kwenye mfumo wa ving'amuzi vya kieletroniki (ECTS), taarifa zisizo sahihi za king'amuzi kwenye mfumo, na kutowiana kwa taarifa kati ya king'amuzi saidizi na king'amuzi mama, hivyo kufanya iwe vigumu kuzima kifaa na kuhakiki bidhaa zinazokwenda nchi jirani kwa haraka na kwa wakati kwenye mfumo wa forodha (TANCIS) mara tu ukaguzi unapokamilika.

Mapitio zaidi yalibaini kuwa miamala 238, ikijumuisha miamala 95 katika mpaka wa Mutukula, miamala 22 katika mpaka wa Rusumo, na miamala 121 katika mpaka wa Tunduma ilikuwa na tatizo kwenye ving'amuzi vya kielekitroni (E-seal). Matatizo haya yalisababisha ucheleweshaji wa uhakiki wa miamala ya bidhaa zinazoenda nchi jirani kwenye mfumo wa forodha (TANCIS), kwani sanduku la kuhakiki lilikuwa halifanyi kazi au halipatikani. Wakati mwingine, hali hii ilisababisha kutumia muda mrefu zaidi kukamilisha taratibu za kutoa mizigo kutoka katika Kitengo cha Kufuatilia Usafirishaji wa Bidhaa Zinazoenda Nchi Jirani Kupitia Nchini (Trasit Monitoring Unit).

Ninapendekeza Serikali, kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania, ifanye uchambuzi wa mara kwa mara wa upungufu kwenye ving'amuzi vya kielekitroni kwa kutambua wauzaji (vendors) wenye kiwango kikubwa cha matatizo na kuchukua hatua stahiki, ambayo inaweza kujumuisha

kubadilisha wauzaji au kushiriki moja kwa moja katika ununuzi wa vifaa. Zaidi ya hayo, menejimenti inapaswa kushughulikia kwa haraka na kwa ufanisi upungufu wa ving'amuzi vya kielekitroni ili kuzuia kutokea tena kwa hitilafu na kutatua matatizo ya mfumo na kuzuia ucheleweshaji wa taratibu za kutoa mizigo.

#### 5.2.5 Mafuta Yaliyopitiliza Muda wa Kukaa Nchini Yaliyopaswa kwenda Nchi Jirani Lakini Hayakutozwa Ushuru wa Forodha

Ukaguzi wangu wa mwaka 2022/2023 ulibaini kuwapo kwa bakaa ya lita za mafuta 1,105,466.01 zilizoingizwa nchini kwa ajili ya kusafirishwa kwenda nchi jirani zenye makadirio ya kodi ya Sh. milioni 929.6, ambayo hayakusafirishwa kwenda nchi husika kwa muda wa zaidi ya siku 30 lakini ushuru wa forodha haukukusanywa.

Ninapendekeza Serikali, kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania, ifanye maboresho ya kimfumo katika ufuatiliaji wa usafirishaji wa mafuta yanayoenda nchi jirani kupitia nchini ili kuhakikisha kiasi chote cha mafuta kinafika sehemu iliyokusudiwa. Hatua hii inalenga kuzuia utofauti na kuhakikisha ushuru wa forodha unakusanywa kwa wakati kwenye bakaa ya mafuta yanayokwenda nchi jirani.

#### 5.2.6 Kukosekana kwa Uthibitisho wa Kupokelewa kwa Mafuta yaliyosafirishwa kwenda Zanzibar yenye Thamani ya Kodi ya Sh. Milioni 368.6

Katika mapitio yangu ya taarifa za mafuta kwenye mfumo wa forodha (TANCIS) kwa ajili ya kusafirishwa kwenda Zanzibar nilibaini kuwa jumla ya miamala miwili ya thamani ya Sh. milioni 368.6 haikuhakikiwa kuwa imefika mahali kulikokusudiwa. Kukosa uthibitisho wa kufika kwa mafuta hayo kunazua hofu ya mafuta hayo kuuzwa nchini bila kulipa ushuru stahiki.

Ninapendekeza Serikali, kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania, (a) ifanye ufuatiliaji katika kampuni za uuzaji mafuta zilizohusika ili kuthibitisha usafirishaji wa mafuta yaliyotumwa kwenda Zanzibar, au vinginevyo, kodi husika ikusanywe; na (b) ishughulikie tatizo la mfumo lililosababisha tatizo hili.

### 5.2.7 Ritani 193,993 za kodi ya ongezeko la thamani hazikuwasilishwa na walipakodi 17,575

Ukaguzi wangu wa mfumo wa kieletroniki wa kuwasilisha ritani za kodi ya ongezeko la thamani kwa mwaka wa fedha 2022/23 ulibaini kuwa, mikoa 9 ya kikodi ilikuwa na jumla ya walipakodi 35,642 waliosajiliwa na kodi ya ongezeko la thamani. Kati ya hawa, walipakodi 18,067, sawa na asilimia 51, walifanikiwa kuwasilisha ritani za kodi ya ongezeko la thamani.

Hata hivyo, walipakodi 17,575, sawa na 49%, hawakutumiza wajibu wao wa kuwasilisha ritani za kodi ya ongezeko la thamani. Kutojaza ritani za kodi ya ongezeko la thamani kunaweza kuwa na athari kwenye malengo ya mapato, hivyo kusababisha upotevu wa mapato ya Serikali.

**Ninaishauri Serikali, kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania, (a) ichukue hatua zitakazohakikisha uzingatiaji wa sheria kuhusu uwasilishaji wa ritani za kodi ya ongezeko la thamani na kuchukua hatua stahiki kwa wale ambao hawakuwasilisha ritani 193,993; (b) ihakikishe ukusanyaji wa mapato ya ndani ya kodi zilizochelewa na kutozwa kwa adhabu kwa kuchelewa kuwasilisha ritani hizo.**

## 5.3 Usimamizi wa Mapato Yasiyotokana na Kodi

Usimamizi wa mapato yasiyotokana na kodi ni chanzo muhimu na endelevu katika mipango ya kifedha ya serikali. Ili kusimamia kwa ufanisi mapato yasiyotokana na kodi, serikali inapaswa kubaini na kutathmini vyanzo endelevu vya makusanyo haya na kutoza ada stahiki. Aidha, serikali inapaswa kudhibiti upotevu wa mapato yaliyokusanywa na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya usimamizi wa mapato yasiyotokana na kodi ili kupima utendaji katika mapato na kutambua maeneo yanayohitaji kuboreshwa ikiwa pamoja na upanuzi wa mawanda ya ukusanyaji wa mapato. Sura hii inaangazia mikakati ya kukuza makusanyo yasiyotokana na kodi, kama vile ada, faini, leseni, tozo za vibali, pamoja na makusanyo yanayotokana na mauzo ya bidhaa na huduma.

Katika mwaka wa fedha 2022/23, Serikali ilipanga kukusanya jumla ya Sh. trilioni 3.35 kama mapato yasiyotokana na kodi sawa na asilimia nane ya Bajeti. Nilifanya tathmini ya ufuatiliaji wa sheria, kanuni, na maelekezo mbalimbali yanayosimamia ukusanyaji wa mapato yasiyotokana na kodi na kubaini mapungufu katika ukusanyaji wa mapato kama ilivyoelezwa hapa chini:

### 5.3.1 Mapato ambayo Hayakukusanywa kutokana na Ukosefu wa Ufanisi katika kutoa Huduma

Nilipitia mwenendo wa ukusanyaji wa mapato katika idara na wakala zinazotoa huduma mbalimbali kama sehemu ya majukumu yake na kubaini kuwa jumla ya Sh. bilioni 1.86 hazikukusanywa na Kampuni ya Ulinzi ya SUMA JKT pamoja na Jeshi la Zima Moto (Fungu 14) kutokana na ukosefu wa ufanisi katika kutoa huduma.

Kampuni ya Ulinzi ya SUMA JKT ni kampuni tanzu ya SUMA JKT iliyoanzishwa kwa lengo la kutoa huduma za ulinzi na usalama wa wananchi, viongozi, na mali za serikali. Hata hivyo, nilibaini kwamba kampuni hii haikuweza kutekeleza kikamilifu mikataba ya huduma za ulinzi na usalama kama ilivyopangwa kutokana na ukosefu wa vifaa muhimu na wafanyakazi wakutosha. Changamoto hizi zilisababisha kutokusanya mapato ya Sh. milioni 750.30 katika mwaka wa fedha 2022/23. Badala yake, kampuni ilikusanya Sh. bilioni 46.86 tu kati ya Sh. bilioni 47.61 zilizokuwa kwenye mikataba.

Aidha, Kifungu cha 22(2) cha Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ya Mwaka 2021 (iliyorekebishwa), na Kanuni ya 14(1) ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji (Uchunguzi na Vyeti vya Usalama) ya Mwaka 2014 (iliyorekebishwa) imelipa mamlaka Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kufanya ukaguzi wa mipango ya usalama wa majengo kwa ajili ya kinga dhidi ya majanga ya moto kabla ya kutoa vibali vya ujenzi na kukusanya ushuru wa ukaguzi. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini ofisi sita za kikanda za jeshi la zimamoto na Uokoaji hazikufanya ukaguzi wa usalama dhidi ya majanga ya moto katika majengo 7,578 hivyo kusababisha kutokusanywa kwa mapato ya Sh. bilioni 1.11. Kutokusanywa kwa mapato katika chanzo hiki kunatokana na upungufu wa rasilimali watu, mipango hafifu ya ukusanyaji wa mapato, na kukosekana kwa usimamizi wa kutosha. Hivyo, ni muhimu Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kuwa na mpango-mkakati utakaohakikisha kaguzi za usalama dhidi ya majanga ya moto zinafanyika ili kukusanya mapato na kuongeza usalama wa majengo.

**Ninapendekeza Serikali, kupitia taasisi husika, iongeze juhudi na uwezo katika kutoa huduma na kukusanya mapato stahiki.**

### 5.3.2 Mapato ya Sh. Milioni 418.32 Yasiyowasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali

Kifungu cha 12 cha Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348 kama ilivyorekebisha mwaka 2020 kinaeleza kwamba kwa mujibu wa Ibara ya 135 ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, mapato yote yanayopokelewa kwa madhumuni ya Serikali (isipokuwa mapato mengine yanayokusanywa chini ya sheria zingine kwa madhumuni maalumu au makusanyo yaliyoamriwa kutumiwa na mamlaka zinazokusanya bila kuwasilishwa kwenye Mfuko Mkuu) yanapaswa kuwasilishwa kwenye mfuko mkuu wa hazina ya serikali.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa katika mwaka wa fedha 2022/23, ubalozi wa Tanzania Maskati, Omani ulikusanya mapato ya jumla ya Sh. milioni 418.32 yanayotokana na uthibitishaji wa nyaraka mbalimbali katika ubalozi. Hata hivyo, mapato hayo hayakuwasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina kinyume na kifungu kilichotajwa.

Kutowasilishwa kwa mapato hayo katika Mfuko Mkuu wa Hazina kumeinyima serikali mapato ambayo yangeweza kutumiwa katika shughuli zingine za maendeleo. Aidha, kutowasilishwa kwa mapato hayo katika Mfuko Mkuu wa Hazina kunaweza kusababisha kutumiwa kwa shughuli zisizokusudiwa.

**Ninapendekeza Serikali, kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki (Fungu 34), ihakikishe kwamba kiasi kilichokusanywa kinawasilishwa kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina kwa mujibu wa sheria.**

### 5.3.3 Wizara ya Ardhi Kushindwa Kukusanya Fedha za Mikopo ya Programu ya “KKK” kutoka kwa Wanufaika

Wizara ya Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi inahusika na uandaaji wa mpango wa matumizi ya ardhi, utoaji wa usajili, na umiliki wa hati za umiliki wa ardhi, kuhamasisha na kuwezesha wananchi kupata makazi bora, kutatua migogoro ya ardhi na makazi, kusimamia upatikanaji na uhifadhi wa kumbukumbu za ardhi, na kusimamia ukusanyaji wa mapato ya serikali yanayotokana na huduma za sekta ya ardhi.

Ili kurahisisha usimamizi wa ardhi na ukusanyaji wa mapato, Wizara ilianzisha mikakati mbalimbali ikiwa pamoja na Mkakati wa Urasimishaji wa Ardhi kupitia Programu ya “Kupima, Kupanga, na Kumilikisha Ardhi” (KKK).



Tarehe 8 Novemba 2021, Wizara ya Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi ilisaini makubaliano na Wizara ya Fedha, na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kupata mkopo wa Sh. bilioni 50 wa kutekeleza programu hiyo kutoka Wizara ya Fedha. Wizara ya Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi iligawa Sh. bilioni 41.14 kwa mamlaka 54 za serikali za mitaa na taasisi zingine tano za serikali ili zitekeleze programu ya KKK. Lengo lilikuwa kusajili hatimiliki za ardhi 218,618 ifikapo mwezi Juni 2022 na kurejesha kikamilifu fedha zilizotolewa ndani ya miezi sita tangu tarehe ya kusaini makubaliano.

Nimebaini tangu kuanza kwa programu hiyo, Wizara ya Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi ilifanikiwa kusajili na kuidhinisha hatimiliki za ardhi 212,892 tu, ikiwa ni pungufu ya lengo kwa hatimiliki 5,726. Aidha, kati ya Sh. bilioni 41.14 zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa programu, Wizara ilipokea Sh. bilioni 8.71 pekee kama marejesho ya fedha zilizotolewa. Hali hii inamaanisha kuwa kiasi cha Sh. bilioni 32.43 kilichotolewa kwa mamlaka za serikali za mitaa hakikurejeshwa licha ya muda wa kurejesha kumalizika tarehe 30 Juni 2022. Zaidi nimebaini Sh. milioni 876.18 zilizokusanywa kutokana na hatimiliki za ardhi zilizotolewa katika mamlaka sita<sup>6</sup> za serikali za mitaa hazikuwasilishwa Wizara ya Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi, jambo ambalo linaathiri ukusanyaji wa fedha zilizotolewa kupitia programu hii na uendeleu wa programu kwa ujumla.

**Ninapendekeza Serikali, kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48) iandae mpango-mkakati wa ukusanyaji wa fedha za Serikali zilizotolewa kupitia utekelezaji wa Programu ya KKK ili kuhakikisha programu hiyo inakuwa endelevu.**

#### 5.3.4 Kukosekana kwa Chanzo Mbadala cha Mapato ya Mfuko wa Kuendeleza Sekta ya Madini

Mfuko wa Kuendeleza Sekta ya Madini ulianzishwa mwaka 2012 chini ya Sheria ya Uwezesaji wa Taifa “*National Empowerment Act*” ya Mwaka 2004 ili kuwawezesha wachimbaji wadogo na wa kati wa madini, kuendeleza mafunzo ya ujasiriamali katika sekta ya madini, kuongeza uwezo wa maofisa wa serikali kufuatilia shughuli za kiuchumi katika sekta hiyo, na kuongeza mchango wa sekta katika uchumi wa taifa.

<sup>6</sup>Halmashauri ya Wilaya ya Musoma, Halmashauri ya Mji Babati, Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga, na Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze.

Awali, chanzo kikuu cha mapato ya Mfuko kilikuwa michango iliyotokana na kampuni za uchimbaji madini zilizofanya kazi chini ya Mikataba ya Maendeleo ya Madini na Serikali “*Mining Development Agreements*”<sup>7</sup>. Hata hivyo, marekebisho yaliyofanywa kupitia Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 (kama ilivyorekebisha na Sheria ya Madini ya Mwaka 2017) ilifuta mikataba hiyo na kuondoa chanzo hiki cha mapato kwa Mfuko bila kuanzisha chanzo mbadala cha mapato. Kukosekana kwa chanzo mbadala na endelevu cha mapato ya Mfuko kunakwamisha malengo na mikakati yake na kuzuia ukuaji wa sekta ya madini.

**Ninapendekeza Serikali, kupitia Wizara ya Madini (Fungu 100) na Mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya Madini, itafute chanzo mbadala cha mapato yatakayotumika kutekeleza shughuli za maendeleo endelevu katika sekta ya madini kwa kuwawezesha wachimbaji wadogo na wa kati.**

### 5.3.5 Kutokusanywa kwa Sh. Bilioni 4.80 za Kodi ya Pango la Nyumba Zilizopangishwa kwa Taasisi za Serikali na Watumishi wa Umma

Wakala wa Majengo Tanzania ulianzishwa kwa lengo la kutoa makazi bora kwa Serikali na watumishi wa umma. Wakala uliingia mikataba 112 na taasisi mbalimbali za serikali ili kutoa makazi kwa watumishi wa umma wa taasisi husika ambapo taasisi hizo zinapaswa kuulipa Wakala kodi ya pango ya kila mwezi kama ilivyoainishwa kwenye mikataba ya upangaji.

Hata hivyo, nilibaini kuwa taasisi za serikali zilichelewa kulipa kodi ya pango ya jumla ya Sh. bilioni 4.80 kwa mujibu wa mikataba ya upangaji. Ucheleweshaji wa kulipa kodi husika ulikuwa kwa muda wa miezi 10 hadi miaka 10, hivyo kupunguza ukusanyaji wa mapato wa Wakala kupitia chanzo hiki. Mapato ya kodi hizo yangeweza kuelekezwa katika kutekeleza shughuli zilizopangwa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa nyumba mpya na ukarabati wa nyumba zilizochakaa za Wakala.

**Ninapendekeza Wakala wa Majengo Tanzania uhakikishe wapangaji wote wanalipa kodi zote wanazodaiwa. Aidha, Wakala unashauriwa kuanzisha utaratibu wa makato ya kodi moja kwa moja kutoka kwenye mishahara ya**

<sup>7</sup>Mikataba ya Maendeleo ya Madini “*Mining Development Agreements* ni makubaliano kati ya Serikali na kampuni za uchimbaji wa madini ambayo hutoa ruzuku kwa kampuni za uchimbaji kwa makubaliano kwamba kampuni hizo zitalipa ada ya kila mwaka kwa Serikali kupitia Mfuko wa Kuendeleza Sekta ya Madini.

watumishi wa umma wanaokaa katika nyumba za Serikali badala ya kutegemea malipo ya hiari kutoka kwa wapangaji.

### 5.3.6 Kukosekana kwa Nyaraka za Mikataba Inayosimamia Ukusanyaji wa Mapato

Kanuni ya 57(1 na 2) ya Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2001 inawataka maofisa masuuli kuhakikisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali na fedha za umma ndani ya idara zao ikiwa pamoja na kuwajulisha watu binafsi au taasisi zinazodaiwa madeni yao kupitia ankara na hati za madai.

Nilifanya ukaguzi wa taratibu za ukusanyaji wa mapato katika taasisi mbili za Serikali, ambazo ni Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA), Kampasi ya Dar es Salaam; na Wizara ya Fedha (Fungu 50), na kubaini yafuatayo:

- a) TIA ilipangisha eneo katika lango kuu la Taasisi kwa ajili ya ujenzi wa jengo la mashine ya kutolea fedha (ATM) kwa Benki ya CRDB kwa miaka 13 tangu mwaka 2010 bila kuwapo kwa nyaraka za mkataba inayosimamia makubaliano ya upangishaji huo. Mwaka 2023, Chuo kilifanya majadiliano na CRDB juu ya makadirio ya makusanyo ya Sh. milioni 204.76 ambayo benki inapaswa kulipa kwa kipindi chote cha upangishaji. Hata hivyo, mapato hayo bado hayajakusanywa hadi wakati tunafanya ukaguzi.
- b) Nilibaini kuwa Wizara ya Fedha (Fungu 50) ilikusanya Sh. milioni 218.95 zilizotokana na kodi ya pango kwa wapangaji 50 bila kuwa na nyaraka za mikataba ya makubaliano ya kisheria kati ya pande zilizohusika, jambo ambalo lina athari za kisheria na kifedha kutokana na kukosekana kwa masharti na vigezo vya usimamizi wa upangaji.

Upungufu uliobainika ulitokana na ukosefu wa nyaraka na usimamizi sahihi katika makubaliano ya upangaji na kukosekana kwa taratibu stahiki za uanzishaji na usimamizi wa mikataba, hivyo kusababisha ucheleweshaji na kutolipwa kwa mapato yanayotokana na kodi. Kukosekana kwa mikataba kunatengeneza athari za kisheria na kifedha.

**Ninapendekeza serikali na taasisi husika zifanye makubaliano rasmi ya kimkataba na wapangaji; zipitie taratibu za ndani za ukusanyaji wa mapato; zizingatie sheria katika makusanyo; na ziboreshe uwazi na uwajibikaji katika ukusanyaji wa mapato.**

### 5.3.7 Masharti ya Mkataba Yasiyo na Tija katika Upangishaji wa Eneo la Ardhi katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere

Wizara ya Uchukuzi (iliyokuwa ikijulikana kama Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi, na Mawasiliano), kwa kushirikiana na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania, iliingia makubaliano ya kuimilikisha kwa muda eneo la ardhi katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere tarehe 8 Septemba 1995. Makubaliano hayo yalimpa mpangaji huyo haki ya kutumia mita za mraba 11,458 za ardhi kwa miaka 15 kuanzia mwaka 1995 hadi mwaka 2010 kwa ajili ya kutoa huduma za kantini. Kulingana na makubaliano hayo, mpangaji alipaswa kulipa kiasi cha dola za Marekani 50,000 kila mwaka kama malipo ya kodi ya pango yanayolipwa kwa awamu mbili kila mwaka. Aidha, mmiliki alipaswa kulipa ada ya mpangaji ya asilimia tatu ya mapato ya kila mwaka kulingana na taarifa za fedha zilizokaguliwa. Vilevile, ilikubaliwa kwamba malipo ya kodi ya pango yanapaswa kufanyiwa marekebisho kila baada ya miaka mitano.

Mnamo tarehe 8 Septemba 2010, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania iliongeza muda wa makubaliano ya umiliki wa eneo hilo kwa mpangaji kwa miaka 20 hadi mwaka 2030. Vilevile, mwaka 2018 Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania ilifanya marekebisho ya makubaliano kwa kupunguza ukubwa wa eneo la ardhi kutoka mita za mraba 11,458 hadi 11,000 na kupunguza bei ya malipo ya pango kutoka Dola za Marekani 50,000 hadi 45,000 kwa mwaka na ada ya umiliki ilipunguzwa kutoka asilimia tatu hadi asilimia mbili kwa miaka mitatu.

Hata hivyo, ukaguzi wa mikataba hiyo ulibaini makubaliano ya upangaji yaliyoingwa yalimpa manufaa mpangaji na serikali kukosa mapato stahiki kama inavyoelezwa hapa chini.

- a) Malipo ya kodi ya pango ya dola za Marekani 50,000 kwa mwaka zilizolipwa kuanzia mwaka 1995 hayakufanyiwa marekebisho kwa miaka 23 hadi mwaka 2018 licha ya kuwapo kwa hitaji hilo kwa mujibu wa makubaliano marekebisho yalipaswa yafanyike kila baada ya miaka mitano.
- b) Marekebisho mapya ya mwaka 2018 yalipunguza ada ya umiliki kutoka asilimia tatu hadi asilimia mbili kwa miaka mitatu (2018 hadi 2021). Hata hivyo, Mamlaka iliendelea kutumia asilimia mbili katika mwaka wa fedha uliofuata kuanzia mwaka 2022 hadi mwaka 2023 kinyume bila makubaliano.

- c) Licha ya ongezeko la bei ya soko la upangaji kwa muda, malipo ya pango kwa makubaliano ya mwaka 1995 yalikuwa dola za Marekani 4.36 kwa mita ya mraba, bei ambayo ilipunguzwa hadi dola za Marekani 4.09 kwa mita ya mraba kwa mujibu wa makubaliano ya mwaka 2018 hivyo kumpa manufaa mpangaji na kupunguza mapato ya serikali yaliyokusanywa kuanzia mwaka 2018 ikilinganishwa na mwaka 1995.
- d) Aidha, nililinganisha bei iliyotolewa kama malipo ya kila mwaka kwa wapangaji wenye mikataba inayofanana na kubaini kuwa tarehe 8 Septemba 2020 mpangaji mwingine aliingia makubaliano ya kulipa kodi ya pango ya Sh. 23,200 kwa mita moja ya mraba ikilinganishwa na malipo<sup>8</sup> yanayotolewa na mpangaji niliyemtolea taarifa hapo juu. Hivyo, kiasi cha Sh. milioni 450.80 hakikukusanywa kwa sababu ya utozaji wa bei ndogo ya kodi ya pango. Endapo Mamlaka itashindwa kufanya marekebisho ya bei ya kodi ya pango kwa mpangaji huyo, makadirio ya kiasi cha Sh. milioni 884.66 hakitakusanywa na Mamlaka.

**Ninapendekeza Serikali, kupitia Wizara ya Uchukuzi, ifanye mapitio ya makubaliano ya umiliki na tathmini mpya ya ada ya umiliki na malipo ya kodi ya pango ya kila mwaka kulingana na bei za soko kwa upangishaji wa ardhi katika viwanja wa ndege.**

### 5.3.8 Kutokusanya Ada za Usajili wa Hospitali Binafsi 2,640

Kifungu cha 29(1) na 30 cha Kanuni za Hospitali Binafsi za Mwaka 2018 vinazitaka hospitali binafsi kuwa na vyeti vya usajili kutoka Bodi ya Ushauri ya Hospitali Binafsi, ambavyo vitatumika kwa kipindi cha miaka mitano. Aidha, hospitali hizo zitapaswa kulipa ada ya usajili kila baada ya miaka mitano ili kupata usajili mpya.

Ukaguzi wa Bodi ya Ushauri ya Hospitali Binafsi ulibaini kuwa Bodi hiyo haikukusanya ada za usajili wa miaka mitano zenye thamani ya Sh. milioni 768 katika hospitali binafsi 2,640 zilizosajiliwa tangu kuanzishwa kwa kanuni hiyo mwaka 2018. Kutokusanywa kwa mapato yanayotokana na chanzo hiki kunainyima Serikali makusanyo yaliyokusudiwa ili kutekeleza shughuli za maendeleo.

<sup>8</sup>Sh. 9,384 mwaka 2020; sh. 9,400 mwaka 2021; sh. 9,421 mwaka 2021; na sh. 9,796 mwaka 2023 kwa mita moja kwa mraba

Ninapendekeza Serikali, kupitia Bodi ya Ushauri ya Hospitali Binafsi, ipitie upya taratibu za ukusanyaji wa mapato, iimarishe ufuatiliaji na iongeze uelewa katika kukusanya mapato yatokanayo na chanzo hiki ili kurahisisha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na usajili wa hospitali binafsi.

#### 5.3.9 Kushindwa Kukusanya Ada za Ukaguzi katika Vitengo vya Afya vya Mipakani, Bandarini na Viwanja vya Ndege

Kifungu cha 42 cha Sheria ya Afya ya Umma ya Mwaka 2009 kinataka wamiliki wa meli au ndege, au mawakala wao, kulipa ada za ukaguzi au malipo mengine yanayohusiana na huduma za ukaguzi zinazotolewa na vituo vya afya mipakani, bandarini na viwanja vya ndege. Aidha, Kifungu cha 4.1 cha Mwongozo wa Malipo ya Ukaguzi wa Mipaka iliyoanza Januari 2016 inazitaka meli za kimataifa kulipa dola za Marekani 100 kwa kila meli na Sh. 10,000 kwa mashua na boti za ndani ya nchi.

Ukaguzi uliofanyika katika vituo vya afya vya Arusha, Tarakea, Holili, na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro ulibaini kuwa vituo hivyo vilifanya kaguzi 68,521 bila kukusanya malipo ya ukaguzi ya Sh. milioni 879.11 kwa vyombo husika. Kutokusanya mapato katika chanzo hiki kunasababisha upotevu wa mapato kwa Serikali.

Ninapendekeza Serikali, kupitia Wizara ya Afya (Fungu 52), iimarishe udhibiti wa ndani katika ukusanyaji wa mapato katika vituo vya afya mipakani, bandarini, na viwanja vya ndege, na ihakikishe ada za ukaguzi zinakusanywa kama ilivyokusudiwa.

#### 5.3.10 Mikopo ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake Iliyotolewa bila Kurejeshwa na bila Kukatiwa Bima.

Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ulianzishwa kwa lengo la kuwawezesha wanawake kiuchumi kwa kutoa mikopo nafuu kwa wanawake wajasiriamali na wasio na kazi ili kuboresha kipato na ustawi wao. Urejeshaji wa mikopo hiyo unatarajiwa kufanyika baada ya miezi sita. Ukaguzi ulibaini kuwa Mfuko ulitoa mikopo ambayo haikurejeshwa kwa muda mrefu na isiyo na bima yenye jumla ya Sh. bilioni 1.13 kama inavyoelezwa hapa chini.

### a) Mikopo Isiyorejeshwa kwa Muda Mrefu

Nilibaini kuwa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake una mikopo isiyorejeshwa kwa muda mrefu yenye thamani ya Sh. milioni 475.48 iliyotolewa kwa walengwa kupitia mamlaka 44 za serikali za mitaa kati ya mwaka 2004 na 2017.

Nilibaini pia kuwa mikopo hii imeshindwa kurejeshwa ndani ya kipindi cha miaka 7 hadi 20, jambo linaloashiria kutokuwapo kwa uwezekano wa kurejeshwa. Aidha, nimebaini kuwa mikopo hii ilitolewa bila kuwapo kwa miongozo inayosimamia masharti ya urejeshaji wake.

### b) Mikopo ya Thamani Sh. milioni 664.50 iliyotolewa Bila kukatiwa Bima

Aya ya 2.6(vi) ya Mwongozo wa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ya Mwaka 2022 inataka mikopo inayotolewa kukatiwa bima na mkopaji, na gharama ya bima itapunguzwa kwenye mkopo husika.

Katika mwaka wa fedha 2022/23, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, na Watoto kwa kushirikiana na Idara ya Ustawi wa Jamii ilitoa mikopo kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kwa walengwa 25, ikiwa pamoja na vikundi 11 vya wanawake na wanawake wasio na vikundi 14 yenye thamani ya Sh. milioni 664.50. Hata hivyo, mikopo hiyo ilitolewa bila ya bima. Kukosekana kwa bima ya mikopo kunaongeza athari zinazoweza kutokea endapo wakopaji watahindwa kurejesha mikopo kama ilivyokusudiwa kutokana na kutokea kwa matukio yasiyotarajiwa kama vile kifo au ajali.

Ili kuhakikisha Mfuko unakuwa endelevu, ninapendekeza Serikali, kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake, na Makundi Maalumu (Fungu 53) pamoja na Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, ihakikishe kuwa mikopo yote iliyotolewa inakatiwa bima na wakopaji ili kupunguza hatari za kutorejeshwa. Aidha, Mfuko uhakikishe mikopo yote iliyotolewa inarejeshwa.

#### 5.3.11 Mapato yaliyokusanywa nje ya mifumo ya makusanyo

Kifungu cha 7 cha Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348 (iliyorekebisha mwaka 2020) kinataka makusanyo yote ya fedha za umma yafanywe kupitia mfumo wa kielekitroni wa malipo serikalini (GePG). Aidha, Serikali kupitia bajeti ya mwaka wa fedha 2022/23 iliweka sera, mikakati, na hatua mbalimbali za kiutawala ili kusimamia ukusanywaji wa mapato. Hatua hizi zinasisitiza matumizi ya mifumo ya kielekitroni ya makusanyo ya fedha za serikali pamoja na umuhimu wa kutumia namba za udhibiti wa malipo ya serikali.

Hata hivyo, nilibaini kutozingatiwa kwa sheria hii katika mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2023; Taasisi tatu za Serikali zilikusanya jumla ya Sh. Bilioni 7.73 bila kutumia namba za udhibiti wa malipo na mifumo ya makusanyo, yaani Wizara ya Elimu (Fungu 46) ilikusanya Sh. bilioni 3.99 na vyombo vya watoa huduma ya maji vilikusanya Sh. 3.01 bilioni nje ya mfumo wa GePG, wakati Wizara ya Uvuvi (Fungu 64) ilikusanya Sh. milioni 730.51 nje ya Mfumo wa Usimamizi wa Mapato yatokanayo na Uvuvi. Kutotumiwa kwa mifumo ya ukusanyaji wa mapato kunaweza kuleta athari za upotevu na ubadhirifu wa mapato, hivyo kuongeza nakisi ya bajeti.

Ninapendekeza taasisi zote za Serikali zilizopewa jukumu la kukusanya mapato kutafuta suluhisho juu ya changamoto za ukusanyaji wa mapato; kutekeleza mikakati, sera, na hatua za kiutawala zilizowekwa na Serikali kusimamia ukusanyaji wa mapato; na kuhakikisha mapato yote yanakusanywa kupitia Mfumo wa Kielekitroni wa Malipo ya Serikali.

### 5.3.12 Kutokusanywa kwa Mapato yasiyotokana na Kodi ya Thamani ya sh. Bilioni 61.09

Makusanyo yasiyotokana na kodi yanaweza kujumuisha vyanzo mbalimbali kama vile faini, ada, mrabaha, na vyanzo vinginezo vya makusanyo isipokuwa kodi. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, makusanyo yasiyotokana na kodi yalikalidiriwa kuchangia asilimia nane<sup>9</sup> ya bajeti ya Serikali ikiwa ni chanzo muhimu cha makusanyo ya Serikali.

Nilipitia taarifa za fedha za wizara, wakala na taasisi mbalimbali na kubaini madai ya Sh. bilioni 61.09 yaliripotiwa kama madai ambayo hayakukusanywa hadi tarehe 30 Juni 2023 baada ya huduma mbalimbali kutolewa. Sehemu kubwa ya madai hayo yalikuwa hayajakusanywa kwa zaidi ya miezi 12, hivyo kuzuia mchango wake katika kugharamia matumizi ya Serikali. **Jedwali Na. 15** linaonesha orodha ya taasisi zilizokuwa na madeni ambayo hayakukusanywa.

**Jedwali Na. 15: Taasisi Zilizokuwa na Mapato ambayo Hayakukusanywa**

Na.	Taasisi	Kiasi (Sh.)
1.	Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa	11,435,850,221
2.	Kampuni ya Ujenzi - SUMA JKT	990,659,090
3.	Shirika la Mzinga	957,707,234
4.	Shirika la Nyumbu	1,224,545,876
5.	Tume ya TEHAMA	34,125,000
6.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Ludewa	8,261,900

<sup>9</sup> Hotuba ya Bajeti ya Mwezi Juni 2022 kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023



Na.	Taasisi	Kiasi (Sh.)
7.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Sengerema	408,086,478
8.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kishapu	47,591,548
9.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Chunya	32,463,039
10.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kibondo Mji	36,434,315
11.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Biharamulo	87,673,219
12.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kilindoni	27,343,611
13.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kasulu	60,514,247
14.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Songwe Kilindi	25,378,880
15.	Bodi la Maji Bonde la Mto Pangani	271,926,000
16.	Bodi la Maji Bonde la Mto Wami-Ruvu	100,000,000
17.	Hospitali ya Rufaa Mbeya	84,800,527
18.	Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu	151,330,000
19.	Mamlaka ya Viwanja vya Ndege	11,667,326,498
20.	Wizara ya Nishati - Mkataba wa Uzalishaji na Ugawanaji Mapato	663,070,264
21.	Tume ya Madini	29,363,371,841
22.	Mamlaka ya Wanyamapori	1,687,943,194
23.	Wizara ya Utamaduni, Sanaa, na Michezo (Fungu 96)	590,445,400
24.	Hospitali ya Rufaa Morogoro	46,499,353
25.	Hospitali ya Rufaa Tumbi	25,020,138
26.	Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu	62,060,000
27.	Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi	46,642,500
28.	Hospitali ya Rufaa Temeke	108,218,610
29.	Bodi ya Maabara Binafsi	852,680,000
<b>Jumla</b>		<b>61,097,968,983</b>

Chanzo: Ripoti za Ukaguzi kwa Menejimenti

Ninapendekeza Serikali na mamlaka zinazohusika ziandae utaratibu wa kukusanya madeni ya mapato yasiyotokana na kodi ili kuongeza ukwasi wa taasisi husika na kugharamia bajeti ya Serikali.

### 5.3.13 Fedha Sh. Bilioni 4.058 zilizoachwa bila kutumika kwa muda mrefu

Nimepitia taratibu za usimamizi wa fedha katika mwaka wa fedha 2022/23 na kubaini kuwa kiasi cha Sh. bilioni 4.058 kilikuwa kimebaki katika akaunti za benki za taasisi 6 bila kutumiwa kwa kipindi kirefu kuanzia mwaka 2018 hadi mwaka 2023.

Aidha, nilibaini kuwa Sh. bilioni 2.110 zilizoshikiliwa na Wakala wa Ndege za Serikali zilikosa idhini ya matumizi kwa shughuli za maendeleo zilizopangwa. Fedha Sh. milioni 948.20 katika Wizara ya Uchukuzi (Fungu 62); Wizara ya

Utamaduni, Sanaa, na Michezo (Fungu 96); na Mfuko wa Tuzo na Tozo wa Jeshi la Polisi Tanzania zilipaswa kuwasilishwa kwenye Mfuko Mkuu. Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Sekoutoure ilishindwa kutumia fedha Sh. bilioni 1 za maendeleo zilizotengwa, hivyo kuchelewesha utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya kijamii na kiuchumi. **Jedwali Na. 16** linaonesha orodha ya taasisi na kiasi cha fedha zilizoachwa kwa muda mrefu bila kutumiwa.

**Jedwali Na. 16: Taasisi Zilizokuwa na Fedha Zilizochwa kwa Muda Mrefu bila Kutumiwa**

Taasisi	Maelezo	Kiasi (Sh.)
Wakala wa Ndege Serikali	Fedha za Kampuni ya M/S C-Series za fidia ya athari za kufirisika zilizoziuliwa kati ya mwaka 2018 na mwaka 2022 kutokana na kushindwa kuwasilisha ndege iliyonunuliwa kulingana na makubaliano ya ratiba. Fedha zimehifadhiwa katika akaunti ya Benki Kuu (akaunti ya mapato)	2,110,294,521
Mfuko wa Tuzo na Tozo wa Jeshi la Polisi Tanzania	Amana zilipelekwa kimakosa kwenye akaunti ya Mfuko wa Fedha za Tuzo na Tozo wa Jeshi la Polisi Tanzania badala ya akaunti ya makusanyo ya Jeshi la Polisi tangu mwaka 2019.	148,241,679
Wizara ya Uchukuzi (Fungu 62)	Fedha sh. 409,721,813 ambazo zimehifadhiwa tangu mwaka 2021 hadi mwaka 2023 bila kutumika katika akaunti ya amana	409,712,813
Wizara ya Utamaduni, Sanaa, na Michezo (Fungu 96)	Fedha za zuio kwa ajili ya ujenzi wa Uwanja wa Michezo wa Benjamin Mkapa zilizohifadhiwa kwa zaidi ya miaka mitano katika akaunti ya amana	390,252,110
Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Sekoutoure	Fedha za maendeleo zilizotolewa kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya hospitali tangu tarehe 10 Novemba 2022 na kuwekwa katika akaunti ya amana	1,000,000,000
Jumla		4,058,501,123

Chanzo: Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti

Kukosekana kwa muda mrefu kwa idhini ya matumizi ya fedha hizi kunamaanisha kuwapo kwa usimamizi na uwajibikaji hafifu katika utekelezaji wa bajeti; kutorejeshwa kwa fedha katika Mfuko Mkuu kunazuia matumizi ya fedha zilizokusanywa katika maeneo mengine ya kipaumbele; na Hospitali ya Rufaa Sekoutoure kushindwa kutumia fedha zilizotengwa kwa wakati kunaonesha udhaifu katika mipango, hivyo kukosa fursa za maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

**Ninapendekeza Serikali na taasisi husika zitoe idhini ya matumizi kwa fedha zilizokaa muda mrefu bila kutumika ili zitumike kwa shughuli za maendeleo**

zilizopangwa. Aidha, taasisi zihakikishe makusanyo yote yanawasilishwa kwenye Mfuko Mkuu ili kutekeleza vipaumbele vya kibajeti.

### 5.3.14 Kutokusanywa Mapato ya Matibabu kutoka Kampuni Zingine za Bima za Afya na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi

Licha ya kuwa na makubaliano na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, hospitali za rufaa za mikoa zimeingia makubaliano ya utoaji wa huduma za matibabu kwa wagonjwa na kampuni zingine za bima ya afya kama vile Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, bima ya Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania, bima ya bunge, bima ya Kampuni ya Strategies, na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi.

Ukaguzi wa nyaraka za madai ya bima katika hospitali za rufaa za mikoa ulibaini kuwa kwa mwaka wa fedha 2022/23, hospitali nne za rufaa hazikukusanya mapato ya kiasi cha Sh. milioni 452.63 kutoka kwenye kampuni zingine za bima ya afya kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 17.

**Jedwali Na. 17: Mapato Yasiyolipwa kutoka kwa Kampuni Zingine za Bima za Afya na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi**

Na.	Jina la Hospitali ya Rufaa ya Mkoa	Kampuni ya bima/Mfuko	Kiasi (Sh.)
1	Morogoro	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)	19,635,365
		Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF)	1,656,130
		Bima ya kampuni ya Strategies	5,042,458
		Bima ya Bunge	15,799,670
		Bima ya kampuni ya Jubilee	4,365,730
2	Musoma	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)	60,545,236
		Bima ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania	6,917,025
		Bima ya Bunge	4,882,718
		Bima ya kampuni ya Strategies	5,017,310
3	Sekoutoure	Bima ya kampuni ya Jubilee	265,531,315
		Bima ya kampuni ya Strategies	5,223,445
		Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)	9,592,450
4	Shinyanga	Bima ya AAR Health Services (T) LTD	6,403,130
		Bima ya Strategies Insurance (T) LTD	10,201,316
		Bima ya Jubilee Insurance (T) LTD	1,794,900
		Bima ya Community Health Fund (CHF)	30,025,450
<b>Jumla</b>			<b>452,633,648</b>

Chanzo: Taarifa za Ukaguzi za Mwaka 2022/2023

Kutokusanywa kwa mapato ya matibabu kutoka katika kampuni zingine za bima ya afya kunasababishwa na ufuatiliaji hafifu wa menejimenti za hospitali husika.

Ninapendekeza Serikali, kupitia Wizara ya Afya na hospitali za rufaa za mkoa ziimarisha ufanisi katika ufuatiliaji wa mapato yanayotokana na matibabu ya watumiaji wa Bima za Afya.

### 5.3.15 Upotevu wa Mapato ya Sh. Milioni 111.76 unaotokana na Misamaha ya gharama za Matibabi isiyofaa.

Ili kuhakikisha Hospitali za Rufaa za Mikoa zinakusanya mapato yanayotarajiwa na misamaha ya gharama za matibabu inatolewa kwa wagonjwa wenye sifa pekee, mwongozo wa uchangiaji wa gharama za matibabu ulitolewa na Wizara ya Afya (Fungu 52). Aya ya 5.5.1(e) ya mwongozo huo inazitaka hospitali za rufaa kufanya tathmini za kina ili kupata taarifa muhimu za wagonjwa ikiwa ni pamoja na kupitia historia ya matibabu ya mgonjwa, barua ya rufaa na historia ya familia. Aidha, hospitali zinapaswa kutambua makundi maalum yanayostahili misamaha ya gharama za matibabu, kama vile watu wenye magonjwa sugu; Virusi vya Ukimwi (VUU), kifua kikuu, kansa, na matatizo ya akili, watu wenye umri zaidi ya miaka 60, wajawazito, watoto walio chini ya miaka mitano, na watu wenye uhitaji wa kifedha.

Ukaguzi ulibaini hospitali tatu za rufaa za mikoa hazikukusanya jumla ya Sh. milioni 111.76 baada ya kutoa misamaha ya gharama za matibabu kwa wagonjwa wasio na sifa ikijumuisha misamaha ya matibabu ya wafungwa na watu wengine bila kuwepo kwa nyaraka za kuthibitisha vigezo vilivyotumika. Badala yake, hospitali hizi zilipaswa kuwasilisha hati za madai ya gharama za matibabu ya wafungwa katika idara husika ya Magereza (Fungu 29). Upotevu huu wa mapato unasababishwa na kutofanyika kwa tathmini ya vigezo vya utoaji wa misamaha ya gharama za matibabu. Maelezo yanapatikana kwenye **Jedwali Na. 18**.

#### Jedwali Na. 18: Hospitali na Kiasi cha Fedha za Misamaha Zilizotolewa kwa Wagonjwa Wasiostahili

Na.	Jina la Hospitali ya Rufaa	Kiasi cha Fedha Kilichosamehewa (Sh.)
1.	Mount Meru	25,365,941
2.	Sekou Touré	7,297,490
3.	Songwe	79,099,350
<b>Jumla</b>		<b>111,762,781</b>

Chanzo: Taarifa za ukaguzi za Mwaka 2022/2023

Ninapendekeza Serikali, kupitia Wizara ya Afya na hospitali za rufaa za mkoa, zihakikishe misamaha ya gharama za matibabu inatolewa kwa wagonjwa wanaostahili ili kuepusha upotevu wa mapato pale inapotolewa kwa makundi ya wagojwa wasiostahili.

#### 5.4 Usimamizi wa Deni la Serikali


Deni la taifa linajumuisha madeni yote ambayo Serikali inadaiwa ndani na nje ya nchi kupitia Serikali kuu na wakala zake. Kwa madhumuni ya ufanisi katika usimamizi wa deni, Waziri wa Fedha amepewa mamlaka ya kipekee ya kukopa kwa niaba ya Serikali mikopo ya nje na ndani na kutoa dhamana kwa niaba ya Serikali kama ilivyobainishwa chini ya Vifungu vya 3, 6, na 13 vya Sheria ya Mikopo, Dhamana, na Misaada, Sura ya 134.

##### 5.4.1 Mchanganuo wa Deni la Serikali

Kufikia tarehe 30 Juni 2023, deni la Serikali lilikuwa Sh. bilioni 82,254.71 ikilinganishwa na Sh. bilioni 71,312.42 lililoripotiwa mwaka 2021/22. Kuna ongezeko la Sh. bilioni 10,942.30 (15%) ikilinganishwa na ongezeko la Sh. bilioni 6,792.79 (10.5%) kwa mwaka 2021/22.

Deni la Serikali linajumuisha deni la ndani Sh. bilioni 28,926.37 na la nje Sh. bilioni 53,328.33 kwa mwaka wa fedha 2022/2023, ikilinganishwa na deni la ndani Sh. bilioni 24,040.11 na deni la nje Sh. bilioni 47,272.31 kwa mwaka 2021/2022. **Kielelezo Na. 5** kinaonesha mwenendo wa ukuaji wa deni la serikali kuanzia mwaka 2020/21 hadi 2022/23.

## Kielelezo Na. 5: Mwenendo wa Ukuaji wa Deni la Serikali



**Chanzo:** Hesabu za Fedha Fungu 001-Deni la Serikali kuanzia Mwaka 2020/21 hadi 2022/23

## 5.4.2 Mwenendo wa Deni la Ndani

Kwa mwaka 2022/2023, deni la ndani limeongezeka kwa Sh. bilioni 4,886.26 sawa na asilimia 20 ya deni la ndani lililoripotiwa mwaka 2021/2022. Mwenendo wa ukuaji wa deni la ndani kuanzia mwaka 2020/2021 hadi 2022/2023 umeoneshwa kwenye Jedwali Na. 19.

## Jedwali Na. 19: Mwenendo wa Deni la Ndani (Deni Halisi)

Mwaka wa Fedha	Thamani ya	Ongezeko	
	(Sh. Bilioni)	(Sh. Bilioni)	Asilimia
2022/2023	28,926	4,886.26	20
2021/2022	24,040	5,105	27
2020/2021	18,935	3,420	22

**Chanzo:** Hesabu za Fedha Fungu 001-Deni la Serikali kuanzia Mwaka 2020/2021 hadi 2022/2023

Vilevile, ukaguzi wangu ulibaini kuwa Serikali ilikopa jumla ya Sh. bilioni 6,374.63. Kati ya hizo, Sh. bilioni 2,129.25 (33%) zilikuwa mikopo ya muda mfupi

na Sh. bilioni 4,245.39 (67%) zilikuwa mikopo ya muda mrefu kama ilivyooneshwa katika Jedwali Na. 20.

#### Jedwali Na. 20: Mwenendo wa Ukopaji wa Ndani (Thamani Halisi)

Ukopaji	2022/23		2021/22		2020/21	
	Sh. Bilioni	%	Sh. Bilioni	%	Sh. Bilioni	%
Muda Mfupi	2,129.25	33.4	1,757.75	21	3,331.21	51
Muda Mrefu	4,245.39	66.6	6,797.88	79	3,218.96	49
<b>Jumla</b>	<b>6,374.63</b>	<b>100</b>	<b>8,555.6</b>	<b>100</b>	<b>6,550.18</b>	<b>100</b>

Chanzo: Hesabu za Fedha Fungu 001-Deni la Serikali kuanzia Mwaka 2020/21 hadi 2022/23

Ongezeko la deni la ndani linatokana na kukopa kwa malengo ya kulipia dhamana za Serikali zilizoiva na kufidia upungufu wa kibajeti.

#### 5.4.3 Mwenendo wa Deni la Nje

Deni la nje kufikia tarehe 30 Juni 2023 lilikuwa Sh. bilioni 53,328.33 ikiwa ni ongezeko la Sh. bilioni 6,056.04 sawa na asilimia 11 ikilinganishwa na deni la Sh. bilioni 47,272.29 lililoripotiwa mwaka 2021/2022 kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 21.

#### Jedwali Na. 21: Mwenendo wa Deni la Nje

Wakopeshaji	2022/2023		2021/2022		2020/2021	
	Sh.	%	Sh.	%	Sh.	%
Taasisi za Kimataifa	33,578.24	63	28,729	61	26,556	58
Nchi Marafiki	5,163.57	10	5,208	11	5,098	11
Benki za Kuwezesha Biashara ya Forodha	5,655.54	11	5,973	13	6,384	14
Wakopeshaji	8,930.99	17	7,363	16	7,547	17
<b>Jumla</b>	<b>53,328.33</b>	<b>100</b>	<b>47,272</b>	<b>100</b>	<b>45,585</b>	<b>100</b>
<b>Ongezeko</b>	<b>6,056.04</b>	<b>11</b>	<b>1,687</b>	<b>4</b>	<b>4,343</b>	<b>10</b>

Chanzo: Jedwali la Mwenendo wa Deni la Serikali kuanzia Mwaka 2020/21 hadi 2022/23

#### 5.4.4 Uhimilivu wa Deni

Katika mapitio yangu ya taarifa ya uchambuzi wa uhimilivu wa deni iliyoandaliwa na Wizara ya Fedha mwezi Desemba 2023, nilijiridhisha kuwa deni la Serikali ni himilivu.

Uwiano wa thamani ya sasa (present value) wa deni la Serikali (deni la nje na deni la ndani) na pato la taifa ni asilimia 19.0 ambayo ni chini ya kiwango ukomo/elekezi cha asilimia 40 kwa kipindi chote cha makadirio.

Hali kadhalika, uwiano wa thamani ya sasa ya deni la nje na pato la taifa ni asilimia 35.6 ikiwa pia chini ya kiwango ukomo/elekezi cha asilimia 40 kwa kipindi chote cha makadirio. Uwiano wa thamani ya sasa ya deni na mauzo ya nje ni asilimia 113.2 chini ya kiwango ukomo/elekezi cha asilimia 180. Uwiano wa kulipa madeni na mauzo ya nje ni asilimia 12.7 chini kidogo ya kiwango ukomo/elekezi cha asilimia 15 na uwiano wa malipo ya madeni na mapato ni asilimia 14.3 chini kidogo ya kiwango ukomo/elekezi cha asilimia 18.

**Ninaishauri Serikali iboreshe ukusanyaji wa mapato ya ndani na mauzo ya bidhaa nje ya nchi ili kusaidia kuboresha viashiria vya ukwasi katika usimamizi wa deni la Serikali; na ihakikishe mapato yatokanayo na mikopo ya kibiashara yanawekezwa katika miradi ya kimkakati yenye manufaa ya moja kwa moja kwenye ukuaji wa pato la taifa.**

#### 5.4.5 Kutohuishwa kwa wakati sheria za usimamizi wa deni la serikali

Fungu 1-Deni la Serikali lilianzishwa tarehe 25 Agosti 2021 kisha kufuatiwa na muundo mpya wa Wizara ya Fedha ulioidhinishwa tarehe 23 Desemba 2021. Nilibaini kuwa Sheria na Kanuni za Mikopo, Dhamana, na Misaada haikuhuishwa kuakisi mabadiliko haya makubwa katika usimamizi wa deni la serikali nchini. Kwa mfano, sheria na kanuni zilizotajwa hapo juu bado zinatambua Idara ya Mhasibu Mkuu kama sehemu ya usimamizi wa deni la serikali, ingawa marekebisho ya hivi karibuni katika muundo wa Wizara ya Fedha yamemuondolea Mhasibu Mkuu wa Serikali majukumu hayo. Changamoto hii ina madhara yanayoweza kusababisha kutozingatiwa kwa sheria zilizopo za utawala na kudhoofisha umuhimu wa kuwapo kwa muundo mpya wa Wizara ya Fedha.

Niliarifiwa kuwa menejimenti iko katika mchakato wa kuhuisha sheria na kanuni za mikopo, dhamana, na misaada ili kuakisi muundo mpya wa wizara.



Ninapendekeza menejimenti iandae mpangokazi utakaonesha hatua zilizopangwa za mapitio ya sheria husika na kanuni zake ili kuhakikisha zoezi hilo linakamilika kwa wakati hivyo sheria zilizopo zinarekebishwa.

### 6.1 Utangulizi

Usimamizi wenye ufanisi wa matumizi ni muhimu kwa mafanikio ya taasisi za umma kwani hudumisha matumizi yenye ufanisi wa rasilimali ili kufikia malengo yao. Ukaguzi wangu ulibaini mapungufu mbalimbali katika usimamizi wa matumizi ya taasisi za umma yaliyohitaji utatuzi wa haraka kutoka kwa menejimenti husika. Sura hii inaelezea kwa undani dosari zilizobainika na inatoa mapendekezo kwa menejimenti ya taasisi husika kwa ajili ya uboreshaji.

### 6.2 Malipo Yaliyofanywa bila Kudai Stakabadhi za Kielektroniki

Kifungu 36(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Kanuni 28(1) ya Kanuni za Kodi ya Mapato (Mashine ya Kutoa Risiti za Kielektroniki) za Mwaka 2012 zinataka pande zote, yaani mnunuzi na muuzaji, kutoa na kudai stakabadhi za kielektroniki. Hata hivyo, nilibaini kuwa taasisi 13 zilifanya malipo ya Sh. bilioni 2.87 bila kudai stakabadhi za kielektroniki kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 22** hapa chini.

#### Jedwali Na. 22: Taasisi Zilizofanya Malipo bila Kudai Stakabadhi za Kielektroniki

Na.	Taasisi	Kiasi (Sh.)
1.	Ofisi ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Zanzibar	154,273,482
2.	Chuo cha Ardhi Morogoro	25,559,939
3.	Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki Tabora	22,798,582
4.	Bodi ya Bonde la Maji ya Ziwa Nyasa	151,738,951
5.	Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Mbinga, Daraja C	12,754,669
6.	Wizara ya Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi	465,549,485
7.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Ushirombo, Daraja C	147,321,132
8.	Wakala wa Majengo Tanzania	541,743,142
9.	Wakala wa Ufundi na Umeme	1,220,250,000
10.	Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini	65,349,662

Na.	Taasisi	Kiasi (Sh.)
11.	Bodi ya Filamu Tanzania	44,556,793
12.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Temeke	24,146,015
13.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Tumbi	3,550,600
	<b>Jumla</b>	<b>2,879,592,452</b>

**Chanzo:** Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti Mwaka 2022/23

Kutokuwapo kwa stakabadhi za kielektroniki kunaleta wasiwasi kuhusu upotevu wa mapato, kuzuia ufuatiliaji, na kutoa taarifa sahihi ya miamala kwa madhumuni ya kodi.

Ninapendekeza Serikali kuchukua hatua madhubuti dhidi ya Taasisi zinazokiuka kanuni za kodi ili kuzuia uwezekano wa upotevu wa mapato. Pia kuimarisha uhibitaji wa ndani wa malipo kwa wazabuni yanatolewa stakabadhi za kielektroniki.

### 6.3 Bakaa katika Akaunti za Benki za Matumizi za Masurufu

Aya ya 3.11 ya Waraka wa Hazina Na 1 wa Mwaka 2021/22 wa tarehe 7 Juni 2022 uliotolewa na Mhasibu Mkuu wa Serikali kuhusu uandaaji wa taarifa ya fedha kwa mwaka 2021/22 inawakumbusha maafisa masuuli kuzingatia maelekezo yaliyotolewa na serikali na kuhakikisha kuwa akaunti ya masurufu haina bakaa mwishoni mwa mwaka wa fedha yaani tarehe 30 Juni 2023.

Nilibaini kuwa kufikia tarehe 30 Juni 2023, kulikuwa na taasisi 7 zilizokuwa na bakaa ya Sh. bilioni 2.45 katika akaunti za benki za matumizi za masurufu kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 23**. Hali hii ilisababisha uvunjaji wa sheria za kifedha pamoja na kuhatarisha kutokuwapo kwa uwazi, uwajibikaji, na usahihi wa taarifa za kifedha. Pia, fedha zilizobaki kwenye akaunti za masurufu zinaweza kutumiwa isivyofaa.

#### **Jedwali Na. 23: Orodha ya Taasisi Zilizokuwa na Bakaa ya Fedha katika Akaunti za Matumizi za Masurufu**

Na.	Taasisi	Kiasi (Sh.)
1	Wizara ya Mambo ya Ndani	195,213,701
2	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mbeya	72,884,405
3	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Sekoutoure	276,295,207
4	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Simiyu	5,926,000
5	Hospitali Maalumu ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto	378,520,569
6	Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia	1,129,466,074
7	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Sokoine	393,012,932
	<b>Jumla</b>	<b>2,451,318,888</b>

**Chanzo:** Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti Mwaka 2022/23

**Ninapendekeza serikali ifanye ufuatiliaji wa mara kwa mara ili kuhakikisha kanuni za fedha zinazingatiwa ili kuzuia matumizi yasiyofaa ya fedha katika akaunti za benki za matumizi za masurufu.**

#### **6.4 Ukarabati wa Jengo la Ofisi ya Balozi Haujaanza Licha ya kuwepo kwa Fedha**

Tarehe 4 Julai 2018 Ubalozi wa Tanzania Kampala, Uganda ulipokea dola za Marekani 783,115.35 sawa na Sh. bilioni 1.78 kwa ajili ya ukarabati wa jengo la Ofisi ya Ubalozi lililopo Barabara ya 6 Kagera, na jengo la makazi ya balozi lililopo Mtaa wa 4 Ridgeway, Barabara ya Kololo.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa, hadi tarehe 30 Juni 2023, fedha hizo hazikuwa zimetumika, ambapo ni miaka mitano tangu zitolewe. Kutokana na uchakavu wa jengo hilo, iliamuliwa Ofisi za Ubalozi zihamishiwe kwenye nyumba ya Ubalozi, iliyokuwa inatumika kwa makazi ya watumishi wa Ubalozi huo. Matokeo yake, watumishi hao waliondolewa na kwenda kukaa kwenye nyumba za kupanga kwa gharama ya Sh. milioni 247.93 kwa mwaka, sawa na Sh. bilioni 1.23 kwa miaka mitano.

Hali hii ilitokana na mchakato mrefu wa uteuzi wa mshauri elekezi, ambapo mwezi Oktoba 2023, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilimteua mshauri elekezi ABECC, Kampuni Tanzu ya Chuo Kikuu cha Ardhi baada ya kushinda zabuni. Hata hivyo, hadi wakati wa ukaguzi wangu, mchakato wa kumpata mkandarasi ulikuwa haujakamilika.

Ni maoni yangu kwamba fedha zisizotumika kwa ajili ya ukarabati wa majengo zinazua wasiwasi kuhusu fursa za uwekezaji zilizopotea, huku mzigo mkubwa wa ulipaji wa kodi ya pango ukiongezeka. Aidha, kushikilia fedha kwa muda mrefu kunaweza kuongeza gharama za ujenzi kutokana na mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma kutokana na mfumuko wa bei.

**Ninapendekeza Serikali kukamilisha taratibu za ununuzi ili kuwezesha kuanza kwa kazi ya ukarabati wa Ofisi ya Ubalozi.**

#### **6.5 Matumizi Yasiyoidhinishwa ya Fedha Kwenye Akaunti ya Amana Katika Ubalozi wa Tanzania New York**

Kanuni ya 32 ya Kanuni za Fedha za Umma ya Mwaka 2001 inataka afisa anayeidhinisha kurejeshwa kwa amana kujiridhisha kwamba madai

yaliyopokelewa ya kurejesha amana yanakidhi lengo ambalo amana hiyo ilichukuliwa kwa kumbukumbu ya risiti ya awali iliyotolewa, kwamba mtu anayedai amana ni mpokeaji halisi wa amana au ana haki ya kurejeshewa amana hiyo.

Ukaguzi wangu wa Ubalizi wa Tanzania New York ulibaini kwamba tarehe 1 Julai 2021, Ubalizi ulipokea dola za Marekani 324,112.43, sawa na Sh. milioni 826.48 kama fedha za dhamana kutoka kwa wapangaji wa jengo la ofisi ya Ubalizi. Kati ya fedha zilizowekwa, Ubalizi ulitumia dola za Marekani 291,112.43, sawa na Sh. milioni 672.51 kwa mwaka wa fedha 2022/23 kugharamia ukarabati wa jengo na gharama zingine za uendesaji wa Ofisi.

Hali hii ilitokana na kutowasilishwa kwa fedha kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Kwa maoni yangu, utumiaji wa fedha za dhamana bila idhini unaweza kusababisha Ubalizi kushindwa kulipa wapangaji wenye amana hizo pindi watakapodai fedha zao ikiwa zitapaswa kurejeshwa.

**Ninapendekeza Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuandaa miongozo inayolenga kusimamia vizuri fedha za amana ndani ya Balozi zake. Zaidi ya hayo, kurejesha kiasi cha amana za wapangaji kilichotumika.**

## **6.6 Gharama Kubwa Zinazotumika Kulipa Kodi ya Pango Katika Balozi za Tanzania Nje ya Nchi**

Ukaguzi wangu katika balozi 43 ulibaini kuwa balozi 39 zilikuwa zinakodi nyumba kwa ajili ya ofisi na makazi ya watumishi, ambapo jumla ya Sh. bilioni 18.46 zilitumika kulipa kodi ya pango kwa mwaka wa fedha 2022/23. Aidha nilibaini zaidi kuwa Ubalizi wa Tanzania Moscow ulilipa kodi kubwa zaidi ya Sh. bilioni 1.58, ikifuatiwa na Ubalizi wa Tanzania Abu Dhabi uliolipa Sh. bilioni 1.42, na Ubalizi wa Tanzania Vienna uliolipa Sh. bilioni 1.19.

Ukaguzi wa mpango wa ununuzi, ukarabati, na ujenzi wa majengo ya balozi za Tanzania nje ya nchi ulibaini kuwa balozi zinazolipa kodi kubwa za pango hazikuorodheshwa kwenye mpango huo kwa ajili ya ununuzi, ukarabati, na ujenzi.

Hali hii ilitokana na serikali kushindwa kuendeleza viwanja vilivyotolewa na nchi wenyeji, kukarabati majengo yaliyochakaa, na majengo yaliyotelekezwa. Ni maoni yangu kuwa, gharama kubwa za kodi kwa kiasi yanapunguza upatikanaji

wa fedha kwa ajili ya shughuli zingine ambazo huathiri Ubalazi katika kutekeleza majukumu yake ya msingi.

**Ninapendekeza Serikali iboreshe mpango wa ununuzi, ukarabati, na ujenzi wa majengo ya balozi za Tanzania nje ya nchi; na itenge fedha zaidi kwa ajili wa ukarabati na ujenzi wa majengo ya balozi za Tanzania nje ya nchi.**

### **6.7 Kutotumia Misamaha ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa Miradi ya Maji Inayokidhi Vigezo**

Kanuni ya 4(2)(a) ya Kanuni za Kodi ya Ongezeko la Thamani (Taratibu za Usimamizi wa Misamaha) za Mwaka 2021 inataka maombi ya msamaha wa kodi yafanywe kwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania ndani ya muda usiopungua siku 60 kabla ya kuanza kwa mradi ikiambatishwa na nakala ya mkataba kati ya taasisi ya Serikali na mkandarasi au mkandarasi mdogo unaonesha kuwa mradi unafadhiliwa na serikali na umeidhinishwa na waziri mwenye dhamana.

Nilibaini kuwa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) ilisaini mikataba 13 yenye thamani ya Sh. bilioni 17.41, ikijumuisha kodi ya ongezeko la thamani ya Sh. bilioni 2.78, licha ya miradi hiyo kukidhi vigezo vya kupata msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kama ilivyoainishwa katika Kanuni ya 4(2)(a). Pia, nilibaini kuchelewa kupatikana kwa hati za misamaha ya kodi ya ongezeko la thamani kwa kipindi cha hadi siku 420 kwa mikataba yenye thamani ya Sh. bilioni 3.05, hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi husika.

Sababu kubwa ilikuwa mchakato mrefu wa kupata misamaha ya kodi ya ongezeko la thamani kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania na Wizara ya Fedha na Mipango na usimamizi wa mikataba usioridhisha. Kulipa kodi ya ongezeko la thamani kwa miradi inayostahili msamaha hupunguza fedha zilizopo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji. Pia, ucheleweshaji wa misamaha hiyo unakwamisha utekelezaji wa miradi, hivyo kuathiri upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi.

**Ninapendekeza Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato kutoa misamaha ya kodi kwa wakati katika utekelezaji wa miradi, aidha wakala wa maji na usafi wa mazingira (RUWASA) ihakikishe inapata misamaha ya kodi katika miradi inayostahili ili kurahisisha utekelezaji wa miradi.**



### 7.1 Utangulizi

Sehemu hii inawasilisha matokeo yaliyobainika wakati wa ukaguzi wangu wa usimamizi wa ununuzi. Kifungu cha 48(1) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2022, Sura ya 418 kinawataka Maafisa Masuuli wote kuhakikisha kuwa ununuzi wa bidhaa, kazi, au huduma unazingatia taratibu zilizowekwa chini ya sheria na kanuni zake.

Ni wajibu wangu kisheria chini ya Kifungu cha 48(3) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2022, Sura ya 418, kutathmini na kutoa taarifa iwapo Maafisa Masuuli wamezingatia ipasavyo taratibu na kanuni zilizoainishwa katika sheria hiyo.

Ukaguzi wangu kwa mwaka wa fedha 2022/23 umebaini maeneo kadhaa ambayo taasisi za umma zilikiuka taratibu zilizowekwa. Maelezo ya upungufu huo pamoja na mapendekezo yangu yameorodheshwa katika aya zinazofuata, zikigawanywa katika hatua ya mpango wa ununuzi; utoaji wa zabuni na uandaaji wa mikataba; pamoja na utekelezaji na usimamizi wa mikataba.

### 7.2 Upungufu katika Hatua ya Mpango wa Ununuzi

Hatua ya mpango wa ununuzi, ni hatua ya awali katika mchakato wa ununuzi, ikijumuisha usanifu na uidhinishaji wa ununuzi. Hatua hii ndiyo msingi wa kuhakikisha kwamba shughuli za ununuzi zinafanyika kwa udhubuti na ufanisi.

#### 7.2.1 Mipango ya Ununuzi Iliyoshindwa kutekelezwa na Ununuzi Uliofanywa bila Kuzingatia Mipango ya Ununuzi ya Mwaka

Kifungu cha 49 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2022, Sura ya 418 inazitaka taasisi nunuzi kuandaa mpango wa ununuzi wa kila mwaka kwa ajili ya ununuzi wake wote ili kuunganisha bajeti yake ya ununuzi na mpango wake wa matumizi na kuzuia ununuzi wa dharura na kugawanya ununuzi.

Nilibaini mipango ya ununuzi iliyoshindwa kutekelezwa na ununuzi uliofanywa bila kuzingatia mipango ya ununuzi ya mwaka yenye jumla ya Sh. bilioni 567.86, ambapo taasisi 25 hazikutekeleza mipango yake ya ununuzi yenye thamani ya Sh. bilioni 565.49; mamlaka nne za maji zilifanya ununuzi wa jumla ya Sh. milioni 537.93 bila kuwa na mipango ya ununuzi ya mwaka; na taasisi sita zilifanya ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 1.82 bila kujumuishwa katika mipango yao ya ununuzi ya mwaka. Orodha ya taasisi hizo imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. II.**

Kutotekelezwa kwa shughuli zilizopangwa kumesababisha ucheleweshaji wa utoaji huduma, hivyo kusababisha kutofikiwa ipasavyo kwa malengo ya Serikali yaliyokusudiwa. Zaidi ya hayo, kutozingatia mpango wa mwaka wa ununuzi kunaleta hatari ya kuwapo kwa ununuzi wa dharura. Vilevile, kushindwa kujumuisha mahitaji, kunaathiri uwazi na uwajibikaji katika shughuli za ununuzi.

**Ninapendekeza kwamba Serikali ihakikishe Wizara, Idara na Wakala za Serikali zinaandaa mipango halisi ya ununuzi na kwamba mipango hii inatekelezwa ipasavyo mwaka mzima ili kuongeza uwazi na uwajibikaji.**

### **7.2.2 Kuanza kwa Miradi bila Cheti cha Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Kijamii**

Kanuni ya 241(3) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inazitaka taasisi ununuzi kutathmini athari za kimazingira kwa kazi zote katika hatua za awali za mradi na kwa vyovyote vile, kabla ya kuanza kwa taratibu za ununuzi. Aidha, sehemu ya 81(3) ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 inataka tathmini ya athari za mazingira ifanyike kabla ya kuanza au kufadhili mradi.

Nilibaini kuwa Wizara ya Afya ilianza utekelezaji wa mradi mmoja wenye thamani ya Sh. bilioni 2.18 kabla ya kufanya tathmini ya athari za kimazingira na kijamii na uchunguzi wa kijioteknolojia. Zaidi ya hayo, Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) ilianzisha miradi 14 yenye thamani ya Sh. bilioni 632.94 kabla ya kupata vyeti vya tathmini ya athari kwa mazingira kutoka Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira. Maelezo yametolewa katika **Kiambatisho Na. III.**



Utekelezaji wa miradi bila kufanya tathmini ya athari kwa mazingira huweza kusababisha hatari za kimazingira, zinazoweza kuathiri jamii zinazozunguka na kusababisha matumizi mabaya ya fedha za umma. Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) unaweza kutozwa faini kulingana na kifungu cha 189 (c) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004. Pia, mabadiliko muhimu yanayoweza kufanyika kwenye hatua za awali za mradi yanaweza kupuuzwa kutokana na kuanza kwa mradi kabla ya kupata vyeti vya mazingira kutoka Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira.

**Napendekeza kwamba Serikali ihakikishe kuwa miradi ya ujenzi katika Wizara, Idara na Wakala za Serikali, inaanza mara tu baada ya kupata vyeti vya tathmini ya athari kwa mazingira kutoka Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira. Hatua hii ya tahadhari ni muhimu ili kuhakikisha utekelezaji wa wa miradi yenye tija, kuzuia hatari za kimazingira na matumizi yasiyofaa ya fedha za Umma.**

### 7.2.3 Ununuzi Uliofanyika bila Kuidhinishwa na Bodi za Zabuni

Kifungu cha 33(1)(c) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2022, Sura ya 418, kinataka bodi za zabuni kuidhinisha ununuzi na uondoshaji mali kwa taratibu za zabuni.

Kinyume na kifungu tajwa hapo juu, nilibaini taasisi 10 zilifanya ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 2.11 bila kuidhinishwa na bodi za zabuni. Zaidi ya hayo, ununuzi wa kiasi cha Sh. bilioni 5.01 ulifanywa na taasisi tano na kuidhinishwa kwa njia ya azimio la waraka, ingawa akidi za bodi za zabuni zilizopitisha ununuzi huo hazikutimbia. Maelezo yanaoneshwa katika **Jedwali Na. 24.**

#### Jedwali Na. 24: Taasisi Zilizofanya Ununuzi bila Kuidhinishwa na Bodi za Zabuni

Na.	Taasisi	Kiasi (Sh.)	Maelezo
1.	Sekta ya Kilimo na Viwanda SUMA JKT	99,247,000	Haijaidhinishwa
2.	Kampuni ya Umeme SUMA JKT	30,000,000	Haijaidhinishwa
3.	Wizara ya Uwekezaji, Viwanda, na Biashara	20,000,000	Haijaidhinishwa
4.	Mfuko wa Misitu Tanzania	10,525,260	Haijaidhinishwa
5.	Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS)	777,836,847	Sh. milioni 346.66 haikuidhinishwa na Sh. milioni 431.17 iliidhinishwa na

Na.	Taasisi	Kiasi (Sh.)	Maelezo
			wajumbe ambao hawakutumiza akidi
6.	Shirika la Mzinga	945,498,946	Haijaidhinishwa
7.	Kampuni Tanzu ya Mzinga	87,352,334	Haijaidhinishwa
8.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Mtwara	262,803,423	Haijaidhinishwa
9.	Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake, na Makundi Maalumu	273,975,513	Haijaidhinishwa
10.	Wizara ya Uchukuzi	38,675,000	Haijaidhinishwa
11.	Bodi ya Maji ya Bonde la Kati	217,469,180	Akidi Haikutimia
12.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Mbeya	48,002,808	Akidi Haikutimia
13.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Musoma	155,283,589	Akidi Haikutimia
14.	Wizara ya Afya	4,160,306,500	Akidi Haikutimia
	<b>Jumla</b>	<b>7,126,976,400</b>	

Chanzo: Ripoti za Ukaguzi 2022/23

Kufanya ununuzi bila kupata vibali vya bodi za zabuni kunadhoofisha jukumu la uangalizi la bodi hizo katika kufuatilia taratibu za ununuzi na kunaweza kuathiri uwazi na uwajibikaji katika michakato ya ununuzi, hivyo kusababisha matumizi mabaya ya rasilimali za umma.

**Ninapendekeza kwamba Serikali ihakikishe Wizara, Idara na Wakala za Serikali, zinafuata kanuni za ununuzi kwa kuhakikisha kuwa ununuzi wote unaidhinishwa na Bodi za Zabuni.**

#### 7.2.4 Mchakato Mrefu wa Uteuzi wa Mshauri Elekezi kwa Ajili ya Usimamizi wa Usanifu wa Miradi ya Ujenzi wa Majengo ya Ubalozi

Kanuni ya 191(3) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inataka muda unaowekwa kwa ajili ya mchakato wa ununuzi wa zabuni kuwa wa kutosha kwa siku zisizozidi 120 tangu siku ya mwisho ya kuwasilishwa kwa zabuni.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa, kupitia magazeti matatu tofauti ya nchini Zambia, tarehe 20 Februari 2023 Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilitangaza zabuni ya uteuzi wa mshauri elekezi. Zabuni hiyo ilihusu usanifu wa miradi ya ujenzi wa Nyerere Plaza, Manda Hill Kilimanjaro Plaza, Tanzanite Exclusive Villas, Ngome Commercial Complex, Ngome Classic Villas, Serengeti Deluxe Villas, Saadani Villas Luxury Homes, Chelston Local Staff Housing Units, Tanzania High Commission New Building, na Zanzibar Executive

Office Park Buildings, zote za Jijini Lusaka, Zambia. Mwisho wa kuwasilisha zabuni hizo ulikuwa tarehe 3 Machi 2023. Hata hivyo, mchakato huu wa ununuzi ulikuwa haujakamilika hadi wakati wa ukaguzi huu.

Ninaamini kuwa kuchelewa kumalizika kwa mchakato huu kuna hatari ya kuongezeka kwa gharama za miradi itokanayo na kuongezeka kwa bei za bidhaa na huduma hivyo kuchelewesha kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**Ninapendekeza Serikali, kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ikamilishe mchakato wa ununuzi wa mshauri elekezi atakayefanya usanifu wa miradi ya ujenzi iliyopo Lusaka Zambia.**

### 7.3 Upungufu wakati wa Utoaji wa Zabuni pamoja na Uandaaji wa Mikataba

Hatua ya utoaji wa zabuni ni hatua ya msingi katika kuchagua wazabuni wanaofaa zaidi kwa njia ambayo huongeza uadilifu, uwajibikaji, ufanisi, uwazi, na thamani ya fedha.

#### 7.3.1 Ununuzi Uliofanywa bila Kutumia Mfumo wa Kielektroniki

Kanuni ya 342 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inazitaka taasisi nunuzi kufanya ununuzi katika mfumo wa kielektroniki wa ununuzi wa Umma.

Katika mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2023, taasisi 16 zilinunua bidhaa na huduma zenye thamani ya Sh. bilioni 149.56 nje ya mfumo wa kielektroniki, kinyume na kanuni tajwa hapo juu. Orodha ya taasisi hizo imeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 25.**

**Jedwali Na. 25: Taasisi Zilizofanya Ununuzi Nje ya Mfumo wa Kielektroniki**

Na.	Taasisi	Kiasi (Sh.)
1.	Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania	26,400,000
2.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Musoma	591,977,855
3.	Shirika la Magereza	6,551,821,367
4.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Sekoutoure	724,158,727
5.	Kituo cha Jemolojia Tanzania	132,464,685
6.	Wakala wa Barabara Tanzania	82,929,007,030
7.	Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni	1,743,663,520
8.	Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu	40,024,437
9.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira, Kasulu	22,894,400
10.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira, Kibondo	574,298,028
11.	Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania	444,213,403
12.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira, Handeni	394,483,669
13.	Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia	51,240,584,534

Na.	Taasisi	Kiasi (Sh.)
14	Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake, na Makundi Maalumu	173,141,754
15	Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini	138,322,426
16	Wakala wa Majengo Tanzania	3,840,689,115
	<b>Jumla</b>	<b>149,568,144,950</b>

Chanzo: Ripoti za ukaguzi 2022/23

Kushindwa kutumia mfumo wa kielektroniki wa ununuzi kunadhoofisha lengo la Serikali la kuongeza ufanisi, kupunguza muda wa mchakato wa ununuzi, na kuboresha uwazi na haki katika ununuzi wa umma.

Ninapendekeza kwamba Serikali ichukue hatua za kina ili kuongeza uwazi na uzingatiaji wa Sheria za ununuzi na kanuni zake kwa utumiaji wa mfumo wa ununuzi wa kielektroniki katika michakato ya ununuzi. Pia, kuchukua hatua stahiki kwa wale waliohusika katika kukiuka kanuni za ununuzi.

### 7.3.2 Ununuzi Uliofanyika bila Kutumia Njia za Ushindani wa Bei

Kanuni 149A (4) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 kama ilivyorekebisha na Kanuni Na. 51 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2016 inazitaka taasisi nunuzi kufanya ushindani kwa kutoa ankara kifani kutoka kwa kila mtengenezaji, muuzaji au mtoa huduma kuhakikisha thamani bora ya fedha inapatikana.

Aidha, Kanuni ya 152 na 159 (1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 kama zilivyorekebisha na Kanuni Na. 55 na 60 za Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2016 zinaruhusu ununuzi kwa njia ya utoaji wa zabuni kwa wazabuni maaalumu na kwa kutumia njia ya mzabuni mmoja mtwalia katika mazingira maalumu yakiwemo mahitaji ya dharura, uwepo kwa mzabuni mmoja ambaye ana haki za kipekee kuhusiana na bidhaa au huduma hiyo, na ununuzi unaohusisha majeshi ya ulinzi au usalama wa taifa.

Nilibaini kuwa, tarehe 31 Machi 2023, Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia iliingia mikataba Na. ME-024/2022-23/HQ/G/44 na Na. ME-024/2022-23/HQ/G/45 na Kampuni ya M/S Alaf (T) Ltd, kwa gharama ya Sh. bilion 31.46 (pamoja na kodi ya ongezeko la thamani kwa mikataba yote) kwa ajili ya usambazaji na ufungaji wa vifaa vya kuzeekea kwa kazi za ujenzi katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi katika wilaya 63 na Mamlaka za Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi ya Mkoa wa Songwe. Hata hivyo, licha ya ununuzi huu kufanywa moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji, hapakuwa na

ushindani kati ya wazalishaji waliorodheshwa kushiriki kwenye mchakato wa ununuzi wa vifaa hivyo.

Aidha, taasisi tano zilifanya ununuzi kwa kutumia njia ya mzabuni mmoja kwa bidhaa na huduma zenye thamani ya Sh. bilioni 46.21 bila kuwa na uhalali wa kimaandishi wa sababu za kutumia njia hiyo. Orodha ya taasisi hizo imeoneshwa katika Jedwali Na. 26.

**Jedwali Na. 26: Tasisi Zilizofanya Ununuzi bila Kutumia Njia za Ushindani wa Bei**

Na.	Taasisi	Kiasi (Sh.)	Njia Iliyotumika
1.	Wizara ya Afya	251,225,000	Mzabuni Mmoja
2.	Wizara ya Mifugo	18,567,263,031	Mzabuni Mmoja
3.	Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania	1,182,782,050	Mzabuni Mmoja
4.	Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini	1,872,751,293	Ununuzi Iliyozuiliwa
5.	Wakala wa Barabara Tanzania	24,338,476,547	Mzabuni Mmoja na Iliyozuiliwa
	<b>Jumla</b>	<b>46,212,497,921</b>	

Chanzo: Ripoti za Ukaguzi ya Mwaka 2022/23

Njia isiyo ya ushindani iliyotumiwa na Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia imekuwa ni kizuizi katika kufanikisha malengo ya bodi yake ya zabuni. Katika mchakato wa zabuni, ushindani wa bei ni muhimu kwenye kupata bei inayofaa na kuhakikisha matumizi sahihi ya fedha za umma. Vilevile, kutumia njia ya mzabuni mmoja na njia ya utoaji wa zabuni kwa wazabuni maaalumu bila sababu zenye uhalali wa kutosha kunaathiri mchakato wa ununuzi na kuzuia kupatikana kwa thamani ya fedha katika michakato hiyo.

Ninapendekeza Serikali ihakikishe kuwa Wizara, Idara na Wakala za Serikali, zinafanya ununuzi kwa uwazi, haki, na uwajibikaji kwa kushindanisha wazalishaji walioteuliwa na kuweka taratibu kali za usimamizi ili kudhibiti matukio ya ununuzi kwa njia ya mzabuni mmoja na njia ya utoaji wa zabuni kwa wazabuni maalumu bila sababu zenye uhalali wa kutosha.

### 7.3.3 Zabuni Tisa zilifanyiwa Tathmini na Wajumbe Pungufu wa Kamati za Tathmini

Kanuni ya 202(1)-(2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 kama ilivyorekebishwa na Kanuni Na. 69 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2016 inamtaka afisa masuuli kuunda kamati ya tathmini ya zabuni itakayojumuisha wajumbe watatu hadi watano. Katika mazingira ya kipekee,

afisa masuuli anaweza kuunda kamati ya tathmini yenye wajumbe zaidi ya watano, kwa kuzingatia thamani na aina ya mchakato wa ununuzi na iwapo kuna sababu za msingi za kuongeza idadi ya wajumbe.

Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) ilitoa zabuni nne zenye thamani ya Sh. bilioni 15.34 na Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania kilitoa zabuni tano zenye thamani ya Sh. milioni 59.68. Hata hivyo, tathmini za zabuni hizi kwa taasisi zote mbili zilifanywa na wajumbe wawili badala ya watatu walioidhinishwa kwa mujibu wa Kanuni zilizotajwa hapo juu.

Tathmini ya zabuni inayofanywa na idadi pungufu ya wajumbe huongeza hatari ya maamuzi ya upendeleo au makosa katika mchakato.

**Ninapendekeza kwamba Serikali ihakikishe Wizara, Idara na Wakala za Serikali, zinadamisha uzingatiaji wa idadi ya wajumbe wa tathmini ya zabuni kwa kuunda kamati zenye idadi inayohitajika ili kuwezesha uwazi, haki na uwajibikaji katika ununuzi.**

#### **7.3.4 Makosa Yaliyorekebishwa Wakati wa Tathmini Hayakuwasilishwa kwa Wazabuni Husika**

Kanuni ya 207 (2)(a) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inazitaka taasisi nunuzi kurekebisha kasoro za hesabu ambazo zitagunduliwa wakati wa uchambuzi wa zabuni na itoe taarifa bila kuchelewa kuhusu makosa hayo kwa mزابuni husika.

Nilibaini kuwa kamati ya tathmini ya zabuni ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilirekebisha kasoro katika mikataba nane yenye thamani ya Sh. bilioni 7.50 kwa kurekebisha kiasi cha zabuni kilichowasilishwa na wazabuni wakati wa mchakato wa tathmini. Hata hivyo, Tume hiyo ilishindwa kuwataarifu wazabuni husika kuhusu masahihisho hayo na mabadiliko ya bei za zabuni zao, jambo ambalo ni kinyume na matakwa ya kanuni za ununuzi.

Kushindwa kuwapa taarifa wazabuni kuhusu kasoro zilizorekebishwa kwenye zabuni zao kunaweza kuibua wasiwasi wa kisheria kuhusu haki na uhalali wa mchakato wa ununuzi uliofanyika. Zaidi ya hayo, kunasababisha kukosekana kwa uwazi kwa vile wazabuni hawajui mabadiliko ambayo yanaweza kuathiri bei za zabuni zao na ushindani wao katika mchakato mzima wa ununuzi.

Ninapendekeza kwamba Serikali ihakikishe Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inatoa taarifa kwa wazabuni kuhusu kasoro zozote za hesabu zilizogundulika wakati wa mchakato wa tathmini na masahihisho yaliyofanywa kwenye nukuu za bei za zabuni zao. Utaratibu huu ni muhimu ili kuhakikisha kwamba wazabuni wanafahamishwa kikamilifu kuhusu mabadiliko yoyote ambayo yanaweza kuathiri zabuni zao, ambayo ni muhimu kwa kudumisha haki na uadilifu katika mchakato wa ununuzi.

### 7.3.5 Ununuzi Uliofanyika bila Kutumia Mikataba

Kanuni ya 164 (2)(j) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inaeleza kwamba, barua ya mwaliko wa nukuu za bei na kiambatisho chochote kitakuwa na fomu ya mkataba au hati ya ununuzi wa ndani (LPO) itakayojumuisha masharti yote ya malipo.

Mapitio yangu ya ununuzi yalibaini taasisi nne zilizofanya malipo ya jumla ya Sh. bilioni 2.16 kwa wazabuni wa bidhaa na huduma bila mikataba au hati za ununuzi wa ndani, kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 27**.

#### Jedwali Na. 27: Ununuzi wa Bidhaa Uliofanyika bila Mikataba

Na.	Taasisi	Kiasi (Sh.)
1.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya	975,229,466
2.	Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Tanganyika	297,423,000
3.	Sirika la Mzinga	322,756,665
4.	Bodi ya Maji ya Bonde la Mto Rufiji	568,763,400
	<b>Jumla</b>	<b>2,164,172,531</b>

Chanzo: Ripoti za ukaguzi 2022/23

Ununuzi unaofanywa bila fomu ya mkataba au hati ya ununuzi wa ndani unaweza kuleta hasara kwa serikali ikiwa wazabuni husika watashindwa kutimiza matakwa yaliyokusudiwa kwa sababu ya kukosekana kwa mikataba ya kisheria ya makubaliano kati ya pande zote mbili.

Ninapendekeza kwamba Serikali ihakikishe uwepo wa mikataba rasmi yenye vigezo na masharti ya kuzingatia baina ya wahusika katika ununuzi wa bidhaa na huduma unaofanywa na Wizara, Idara na Wakala za Serikali.

### 7.3.6 Mikataba iliyosainiwa bila Kupekuliwa na Wanasheria

Kanuni ya 59(1) na 60(1) za Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 kama zilivyorekebisha na kanuni ya 2 na 3 za Kanuni za Ununuzi wa Umma

(Marekebisho) za Mwaka 2016 (Toleo Na. 121) mtawalia inabainisha kuwa mikataba rasmi ambayo thamani yake ni Sh. bilioni moja na zaidi au inayofanywa kupitia zabuni ya ushindani wa kimataifa, inapaswa kupekuliwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na mkataba wa chini ya Sh. bilioni moja utapekuliwa na mwanasheria wa taasisi nunuzi kabla ya wahusika kusaini mikataba hiyo.

Mapitio yangu ya usimamizi wa mikataba yalibaini kuwa taasisi tano zilisaini mikataba na nyongeza za mikataba zenye thamani ya Sh. bilioni 4.78 kabla ya kufanyiwa upekuzi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali au wanasheria wa taasisi husika, kama inavyoainishwa katika **Jedwali Na. 28**.

**Jedwali Na. 28: Taasisi Zilizokuwa na Mikataba Isiyopekuliwa na Wanasheria**

Na.	Taasisi	Kiasi cha Mkataba (Sh.)
1.	Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA)	1,832,250,000
2.	Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS)	2,000,000,000
3.	Wizara ya Afya	393,353,000
4.	Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu	533,884,180
5.	Wakala wa Misititu Tanzania	27,000,000
	<b>Jumla</b>	<b>4,786,487,180</b>

Chanzo: Ripoti za ukaguzi 2022/23

Kutopekuliwa kwa mikataba na wanasheria kunaweza kusababisha hasara kwa taasisi nunuzi endapo itatokea migogoro kwenye utekelezaji wa mikataba yenye vifungu visivyokuwa na tija kwa taasisi za serikali.

Ninapendekeza kuwa Serikali ihakikishe mikataba yote katika Wizara, Idara na Wakala za Serikali, inafanyiwa upekuzi kabla ya kusainiwa kama matakwa ya kanuni za ununuzi zinavyobainisha.

**7.3.7 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Haikufanya Uchunguzi wa Kina kwa Wakandarasi wenye Mikataba ya Miradi ya Umwagiliaji**

Kanuni ya 373 (1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inazitaka taasisi nunuzi kufanya uchunguzi wa kina kwa mkandarasi aliyependekezwa kwa ajili ya zabuni hiyo kwa kuhakiki sifa za uzoefu, utaalumu, na uwezo wa kifedha. Kanuni hiyo pia inaitaka taasisi nunuzi kutathmini iwapo shauri lolote la kisheria au utata unaomuhusu mkandarasi na waajiriwa wake wa awali hautaathiri uwezo wa kutekeleza mkataba.



Aidha, ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kama ilivyoainishwa katika aya ya 11 ya barua ya majibu ya tarehe 5 Agosti 2022 kuhusu kuhakiki mikataba ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, ilisisitiza umuhimu wa kufanya uchunguzi wa kina kuhusu wakandarasi wote kabla ya kukamilisha mikataba.

Kinyume chake, nilibaini kuwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji haikufanya uchunguzi wa kina wa wakandarasi kwenye miradi 25 ya umwagiliaji yenye thamani ya Sh. bilioni 408.14.

Kutofanya uchunguzi wa kina kunaweza kusababisha kuingia mikataba na wakandarasi ambao hawana sifa na uwezo unaostahili, hivyo kuathiri utekelezaji wa mradi.

**Ninapendekeza kuwa Serikali ihakikishe kuwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inalinda rasilimali za umma na kufanikisha utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji kwa kufanya uchunguzi wa kina wa wakandarasi.**

### **7.3.8 Mikataba Iliyosainiwa na Maafisa wa Wazabuni Wasio na Mamlaka**

Kanuni ya 233(1) ya Kanuni za Ununuzi za Umma za Mwaka 2013 kama zilivyorekebisha na kanuni ya 75 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma (Marekebicho) za Mwaka 2016 inaelekeza kuwa mkataba rasmi utasainiwa na afisa masuuli wa taasisi nunuzi na mtu mwenye mamlaka kwa upande wa mzabuni aliyeshinda zabuni ndani ya siku 28 za kalenda baada ya kutimizwa kwa masharti yote yanayopaswa kabla ya kusaini mkataba.

Nilibaini kuwa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ilisaini zabuni nne za ununuzi wa bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni 4.02. Hata hivyo, kwa upande wa wazabuni, mikataba hiyo ilitiwa saini na maafisa ambao hawakuwa na mamlaka ya kisheria ya kusaini mikataba hiyo.

Mkataba uliotiwa saini na muwakilishi ambaye hana mamlaka ya kisheria ni batili na hauwezi kusimamiwa na mahakama katika shauri, hivyo kuufanya uwe na uwezekano wa kusababisha matatizo ya kisheria na hasara ya kifedha kwa serikali.

**Ninapendekeza Serikali ichukue hatua za kuhakikisha mikataba inayotekelezwa na Wakala wa Majengo Tanzania inasainiwa na maafisa wenye mamlaka ya kisheria ya kusaini mikataba hiyo ili kuzuia matatizo ya**

kisheria na upotevu wa fedha unaoweza kujitokeza kutokana na utekelezaji wa mikataba hii.

#### 7.4 Upungufu Katika Utekelezaji na Usimamizi wa Mikataba

Hatua ya utekelezaji na usimamizi wa mikataba inahusiana na kutimiza majukumu ya kimkataba kwa mwajiri na mwajiriwa, ikijumuisha vipengele vinavyohusiana na uwasilishaji, ujenzi, malipo, na usimamizi wa jumla wa mikataba.

##### 7.4.1 Taasisi Nunuzi Kukiuka Masharti ya Malipo ya Kimkataba

Kifungu cha 14.6 hadi 14.8 cha Masharti ya Jumla ya Mwongozo wa Nyaraka za Zabuni kwa Ununuzi wa Kazi za Kati na Kubwa wa Mwaka 2022 vinawataka waajiri kuwalipa wakandarasi kiasi kilichoidhinishwa na wasimamizi wa miradi kama malipo ya kazi iliyofanyika ndani ya siku 28 tangu mwajiri alipopokea hati ya madai. Ucheleweshaji wa malipo utasababisha riba itakayoongezeka kila mwezi na itakayototwa kwenye kiasi ambacho kimechelewa kulipwa.

Nilibaini ukiukaji wa masharti ya malipo kwa wakandarasi, washauri elekezi na wazabuni, ambapo madai ya jumla ya Sh. bilioni 58.11 hayakulipwa kwa wakati na taasisi nunuzi na riba iliyotokana na kuchelewa kwa malipo iliyototwa kwa Wizara ya Ujenzi na Wakala wa Barabara Tanzania ya jumla ya Sh. bilioni 52.30 kama inavyoainishwa zaidi katika aya zifuatazo.

##### 7.4.1.1 Uchelewaji wa Kulipa Madeni ya Sh. Bilioni 58.11 Kinyume na Masharti ya Mikataba

Mapitio yangu ya utekelezaji wa mikataba yalibaini uchelewaji wa kulipa madeni ambapo jumla ya Sh. bilioni 58.11 hazikuwa zimelipwa ndani ya muda wa makubaliano ya kimkataba na taasisi 11. Hii ni pamoja na madai yalioidhinishwa kwa kazi zilizokamilika; bidhaa na huduma zilizotolewa ambazo zilikuwa hazijalipwa zenye thamani ya Sh. bilioni 19.37; na Sh. bilioni 38.73 zilizolipwa kwa kuchelewa ambapo ucheleweshaji wa malipo ulianza siku nne hadi 1193, kama **Kiambatisho Na. IV** kinavyoonesha.

##### 7.4.1.2 Wizara ya Ujenzi Haijalipa Riba Iliyotokana na Uamuzi wa Usuluhishi Uliofikiwa Tangu Mwaka 2014

Tarehe 4 Aprili 2013, Wizara ya Ujenzi ilipokea agizo la usuluhishi kupitia Mahakama ya Kimataifa ya Biashara (ICC) kuhusu mgogoro na M/S Sogea Satom. Mgogoro huo ulitokana na mkataba wa kukarabati Barabara ya Ibanda-Uyole

yenye urefu wa kilomita 97.963 ulioanza mwaka 1991. Wakati wa utekelezaji wa mkataba huo, kazi za ziada zilijitokeza na hivyo utekelezaji wake kuongezeka kwa muda wa siku 110, jambo ambalo mfadhili (EU) hakuridhia na hivyo kusababisha Serikali kupaswa kulipa gharama hizo. Makubaliano nje ya mahakama na mkandarasi yalifikiwa baadaye, na jumla ya dola za Marekani milioni 12 zilipaswa kulipwa na Serikali mwaka 2014.

Hata hivyo, hadi kufikia Juni 2023, kiasi hicho hakikuwa kimelipwa, ambacho ni sawa na Sh. bilioni 28.06. Deni hilo limesababisha kuendelea kuongezeka kwa riba inayokokotolewa kwa asilimia 7 kwa mwaka kama ilivyoainishwa katika sehemu ya 2.1 ya Hati ya Suluhu. Ukaguzi wangu umebaini riba ya mwaka 2022/23 ilikuwa Sh. bilioni 3.61, na kusababisha jumla ya riba ya Sh. bilioni 17.48 hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023.

#### **7.4.1.3 Riba Iliyotozwa kwa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Kutokana na Kuchelewa Kulipa Wakandarasi**

Nilibaini kuwa, Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) ilitozwa riba ya kiasi cha Sh. bilioni 34.82 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/23 kwa kuchelewa kulipa madai ya wakandarasi na washauri elekezi mbali mbali wa miradi ya ujenzi wa barabara.

Kuchelewa kulipa madai ya wakandarasi kunasababisha serikali kulipa kiasi kikubwa cha riba, ambacho kinaweza kuepukika. Jambo linalodhohofisha uendeleu wa utoaji huduma kwa Serikali kwani kinaathiri ukamilikaji wa miradi ya ujenzi na kuzuia upatikanaji wa huduma zilizokusudiwa kwa walengwa kwa wakati. Aidha, uchelewaji huo unaweza kusababisha ongezeko la gharama za miradi kutokana na riba iliyoongezeka.

Ninapendekeza kwamba Serikali ilipe madai ya mkandarasi ili kuepusha limbikizo zaidi la riba. Pia, kuhakikisha malipo ya kazi za ujenzi zilizokamilika yanafanywa kwa wakati ili kuzuia matumizi yasiyo na manufaa ya fedha za umma ili kupata matokeo chanya kwa miradi yenye tija.

#### **7.4.2 Kuchelewa Kukamilika kwa Majengo 21 ya Serikali Yanayojengwa Eneo la Mtumba**

Sambamba na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP III 2021/22 hadi 2025/26), ambao umeweka kipaumbele cha juu katika kuendeleza mji mkuu mpya wa serikali, Serikali ilihamishia Dodoma kitovu cha shughuli za Serikali ili kuweka huduma za umma karibu na wananchi.

Tathmini yangu ya hali halisi ya utekelezaji wa ujenzi wa majengo ya Serikali kwa awamu ya pili katika eneo la Mtumba imebaini kuwa majengo 21 kati ya 29 ya taasisi za Serikali yenye mikataba ya thamani ya sh. bilioni 431.01, yalikuwa hayajakamilika ikilinganishwa na muda wake wa awali uliopangwa kukamilika. Hali halisi ya utekelezaji wa majengo hayo ilikuwa kuanzia asilimi 47 hadi 85 kufikia mwezi Januari 2024, na muda wa utekelezaji ulikuwa umeongezwa ili kuwezesha kukamilika kwa kazi ambazo hazijakamilika.

Sababu kubwa ya kutokamilika kwa majengo haya ni mipango isiyojitosheleza, kutotolewa fedha za kutosha, na kutokuwa na usimamizi na ufuatiliaji uliojitosheleza. Maendeleo ya utekelezaji kwa kila jengo hadi kufikia mwezi Januari 2024 unaoneshwa katika **Kiambatisho Na. V.**

Kuchelewa kukamilika kwa majengo hayo si tu kunaifanya Serikali isifikie azma yake ya kuhamia katika eneo la mji wa serikali Mtumba bali pia kunasababisha kuongezeka kwa gharama za ujenzi na kuongeza gharama za uendeshaji wa Serikali.

**Ninapendekeza Serikali ifuatilie kwa karibu maendeleo na kuchukua hatua zinazohitajika ili kuhakikisha ujenzi wa majengo ya Serikali katika eneo la Mtumba unakamilika. Hatua hizi zitasaidia kupunguza matokeo hasi katika utoaji wa huduma na kupunguza gharama za uendeshaji wa Serikali.**

#### **7.4.3 Utekelezaji wa Mikataba bila Kuwapo kwa Dhamana za Utendaji Kazi**

Kanuni ya 29(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inazitaka taasisi nunuzi kumtaka mzabuni aliyechaguliwa kuwasilisha dhamana ya utendaji kazi ili kuhakikisha kuwa atatekeleza majukumu yake ya kimkataba kwa uaminifu na atalipa malipo yote anayopaswa ikiwa pamoja na vibarua, mafundi, na wazabuni.

Nilibaini kuwa mikataba 46 ya ujenzi yenye thamani ya Sh. bilioni 383.76 haikuwa na dhamana za utendaji kazi licha ya kuwapo kwa vifungu vya mkataba vinavyotaka uwasilishaji wa dhamana hizo kwa njia ya dhamana za bima na dhamana za kifedha kutoka benki. Mikataba hiyo imeendelea kutekelezwa bila dhamana hizo kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 29.**

**Jedwali Na. 29: Mikataba Inayotekelezwa bila Dhamana za Utendaji Kazi**

Na.	Taasisi	Idadi ya Mikataba	Thamani ya Dhamana (Sh.)	Maelezo
1.	Wakala wa Majengo Tanzania	2	295,865,760	Hazikuwasilishwa
2.	Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS)	7	375,514,215,171	Hazikuwasilishwa
		11	962,955,614	Muda wake umeisha
3.	Tume ya Taifa ya Umwagiliaji	3	2,664,511,686	Muda wake umeisha
4.	Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA)	23	4,326,361,445	Muda wake umeisha
	<b>Jumla</b>	<b>46</b>	<b>383,763,909,676</b>	

Chanzo: Ripoti za Ukaguzi 2022/2023

Kutokuwapo kwa dhamana za utendaji kazi kunaweza kusababisha kushindwa kukamilika kwa mikataba ikiwa wakandarasi watahondwa kutekeleza majukumu yao.

Ninapendekeza kwamba Serikali ihakikishe kwamba Wizara, Idara na Wakala za Serikali, zinahakikisha uwepo wa dhamana za utendaji kazi na kuhakikisha kuwa zinahuishwa kwa wakati ili kuepuka hasara inayoweza kutokea endapo mkandarasi atashondwa kutekeleza majukumu yake.

#### 7.4.4 Kuchelewa Kuanza kwa Utekelezaji wa Mikataba

Kanuni ya 69 (3 na 4) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inaitaka taasisi nunuzi kukadiria kwa usahihi mahitaji yake ya bidhaa, kazi, na huduma na kwa kuzingatia huduma au shughuli ambazo tayari zimeratibiwa katika mpango wa ununuzi wa mwaka na kujumuishwa katika bajeti ya mwaka na makadirio hayo yatajumuisha makadirio sahihi ya muda zaidi kwa mwezi wa karibu kwa ajili ya utendaji na kukamilika kwa huduma.

Nilibaini kuwa Wakala wa Barabara Tanzania ulisaini mikataba mitatu yenye thamani ya Sh. bilioni 246.84 katika kipindi cha miezi Disemba 2022 na Aprili 2023. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023, wakandarasi wote watatu walikuwa wamelipwa fedha za awali kiasi cha Sh. bilioni 14.16. Hata hivyo, hadi kufikia mwezi Novemba 2023, miezi mitano ilikuwa imepita tangu malipo hayo yalipwe, lakini wakandarasi wote walikuwa hawajatayarisha mahitaji ya ujenzi ikiwemo wafanyakazi na vifaa vinavyohitajika kwa ajili ya kuanza ujenzi na kambi za wahandisi zilikuwa zimejengwa. Kwa ujumla, ujenzi wa barabara hizo bado haujaanza.

Nilibaini kuwa kati ya mwezi Machi 2023 na Mei 2023, Ofisi ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Dodoma ilitoa zabuni ya miradi tisa ya ujenzi wa barabara kwa wakandarasi mbalimbali, yenye thamani ya Sh. bilioni 37. Hata hivyo, hadi muda wa ukaguzi mwezi Desemba 2023, wakandarasi walikuwa hawajaanza kazi ya ujenzi, kukiwa na ucheleweshaji wa kazi kwa zaidi ya miezi saba. Wakala wa Barabara Tanzania ilieleza kuwa miradi hiyo ilifadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), ambapo ilihitaji kupata kibali “*No Objection*” kutoka Benki hiyo kabla ya kusainiwa kwa mkataba, ambapo vibali hivyo vilitolewa tarehe 06 Julai 2023. Kuchelewa kuanza kwa miradi ya barabara kunakwamisha kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa na kusababisha kuongezeka kwa malalamiko kutoka kwa watumiaji wa barabara, jambo ambalo linaweza kuharibu sifa ya Wakala.

Tarehe 21 Oktoba 2022, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania iliingia mikataba miwili, mmoja wa usambazaji na ufungaji wa rada za hali ya hewa kwa Sh. bilioni 3.94, na mwingine wa usambazaji na ufungaji wa vifaa vya urekebishaji usawa wa vifaa vya maabara kwa Sh. bilioni 2.51. Hata hivyo, hadi tarehe 14 Desemba 2023, utekelezaji wa mikataba hiyo haukuwa umeanza kutokana na ukosefu wa fedha.

Aidha, nilibaini kuwa Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) ilisaini mikataba na kampuni za M/S Songoro na M/S Africa Marine Engineering kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa vivuko kwa jumla ya Sh. bilioni 11.71. Hata hivyo, kazi zote mbili hazikuweza kuanza kutokana na kushindwa kulipwa kwa fedha za awali kiasi cha Sh. bilioni 1.51 na kusababisha uchelewaji wa kati ya siku 147 na 168 hadi kufikia tarehe 18 Septemba 2023, tangu wakandarasi walipowasilisha dhamana za malipo ya awali.

Kuchelewa kutekeleza mikataba kunahathiri utoaji wa huduma muhimu kwa jamii na kunaweza pia kusababisha ukiukaji wa masharti ya mikataba, ikiwa ni pamoja na muda uliowekwa na kusababisha riba na migogoro kwa taasisi husika.

**Ninapendekeza kuwa Serikali ihakikishe kuwa Wizara, Idara na Wakala za Serikali tajwa hapo juu zinaanza utekelezaji wa miradi husika ili kuhakikisha miradi inakamilika kwa wakati.**

#### 7.4.5 Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini kuchelewesha Ununuzi na Usambazaji wa Magari na Pikipiki

Kanuni ya 69(1) ya Kanuni ya Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inaitaka taasisi nunuzi kukadiria mahitaji yake ya bidhaa, huduma, na kufanya kazi kwa usahihi kadiri inavyowezekana kwa kuzingatia huduma au shughuli ambazo tayari zimeratibiwa katika mpango wa ununuzi wa mwaka na kujumuishwa katika bajeti ya mwaka.

Aidha, mkataba wa makubaliano kati ya Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini na Kampuni ya Toyota Tanzania Limited inabainisha muda wa miezi mitatu kwa ajili ya utengenezaji na usambazaji wa magari yaliyoagizwa na taasisi za serikali. Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini huchukua fedha za wateja ambao ni taasisi za Serikali kama amana ili kufanya ununuzi wa magari kwa pamoja, zikilenga kupata thamani ya fedha.

Kinyume na matakwa hayo, nilibaini kuwa taasisi 12 zilihamisha fedha kwenda kwa Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini kwa ajili ya ununuzi wa magari na pikipiki. Hata hivyo, kulikuwa na uchelewaji wa ununuzi na usambazaji wa magari 42 na pikipiki 37 kwa kipindi kati ya miezi minne hadi 20, kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 30**.

#### Jedwali Na. 30: Uchelewaji wa Ununuzi na Usambazaji wa Magari na Pikipiki

Na.	Taasisi	Idadi ya Magari	Kiasi (Sh.)	Muda Uliochelewa (Miezi)
<b>Magari</b>				
1	Mahakama ya Tanzania	3	274,297,762	10
2	Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi	13	1,260,200,599	8
3	Mamlaka ya Udhhibiti wa Usafiri wa Ardhini	3	217,731,407	8
4	Ofisi ya Taifa ya Takwimu	8	580,617,086	7
5	Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini	5	362,885,679	7
6	Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi	4	408,424,220	6
7	Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania	2	197,917,241	6
8	Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji	4	703,155,489	4
<b>Jumla ndogo</b>			<b>4,005,229,483</b>	

Na.	Taasisi	Idadi ya Magari	Kiasi (Sh.)	Muda Uliochelewa (Miezi)
<b>Pikipiki</b>				
1	Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Nzovwe	1	2,900,000	5
2	Wakala wa Huduma za Misituz Tanzania	36	392,400,000	20
	<b>Junla ndogo</b>		<b>395,300,000</b>	
	<b>Jumla kuu</b>		<b>4,400,529,483</b>	

Chanzo: Ripoti za ukaguzi 2022/23

Ucheleweshaji wa ununuzi na usambazaji wa magari na pikipiki unazuia shughuli za taasisi za serikali, hususani katika kurahisisha huduma za usafirishaji.

Ninapendekeza kwamba Serikali ihakikishe kuwa Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini inakadiria kwa usahihi mahitaji yake na kuimarisha taratibu za usimamizi wa mikataba ili kuhakikisha uwasilishaji wa magari na pikipiki kwa wakati kwa Taasisi za Umma.

#### 7.4.6 Kupokea Bidhaa bila Kukaguliwa

Kanuni ya 244(1) na 245 za Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 zinazitaka taasisi zinazopokea bidhaa kukagua bidhaa zinazoletwa na wazabuni na kuzikubali iwapo tu zinakidhi masharti yaliyoainishwa kwenye mikataba.

Kinyume na matakwa hayo, nilibaini kuwa taasisi nne zilifanya malipo kwa wazabuni kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa na huduma zenye thamani ya Sh. milioni 615.15 ingawa bidhaa hizo hazikukaguliwa na kamati za ukaguzi na mapokezi ya bidhaa, kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 31**.

#### Jedwali Na. 31: Taasisi Zilizopokea Bidhaa bila Kukaguliwa

Na	Taasisi	Kiasi (Sh.)
1.	Shirika la Mzinga	256,682,550
2.	Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania	118,305,975
3.	Mmlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwapwa	223,116,019
4.	Bodi ya Filamu Tanzania	17,048,000
	<b>Jumla</b>	<b>615,152,544</b>

Chanzo: Ripoti za ukaguzi 2022/23

Kupokea bidhaa bila kufanya ukaguzi kunaweza kuathiri ubora na uzingatiaji wa masharti ya viwango vya mikataba husika hivyo kusababisha ununuzi wa bidhaa zenye ubora wa chini.



Ninapendekeza kwamba Serikali ihakikishe Wizara, Idara na Wakala za Serikali, inakagua ubora wa bidhaa kabla ya kufanya malipo.

#### 7.4.7 Kushindwa Kudai Malipo ya Dhamana ya Utendaji Kazi na Malipo ya Awali Yaliyolipwa kwa Mikataba Iliyositishwa

Kanuni ya 243 (5) (b) ya Kanuni za Ununuzi ya Umma za Mwaka 2013 inaeleza kuwa endapo mtoa huduma au mkandarasi atashindwa kutoa huduma kwa kiwango kinachotakiwa, kurekebisha makosa, au kukamilisha kazi kama ilivyokusudiwa na taasisi nunuzi, taasisi nunuzi itapaswa kudai dhamana ya utendaji kazi iliyowekwa na mtoa huduma au mkandarasi.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/23, Tume ya Madini na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) hazikudai dhamana ya utendaji kazi na malipo ya awali yaliyofanywa kwa mkandarasi ya thamani ya Sh. milioni 675.90 kwenye mikataba iliyositishwa.

- Nimebaini, Tume ya Madini iliajiri Kampuni ya MCB kujenga jengo lake la makao makuu Jijini Dodoma hadi kufikia tarehe 21 Januari 2022 kwa mkataba wa Sh. bilion 4.06. Hata hivyo, mkataba huo ulisitishwa tarehe 21 Oktoba 2022 malipo yakiwa yamefikia asilimia 34 kutokana na mkandarasi kushindwa kukamilisha kazi ndani ya muda uliokubaliwa. Pamoja na kuwapo kwa dhamana ya utendaji kazi ya thamani ya Sh. milioni 406.98, ambayo uhalali wake unaisha tarehe 16 Novemba 2024, Tume ya Madini haikuwa imedai dhamana hii kutoka kwa taasisi mdhamini.
- Aidha, nilibaini kuwa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) imeshindwa kurejesha malipo ya awali ya Sh. milioni 268.91 iliyomlipa mkandarasi baada ya kusitishwa kwa mkataba Na. AE-102/2020-2021/26/001 uliongia na Kampuni ya M/S Civil Loths Engineering Limited kwa ujenzi wa Bwawa la Kwenkambala na kazi husiani Wilayani Handeni, Mkoa wa Tanga kwa mujibu wa ripoti ya mwisho ya mahesabu ya ujenzi husika.

Kushindwa kurejesha fedha za dhamana ya utendaji kazi na malipo ya awali kunasababisha hasara ya kifedha kwa Tume ya Madini na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), hivyo kusababisha kuongezeka kwa gharama za miradi hii.

Ninapendekeza kwamba Serikali ihakikishe urejeshaji wa fedha za dhamana ya utendaji kazi na malipo ya awali kutoka kwa wakandarasi walioshindwa kutekeleza majukumu yao ili kulinda fedha za umma na kusimamia uwajibikaji katika michakato ya ununuzi.

#### 7.4.8 Miradi ya Maji Iliyotelekezwa

Kifungu cha 69.2 (a) cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kinamtaka mwajiri kusitisha mkataba iwapo mkandarasi ataacha kufanya kazi kwa muda wa siku 28 bila kuainisha katika programu iliyopo ya kazi, na usitishaji huo haujaidhinishwa na msimamizi wa mradi.

Nilibaini kuwa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) ilikuwa na miradi 10 yenye thamani ya Sh. bilioni 7.12 iliyotelekezwa na wakandarasi kwa muda wa hadi miaka minne. Kati ya miradi hiyo, wakandarasi walitelekeza mikataba miwili licha ya kulipwa malipo ya awali ya Sh. milioni 530.76, wakati maendeleo ya ujenzi yakiwa kuanzia asilimia 0 hadi 46.

Aidha, nilibaini kuwa mkandarasi mmoja aliyehusika na mkataba wenye thamani ya Sh. milioni 718.11 kwa ajili ya utafiti wa kijiolojia, kuchimba visima 18 vyenye tija, na kufunga pampu katika maeneo mbalimbali alitelekeza mradi huo tangu tarehe 16 Mei 2023 kutokana na ukosefu wa maji katika maeneo husika.

Sababu kuu ya kutelekezwa kwa miradi ya maji ni kutotolewa kwa fedha za kutosha hivyo kusababisha matatizo ya kifedha miongoni mwa wakandarasi husika; wakandarasi kutokuwa na uwezo wa kutosha wa kutekeleza miradi; na kukosekana kwa maji kuwezesha kuchimba visima vyenye tija katika maeneo husika. Kutelekezwa kwa miradi hiyo ya ujenzi kunasababisha kuchelewa kukamilika kwa miradi, upotevu wa rasilimali fedha, na ukosefu wa huduma za maji katika maeneo yaliyoathirika.

Ninapendekeza kuwa Serikali ihakikishe upatikanaji wa fedha za miradi kwa wakati na kwamba Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) inaimarisha usimamizi wa utekelezaji wa miradi ili kuhakikisha miradi inakamilika ndani ya muda uliokusudiwa. Pia, kuchukua hatua zinazofaa, ikiwa ni pamoja na kurejesha Sh. milioni 530.76 zilizolipwa kama malipo ya awali kwa wakandarasi waliotelekeza miradi, na kuimarisha mchakato wa tathmini ya zabuni ili kuwapa kazi wakandarasi wenye uwezo wa kiufundi na kifedha katika michakato ya ununuzi ijayo.

#### 7.4.9 Kuwapo kwa Zabuni zenye Gharama ya Mkataba Mara Saba Zaidi ya Bajeti Iliyoidhinishwa

Kifungu cha 59(1)-(2)(d) cha Sheria ya Ununuzi ya Umma ya Mwaka 2022 kinataka taasisi nunuzi kutoendelea na zabuni ambazo gharama zake ni kubwa zaidi kuliko bajeti.

Nilipitia mpango wa ununuzi wa mwaka na kubaini kuwa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) ilipanga kutoa zabuni 119 katika bajeti yake iliyoidhinishwa ya Sh. bilioni 45.31. Hata hivyo, zabuni hizo zilitolewa kwa bei ya mikataba ya thamani ya Sh. bilioni 317.75 ambayo ilikuwa ni mara saba zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa.

Utoaji wa zabuni kwa bei ya juu zaidi kuliko bajeti kunasababisha madeni kwa Serikali kutokana na kushindwa kuwalipa kwa wakati wakandarasi, hivyo kuathiri kasi ya utekelezaji wa miradi hiyo na kuathiri thamani ya fedha.

**Ninapendekeza Serikali ihakikishe kuwa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) inazingatia Sheria ya ununuzi wa Umma kwa kukataa zabuni zinazozidi bajeti iliyoidhinishwa. Zaidi ya hayo, RUWASA inapaswa kupitia upya taratibu zake za ununuzi ili kufanya makadirio ya gharama na bajeti kwa usahihi, na hivyo kuzuia madeni ya serikali yasiyo ya lazima, kuhakikisha malipo ya wakandarasi yanafanyika kwa wakati, ili kupata thamani ya fedha.**

#### 7.4.10 Mikataba yenye Malipo ya Awali Yasiyo na Dhamana

Aya ya 15 ya Mwongozo wa Dhamana katika Ununuzi wa Umma wa Mwaka 2022 inaelekeza kuwa, iwapo itahitajika na kuwapo katika mkataba wa ununuzi na baada ya kusainiwa kwa mkataba, mkandarasi atawasilisha kwa taasisi nunuzi ombi la malipo ya awali kwa mwongozo uliotolewa. Ikiwa yapo kwenye nyaraka za zabuni, malipo ya awali yatatolewa tu na taasisi nunuzi baada ya kupokea dhamana ya malipo ya awali kutoka kwa benki inayoaminika.

Nilibaini kuwa dhamana za malipo ya awali ya Sh. bilioni 3.24 kwa mikataba 15 iliyotekelezwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) zilikwisha muda wake kabla ya kurejeshwa kikamilifu wakati mikataba ikiendelea.

Malipo ya awali yasiyo na dhamana yanaiweka serikali kwenye hatari ya kupata hasara ya kifedha iwapo wakandarasi wataashindwa kutekeleza majukumu yao ya kimkataba.

**Ninapendekeza kwamba Serikali ihakikishe kuwa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) inafuatilia kwa karibu uhalali wa dhamana ya malipo ya awali ili kuzuia kuisha kwa kipindi cha dhamana kabla ya mikataba kukamilika. Kwa kutekeleza hatua zinazofaa za usalama kwa malipo ya awali, RUWASA inaweza kupunguza hatari ya hasara ya kifedha kwa Serikali endapo mkandarasi atashindwa kulipa.**

#### 7.4.11 Kuchelewa Kukamilika kwa Miradi 62 ya Maji

Kanuni ya 114 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inazitaka taasisi nunuzi kuwa na ufanisi katika usimamizi wa ununuzi wa kazi inazozifanya kwa kufuatilia gharama, mienendo, na kuhakikisha miradi inakamilika kwa wakati bila ukiukaji wa masharti ya mkataba; kuchukua hatua za kurekebisha au za kinidhamu kwa ukiukaji wa masharti ya mkataba; na kuhakikisha majukumu ya kimkataba yaliyowekwa yanatekelezwa kikamilifu.

Nimebaini kuwa miradi 62 ya maji ya Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) yenye thamani ya Sh. bilioni 149.96 ilichelewa kukamilika kwa kipindi cha kati ya siku 11 na 1564 ikiwa ni zaidi ya tarehe zilizokubaliwa za kukamilika kwa miradi hiyo. Tathmini yangu ilibaini kuwa uchelewaji huo ulichangiwa na uhaba wa fedha, ambao uliathiri malipo ya madai ya wakandarasi.

Kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi ya maji husababisha kuongezeka kwa gharama za ujenzi, hivyo kupunguza upatikanaji wa huduma za uhakika za maji safi kwa jamii inayokusudiwa.

**Ninapendekeza kwamba Serikali ihakikishe upatikanaji wa fedha za miradi ya maji kwa wakati ili kuwezesha malipo ya madai ya wakandarasi bila kuchelewa, hivyo kurahisisha utekelezaji wa mradi na kupunguza ucheleweshaji.**

#### 7.4.12 Kasi Ndogo ya Utekelezaji wa Miradi

Kanuni ya 114 (b), (c) na (d) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inaelekeza kuwa taasisi nunuzi ina jukumu la kusimamia kwa ufanisi ununuzi wa

kazi. Taasisi hizo lazima zifuatilie mienendo ya kazi na kuhakikisha kuwa zinakamilika kwa wakati na kulingana na masharti ya kila mkataba; kuchukua hatua za kurekebisha au za kinidhamu kwa ukiukaji wa masharti ya mkataba; na kuhakikisha majukumu ya kimkataba yaliyowekwa yanatekelezwa kikamilifu. Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) inatekeleza miradi miwili ambayo ni ujenzi wa nyumba za makazi ya mkuu wa mkoa wa Geita na Ujenzi wa wodi, kazi za nje, na jengo la mionzi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Chato. Hata hivyo, tathmini yangu ya utekelezaji ilibaini kuwa hadi kufikia Januari 2024, maendeleo ya kazi za miradi hiyo miwili yenye thamani ya Sh. bilioni 20.05 yalikuwa kwa 11% hadi 22% kutokana na kasi ndogo ikilinganishwa na muda uliokadiriwa wa kukamilika kwa mikataba hiyo.

Aidha, nilibaini kuwa Idara ya Huduma za Uhamiaji iliingia mkataba namba ME 014/2018/2019/HQ/W/06 na Kampuni ya Ujenzi ya SUMA JKT kwa ajili ya ujenzi wa jengo la makao makuu ya Uhamiaji Jijini Dodoma kwa mkataba wa Sh. bilioni 30. Mkataba huo ulipangwa kukamilika mwezi Oktoba 2023. Hata hivyo, hadi wakati wa ukaguzi huu, ujenzi ulikuwa haujakamilika.

Menejimenti zilihusisha kasi ndogo ya maendeleo ya kazi zote mbili na uchelewaji wa upatikanaji wa fedha. Ninaamini kuwa kasi ndogo ya utekelezaji wa miradi hiyo imeathiri kukamilika kwa wakati kwa miradi hiyo na kusababisha ongezeko la gharama na kuchelewesha utoaji wa huduma kwa walengwa.

**Ninapendekeza kuwa Serikali iimarishe usimamizi wa utekelezaji wa miradi na kuhakikisha fedha zinatolewa kwa wakati kwa ili kuhakikisha kuwa miradi inakamilika kwa muda uliopangwa.**

#### **7.4.13 Kiasi cha Malipo ya Ziada Ambacho Hakikurejeshwa kwa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Baada ya Kusitishwa kwa Mkataba**

Tarehe 19 Machi 2018, Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) na Wakala wa Barabara Tanzania walisaini mkataba wa makubaliano namba MOU/2017/2018/HQ/W kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ofisi za makao makuu ya Wakala wa Barabara Tanzania jijini Dodoma wenye thamani ya Sh. bilioni 30.13. Mkataba huo ulipangwa kukamilika tarehe 15 Septemba 2022.

Nilibaini kuwa tarehe 09 Machi 2023, Wakala wa Barabara Tanzania alisitisha mkataba, ikitaja sababu kadhaa ikiwa pamoja na maendeleo yasiyoridhisha ya kazi, mkandarasi kushindwa kuomba kuongezewa muda, kuchelewa kuwasilisha maelezo ya vipimo tangu mwezi Desemba 2022, kutowasilisha programu ya kazi,

na kujitokeza kwa kazi za ziada ambazo hazikuwa na maelezo ya kutosha kuhusu bei zake.

Kufuatia usitishaji huo, taarifa ya mwisho ya hesabu ya mwezi Machi 2023 ilibainisha kuwa Wakala wa Barabara Tanzania ilifanya malipo ya ziada kwa Wakala wa Majengo Tanzania ya Sh. bilioni 2.03 ikilinganishwa na jumla ya thamani ya kazi zilizotekelezwa hadi tarehe ya kusitishwa kwa mkataba yenye jumla ya Sh. bilioni 12.80 (pamoja na malipo ya awali ambayo hayakurejeshwa ya Sh. bilioni 6.40), kwani kiasi halisi kilicholipwa ni Sh. bilioni 14.83.

Wakala wa Majengo Tanzania ulieleza kuwa Mamlaka ya Mapato Tanzania ilitaifisha kiasi hicho cha Sh. bilioni 2.03 katika akaunti yake ya benki kutokana na madeni ya kodi yaliyogunduliwa wakati wa ukaguzi wa kodi, hivyo Wakala wa Majengo Tanzania kushindwa kurejesha malipo hayo ya ziada.

Kwa ujumla, ni maoni yangu kwamba kasoro zilizobainishwa zinaweza kusababisha hasara za kifedha, kupunguza ushindani, kuathiri uadilifu, kuathiri ubora, kusababisha athari za kisheria na kimaadili, kupoteza uaminifu, na kuzorotesha huduma za umma.

**Ninapendekeza kuwa Serikali ihakikishe Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) inarejesha fedha zilizolipwa zaidi kwa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) ili kuhakikisha mradi unakamilika kwa wakati.**

#### **7.4.14 Upungufu katika Utekelezaji wa Ukarabati wa Jengo la Zamani la Ubalozi wa Tanzania, Washington**

Tarehe 17 Oktoba 2022, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki iliingia mkataba Na. ME-0132020-2021/HQ/W/04 na Kampuni ya M/S M&R Inc, 14341 Fox Creek Ct. Cooksville MD 21723 ya Washington DC Marekani wa thamani ya Sh. bilioni 11.57 (dola za Marekani 5,189,862.38) pamoja na kodi ya ongezeko la thamani asilimia 20 kwa kazi za ukarabati wa jengo la zamani la ubalozi wa Tanzania lililopo Barabara ya 2139 Mtaa wa R, NW Washington, DC 20008 Marekani kuanzia mwezi Novemba 2022 hadi mwezi Novemba 2025. Aidha, hadi kufikia mwezi February 2024, malipo ya awali ya Sh. milioni 923.95 sawa na asilimia 8 ya malipo ya mkataba yalilipwa kwa mkandarasi. Wakati wa mapitio yangu kwenye mchakato wa ununuzi wa zabuni hiyo na utekelezaji halisi wa mkataba, nilibaini mapungufu yafuatayo.

**(a) Kiasi cha fedha kilichonukuliwa kwenye mkataba kilizidi kwa asilimia 94 gharama iliyokadiriwa na mshauri elekezi**

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa, wakati thamani ya mkataba iliyokadiriwa na mshauri elekezi, Kampuni ya M/S Aru Built Environment Consulting Company Ltd. mwezi Mei 2021 ilikuwa Sh. bilioni 5.59, kiasi halisi kilichonukuliwa kwenye mkataba kilikuwa Sh. bilioni 11.57. Hii inamaanisha kuwa thamani ya mradi huu ilizidi kiasi kilichokadiriwa na mshauri elekezi kwa Sh. bilioni 5.98 (sawa na asilimia 94). Hakukuwa na sababu iliyotolewa kwa ongezeko hilo. Hali hii ni kinyume na Kanuni ya 69 (3)(7) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inayotaka taasisi nunuzi kukadiria kwa usahihi mahitaji yao ya bidhaa, huduma, na kazi, sambamba na huduma au shughuli zilizoainishwa katika mpango-kazi na makadirio ya bajeti ya mwaka.

**(b) Mradi wa ukarabati haukujumuishwa katika mpango wa ununuzi wa mwaka**

Nilibaini kuwa kazi za ukarabati wa jengo la zamani la Ubalози wa Tanzania Washington, DC lililopo Barabara ya 2139 Mtaa wa R, NW Washington, DC 20008 Marekani hazikujumuisha kwenye bajeti iliyoidhinishwa wala Mpango wa Ununuzi wa kila Mwaka kwa Miaka 2022/2023 - 2023/2024, kinyume na Kanuni ya 75(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za 2013 inayotaka taasisi nunuzi kuhakikisha fedha zinatengwa kabla ya kuanza kwa mchakato wa ununuzi.

**(c) Kujumuishwa kwenye mkataba gharama za usimamizi dola za Marekani 357,428.58**

Kifungu cha 45.2 cha Masharti ya Jumla ya Mikataba kinataka makadirio ya gharama za kazi (bill of quantities) kutumika kupata gharama za mkataba, na mkandarasi alipwe kwa kiasi cha kazi iliyofanyika kulingana na kiwango kilichoorodheshwa katika makadirio ya gharama za kazi kwa kila kipengele.

Nilibaini kuwa gharama za usimamizi wa mradi kiasi cha dola za Marekani 357,428.58 zilijumuishwa katika makadirio ya gharama za kazi hivyo kuongeza gharama za mkataba wakati gharama hizo zilikuwa za Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ambayo iliingia mkataba Na. ME-013/2020/2021/HQ/C/10 wenye thamani ya Sh. milioni 381.65 na Kampuni ya Ushauri ya M/S Aru Built Environment Consulting Company Limited (mshauri elekezi) kwa ajili ya utoaji wa huduma za ushauri elekezi ikiwa pamoja na usimamizi wa kazi za mradi huo.

**(d) Ada za Mamlaka ya Serikali za Mitaa kujumuishwa mara mbili katika makadirio ya gharama ya kazi**

Makadirio ya gharama ya kazi yalijumuisha dola za Marekani 522,000 kama gharama za kibali cha ujenzi, kuthibitisha michoro kulingana na kanuni za ujenzi, na ukaguzi wote uliohitajika. Kiasi hiki kinalipwa kwa Mamlaka ya Wilaya ya Kolombia (Consumer and Regulatory Affairs).

Ukaguzi wangu ulibaini kwamba dola za Marekani 170,204.07 zilijumuishwa katika muhtasari wa jumla wa makadirio ya gharama za kazi kama gharama za usajili na ada zote za mamlaka za serikali za mitaa. Hali hii inaonesha gharama hizi za usajili na vibali kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa (Consumer and Regulatory Affairs) ziliwekwa mara mbili, kwani tayari zilishajumuishwa kwenye gharama za jumla za kazi.

**(e) Malipo ya kodi ya ongezeko la thamani yasiyokuwa na maelezo kamili**

Ukaguzi wangu wa makadirio ya gharama za kazi yalibaini kwamba kiasi cha mkataba kilichonukuliwa kilijumuisha asilimia 20 ya kodi ya ongezeko la thamani. Aidha, tarehe 13 Machi 2023, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilimlipa mkandarasi malipo ya awali ya thamani ya Sh. milioni 923.95 kupitia Hati ya Malipo Na. E2003700V2400008. Malipo hayo yalijumuisha asilimia 20 ya kodi ya ongezeko la thamani ya jumla ya Sh. milioni 153.99. Malipo ya kodi ya ongezeko la thamani ya asilimia 20 yaliyolipwa yalikuwa hayaeleweki kwani hakukuwa na kifungu katika mkataba kilichoelezea malipo hayo. Vilevile, kiwango cha asilimia 20 cha kodi ya ongezeko la thamani kilichonukuliwa kwenye mkataba ni tofauti na kiwango cha kodi ya ongezeko la thamani katika Mji wa Washington, ambacho ni asilimia 6. Hivyo, kiwango hiki cha ongezeko la thamani kilikuwa kikubwa hivyo kukosa uhalisia. Kuna uwekezako fedha za Serikali kutumika vibaya kwa malipo haya ya kodi ya ongezeko la thamani yanayolipwa kwa mkandarasi.

**(f) Kuchelewa kumlipa mkandarasi**

Kifungu cha 50 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kinataka mkandarasi kumpa meneja wa mradi taarifa za makadirio ya kazi kila mwezi. Meneja wa mradi atazikagua taarifa na kuruhusu malipo kulipwa, zoezi ambalo huchukua siku 28. Mwakiri pia hupatiwa siku 28 kuhakikisha malipo ya madai ya mkandarasi yanalipwa. Kucheleweshwa kwa malipo kutahusisha riba inayohesabiwa kutoka tarehe ya mwisho ya malipo yalipotakiwa kulipwa hadi tarehe ya kulipwa kwa kiwango cha riba kinachotolewa na Benki Kuu ya Tanzania kama kilivyokuwa siku ya kusainiwa kwa mkataba tarehe 12 Oktoba 2022.



Mapitio yangu ya mawasiliano kati ya Mkandarasi na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki yalibaini kuwa Mkandarasi aliwasilisha madai ya malipo ya awali na hati za madai mbili. Kumbukumbu za malipo zinaonesha kuwa malipo ya awali yaliyolipwa yalicheleweshwa kwa siku 88 ambayo yanaweza kuongeza siku za utekelezaji mradi. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe ya ukaguzi wangu mwezi Novemba 2023, hati za madai Na. 1 na 2 zilizotolewa tarehe 15 Machi 2023 na tarehe 5 Mei 2023 mtawalia zilikuwa hazijalipwa, hivyo kusababisha kucheleweshwa kwa siku 253 na siku 202 mtawalia.

**(g) Gharama ya dola za Marekani 418,790 kuongezeka pasipo kuidhinishwa** Kifungu cha 48 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kinamtaka mkandarasi kumpa meneja wa mradi ankara ya kutekeleza mabadiliko ya wigo wa kazi pale meneja wa mradi anapoomba.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki iliamua kubadilisha madirisha kwa gharama ya dola za Marekani 58,790 na lifti kwa dola za Marekani 360,000. Gharama za jumla ya marekebisho hayo zilifikia dola za Marekani 418,790. Hivyo, mkandarasi aliomba kiasi cha dola za Marekani 248,790 kwa kubadilisha madirisha na asilimia 50 ya malipo ya awali kwa kubadilisha lifti.

Hata hivyo, sikupeva ushahidi wa idhini ya ongezeko hili la gharama. Hali hii ilitokana na maofisa wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kutosimamia ipasavyo mradi huu. Ni maoni yangu kwamba Serikali inaweza kupata hasara pasipo kubaini.

**(h) Usimamizi usioridhisha wa mradi wa ukarabati**

Kifungu cha 5 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kinamtaka meneja wa mradi kusimamia utekelezaji wa mkataba. Mapitio yangu ya Kifungu cha 1.1 cha Masharti Maalumu ya Mkataba yalibaini kuwa Kampuni ya M/S ARU Built Environment Consulting Company Limited iliteuliwa kuwa msimamizi wa mradi. Hata hivyo, mkandarasi alikuwa akiwasiliana moja kwa moja na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki badala ya Kampuni ya M/S ARU Built Environment Consulting Company Limited ili kuthibitisha madai ya malipo ya mkandarasi.

**(i) Kusitishwa kwa kazi ya ukarabati**

Nilifanya ukaguzi wa mradi huu tarehe 19 Julai 2023 na 15 Novemba 2023 na nilibaini kuwa mkandarasi alikuwa amesimamisha utekelezaji wa kazi. Hata hivyo, sikupeva taarifa ya muda kamili ambao mkataba uliposimama na hali

halisi ya utekelezaji. Maofisa wa Ubaloji wa Tanzania Washington DC walinijulisha kwamba usitishaji wa kazi ulikusudia kupisha uchunguzi uliokuwa na lengo la kubaini iwapo mwajiri anaweza kukaa na mkandarasi kupitia upya gharama za mradi ambazo zilionekana ni za juu hivyo kukosa uhalisia. Uchunguzi huu ulianzishwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Ni maoni yangu kuwa, kusitisha kazi kunaweza kusababisha kuchelewesha utekelezaji wa mradi na hivyo kusababisha tozo ya riba ya ucheleweshaji.

**(j) Kuidhinishwa kwa Kampuni zilizochaguliwa bila kufanya tathmini ya uwezo wa kampuni hizo**

Kanuni ya 286 (5) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 (Gazeti la Serikali Na. 446) inataka taasisi nunuzi kufanya tathmini na kuandaa orodha ya zabuni zilizochaguliwa ambayo itaidhinishwa na bodi ya zabuni, ikijumuisha kampuni zenye sifa zinazotakiwa.

Nilikagua muhtasari wa kikao cha Bodi ya Zabuni ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kilichofanyika tarehe 16 Novemba 2020, ambacho kiliidhinisha majina yaliyochaguliwa ya kampuni za ushauri elekezi kwa usanifu na usimamizi wa kazi za ukarabati wa jengo la zamani la Ubaloji wa Tanzania, Washington. Ukaguzi wangu ulibaini kwamba hakukuwa na ripoti iliyowasilishwa na Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi kwenda kwa Bodi ya Zabuni kwa ajili ya idhini, ikionesha uwezo wa kampuni zilizochaguliwa kutekeleza jukumu hilo.

**Ninapendekeza Serikali, kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:**

- (a) ipitie makaridio ya gharama za kazi na kurekebisha gharama ya mkataba iliyonukuliwa;
- (b) meneja wa mradi asimamie ipasavyo mradi;
- (c) imlipe kwa wakati mkandarasi ili kuepuka adhabu na malipo ya riba;
- (d) izungumze na mkandarasi kuhusu changamoto za utekelezaji zilizojitokeza na kuhakikisha ukarabati unaendelea baada ya kurekebisha kasoro zilizobainika;
- (e) ichukue hatua za kinidhamu dhidi ya maofisa waliohusika katika maandalizi ya mkataba; na
- (f) kwa siku zijazo, mikataba yote inayotekelezwa nje ya nchi katika ofisi za ubalaji na vituo vya kibalaji iwatambue mabalaji wa sehemu husika kama sehemu ya mikataba kwa utekelezaji na uratibu wa miradi, tofauti na mazoea ya sasa ambapo mikataba haiwatambui.

## 7.5 Matokeo ya Ukaguzi Maalumu Uliofanyika katika Wizara ya Afya kuhusu Ununuzi na Usambazaji wa Vifaatiba

Mwaka 2015, Serikali ya Tanzania ilianzisha mpango unaolenga kupunguza vifo vya wajawazito na watoto wachanga katika jamii kwa kuwekeza na kuboresha upatikanaji wa huduma za kibingwa za uzazi (CEmONC). Hata hivyo, Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo wa mfuko wa afya, zilitenga fedha kuanzia mwaka 2017 hadi 2023 kwa ajili ya kununua vifaa muhimu vya CEmONC kwa ajili ya uboreshaji wa huduma za afya na kusambaza vifaatiba kwa vituo vya afya kote nchini. Bohari Kuu ya Dawa ilipewa jukumu la kununua na kusambaza vifaatiba vya CEmONC kwa vituo vya afya 217 kwa ajili ya kutoa huduma hizo.

Katika mwaka wa fedha 2022/23, Wizara ya Afya ilinipa jukumu la kufanya ukaguzi maalumu katika kipindi cha kuanzia tarehe 1 Julai 2017 hadi tarehe 16 Machi 2023. Ukaguzi ulilenga kutathmini ununuzi, usambazaji, na ufanisi wa vifaatiba ndani ya mfumo wa CEmONC. Malengo ya msingi yalikuwa kubainisha iwapo vifaa viliakisi thamani ya fedha, kutambua sababu za ucheleweshaji wa ununuzi na usambazaji wa vifaatiba, kufuatilia mienendo ya fedha, na kutoa mapendekezo ya kuongeza ufanisi ili kuharakisha mafanikio ya malengo yaliyokusudiwa. Nimeelezea matokeo ya ukaguzi na kutoa mapendekezo kama ilivyoainishwa hapa chini.

### 7.5.1 Kutozingatia Kanuni na Taratibu za Ununuzi

Ukaguzi wangu wa taarifa za zabuni na mikataba kuhusiana na huduma za CEmONC ulibaini masuala yafuatayo ya ukiukaji wa sheria.

#### 7.5.1.1 Kumtoa kimakosa mzabuni mwenye bei ya chini kulikosababisha gharama ya ziada ya Sh. milioni 33.48

Kanuni ya 212(a) ya Kanuni za Ununuzi ya Umma za Mwaka 2013 inataka tuzo ya mkataba itolewe kwa mzabuni aliyefanyiwa tathmini na kuonekana ana bei ya chini zaidi kuliko wazabuni wengine.

Nilibaini kuwa Bohari Kuu ya Dawa ilinunua mashine 10 za kuondoa maumivu, ukakamavu na mkazo wa misuli (Diathermy) kwa njia ya kuitisha (Call-off order) kutoka Kampuni ya Medionics Healthcare LTD kwa bei ya Sh. milioni 136.7. Hata hivyo, mzabuni huyo Kampuni ya Medionics Healthcare Ltd hakuwa mzabuni

mwenye bei ndogo, ambapo tarehe 23 Juni 2017, kamati ya tathmini ilipendekeza zabuni kutolewa kwa Kampuni ya M/S Quayley Dental Manufacturing kwa bei ya Sh. milioni 103.2. Kwa sababu hiyo, mashine hizo zimenunuliwa kwa bei ya juu na kusababisha gharama ya ziada ambayo ingeweza kuepukika ya Sh. milioni 33.48.

**Ninapendekeza kuwa Serikali kupitia Bohari Kuu ya Madawa iimarishe udhibiti wa ndani wa tathmini ya zabuni na kuzingatia Kanuni ya 212(a) ya Kanuni za ununuzi ya Umma ya mwaka 2013 ili kuepusha ongezeko la gharama zisizo za lazima.**

#### **7.5.1.2 Maombi ya wauzaji 32 wa vifaatiba bila uthibitishaji wa awali na bila idhini ya bodi ya zabuni kwa zabuni zilizotolewa**

Kanuni ya 119 (c) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inaeleza kuwa uthibitishaji wa awali unaweza kutumiwa ikiwa orodha ya wazabuni wenye uwezo inahitajika kwa ajili ya kutoa zabuni. Zaidi ya hayo, Kanuni ya 148 ya Kanuni hizo inazitaka taasisi nunuzi kuzingatia uthibitishaji wa awali wa zabuni ili kubaini wazabuni ambao wana rasilimali muhimu na uwezo wa kukamilisha mikataba.

Tarehe 25 Machi 2021, bodi ya zabuni ya Bohari Kuu ya Dawa iliidhinisha ununuzi wa vifaatiba 18 kwa zabuni Na. 009/2020/2021/HQ/G/182 kutoka kwa watengenezaji moja kwa moja. Hata hivyo, kinyume na uamuzi huo, Bohari Kuu ya Dawa iliwaita wazabuni 24 kwa zabuni namba 009/2020/2021/HQ/G/153 na wazabuni 26 wa zabuni namba IE-009/2020/2021/HQ/G/182 kupitia utoaji wa nukuu za bei (quotations) bila kutumia njia ya uthibitishaji wa awali ili kusaidia uwekaji wa ukomo kwa wazabuni ambao ni watengenezaji au mawakala walioidhinishwa. Pia, nilibaini kuwa orodha ya wazabuni walioombwa kutoa mapendekezo ya bei haikuidhinishwa na bodi ya zabuni. Zabuni hizo zilitolewa kwa wazabuni mbalimbali kwa jumla ya Sh. bilioni 4.14 (dola za Marekani 1,784,422.10).

Pia, nilibaini hali hiyo ya kuomba ankara kifani za bei kutoka kwa wazabuni ilisababisha wazabuni 20 wa zabuni namba 009/2020/2021/HQ/G/153 na 14 kwa zabuni namba IE-009/2020/2021/HQ/G/182 kutowasilisha bei zao. Zaidi ya hayo, hakukuwa na ushahidi kuwa wazabuni wote walioitwa walikuwa watengenezaji au mawakala walioidhinishwa. Kwa mfano, muuzaji mmoja, ambaye ni Kampuni ya S.H. Industrials alitwa kushiriki katika zabuni namba 009/2020/2021/HQ/G/153 na alijibu kwa kusema kuwa hashughuliki na usambazaji wa vifaa vya matibabu.

Kuita wauzaji bila uthibitisho wa awali na bila idhini kutoka bodi ya zabuni kunaathiri ushindani, hivyo kukosekana kwa thamani ya fedha, na kuzuia kupatikana kwa bei nafuu zaidi za vifaa.

**Ninapendekeza kuwa Serikali kupitia Bohari Kuu ya Madawa iimarishe udhibiti wa ndani wa uthibitishaji wa awali na uidhinishaji wa wazalishaji walioteuliwa kabla ya kushindanishwa.**

### **7.5.1.3 Kupokelewa kwa maombi ya zabuni 4 baada ya muda wa kupokea maombi ya zabuni kufungwa**

Kanuni ya 196 (2, 3) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inataka muda wa ufunguzi wa zabuni uwe sawa na muda uliowekwa wa tarehe ya mwisho ya kupokea zabuni na zabuni zote zilizowasilishwa kabla ya tarehe ya mwisho ya kuwasilisha zitafunguliwa hadharani, mbele ya wazabuni au wawakilishi wao au kwa yoyote mwenye maslahi halali katika taratibu za zabuni. Majina ya wote waliokuwapo kwenye ufunguzi wa zabuni na wanaowakilisha yataandikwa na katibu wa bodi ya ufunguaji wa zabuni husika.

Nilikagua mchakato wa tathmini ya zabuni Na. IE-009/2020/2021/HQ/G/182 na kubaini tofauti katika tarehe ya mwisho ya uwasilishaji wa zabuni ambayo ni 1 Septemba 2021 saa 8:00 mchana. Hata hivyo, ilibainika kuwa wazabuni watatu, ambao ni Kampuni ya Shandong Horse International Co, Kampuni ya Norfolk International Ltd, na Kampuni ya Shenzhen Anglcell Technology Co. Ltd walichelewa kuwasilisha zabuni zao. Anwani ya baruapepe ilionesha kuwa mawasilisho ya zabuni kwa wazabuni hao ni saa 9:01 mchana, saa 9:56 mchana, na saa 10:53 jioni mtawalia. Licha ya kuchelewa kuwasilisha zabuni, Bohari Kuu ya Dawa ilifungua zabuni hizo na kuendelea na mchakato wa ununuzi, na ikabainika kuwa Kampuni ya Shandong Horse International Co., ambayo ni miongoni mwa wazabuni waliochelewesha kuwasilisha zabuni, ilishinda na kupewa zabuni ya kusambaza mashine ya kufulia yenye uzito wa kilo 25 kwa bei ya Sh. milioni 15.59.

Aidha, nilibaini kuwa barua ya wito wa zabuni Na. IE-009/2020/2021/HQ/G/153 ya tarehe 21 Mei 2021 iliwataka wazabuni kuwasilisha zabuni zao kabla au tarehe 28 Mei 2021. Hata hivyo, Bohari Kuu ya Dawa ilimpatia zabuni mzabuni Kampuni ya Medical Equipment Limited, ambaye aliwasilisha zabuni husika tarehe 2 Juni 2021, siku nne zaidi ya muda uliowekwa. Zabuni iliyotolewa ni ya usambazaji wa vifaatiba vyenye thamani ya dola za Marekani 381,455 (sawa na Sh. milioni 881.13 kwa kiwango cha ubadilishaji kilichotumika wakati wa tathmini). Pia, nilibaini kuwa zabuni hii haikufunguliwa hadharani kinyume na

Kanuni ya 196 (3) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inayomtaka katibu wa bodi ya zabuni kuitisha na kuongoza kikao cha kufungua zabuni.

Kukubalika kwa zabuni zilizochelewa kuwasilishwa kunaashiria upendeleo kwa wazabuni wachache, na ukiukaji wa kanuni za haki, uwazi na uwajibikaji ambazo ni muhimu kwa utendaji mzuri na wa maadili wakati wa ununuzi.

**Ninapendekeza kwamba, katika siku zijazo, Bohari Kuu ya Madawa ihakikishe maombi ya zabuni yanapokelewa ndani ya muda ulioainishwa kwenye nyaraka za zabuni.**

#### **7.5.1.4 Muda mfupi waliopewa wazabuni kwa ajili ya utayarishaji na uwasilishaji wa nyaraka za zabuni na kutotumia mfumo wa kielektroniki wa ununuzi**

Jedwali la 8 la Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inatoa muda wa chini kabisa wa kuandaa na kuwasilisha zabuni, ambapo kwa ununuzi wa kimataifa, muda unapaswa usiwe chini ya siku 8.

Tarehe 21 Mei 2021, Bohari Kuu ya Dawa ilitayarisha barua ya wito wa wazabuni 24 kwa ajili ya zabuni Na. IE-009/2020/2021/HQ/G/153. Hata hivyo, nilibaini kuwa muda mfupi ulitolewa kwa wazabuni, kwani barua za wito zilitumwa kwa wazabuni tarehe 24 Mei 2021, na wazabuni walitakiwa kuwasilisha zabuni zao kabla au tarehe 28 Mei 2021, siku 4 tu tangu tarehe ya wito wa zabuni.

Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa mchakato wa ununuzi wa zabuni Na. IE-009/2020/2021/HQ/G/182 na Na. IE-009/2020/2021/HQ/G/153 haukuchakatwa kwa kielektroni kinyume na Kanuni ya 342 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 kama ilivyorekebishwa mwaka 2016.

Muda mfupi wa utayarishaji na uwasilishaji wa zabuni huzuia wazabuni kushiriki mchakato wa ununuzi, hivyo kupunguza ushindani na uwezo wa taasisi nunuzi kupata vifaa kwa bei nafuu zaidi. Pia, kushindwa kutumia mfumo wa kielektroniki wa ununuzi huathiri uwazi na haki katika michakato ya ununuzi wa umma.

**Ninapendekeza kuwa Bohari Kuu ya Madawa ihakikishe mchakato wa mwaliko, uwasilishaji na ufunguzi wa zabuni unafanywa ipasavyo kupitia mfumo wa kielektroniki kama inavyotakiwa na sheria na kanuni za ununuzi.**

#### **7.5.1.5 Mikataba ya thamani ya Sh. bilioni 4.22 ambayo haikupekuliwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

Nilibaini kuwa Bohari Kuu ya Dawa iliingia mkataba Na. IE-009 /2020/21/HQ/G/153/02 kwa bei ya dola za Marekani 716,110 (Sh. bilioni 1.64) ikijumuisha gharama za vifaa vya CEmONC vya thamani ya dola za Marekani 472,601 (Sh. bilioni 1.08).

Hata hivyo, mkataba huo ulitekelezwa bila kufanyiwa uhakiki na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kinyume na Kanuni ya 59(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 zilizofanyiwa marekebisho na Kanuni ya 2 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2016 (T.S. Na 121 lililochapishwa tarehe 22 Aprili 2016) inayotaka mkataba wenye thamani inayozidi Sh. bilioni 1 kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili uhakikiwe. Kutohakikiwa mikataba ya namna hii kunaweza kusababisha madhara hasi iwapo kutatokea migogoro.

**Ninapendekeza kuwa Bohari Kuu ya Madawa ihakikishe mikataba yote inayozidi Sh. bilioni moja inapekuliwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuepusha hatari za kimkataba.**

#### **7.5.2 Ununuzi usioridhisha wa vifaatiba na ukosefu wa ufanisi katika zoezi la usambazaji**

Mapitio yangu ya zabuni zinazohusiana na ununuzi na usambazaji wa vifaatiba vya CEmONC na uhakiki niliufanya ulibaini upungufu unaofafanuliwa hapa chini.

##### **7.5.2.1 Bohari Kuu ya Dawa kutokamilisha ununuzi wa vifaatiba**

Aya ya 9 (a) ya Mkataba wa Huduma kwa Mteja ya Bohari Kuu ya Dawa wa Mwaka 2017-2020 inataka mchakato wa oda maalumu ya vifaa kwa vituo vya huduma za afya kuchukua angalau miezi miwili tangu tarehe ya kuagiza. Pia, Aya ya 10.1 ya mkataba huo inataka upatikanaji wa vifaatiba kwa bei ya chini, upatikanaji huo uendane na mahitaji ya mteja kama alivyoomba, na mchakato wa ununuzi maalumu kuchukua muda wa miezi mitatu tangu mteja alivyolipia oda hadi mahitaji yanatimizwa.

Mpango wa usambazaji wa vifaa vya CEmONC ulianza mwaka wa fedha 2017/2018. Nilipitia ripoti ya utekelezaji ya Bohari Kuu ya Dawa yenye Kumb. Na. EB.169/225/01B/49 ya tarehe 16 Machi 2023 na ripoti za mauzo ya mfumo wa EPICOR kwa vifaatiba vya CEmONC vilivyosambazwa kwenye vituo vya huduma za afya na kubaini kuwa Bohari Kuu ya Dawa ilishirikishwa kwenye

ununuzi na usambazaji wa vifaatiba 295 katika vituo 217 vya huduma ya afya. Hata hivyo, hadi mwezi Machi 2023, ni vifaatiba 213 tu vyenye thamani ya Sh. bilioni 57.53 ndivyo vilinunuliwa na kusambazwa kwenye vituo vya afya na kuacha vifaatiba 82 vyenye thamani inayokadiriwa kuwa Sh. bilioni 13.37 vikiwa ununuzi wake haujaanza.

Menejimenti ilieleza kuwa ugonjwa virusi vya korona (UVIKO-19) ndio sababu kuu ya ucheleweshaji huo wa ununuzi. Hata hivyo, kwa maoni yangu, ucheleweshaji unaoendelea unazuia kukamilika kwa utekelezaji wa CEmONC na kusababisha ucheleweshaji wa ufikiaji wa malengo yaliyokusudiwa.

**Ninapendekeza kuwa Serikali kupitia Wizara ya Afya, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Bohari Kuu ya Madawa ziingie katika makubaliano ya kukamilisha ununuzi wa vifaatiba ambavyo havijakamilika na kuvisambaza kwenye vituo vya kutolea huduma za afya bila kuchelewa zaidi.**

#### **7.5.2.2 Vifaa vya CEmONC vilivyogawiwa kwenye vituo vya huduma za afya visivyostahili**

Kanuni ya 242 ya Kanuni za Fedha za Bohari Kuu ya Dawa za mwaka 2011 inataka fedha zitumike kwa madhumuni ambayo msaada umetolewa, matumizi yatakuwa ndani ya bajeti iliyotolewa kwa kila kundi katika makubaliano ya ruzuku au mikopo, na uhamishaji wa fedha hautafanywa hadi uidhinishwe na mfadhili.

Nilibaini kuwa kati ya vifaatiba 213 vyenye thamani ya Sh. bilioni 57.53 vilivyoununuliwa na kusambazwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, vifaatiba vya thamani ya Sh. bilioni 4.34 vilinunuliwa na kugawiwa katika vituo 3886, ambavyo havikuwa kwenye lengo. Kati ya vifaatiba hivyo, Sh. bilioni 2.70 ni vifaatiba vya kutolea huduma ambavyo vilinunuliwa na kusambazwa katika vituo vya afya visivyolengwa kufuatia maelekezo yaliyotolewa na Wizara ya Afya kupitia barua yenye Kumb. Na. WAMJW/JUM/02 ya tarehe 27 Desemba 2018 na GA.222/558. /01/10. Maagizo haya yaliruhusu ununuzi wa vifaatiba nje ya vilivyoorodheshwa katika jedwali la mahitaji.

Uchepushaji huu wa fedha kwa ajili ya vituo vya afya ambavyo havijalengwa umeathiri utekelezaji wa ununuzi na usambazaji wa vifaatiba kwa vituo 217 vilivyolengwa na mradi.



Ninapendekeza kwamba katika siku zijazo, Serikali kupitia Wizara ya Afya, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Bohari Kuu ya Madawa zihakikishe kuwa shughuli tarajiwa zinatekelezwa kama ilivyokusudiwa na wadau na pale ambapo mabadiliko hayaepukiki basi ni lazima idhini ipatikanane kabla ya utekelezaji.

#### 7.5.2.3 Kutolingana kwa namba za utambulisho za mashine zilizotolewa kwenye vituo vya huduma za afya

Ziara yangu katika vituo vya huduma za afya ilibaini kuwa namba za utambulisho katika ripoti ya mauzo ya Bohari Kuu ya Dawa kwa mashine 23 hazikufanana na namba halisi za mashine zilizofikishwa katika vituo vya huduma za afya. Pia, nilibaini upungufu katika kurekodi taarifa za namba za utambulisho wa vifaatiba vilivyowasilishwa kwenye vituo vya afya.

Kutowiana kwa namba za utambulisho kati ya vifaa hivyo na rekodi husababisha ugumu katika kufuatilia bidhaa zilizowasilishwa na kunaweza kuibua migogoro kwa masuala yanayohusiana na matengenezo na vibali katika kipindi cha matazamio ya kasoro.

Ninapendekeza kwamba Serikali kupitia Bohari Kuu ya Madawa iharakishe ulinganifu wa namba za utambulisho katika ripoti ya mauzo na namba halisi za mashine zilizofikishwa katika vituo vya huduma za afya.

#### 7.5.2.4 Kusambazwa kwa vifaa vya CEmONC kwenye vituo vya afya ambavyo havikuwamo kwenye jedwali la mahitaji

Ulinganisho uliofanywa kati ya jedwali la mahitaji na bidhaa halisi zilionunuliwa katika vituo vitano vya afya, ulibaini kuwapo kwa bidhaa 15 zenye thamani ya Sh. milioni 79.97 zilionunuliwa na Bohari Kuu ya Dawa, ambazo hazikuwapo kwenye jedwali la mahitaji. Aidha, ilibainika kuwa bidhaa hizo zilionunuliwa kufuatia maelekezo yaliyotolewa na Wizara ya Afya kupitia barua yenye kumbukumbu Na WAMJW/JUM/02 ya tarehe 27 Desemba 2018 na GA.222/558/01/10 ya 14. Barua hiyo ilielekeza kuwa jumla ya Sh. bilioni 2.70 zitatumika kununua na kusambaza vifaa vya Kujifungulia kwenye Mikoa yenye viwango vya chini vya uhudhuriaji wa kliniki na vituo vya afya yenye viwango vidogo vya kujifungulia watoto. Maelezo yameoneshwa kwenye Jedwali Na. 32.

**Jedwali Na. 32: Vituo vya Afya Vilivyopokea Vifaatiba ambavyo Havikuwamo kwenye Jedwali la Mahitaji**

Na.	Jina la Kituo	Namba za Vifaa	Kiasi (Sh.)
1.	Mjesani	2	30,663,600

Na.	Jina la Kituo	Namba za Vifaa	Kiasi (Sh.)
2.	Songe	2	26,408,874
3.	Mauno	5	17,921,860
4.	Bahi	4	4,740,100
5.	Bereko	2	243,400
	<b>Jumla</b>		<b>79,977,834</b>

Chanzo: Uhakiki wakati wa ukaguzi

Ubadilishaji huu wa vifaatiba kinyume na jedwali la mahitaji unaathiri malengo ya usambazaji uliokusudiwa wa vifaatiba.

Ninapendekeza kwamba katika siku zijazo, Wizara ya Afya izingatie jedwali la mahitaji katika kusambaza vifaatiba na ikiwa kuna mabadiliko ambayo hayawezi kuepukika, uidhinishaji sahihi wa kimaandishi kabla ya kufanya uamuzi wowote unaokiuka malengo yaliyokusudiwa unapaswa kuwepo.

#### 7.5.2.5 Vifaatiba vya CEmONC vilivyofikishwa kwenye vituo vya afya lakini havitumiki

Uhakiki wangu niliofanya katika vituo 23 vya afya kati ya tarehe 10 hadi 18 Aprili 2023 ulibaini kuwa vituo vya afya 21 vilipokea vifaatiba vya CEmONC vyenye thamani ya Sh. bilioni 1.68, ambavyo vilikuwa havijaanza kutumika.

Nilibaini kuwa vifaa hivyo havikutumika kutokana na kukosekana kwa wataalamu maalumu kama vile radiografa, miundombinu isiyoridhisha ya kwa ajili ya vifaatiba vya CEmONC kama vile ukosefu wa umeme wa njia tatu, kutokamilika kwa majengo, ufinyu wa nafasi ya kuweka vifaatiba, ukosefu wa mafunzo ya kutosha kwa watumishi, na upungufu wa vitendanishi. Majina ya vituo vya afya vilivyopokea vifaatiba na kiasi cha vifaatiba hivyo, ambavyo havitumiki inaoneshwa kwenye **Jedwali Na. 33**.

#### Jedwali Na. 33: Vituo vya Afya Vilivyopokea Vifaatiba na Kiasi cha Vifaatiba

Na.	Kituo	Idadi	Kiasi (Sh.)
1.	Karema	4	16,649,400
2.	Ipwaga	10	20,541,000
3.	Nyakahura	25	64,350,000
4.	Nyakitonto	4	<b>155,194,370</b>
5.	Kayanga	3	<b>132,782,900</b>
6.	Karume	4	171,048,870
7.	Kahangara	4	134,818,400
8.	Bahi	5	695,384,940
9.	Bereko	2	23,874,808
10.	Buguruni	2	119,657,300
11.	Daudi	2	22,712,900

Na.	Kituo	Idadi	Kiasi (Sh.)
12.	Endabash	2	4,211,248
13.	Mauno	3	50,683,573
14.	Mjesani	7	253,996,595
15.	Pwaga	5	1,865,906,304
16.	Nduruma	5	60,796,670
17.	Songe	2	137,452,508
18.	Tlawi	5	176,464,970
19.	Zogolo	1	3,918,700
20.	Uyowa (Songambebe) (Kaliua Dc)	11	12,727,760
21.	Makonge	11	5,921,400
	<b>Jumla</b>	<b>117</b>	<b>4,129,094,616</b>

Chanzo: Uhakiki wakati wa ukaguzi

Thamani ya fedha na faida iliyokusudiwa kutokana na vifaa vilivyoununuliwa vyenye thamani ya Sh. bilioni 1.68 bado haijapatikana.

Ninapendekeza kuwa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ihakikishe kuwa vifaatiba vilivyoununuliwa kwa ajili ya afua ya CEmONC vinatumika kwa kukamilisha miundombinu inayohitajika pamoja na kutoa mafunzo kwa watumishi ipasavyo.

#### 7.5.2.6 Vifaatiba ambavyo kwa awamu ya kwanza ya CEmONC vilisambazwa zaidi ya mahitaji

Nilibaini kuwa vifaatiba 76 vya awamu ya kwanza ya CEmONC vyenye thamani ya Sh. milioni 417.99 vilisambazwa kwenye vituo 46 vya kutolea huduma za afya zaidi ya mahitaji yaliyoainishwa. Uhakiki wa uwasilishaji wa Bohari Kuu ya Dawa ulithibitisha usambazaji huu wa zaidi ya mahitaji kama ilivyooneshwa katika Jedwali Na. 34.

Jedwali Na. 34: Vifaa Vilivyosambazwa zaidi ya Mahitaji

Na.	Jina la Kifaatiba	Idadi ya Vituo vya Afya	Idadi Iliyoongezeka	Thamani (Sh.)
1.	Laparotomy Set - Superior Quality with Self-Sterilization Tray	4	17	150,152,500
2.	Mobile Anesthesia Gas Machine (Mobile Ventilator) Machine	2	2	104,675,800
3.	Portable ultrasound Machine	4	4	58,337,200
4.	Mortuary Cabinet (Six Bodies)	1	1	29,727,500

Na.	Jina la Kifaatiba	Idadi ya Vituo vya Afya	Idadi Iliyongezeka	Thamani (Sh.)
5.	Centrifuge (For 8X15 MLS Tubes) Electrically Operated	8	10	27,555,200
6.	Autoclave 100 litres, Electrical and gas heated or Autoclave 63 litres	5	5	18,999,000
7.	Haemocue Blood Hemoglobin (Hemocue Hb201+) Photometer	3	3	7,061,700
8.	Operating light	1	1	6,057,800
9.	Drip Stand Double-Hook ADJ to 2.5 M Height	4	16	5,972,800
10.	Examination Lamp Light	9	11	4,616,000
11.	Linen Trolley	4	5	3,297,500
12.	Nebulizer Pump Machine	1	1	1,539,400
			<b>Total</b>	<b>417,992,400</b>

**Chanzo:** Nyaraka za Kusambaza Vifaa

Usambazaji wa vifaatiba vya CEmONC zaidi ya mahitaji umesababisha matumizi makubwa ya fedha za mradi.

**Ninapendekeza kuwa Bohari Kuu ya Madawa ihakikishe vifaatiba vilivyounuliwa kwa ajili ya afua ya CEmONC vinasambazwa kwa kuzingatia mahitaji yaliyoainishwa ili kuepuka matumizi mabaya ya fedha za mradi na kufikia lengo lililokusudiwa la kutekeleza afua ya CEmONC.**

#### **7.5.2.7 Makosa ambayo hayakusuluhishwa ya Sh. milioni 145.36 katika taarifa za mauzo za Bohari Kuu ya Dawa**

Nilifanya usuluhishi kati ya ripoti za mauzo ya Bohari Kuu ya Dawa na uthibitisho wa upelekaji wa vifaa kwenye vituo vitano vya huduma za afya nilivyovitembelea na nilibaini makosa katika ripoti hiyo kwa kuwa vifaatiba vyenye thamani ya Sh. milioni 145.36 viliripotiwa kuwasilishwa katika vituo vya afya husika kwa mujibu wa ripoti ya mauzo. Hata hivyo, sikuweza kuthibitisha ushahidi wa vifaa hivyo kuwasilishwa kwenye vituo hivyo. **Jedwali Na. 35** linaonesha majina ya vituo vya huduma za afya vilivyodaiwa kupokea vifaatiba lakini hakukuwa na ushahidi wa uwasilishaji wake.

**Jedwali Na. 35: Tofauti kati ya Ripoti za Mauzo za Bohari Kuu ya Dawa na Uwasilishaji Halisi**

Na.	Kituo	Idadi	Kiasi (Sh.)
1.	Karema	2	1,649,600
2.	Ipwaga	2	3,545,600
3.	Rungwe Mpya	1	329,200
4.	Mauno	1	58,337,900
5.	Pwaga	2	81,506,500
<b>Jumla</b>			<b>145,368,800</b>

**Chanzo:** Ripoti ya Mauzo ya Bohari Kuu ya Dawa na Taarifa ya Uwasilishaji katika Vituo vya Afya

Hitilafu ambazo hazijasuluhishwa katika ripoti za mauzo za Bohari Kuu ya Dawa hupotosha watumiaji kwa kuonesha kuwa vifaatiba vimewasilishwa ilhali havijawasilishwa.

Ninapendekeza kwamba Bohari Kuu ya Madawa irekebishe mapungufu yaliyobainika katika Mfumo wa EPICOR na kuwasilisha bidhaa ambazo hazijawasilishwa.

### 7.5.3 Ucheleweshaji wa Ununuzi na Usambazaji wa Vifaatiba katika Vituo vya Afya

Mapitio yangu ya nyaraka za ununuzi na usambazaji wa vifaatiba katika vituo vya afya yalibaini ucheleweshaji kutoka siku 23 hadi 1,458. Ulinganishi huu ulifanywa kati ya tarehe ya kutolewa kwa fedha Bohari Kuu ya Dawa na tarehe ya utoaji wa vifaatiba katika vituo vya afya. Ucheleweshaji huu ulihusishwa na upungufu ufuatao:

#### 7.5.3.1 Kukinzana kwa maelekezo ya utoaji fedha na kuchelewa kuanza kwa utekelezaji wa awamu ya kwanza

Aya ya pili ya Usimamizi wa Oda Maalumu ya Bohari Kuu ya Dawa ya mwaka 2015 inaeleza utaratibu wa wateja kuanzisha oda. Wateja waliagizwa kuwasilisha mahitaji yao Bohari Kuu ya Dawa wakielezea kwa kina taarifa za bidhaa zinazohitajika. Bohari Kuu ya Dawa itachukuwa jukumu la kutafuta mzabuni, kupata bei, kukokotoa gharama, na kuweka ukomo ili kubaini bei ya soko. Mara tu wateja wanapothibitisha oda, wanatakiwa kufanya malipo. Baadaye, Bohari Kuu ya Dawa hununua bidhaa kwa niaba ya wateja, kuzifunga, kutoa mafunzo, na kuruhusu kuanza kutumika.

Kinyume chake, nilibaini taarifa zinazokinzana kuhusu kiasi kilichowekwa kwa ajili ya utekelezaji wa awamu ya kwanza ambayo inahusisha vituo 44 vya huduma za afya. Ripoti ya maridhiano ya Bohari Kuu ya Dawa kuhusu CEmONC ilionesha kiasi cha fedha kilichowekwa kwa ajili ya utekelezaji katika vituo vya afya 44 ni Sh. bilioni 8.64. Hata hivyo, maagizo yaliyotolewa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa Bohari Kuu ya Dawa yenye Kumb. Na. AH. Na. 161/164.02/85 ya tarehe 24 Septemba 2018 yalitaka Bohari Kuu ya Dawa kutumia Sh. bilioni 5.70 kwa vituo vya afya 44 kwa awamu ya kwanza. Uelekezaji upya huu ulichelewesha kuanza kwa utekelezaji wa huduma za CEmONC. Aidha, ilibainika kuwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI iliwasilisha Bohari Kuu ya Dawa orodha ya wanufaika na mahitaji ya awamu ya kwanza kupitia barua yenye Kumb. Na. CB.161/227/01 ya tarehe 26 Januari 2018 bila kuchambua gharama za bidhaa zitakazonunuliwa pamoja na muda wa utekelezaji wa awamu ya kwanza.

Zaidi ya hayo, nilibaini ucheleweshaji wa utoaji wa fedha Bohari Kuu ya Dawa kwa awamu ya kwanza, jambo lililokwamisha utekelezaji wa shughuli hizo. Muda kati ya awamu ya kwanza na awamu ya mwisho ya utoaji wa fedha za awamu ya kwanza ulikuwa miezi 8. Ofisi ya Rais - TAMISEMI iliweka Sh. bilioni 8.64 Bohari Kuu ya Dawa kwa awamu nne kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 36.**

**Jedwali Na. 36: Uchambuzi wa Fedha Zilizopokelewa Bohari Kuu ya Dawa**

Awamu	Tarehe ya Kuweka Fedha	Kiasi (Sh.)
1.	19 Oktoba 2017	5,000,000,000
2.	05 Mei 2018	440,000,000
3.	18 Juni 2018	2,500,000,000
4.	26 Juni 2018	700,000,000
<b>Jumla</b>		<b>8,640,000,000</b>

**Chanzo:** Taarifa ya Benki

Taarifa zinazokinzana na kuchelewa kwa utoaji wa fedha kwenda Bohari Kuu ya Dawa kwa awamu ya kwanza kumesabibisha huduma za CEmONC kutotekelezwa kwa wakati.

**Ninapendekeza kwamba Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Afya kuhakikisha:-**

- kuweka makubaliano ya muda wa kukamilisha shughuli zote za ununuzi na usambazaji wa vifaatiba katika awamu zote;
- kutoa fedha na maelekezo sahihi ya ununuzi wa vifaatiba kwa wakati kwa Bohari Kuu ya Madawa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli hizo; na

- (c) utekelezaji wa shughuli za ununuzi na usambazi wa vifaatiba unazingatia vipengee vilivyokubaliwa, gharama na muda wa utekelezaji.

### 7.5.3.2 Makadirio yasiyotosheleza na kutofautiana katika utekelezaji wa miradi

Kanuni Na. 69 (3) na (4) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inazitaka taasisi nunuzi kukisia mahitaji yake ya bidhaa, huduma, na ujenzi kwa usahihi kadiri iwezekanavyo, kwa kuzingatia huduma au shughuli ambazo tayari zimeratibiwa katika mpangokazi wa mwaka na kujumuishwa katika makadirio ya kila mwaka. Makisio yajumuishe makadirio ya muda muafaka kwa mwezi wa karibu wa utendaji kazi na kukamilika kwa huduma.

Nilibaini kuwa kutokana na makadirio yasiyoridhisha na kutofautiana katika utekelezaji, Wizara ya Afya iliweka Sh. bilioni 29.92 Bohari Kuu ya Dawa kwa awamu ya pili na ilitumia Sh. bilioni 22.10 na ilikuwa na deni la Sh. bilioni 4.32. Hali hii ilisababisha malipo ya ziada ya Sh. bilioni 3.49 kutokana na makadirio yasiyo ya kweli ambayo baadaye yalielekezwa kwenye ununuzi wa vifungashio kwa mikoa yenye mahudhurio madogo ya kliniki na viwango vya chini vya kujifungua, shughuli ambayo haikuwa sehemu ya afua za CEMONC.

Zaidi ya hayo, nilibaini kuanzishwa kwa awamu ya tatu kwa vituo 66 vya kutolea huduma za afya kabla ya kufungwa kwa awamu ya kwanza na ya pili. Pia, awamu ya nne ilianzishwa kwa vituo 7 vya kutolea huduma za afya bila kufungwa kwa makubaliano kutoka awamu ya kwanza hadi awamu ya tatu, ikionesha ukosefu wa muda wa utekelezaji.

Kulikuwa na usimamizi duni wa afua za CEmONC, uliokuwa na sifa ya kutokamilika, awamu zinazolingiliana, na zinazoweza kufikiwa. Hali hii ilisababisha kuchelewa kwa utekelezaji wa shughuli zilizolengwa za CEmONC.

**Ninapendekeza kwamba Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zihakikishe:-**

- (a) katika siku zijazo, makadirio ya gharama yanafanywa kwa usahihi na kabla ya fedha kupelekwa Bohari Kuu ya Madawa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli iliyokusudiwa;
- (b) utekelezaji wa ununuzi na usambazaji unazingatia vifaatiba vilivyokuwa kwenye makubaliano, gharama, na muda uliopangwa na ikiwa mabadiliko ni hayaepukiki, idhini ya awali inapaswa kupatikana kutoka kwa mamlaka husika; na

- (c) katika siku zijazo, kuwa na mpango madhubuti wa kukamilisha awamu za awali kabla ya kuanzishwa kwa awamu inayofuata ili kuwa na usimamizi mzuri wa ununuzi na usambazaji wa vifaatiba.

#### 7.5.3.3 Utayari na tathmini ya uhitaji wa uingiliaji wa CEMONC kutofanywa ipasavyo

Kanuni Na. 69(3) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inazitaka taasisi nunuzi kukadiria kwa usahihi kadiri inavyowezekana mahitaji yake ya bidhaa kwa kuzingatia huduma au shughuli ambazo tayari zimeratibiwa katika mpangokazi wa mwaka na kujumuishwa katika makadirio ya mwaka.

Kinyume chake, nilibaini kuwa Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais - TAMISEMI ziliipa jukumu Bohari Kuu ya Dawa kununua na kusambaza vifaatiba kwa ajili ya CEmONC katika vituo 217 vya kutolea huduma za afya kati ya mwaka 2017/2018 na mwaka 2020/21 kwa awamu nne bila kufanya tathmini ya kutosha ya mahitaji. Hii ni kwa sababu nilibaini kuwa majengo yaliyokusudiwa hayakuwa yakijitosheleza au yamekamilika ili kuwezesha kufungwa kwa vifaa vilivyopokelewa.

Kutotumika kwa vifaa hivyo kumesababisha kushindwa kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**Ninapendekeza kwamba, katika siku zijazo, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ihakikishe kuwa kuna utayari wa kutosha na tathmini ya mahitaji kabla ya utekelezaji wa shughuli za ununuzi na usambazaji wa vifaatiba.**

#### 7.5.3.4 Kutokuwapo kwa hati ya makubaliano kati ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Bohari Kuu ya Dawa

Kanuni Na. 242 ya Kanuni za Fedha za Bohari Kuu ya Dawa za Mwaka 2011 inataka fedha zitumike kwa madhumuni yaliyokusudiwa, matumizi yawe ndani ya bajeti iliyotolewa kwa kila kundi katika makubaliano ya ruzuku au mikopo, na uhamishaji wa fedha hautafanywa bila kuidhinishwa na wakala wa ufadhili. Ununuzi wa bidhaa na huduma utafanywa kwa mujibu wa sheria na masharti yaliyotolewa katika makubaliano ya mkataba (MoU).

Nilibaini kuwa Bohari Kuu ya Dawa ilipokea jumla ya Sh. bilioni 65.64 kutoka kwa washirika wa maendeleo zilizotolewa kupitia Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa ajili ya ununuzi na usambazaji wa vifaatiba vya CEmONC kwa vituo 217 vya Afya. Ingawa Ofisi ya Rais - TAMISEMI ilipewa jukumu la kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa afua ya CEmONC, hakuna makubaliano kati ya



TAMISEMI na Bohari Kuu ya Dawa yaliyoainisha majukumu, mkakati, na muda wa utekelezaji uliopangwa.

Kutokuwapo kwa makubaliano kulichangia kuchelewa kukamilika kwa utoaji wa vifaatiba hivyo.

Ninapendekeza kwamba, katika siku zijazo, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Bohari Kuu ya Madawa wahakikishe maagizo yote maalum yanakuwa na hati ya makubaliano inayoainisha vigezo na masharti ya agizo hilo maalum.

#### **7.5.3.5 Kutokuwapo kwa taarifa za utekelezaji za kila robo mwaka kwa ufuatiliaji na usimamizi wa karibu**

Kanuni Na. 251 ya Kanuni za Fedha za Bohari Kuu ya Dawa za Mwaka 2011 kuhusu malipo ya fedha taslimu inamtaka mkurugenzi anayehusika na fedha kuwasilisha kwa mfadhili taarifa za robo mwaka za hesabu za miradi au programu ili kusaidia ulipaji wa fedha za awali zilizopokelewa.

Nilibaini kuwa Bohari Kuu ya Dawa ilipokea jumla ya Sh. bilioni 65.64 kuanzia mwaka 2017/2018 hadi 2020/21 kutoka Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa ajili ya ununuzi na usambazaji wa vifaatiba kwa ajili ya afua ya CEmONC. Hata hivyo, hadi mwezi Aprili 2023, menejimenti ya Bohari Kuu ya Dawa uliwasilisha ripoti 6 tu za kila mwezi kwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Bodi za Wizara ya Afya na hakuna ripoti ya robo mwaka au mwaka iliyoandaliwa kuhusu fedha zilizopokelewa, ununuzi, na usambazaji wa vifaatiba kwa ajili ya ufuatiliaji na usimamizi. Kutokuwapo kwa ripoti za utekelezaji za robo mwaka na mwaka kulileta ugumu katika ufuatiliaji na utekelezaji kwa afua ya CEmONC.

Ninapendekeza kwamba Bohari Kuu ya Madawa kuzingatia Kanuni za Fedha za Bohari Kuu ya Madawa za mwaka 2011 na kuhakikisha kuwa taarifa za utekelezaji za mwaka na robo mwaka zinatayarishwa kwa wakati na kuwasilishwa kwa wadau husika kwa ajili ya kufanya maamuzi.

#### **7.5.3.6 Usimamizi usio na ufanisi na sababu zilizozuia ununuzi na usambazaji wa vifaatiba kwa afua ya CEMONC**

Aya ya 9 (a) ya Mkataba wa Huduma kwa Mteja wa Bohari Kuu ya Dawa wa Mwaka 2017-2020 unataka mchakato wa oda maalumu kwa vituo vya huduma za afya kuchukua angalau miezi miwili tangu tarehe ya kuagiza. Pia, Aya ya 10.1 ya Mkataba wa Huduma kwa Mteja wa Bohari Kuu ya Dawa wa Mwaka 2021 unataka upatikanaji wa vifaatiba kwa wakati kwa bei ya chini, upatikanaji wa

mahitaji ya mteja kama ilivyoombwa, na mchakato wa ununuzi maalumu kuchukua muda wa miezi mitatu tangu oda ilipolipwa, na mahitaji ya mteja yawe yametimizwa.

Nilibaini ucheleweshaji wa kuanzia siku 60 hadi 951 tangu tarehe ya fedha kulipwa Bohari Kuu ya Dawa hadi tarehe ambayo maagizo ya kusitisha yalitolewa kwa wauzaji. Zaidi ya hayo, wasambazaji walichukuwa muda wa siku 201 hadi 341 kuwasilisha vifaatiba vilivyoagizwa kwa walengwa, ingawa maagizo nane ya kusitishwa yalibainisha uwasilishaji ndani ya siku 60 hadi 180, na maagizo tisa hayakuwa na tarehe inayotarajiwa ya kupokea vifaa.

Pia, nilibaini mabadiliko ya mara kwa mara ya wakurugenzi wa kitengo cha usimamizi wa ununuzi kati ya mwaka 2016 na 2023, ambapo jumla ya mabadiliko 9 yalifanyika. Mabadiliko haya yalikuwa na athari kubwa katika utekelezaji wa afua ya CEmONC. Mlipuko wa janga la UVIKO-19 mwanzoni mwa mwaka 2020 ulizidisha hali hiyo, ambapo Bohari Kuu ya Dawa pia ilichukulia ununuzi na usambazaji wa vifaatiba kwa afua ya CEmONC kama ununuzi wa kawaida kuanzia kupanga hadi kusaini mikataba ya ununuzi.

**Ninapendekeza kwamba Serikali kupitia Bohari Kuu ya Madawa ihakikishe udhibiti wa ndani wa ununuzi na usambazaji wa vifaatiba unaimarishwa. Zaidi ya hayo, mambo yote yaliyochangia kuchelewa kwa usambazaji wa vifaatiba katika kutekeleza afua ya CEmONC yanarekebishwa na kuhakikisha utoaji wa vifaatiba vilivyobaki unafanywa bila kucheleweshwa zaidi.**

#### 7.5.4 Upungufu wa Usimamizi wa Fedha za CEmONC

Wakati wa ukaguzi wa CEmONC, nilipitia nyaraka za utoaji wa fedha na kubaini upungufu kama unavyofafanuliwa hapa chini.

##### 7.5.4.1 Kutokuwapo kwa taarifa za akaunti za kila robo katika Mfumo wa Epicor kwa Fedha za CEmONC

Kanuni ya 251 ya Kanuni za Fedha za Bohari Kuu ya Dawa za Mwaka 2011 inamtaka mkurugenzi anayehusika na fedha kuwasilisha kwa mfadhili taarifa za hesabu za kila robo mwaka za miradi ili kusaidia ulipaji wa fedha za awali zilizopokelewa.

Bohari Kuu ya Dawa ilipokea jumla ya Sh. bilioni 65.64 kutoka Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa ajili ya CEmONC. Hata hivyo, licha ya kutokuwa na akaunti tofauti ya benki, hakukuwa na kifungu katika Mfumo wa EPICOR

kutambua fedha zilizopokelewa na matumizi yake husika wala mkurugenzi anayehusika na fedha hakuwasilisha kwa mfadhili taarifa za kila robo za hesabu za CEmONC kusaidia utoaji wa taarifa za fedha za awali zilizopokelewa.

Upungufu huo ulitokana na kukosekana kwa mawasiliano na nyaraka kati ya wahusika kuhusu aina ya fedha zilizohamishiwa Bohari Kuu ya Dawa.

Kushindwa kuandaa taarifa za hesabu za kila robo ya mwaka na vifungu tofauti katika Mfumo wa Epicor kwa fedha za CEmONC kumezuia utaratibu wa kuripoti wa Bohari Kuu ya Dawa, hivyo kusababisha utoaji duni wa huduma zilizokusudiwa kwa jamii. Aidha, upungufu huu umesababisha ugumu wakati wa ukaguzi wa fedha hizo.

Ninapendekeza kwamba Serikali kupitia Bohari Kuu ya Madawa ihakikishe kuwa kuna nambari ya kipekee ya utambulisho katika mfumo wa Epicor inayotambulisha mapato na matumizi ya Fedha za CEmONC na kudumisha taarifa za hesabu za kila robo mwaka kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli husika kwa urahisi.

#### 7.5.4.2 Bei za vifaatiba vilivyonunuliwa kwa awamu ya kwanza ilitozwa zaidi

Kifungu cha 5.1 cha Taratibu za Viwango vya Bohari Kuu ya Dawa za Uwekaji Bei za Tarehe 30 Juni 2019 kinaitaka Bohari Kuu ya Dawa kutumia kiwango cha kawaida kutoza asilimia 20.4 kwenye bidhaa zote zinazouzwa na gharama zinazotumika za upakiaji zinakadiriwa kuwa asilimia 5.9.

Nilipitia bei zinazotozwa na wazabuni kulinganisha na bei kwenye ankara ya mauzo ya Bohari Kuu ya Dawa baada ya kutumia viwango vya kawaida vya malipo na kubaini kuwa bei zilizoorodheshwa kwa vifaatiba 12 kwa awamu ya kwanza ya CEmONC, kwa mujibu wa taratibu za kawaida za Bohari Kuu ya Dawa, ni Sh. bilioni 1.66. Hata hivyo, bei iliyotozwa kwa mujibu wa ankara za Bohari Kuu ya Dawa ilikuwa Sh. bilioni 2.85 na kusababisha ongezeko la bei la Sh. bilioni 1.19 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 37**.

**Jedwali Na. 37: Orodha ya Bidhaa Zilizotozwa Bei Kubwa**

Na.	Kifaa	Idadi	Bei Elekezi (Sh.)	Bei Zilizotozwa (Sh.)	Kiasi Kilichozidi (Sh.)
1.	Autoclave 100 litres,	16	47,878,440	194,355,200	146,476,760

Na.	Kifaa	Idadi	Bei Elekezi (Sh.)	Bei Zilizotozwa (Sh.)	Kiasi Kilichozidi (Sh.)
	electrical and gas heated				
2.	Caesarian Section Set	8	4,031,122	16,887,200	12,856,078
3.	Centrifuge (For 8X15 MLS Tubes) Electrically Operated	29	35,266,831	71,108,800	35,841,969
4.	Drip Stand Double-Hook ADJ to 2.5 M Height	56	4,751,597	20,904,800	16,153,203
5.	Examination Lamp light	37	3,942,937	11,846,348	7,903,411
6.	Flat Iron Industry	39	1,064,601,392	1,127,340,630	62,739,238
7.	Laparotomy Set	99	190,754,572	621,328,300	430,573,728
8.	Operating light	2	11,488,392	68,063,870	56,575,478
9.	Operating theatre table	42	247,939,560	652,012,200	404,072,640
10.	Suction Pump Heavy Duty, Electric Capacity 6Litres	34	43,683,042	52,050,600	8,367,558
11.	Semi-Automatic Haematology Analyser	1	8,307,601	18,469,360	10,161,759
<b>Total</b>			<b>1,662,645,486</b>	<b>2,854,367,308</b>	<b>1,191,721,822</b>

**Chanzo:** Uchambuzi wa Mkaguzi kulingana na wazabuni wengine na Ankara za Bohari Kuu ya Dawa

Kuongezeka kwa bei ya ankara za Bohari Kuu ya Dawa kulisababisha kuongezeka kwa matumizi kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba kwa CEMONC awamu ya kwanza na hatimaye kuathiri kufikiwa kwa lengo lililokusudiwa.

**Ninapendekeza kwamba Serikali kupitia Bohari Kuu ya Madawa ifanye marekebisho ya bei ya bidhaa zilizotozwa zaidi kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba katika afua ya CEMONC awamu ya kwanza ili kuakisi thamani halisi ya bidhaa zilizosambazwa kwa awamu ya kwanza.**



## USIMAMIZI WA MALI NA MADENI

### 8.1 Utangulizi

Usimamizi mzuri wa mali ni msingi wa shughuli za Serikali kwa kuwa, unaweka msukumo kwa utoaji wa huduma bora, kudumisha uwajibikaji, na kuboresha matumizi ya rasilimali. Serikali inaweza kugawa rasilimali kwa ufanisi na kuchochea ukuaji wa uchumi kwa kusimamia ipasavyo ununuzi, matengenezo, na uondoshwaji wa mali. Kuweka kipaumbele katika usimamizi wa mali si tu muhimu kwa utawala bora bali pia ni msingi wa maendeleo endelevu. Kwa upande mwingine, usimamizi mzuri wa madeni ya serikali ni muhimu kwa kudumisha utulivu wa kifedha, kulinda heshima ya serikali, na kupunguza hatari za kupoteza fedha.

Katika sura hii, nimeelezea muhtasari wa upungufu uliobainika wakati wa ukaguzi wa usimamizi wa mali na madeni ya Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala za Serikali.

### 8.2 Usimamizi wa Mali

Nilifanya ukaguzi wa nyaraka na kuhakiki mali zinazomilikiwa na serikali ili kuthibitisha uwepo wa mali hizo pamoja na kufanya tathmini ya ufanisi wake katika kufanya kazi na kubaini yafuatayo.

#### 8.2.1 Upungufu katika Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMIS)

Waraka Namba 2 wenye Kumb. Na. JA.32/233/01 wa tarehe 15 Julai 2021 unawataka maafisa masuuli kuhakikisha kuna matumizi sahihi ya Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMIS) kwa ajili ya kuhifadhi na kusimamia kumbukumbu sahihi za mali. Kwa mujibu wa waraka huo, muda wa mwisho wa kujiunga na matumizi ya mfumo ulikuwa tarehe 31 Agosti 2021. Mfumo huu unatumika kama kanzidata kuu ya kusimamia mali zote za serikali,

ukiruhusu uwiano katika kutafuta uchakavu na kuhuisha muda wa matumizi wa mali hizo.

Nilifanya tathmini ya matumizi ya mfumo huu katika kanzidata kuu ya Wizara ya Fedha - Huduma za Hazina na kubaini upungufu kadhaa:

- a) Kupishana kwa idadi ya taasisi za umma zilizosajiliwa katika mfumo ikilinganishwa na idadi ya taasisi zilizo rodheshwa; Uhakiki niliofanya tarehe 7 Septemba 2023 ulionyesha kwamba mfumo ulirekodi taasisi 555, ikilinganishwa na taasisi 628 zilizo rodheshwa katika hesabu jumuiishi zilizokaguliwa, ikiashiria taasisi 73 hazikurekodiwa kwenye mfumo kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2023.
- b) Taarifa zisizosahihi za thamani za mali: Nilibaini mfumo unaonesha kwamba mali za taasisi 197 zilionunuliwa miaka ya nyuma hazioneshi thamani jumuiifu ya uchakavu, wakati mali 192 za Kituo cha Maendeleo cha Dakawa zimerekodiwa bila kuonesha thamani halisi ya mali hizo na badala yake zimeoneshwa kuwa na thamani sifuri. Zaidi, nilibaini mali zenye thamani ya Sh. milioni 961.36 zilirekodiwa bila kuonesha taasisi zinazomiliki.
- c) Kujirudia kwa idadi ya taasisi zilizosajiliwa katika mfumo: Usajili wa taasisi 16 kwenye mfumo ulijirudia ambapo taasisi moja ilisajiliwa mara tatu hadi tisa.

Vilevile, ukaguzi wangu wa usimamizi wa mali katika taasisi za serikali ulibaini kuwa mali zenye thamani ya Sh. bilioni 243.71 kutoka kwa taasisi 33 kama ilivyo oneshwa kwenye

**Kiambatisho Na. VI** hazikuwa zimerekodiwa kwenye mfumo. Taasisi zilieleza kuwa kasoro hiyo ilitokana na kukosekana kwa mafunzo ya jinsi ya kurekodi na kusimamia mali katika mfumo huo.

Ninahusisha upungufu huu si tu na hatari ya matumizi madogo ya mfumo pia na uwajibikaji wa watumiaji wa mfumo.

Licha ya upungufu huo na kutokurekodiwa kwa mali hizi katika mfumo, taasisi hizi zilitumia njia mbadala kutayarisha taarifa zao za fedha kwa kutumia rejista zao za mali za kudumu. Rejista hizi zilikuwa na taarifa muhimu za mali hizo, hivyo kuhakikisha uandaaji wa taarifa za fedha zenye usahihi.

Ninapendekeza kwamba Serikali ihakikishe inafuatilia utekelezaji wa maelekezo ya usimamizi wa mali ili kuhakikisha kwamba taasisi zote zinatumia mfumo wa usimamizi wa mali kwa ufanisi na utunzaji wa taarifa sahihi.

### 8.2.2 Kutoondoshwa kwa Mali Zilizohifadhiwa katika Vituo vya Polisi Baada ya Kutaifishwa

Amri Na. 223 (12) ya Amri za Jumla za Polisi (PGO), inataka mali zilizotaifishwa kuondoshwa mara moja. Kama Mahakama haina mahali sahihi pa kuhifadhi kwa ajili ya uondoshaji, mali hizo zinaweza kuhifadhiwa katika eneo la Polisi na kusimamiwa kulingana na utaratibu uliowekwa na Amri Na. 229 ya Amri za Jumla za Polisi.

Ukaguzi wangu na uhakiki wa usimamizi wa mali zilizotaifishwa zilizohifadhiwa katika vituo vya polisi ulibaini kuwapo kwa mali hizo katika vituo saba vya polisi kwa muda wa hadi miaka minne bila kuondoshwa, licha ya maamuzi ya mahakama. Mali hizo zilizopo katika vituo vya polisi ni pamoja na magari mawili, moja katika Kituo cha Polisi Chato na na jingine katika Kituo cha Polisi Geita, pikipiki tano zilizotaifishwa tangu mwaka 2019 katika Kituo cha Polisi Nanyumbu, pikipiki 12 zilizotaifishwa tangu mwaka 2020 katika Kituo cha Polisi Mtwara, pikipiki 16 na magari manne yaliyotaifishwa tangu 2019 katika Kituo cha Polisi Mbarali, gari moja lililotaifishwa tangu mwaka 2022 katika Kituo cha Polisi Chunya, na gari moja lililotaifishwa tangu mwaka 2021 katika Kituo cha Polisi Buguruni.

Ninahusisha upungufu huu na kucheleweshwa kwa idhini kutoka kwa Mkurugenzi wa Usimamizi wa Mali za Serikali ili kufanyika ugawaji na uondoshaji wake. Kuchelewesha uondoshaji kunasababisha kuongezeka kwa gharama za uhifadhi na kusababisha mali hizo kuchakaa na kuwekwa katika hatari ya kuibiwa au kutumiwa vibaya.

Ninapendekeza kwamba Serikali iharakishe mchakato wa idhini ya kuondoa mali zilizotaifishwa na kuhifadhiwa katika vituo vya polisi ili kupunguza gharama za kuhifadhi na kupunguza hatari za uchakavu na ubadhirifu.

### 8.2.3 Mali Zilizotelekezwa kwa Muda Mrefu bila Matengenezo au Kuuzwa

Kanuni ya 254(1) ya Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2001 inataka magari, mitambo, au vifaa ambavyo havitumiki tena au havirekebishi kuhifadhiwa hadi

hapo kutakapokuwa na vifaa vya kutosha kwa ajili ya ukaguzi utakaofanywa na bodi. Aidha, kifungu kidogo cha 2 kinataka kuandaliwa kwa orodha za mali hizo ikieleza muda wa matumizi na thamani yake, na kuwasilisha nakala nne kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali sambamba na maombi ya kukaguliwa na mapendekezo ya kuuzwa kwake.

Hata hivyo, ukaguzi wangu ulibaini kuwa taasisi 27 zilikuwa na mali 522 zilizotelekezwa kwa muda mrefu, ambazo ni pamoja na magari na pikipiki 202 kutoka taasisi 20 na mitambo na vifaa 320 kutoka taasisi saba. Mali hizi zilikuwa zimetelekezwa kwa muda mrefu bila kutumika, kutengenezwa, au kuuzwa. Orodha ya taasisi na idadi ya mali inaoneshwa katika **Jedwali Na. 38**.

**Jedwali Na. 38: Taasisi Zilizokuwa na Mali Zilizotelekezwa kwa Muda Mrefu bila Matengenezo au Kuuzwa**

Na	Taasisi	Idadi ya Mali
	<b>Magari ya Yaliyotelekezwa kwa Muda Mrefu</b>	
1.	Tume ya Marekebisho ya Sheria	Magari manne.
2.	Ubalozi wa Tanzania, Brazil	Gari moja.
3.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Utete	Magari matatu.
4.	Tume ya Madini	Magari 42.
5.	Bodi ya Maji Bonde la Mto Pangani	Magari mawili.
6.	Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara	Magari matano.
7.	Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini	Magari sita.
8.	Wakala wa Maabara ya Mifugo Tanzania	Magari 10.
9.	Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania	Magari nane.
10.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Uwanda wa Juu wa Makonde	Magari sita.
11.	Bodi ya Ushauri kwa Hospitali Binafsi	Gari moja.
12.	Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo	Magari sita.
13.	Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu	Gari moja.
14.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Sumbawanga	Gari moja.
15.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Songea	Magari matatu.
16.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Sokoine	Magari matano.
17.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Mwananyamala	Magari mawili.
18.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Mawenzi	Magari manne.
19.	Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali	Magari matano.
20.	Wizara ya Afya	Magari 87.
	<b>Mitambo na Vifaa Vilivyotelekezwa</b>	
1.	Kampuni ya Utengenezaji Samani ya SUMA JKT, Chang'ombe	Mitambo mitatu na mashine 22.
2.	Bodi ya Maji Bonde la Mto Pangani	Vifaa vya ofisi 120.
3.	Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini	Mitambo saidizi 15, mitambo 20 ya kuchimba visima, mitambo mitatu ya maji, jenereta 10,



Na	Taasisi	Idadi ya Mali
		mitambo 12 saidizi, na pampu tano.
4.	Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania	Mitambo mitatu.
5.	Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu	Samani 20 za ofisi, kompyuta 60 na vifaa vya tehama.
6.	Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya	Viyoyozi 21.
7.	Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu	Mitambo, mashine, vifaa vya ofisi, na vifaa vya Tehama.

**Chanzo:** Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti za Mwaka 2022/23

Upungufu huu unatokana na mchakato mrefu wa kupata idhini ya kuuzwa kwa mali hizo, pamoja na ufinyu wa fedha za matengenezo. Kuchelewesha uzaji wa magari, mitambo, na vifaa ambavyo havitumiki kwa muda mrefu si tu kunachangia kuendelea kuchakaa lakini pia hupunguza mapato yanayoweza kupatikana wakati wa kuuza.

**Ninapendekeza Serikali itenge fedha za kutosha na kuandaa mipango ya matengenezo kwa ajili ya kutengeneza mali zinazotumika ili kuongeza muda wa matumizi yake, na pia kuharakisha mchakato wa kuondoa mali zisizotumika.**

#### 8.2.4 Kuwapo kwa Majengo Yaliyotelekezwa, Yaliyochakaa, na Viwanja Visivyoendelezwa

Nilifanya uhakiki wa majengo na viwanja ambavyo vinamilikiwa na Serikali kupitia wizara, idara zinazojitegemea, na wakala za serikali, pamoja na ofisi za balozi za Tanzania. Nilibaini kuendelea kuwapo kwa majengo yaliyotelekezwa, majengo yaliyochakaa, na viwanja visivyoendelezwa, kama nilivyoonesha katika ukaguzi wa mwaka uliopita. Nilibaini yafuatayo;

Nilibaini uwapo wa majengo chakavu na yaliyotelekezwa katika ofisi tano za balozi, kinyume na kanuni ya 83 (4) ya Kanuni za Utumishi wa Umma (Huduma za Nje ya Nchi), 2016, inayohitaji ukarabati wa majengo ya ofisi za balozi kila baada ya miaka mitatu. Jambo hili limesababisha kuendelea kuongezeka kwa gharama za kodi za majengo na faini kutoka kwa nchi wenyeji kutokana na kutokukarabatiwa kwa majengo na kutofanyiwa maendeleo viwanja vya ofisi za balozi, na hatimaye, kusababisha kupoteza kinga za kidiplomasia. Zaidi, nilibaini majengo yaliyochakaa katika wizara na wakala za serikali tano, kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 39**.

**Jedwali Na. 39: Taasisi Zilizoa na Majengo Yaliyochoa na Kutelekezwa**

Na.	Taasisi	Maelezo	Upungufu Uliobainika
1.	Ubalozi wa Tanzania wa Uingereza	Jengo hili lilinunuliwa mwaka 1979 ambalo lipo Barabara ya 6, Colin Deep Gardens.  Jengo la ofisi lililojengwa 1774 ambalo lipo mtaa wa 3 wa Stratford.	<ul style="list-style-type: none"> <li>Jengo hili limeachwa bila kufanyiwa ukarabati.</li> <li>Ubalozi unatumia kodi kiasi cha paundi 108,000, ambayo ni sawa na Sh. milioni 320 kila mwaka.</li> <li>Jengo lina muundo wa zamani, nyufa kubwa, na kuta zilizoharibika.</li> <li>Watathmini wa mali wa Serikali ya Uingereza walitoa onyo kuwa matumizi ya jengo hayawezi kuendelezwa kutokana na uchakavu wake ambao si salama kulingana na kanuni za Uingereza.</li> </ul>
2.	Ubalozi wa Kudumu wa Umoja wa Mataifa- New York	Jengo lilionunuliwa tarehe 30 Septemba 2011 kwa dola za Marekani 24,886,698 lililopo mtaa wa 307 East 53rd, New York, NY 10022	<ul style="list-style-type: none"> <li>Jengo hili limeachwa bila kufanyiwa ukarabati.</li> <li>Jengo lina mita za mraba 2,926, halitumiki ipasavyo ambapo ni ghorofa mbili tu zinazotumika, sawa na mita za mraba 975 (33%), na kuacha mita za mraba 1,951 (67%) bila matumizi.</li> </ul>
3.	Ubalozi wa Tanzania wa Washington, DC, Marekani	Jengo la ghorofa sita lililoko katika Mtaa wa 1232 22, Washington DC, 20037 lililonunuliwa 14 Agosti 2009.	<ul style="list-style-type: none"> <li>Jengo linahitaji matengenezo ya mifumo ya joto na maji.</li> <li>Ubalozi ulipokea notisi na faini kutokana na uchakavu wa jengo, ambayo ilisababisha kupoteza kinga ya kidiplomasia.</li> </ul>
4.	Ubalozi wa Tanzania wa Ottawa, Kanada	Jengo Na. 2191 la makazi ya Balozi lililonunuliwa tarehe 21 Agosti 1967 lipo kwenye Barabara ya Niagara, K1H 6G5.	<ul style="list-style-type: none"> <li>Jengo linahitaji marekebisha ya mifumo ya joto na baridi, mifumo ya majitaka, maegesho ya magari, madirisha yasiyofaa wakati wa kipindi cha baridi, na uchakavu wa samani.</li> </ul>
5.	Ubalozi wa Tanzania wa Harare, Zimbabwe	Majengo 8 yalinyonunuliwa mwaka 1980 katika mikoa mbalimbali.	<ul style="list-style-type: none"> <li>Majengo yanahitaji ukarabati wa nyumba zote.</li> <li>Hili limepelekea ongezeko la gharama za bima za majengo kwa mwaka kutoka Sh. milioni 49.89 hadi Sh. milioni 58.31 kwa mwaka.</li> </ul>
6.	Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu	Majengo matano yalinyonunuliwa mwaka 2016/17 yaliyopo Bagamoyo.	<ul style="list-style-type: none"> <li>Majengo haya yameharibika na sio salama kwa matumizi.</li> </ul>

Na.	Taasisi	Maelezo	Upungufu Uliobainika
7.	Hospitali ya Rufaa ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto	Nyumba za wafanyakazi 33 katika hospitali ya Kibong'oto.	<ul style="list-style-type: none"> <li>Majengo haya ya makazi ya wafanyakazi yamechakaa na sio salama kwa matumizi.</li> </ul>
8.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Sumbawanga	Majengo matatu ya hospitali yaliyojengwa miaka mbalimbali.	<ul style="list-style-type: none"> <li>Paa za majengo haya zinavuja; sakafu imeharibika; na milango na madirisha yameharibika.</li> </ul>
9.	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	Majengo 57 katika vyuo.	<ul style="list-style-type: none"> <li>Majengo haya yameharibika kwa muda mrefu.</li> </ul>

**Chanzo:** Ripoti ya Ukaguzi kwa Menejimenti ya mwaka 2022/23

Pia, nilibaini kuwapo kwa viwanja visivyoendelezwa katika ofisi za balozi tatu, kama ilivyooneshwa katika **Jedwali Na. 40**. Hii si tu inaharibu taswira ya nchi, bali pia inaweza kusababisha viwanja hivyo kuchukuliwa na kupoteza kinga ya kidiplomasia.

#### **Jedwali Na. 40: Ofisi za Balozi Zilizoa na Viwanja ambavyo Havijaendelezwa**

Na.	Taasisi	Upungufu Uliobainika
1.	Ubalozi wa Tanzania Abuja, Nigeria	<ul style="list-style-type: none"> <li>Mnamo tarehe 24 Aprili 1989, Serikali ya Nigeria ilitoa viwanja viwili vyenye thamani ya Sh. bilioni 7.03 kwa ubalozi wa Tanzania. Kimoja kwa ajili ya ofisi ya ubalozi na kingine kwa ajili ya makazi ya ubalozi.</li> <li>Hata hivyo, tarehe 20 Oktoba 2023, wizara ya mambo ya nje ya Nigeria ilifuta umiliki wa viwanja hivyo kutokana na kutokuendelezwa kwa zaidi ya miaka 33. Hii ilisababisha Wizara ya mambo ya nje ya Tanzania kutuma ujumbe wake Nigeria kuomba urejeshwaji wa umiliki huo. Hata hivyo, Serikali ya Tanzania bado haijapokea majibu kutoka Serikali ya Nigeria.</li> </ul>
2.	Ubalozi wa Tanzania Uingereza	<ul style="list-style-type: none"> <li>Uwepo wa kiwanja ambacho hakijaendelezwa, kilichopo katika mtaa wa 19 Denewood, N6 4AQ, kilichonunuliwa mwaka 1978. Kiwanja hicho kimekuwa na vichaka ambavyo vimekuwa kero kwa majirani.</li> <li>Kutokana na hali ya kiwanja hicho, ubalozi umekuwa ukilalamikiwa na majirani na serikali ya Uingereza juu ya hali hiyo.</li> </ul>
3.	Ubalozi wa Tanzania Moroni, Comoro	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kiwanja, kilichotolewa kwa Serikali ya Tanzania kwa matumizi ya kibalozi chenye ukubwa wa mita za mraba 3,811, kina majengo matatu.</li> <li>Ukaguzi ulibaini uvamizi katika kiwanja hiki, ambapo wavamizi wanajihusisha na shughuli zisizoruhusiwa, ikiwa ni pamoja na kuegesha magari, kutupa taka, na kujenga majengo nje ya mipaka ya viwanja.</li> <li>Pia, kiwanja hicho hakikuwa na uzio ambao ungezuia wavamizi na shughuli zisizoruhusiwa.</li> </ul>

**Chanzo:** Ripoti ya Ukaguzi kwa Menejimenti ya mwaka 2022/23

Kuchakaa kwa majengo na kutokuendelezwa kwa viwanja hivyo kunasababishwa na ufinyu wa bajeti. Kwa maoni yangu, hali hii inaweza kusababisha uhusiano mbaya wa kidiplomasia, kupoteza uaminifu kati ya ubalozi na serikali wenyeji, na mazingira hatarishi ya kufanya kazi.

**Ninapendekeza kwamba Serikali iandae mipango ya matengenezo, itenge fedha za kutosha kwa ukarabati wa majengo yaliyoharibika, na kuanzisha matumizi ya viwanja vilivyoachwa kwa muda mrefu katika ofisi za balozi ili kulinda kinga za kidiplomasia.**

### **8.2.5 Kuwapo kwa Majengo Chakavu katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, Makazi ya Wazee, na Makazi ya Watoto**

Aya ya 14 ya Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Umma wa Mwaka 2019 unataka kila ofisa masuuli awajibike kuhakikisha mpango wa matengenezo ya mali unatayarishwa na kuzingatiwa.

Uhakiki niliofanya katika vyuo vya mafunzo ya maendeleo ya jamii, makazi ya wazee, na makazi ya watoto katika mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara, ulibaini hali ya uchakavu wa majengo yanayotumika. Majengo hayo yanajumuisha vyuo 8, nyumba 5 za wazee, na nyumba 3 za makazi ya watoto, ambazo zilikuwa hazijakarabatiwa kwa muda mrefu na kuhatarisha usalama wa watumiaji kinyume na matakwa ya mwongozo tajwa hapo juu. **Kiambatisho Na. VII** ni orodha vituo vyenye majengo chakavu.

Kutolipa kipaumbele swala la ukarabati wakati wa kuandaa bajeti ya wizara, pia ukosefu wa pesa ya kutosha kwa shughuli za ukarabati wa majengo umechangia majengo hayo kutofanyiwa ukarabati kwa muda mrefu. Uchakavu wa majengo hayo si tu ni hatari kiafya na yanahatarisha maisha ya watumiaji bali pia serikali italazimika kuyafanyia ukarabati mkubwa kwa gharama kubwa zaidi.

**Ninapendekeza kwamba Serikali itenge fedha za kutosha kwa ukarabati wa majengo yaliyoharibika katika vyuo vya maendeleo ya jamii, makazi ya wazee, na makazi ya watoto ili kupunguza hatari na kuhakikisha mazingira mazuri kwa watumiaji.**

### 8.2.6 Ukosefu wa Hatimiliki za Ardhi zinazomilikiwa na Serikali

Kifungu cha 29(1)(a)(b) na (c) cha Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 (Toleo la Mwaka 2019) kinataka pale kamishna anapoamua kutoa haki ya umiliki wa ardhi kwa mwombaji au yuko katika umiliki wa ardhi chini ya haki ya umiliki au chini ya kukubaliwa kwa toleo la haki ya umiliki, au vinginevyo, mtu au taasisi hiyo inastahili kupewa haki ya umiliki, na kamishna atatoa hati inayojulikana kama "hatimiliki" kwa mtu huyo. Zaidi ya hayo, Katibu Mkuu Kiongozi na Msajili wa Hazina, kwa nyakati tofauti, walitoa maagizo na kuzihimiza taasisi za serikali kuhakikisha zinapata hatimiliki kwa ardhi inayomilikiwa na serikali.

Licha ya sheria, maagizo na msisitizo huo, ukaguzi wangu ulibaini kwamba taasisi 16 zilizoordheshwa katika **Jedwali Na. 41** hazikuwa na hatimiliki za viwanja vya serikali.

#### Jedwali Na. 41: Taasisi ambazo Hazikuwa na Hatimiliki za Ardhi Inayomilikiwa na Serikali

Na	Taasisi	Kundi	Sekta	Maelezo
1.	Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Magereza	Taasisi nyingine	Utawala	Ekari 29,287
2.	SUMAJKT Makao Makuu	Taasisi nyingine	Utawala	Viwanja 13
3.	Shirika la Jeshi la Polisi Tanzania	Taasisi nyingine	Utawala	Kiwanja kimoja
4.	Mamlaka ya Mai Safi na Usafi wa Mazingira Chato	Taasisi nyingine	Kiuchumi	Viwanja 13
5.	Mamlaka ya Mai Safi na Usafi wa Mazingira Utete	Taasisi nyingine	Kiuchumi	Viwanja 3 (Mita za mraba 6,900)
6.	Wakala wa Mbegu za Kilimo	Taasisi nyingine	Kiuchumi	Viwanja saba
7.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Busega	Taasisi nyingine	Kiuchumi	Viwanja 11
8.	Tume ya Madini	Taasisi nyingine	Kiuchumi	Kiwanja kimoja
9.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbinga	Taasisi nyingine	Kiuchumi	Viwanja vinne
10.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Namanyere	Taasisi nyingine	Kiuchumi	Viwanja saba
11.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Lushoto	Taasisi nyingine	Kiuchumi	Viwanja vitatu
12.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Makete	Taasisi nyingine	Kiuchumi	Viwanja saba

Na	Taasisi	Kundi	Sekta	Maelezo
13.	Mamlaka ya Mapato Tanzania (Matumizi)	Taasisi nyingine	Akaunti za Taifa	Viwanja 28
14.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Shinyanga	RRH	Kijamii	Ekari 133
15.	Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu	Fungu 65	Kijamii	Ekari 23llonga, Ekari 1,010 zilizopo Sasanda Songwe na ekari 35 Marangu
16.	Wizara ya Afya	Fungu 52	Kijamii	Viwanja 14

**Chanzo:** Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti za 2022/23

Kukosekana kwa hatimiliki kunachangiwa na ufuatiliaji usioridhisha wa taasisi husika. Kukosekana na hatimiliki hizo za ardhi inayomilikiwa na serikali kunaleta hatari ya kupotea kwa viwanja hivyo au kusababisha migogoro.

**Ninapendekeza kwamba Serikali, kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na taasisi husika, ihakikishe kupatikana kwa hati za umiliki ili kuwezesha umiliki wa viwanja hivyo.**

#### 8.2.7 Hasara Inayotarajiwa ya Sh. Bilioni 20.43 kwenye Mikopo Chechefu

Utengaji wa kiasi cha hasara kitakachotokana na kushindwa kufanya marejesho ya mikopo ni maneno ya kihasibu yanayotumiwa na taasisi za fedha kutarajia hasara inayoweza kutokea kwa mikopo ambayo huenda isirejeshwe kikamilifu. Ukaguzi wangu wa Mfuko wa Pembejeo za Kilimo (AGITF) ulibaini kuwa Mfuko ulikuwa na mikopo ambayo ilikuwa haijarejeshwa yenye thamani ya Sh. bilioni 25.42 hadi tarehe 30 Juni 2023. Kati ya mikopo hiyo, Mfuko ulitenga kiasi cha hasara tarajiwa kutokana na wakopaji kushindwa kurejeshwa mikopo jumla ya Sh. bilioni 20.43, ikiashiria matarajio ya kupata hasara ya takribani asilimia 80 ya mikopo iliyotolewa. Kwenye kiasi hicho kilichotengwa cha Sh. bilioni 20.43, Mfuko ulitarajia hasara ya asilimia 100 kwenye mikopo ambayo ilikuwa haijarejeshwa kwa muda wa siku 721, ambayo ni jumla ya Sh. bilioni 19.83. Kwa mikopo iliyobaki ya Sh. milioni 600, Mfuko ulitarajia hasara ya kati ya asilimia moja hadi 50.

Aidha, nilibaini kuwa kati ya mikopo ambayo haikurejeshwa, Sh. bilioni 1.71 ni mikopo ambayo haikurejeshwa kuanzia mwaka 1995 hadi 1997, ikionesha ucheleweshaji wa kati ya miaka 26 na 28. Pia, inajumuisha mikopo ya jumla ya Sh. milioni 801.38 ilitolewa kwa benki nne zilizofungwa na Benki Kuu ya

Tanzania kati ya mwaka 2017 na 2018, kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 42 hapa chini.

**Jedwali Na. 42: Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Zilizofungwa**

Na.	Maelezo	Kiasi (Sh.)	Tarehe ya Kufungwa
1.	Kagera Farmers' Cooperative Bank Ltd.	294,301,070	17/03/2018
2.	Mbinga Community Bank Plc	286,421,895	12/05/2017
3.	Meru Community Bank	150,000,000	04/01/2018
4.	Njombe Community Bank Ltd.	70,666,667	04/01/2018
	<b>Jumla</b>	<b>801,389,632</b>	

**Chanzo:** Notisi ya Kufungwa Benki husika kutoka Bodi ya Bima ya Amana

Utengaji wa hasara hii tarajiwa ya ushindwaji wa urejeshaji wa mikopo inaonesha kutokuwapo kwa uhakiki na uchunguzi wa kutosha wa uwezo wa kurejesha mikopo kwa wakopaji na usimamizi usioridhisha wa dhamana ambapo menejimenti imeshindwa kufanya uhakiki wa dhamana husika. Pia, sababu nyingine ni juhudi za ukusanyaji mikopo zisizo na tija. Athari za kutorejeshwa kwa mikopo husika ni pamoja na kupungua kwa uwiano wa faida na utoshelevu wa mtaji kwa Mfuko, ambako kunaweza kusababisha athari za kifedha kwa shughuli za ukopeshaji siku zijazo.

**Ninapendekeza kwamba Serikali, kupitia Mfuko wa Pembejeo za Kilimo, iboreshe udhibiti wa mifumo ya ndani katika ukusanyaji wa mikopo iliyosalia ili kuzuia hasara zaidi.**

### 8.2.8 Hasara ya Sh. Bilioni 5.73 Iliyotokana na Mikopo Isiyorejeshwa

Aya ya 7.4 ya Waraka Namba 3 wa tarehe 30 Juni 2011 (uliorekebishwa tarehe 22 Machi 2012) kuhusu mikopo ya fedha kwa watumishi wa Serikali kwa ajili ya ununuzi wa magari, pikipiki, samani, na ukarabati, inawataka maofisa masuuli kuhakikisha marejesho yanakatwa kwa wakati kutoka kwenye mishahara ya watumishi waliokopeshwa. Zaidi ya hayo, Aya ya 2.8 ya Mwongozo wa Uendeshaji wa Hazina ya Maendeleo wa Mwaka 2021 (Toleo lililorekebishwa mwezi Desemba 2022) inaeleza wajibu wa wakopaji, ikiwa pamoja na hitaji la kuijulisha Hazina iwapo makato ya mkopo kutoka kwenye mishahara yao hayaanza au yamesimamishwa.

Wakati wa mapitio ya uendeshaji wa Mfuko wa Mikopo kwa Watumishi wa Umma, nilibaini kuwa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 5.73 ilikuwa na

makato ambayo awali yalianza lakini yalisitishwa (yaliainishwa kwenye kundi la makato yaliyositishwa). Nilibaini kuwa kusitishwa kwa makato hayo kulitokana na sababu mbalimbali, ikiwa pamoja na vifo vya watumishi, kufukuzwa kazi, kujiuzulu, au kusitishwa kwa ajira kwa watumishi waliokopeshwa, pamoja na mabadiliko ya tasisi au udhaifu wa maofisa rasilimaliwatu wa kusitisha makato ya mikopo hiyo.

Pia, nilibaini kuwa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 2.10 ilikuwa na makato ambayo hayakuanza kwa sababu mikopo ilitolewa kwa wafanyakazi ambao mishahara yao halisi baada ya makato yote ilikuwa chini ya theluthi moja.

Ni maoni yangu kuwa kuna hatari ya watumishi kushindwa kunufaika na Mfuko wa Mikopo kwa Watumishi wa Umma kwa sababu ya hasara inayotokana na mikopo ambayo haijarejeshwa ya Sh. bilioni 5.73 na kuchelewa kwa marejesho ya mikopo ya Sh. bilioni 2.10.

**Ninapendekeza kwamba Serikali, kupitia Mfuko wa Mikopo kwa Watumishi wa Umma, iimarisha udhibiti wa mifumo ya ndani ili kutatua masuala ya mikopo ambayo makato yake yamekoma au hayaanza, pamoja na kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara wa malipo ya mikopo.**

### 8.3 Usimamizi wa Madeni

Nilifanya ukaguzi wa usimamizi na ulipaji wa madeni katika wizara, idara zinazojitegemea, na wakala za Serikali na kubaini yafuatayo:

#### 8.3.1 Malimbikizo ya riba ya Sh. Bilioni 103.22 kwa Kushindwa Kulipa Madai ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ya Ujenzi wa Daraja la Nyerere (Kigamboni)

Tarehe 20 Novemba 2014, Wizara ya Ujenzi iliingia mkataba na Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa Daraja la Kigamboni (Nyerere) na barabara zake Mkoani Dar es Salaam. Gharama zote za mradi zilikuwa dola za Marekani milioni 143.50, sawa na Sh. bilioni 238.71 (zilizorekebishwa mwaka 2016 hadi kufikia Sh. bilioni 328.90).

Kwa mujibu wa Ibara ya 2, 4, na 5 ya mkataba, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii ulitakiwa kuchangia 60% ya gharama za mradi huku Serikali ikitakiwa kuchangia 40%. Michango kutoka kwa kila muhusika ilipaswa kutolewa kwa kuzingatia madai ya kazi zilizokamilika, huku riba ikitozwa kwa ucheleweshaji



wa malipo baada ya siku 90 kulingana na kiwango cha riba cha Benki Kuu ya Tanzania. Pia, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii ulipewa haki za usimamizi wa daraja hilo kwa miaka 30 baada ya ujenzi, ikijumuisha ukusanyaji wa ushuru wa magari na pikipiki zinazovuka daraja hilo ili kurejesha uwekezaji wake.

Katika ripoti yangu ya mwaka wa fedha 2020/2021, nilibaini kuwa, kutokana na upungufu wa fedha Serikalini, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii ulitoka gharama zote za mradi. Serikali ilikubali kuurejeshea Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii Sh. bilioni 215.03, ikijumuisha gharama za ulipaji fidia wa eneo la ujenzi kiasi cha Sh. bilioni 14.14; asilimia 40 sawa na Sh. bilioni 124.54 ya mchango wa Serikali katika mradi; pamoja na riba ya Sh. bilioni 76.34 hadi tarehe 30 Juni 2021.

Hata hivyo, hadi kufikia mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023, Serikali haikuulipa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii jumla ya gharama za mradi wa Sh. bilioni 215.03 hivyo kusababisha riba iliyotokana na ucheleweshaji huo wa malipo kuongezeka kutoka Sh. bilioni 76.34 tarehe 30 Juni 2021 hadi Sh. bilioni 103.22 tarehe 30 Juni 2023.

Nilifahamishwa kuwa sababu kubwa ya kuchelewa kulipa madeni ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii ni kutotolewa kwa fedha na Wizara ya Fedha. Hivyo, ucheleweshaji huo wa malipo kwa Mfuko kunaweza kuhatarisha hali ya kifedha ya Mfuko na kusababisha ucheleweshaji wa malipo ya pensheni kwa wastaafu. Ucheleweshaji huo wa malipo ya pensheni unaweza kuathiri vibaya ustawi na ubora wa maisha ya wastaafu na wategemezi wao.

**Ninapendekeza Serikali kuhakikisha malipo ya fidia ya madai ya NSSF kwa mradi wa Daraja la Nyerere yanafanyika ili kulinda utulivu wa mfuko wa pensheni.**

### 8.3.2 Kutolipwa kwa Kodi ya Majengo Pamoja na Riba

Ukaguzi wangu katika Ubalizi wa Tanzania New York ulibaini kwamba majengo mawili yalikuwa yanadaiwa kodi ya majengo jumla ya dola za Marekani 847,888.40 sawa na Sh. bilioni 2.16 kutokana na majengo hayo kupoteza kinga ya kidiplomasia.

Ukaguzi wangu ulibaini zaidi kuwa jengo moja lililopo mtaa wa 307 East 53rd, New York, NY 10022, lilikuwa linadaiwa kodi ya majengo jumla ya dola za Marekani 661,753.83 hadi tarehe 2 Oktoba 2023 (sawa na Sh. bilioni 1.68) ikiwa

ni pamoja na riba ya kuchelewesha kulipa kodi ambayo itaendelea kuongezeka hadi malipo haya yatakapolipwa.

Jengo lingine lililopo Barabara ya 201 East, Mtaa wa 42, New York, NY 10017 5704, ambalo lilikuwa nyumba ya makazi ya Balozzi lililoachwa katika hali ya uchakavu tangu 2010, lilikuwa linadaiwa kodi ya majengo dola za Marekani 186,134.57 (sawa na Sh. milioni 474.64) iliyokuwa imechelewesha tangu mwaka 2006, kwa mujibu wa notisi kutoka kwa Mdhhibiti wa Jiji la Mount Vernon, N.Y. ya tarehe 24 Aprili 2023. Hiyo ilikuwa notisi ya tatu na ya mwisho kuhusu ulipaji wa kodi ya majengo inayodaiwa kabla ya Jiji kuanzisha hatua za kisheria kutwaa mali.

Ukaguzi zaidi ulibaini kwamba mwezi Julai 2023, Serikali ya Tanzania ilitoa kiasi cha dola za Marekani 620,715 sawa na Sh. bilioni 1.58 kwa ajili ya kulipa kodi ya majengo iliyokuwa kinadaiwa huku ikisubiri mrejesho kutoka kwa Ofisi ya Jiji la Mount Vernon kuhusu ombi la kufutiwa kodi hii ya majengo kwa kuzingatia kwamba hali ya jengo ilikuwa inakidhi vigezo vya kuwa na kinga ya kidiplomasia, na hivyo, Ubalozzi haukupaswa kutozwa kodi ya jengo hilo.

Aidha, Ubalozzi wa Tanzania New York unasubiri mrejesho kutoka Idara ya Majengo ya Jiji la New York kuhusu ombi la kuondolewa kwa faini na riba zilizolimbikizwa kama kodi ya jengo lilipo mtaa wa 53 307 E kabla ya kufanya malipo.

Hali hii ilitokana na kuchakaa kwa majengo ya Ubalozzi hivyo kupoteza kinga ya kidiplomasia. Hali hii inachafua sifa ya Tanzania na inaweza kusababisha mvutano wa kidiplomasia. Ni maoni yangu kwamba Serikali ya Tanzania inaweza kupata hasara ya Sh. bilioni 2.16 kwa malipo ya kodi ya majengo ambayo ingeweza kutumika kwa shughuli zingine za kibalozzi.

**Ninapendekeza kwamba Serikali, kupitia ubalozzi wake, ichukue hatua kwa kutafuta msamaha wa kodi na kulipa madeni ili kulinda taswira yake na kuepusha hasara za kifedha zinazoweza kutokea.**

### **8.3.3 Ongezeko la Deni Linalotokana na Kupanda kwa Viwango vya Kubadilisha Fedha za Kigeni**

Ukaguzi wangu katika Jeshi la Polisi Tanzania ulibaini kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023, Jeshi la Polisi lilikuwa na jumla ya madeni yenye thamani ya Sh. bilioni 621.9. Kati ya hizo, Sh. bilioni 268.61 zilikuwa madeni kwa wazabuni watatu wa kigeni sawa na dola za Marekani 114,837,957.02. Kati ya madeni

hayo, dola za Marekani 40,538,708 zilikuwa zinadaiwa na wazabuni wawili tangu mwaka 2015. Dola za Marekani 74,299,249 zilikuwa zinadaiwa na mzabuni mmoja tangu mwaka 2017.

Uchambuzi wangu ulibaini kuwa, endapo Jeshi la Polisi lingelipa madeni haya kwa wakati, lingelipa jumla ya Sh. bilioni 244.51, sawa na dola za Marekani 114,837,957.02 kwa wakati huo. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023, malipo haya hayakuwa yamelipwa, hivyo Jeshi la Polisi kudaiwa jumla ya Sh. bilioni 268.61, sawa na dola za Marekani 114,837,957.02. Hii inaonesha ongezeko la Sh. Bilioni 24.10, sawa na asilimia 10 kutoka kiasi ambacho kingelipwa kwa wakati. Aidha, kutokana na kupanda kwa viwango vya kubadilisha fedha za kigeni kwa mwaka wa fedha 2022/23 pekee, kulikuwa na ongezeko la Sh. bilioni 2.69 kutoka Sh. bilioni 265.92 za tarehe 30 Juni 2022.

Ni maoni yangu kuwa, ongezeko kubwa la deni kama hilo limechangiwa na kucheleweshwa kwa malipo ambayo yanatokana na kuchelewa kupokea fedha kutoka Hazina. Sababu nyingine ni udhaifu katika kuchagua mikakati ya kujikinga na mabadiliko ya fedha za kigeni wakati wa makubaliano ya malipo na wazabuni.

Kushindwa kulipa madeni haya kunaweza kusababisha ongezeko endelevu la deni kwa kutokana na kuendelea kupanda kwa viwango vya kubadilisha fedha za kigeni, hivyo kusababisha uhaba wa fedha zitakazotengwa kwa matumizi mengine.

**Ninapendekeza kwamba Serikali, kupitia Wizara ya Fedha, ihakikishe fedha zinatolewa kwa wakati kulipa madeni na kutumia njia za kujilinda dhidi ya mabadiliko ya fedha za kigeni kwa mikataba iliyosainiwa katika fedha za kigeni, kupunguza hatari za mabadiliko ya fedha za kigeni.**

#### **8.3.4 Madeni Yaliyokaa Muda Mrefu bila Kulipwa katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, na Wakala za Serikali**

Kifungu cha 44(1) cha Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 kinaeleza kwamba, ili kuzisaidia kampuni za ndani na kuziwezesha kutekeleza majukumu yao ya mkataba, taasisi nunuzi lazima zihakikishe malipo yanafanyika kwa wakati kwa wazabuni. Pia, Kanuni E. 23 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za Mwaka 2009 inataka madai ya wafanyakazi kulipwa wakati yanapojitokeza.

Hata hivyo, baada ya kukagua na kuthibitisha taarifa za kifedha za wizara, idara zinazojitegemea, na wakala za serikali, nilibaini kuwapo kwa madeni ambayo hayakulipwa yenye thamani ya Sh. trilioni 3.39 kufikia tarehe 30 Juni 2023 katika taasisi 20 kama zinavyoonekana katika **Kiambatisho Na. VIII**. Kati ya kiasi hicho, Sh. bilioni 228.16 (7%) zilikuwa madai ya wafanyakazi; Sh. trilioni 1.37 (40%) zilikuwa madeni ya wazabuni; na Sh. trilioni 1.79 (53%) zilikuwa madeni mengine.

Jambo la kuzingatiwa ni kwamba madeni yenye thamani ya Sh. trilioni 1.88 (56%) ni ya muda mrefu, yakiwa yamelimbikizwa kwa zaidi ya miezi 12; na madeni yenye thamani ya Sh. trilioni 1.51 (44%) ni ya kipindi cha chini ya miezi 12. Takwimu hizi zinaonesha umuhimu wa kuweka jitihada zaidi ili kuzuia madeni haya kuongezeka zaidi.

Kuwapo kwa madeni ya muda mrefu kumesababishwa na ufinyu wa bajeti, Wizara ya Fedha kuchelewa kutoa fedha, na kusubiri uhakiki kutoka kwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali.

**Ninapendekeza kwamba Serikali, kupitia Wizara ya Fedha, itoe kipaumbele katika utoaji wa fedha kwa ajili ya kulipa madeni ili kupunguza hatari zinazoweza kutokea kwa kuchelewesha malipo.**

### 8.3.5 Kuwapo kwa Madeni Tarajiwa

Madeni tarajiwa yanajumuisha madeni yanayoweza kutokea kutokana na maamuzi yanayotarajiwa na ambayo yapo nje ya uamuzi wa taasisi. Katika ukaguzi wangu wa madeni tarajiwa katika taasisi za serikali, nilibaini kuwapo kwa mashauri ya kisheria yanayosubiri uamuzi wa mahakama ambayo yametokana na matukio mbalimbali. Mashauri hayo yanahusiana na madai ya wafanyakazi baada ya kustaafu, posho za uhamisho, migogoro ya ardhi, ukiukaji wa matakwa ya mikataba, na mambo mengine ambayo taasisi hizi ni washtakiwa. Nilibaini kuwa taasisi 17 zilikuwa na mashauri katika mahakama mbalimbali, kila moja ikiwa katika hatua tofauti za usikilizaji, zikitakiwa kulipa fidia zinazokadiriwa kuwa Sh. bilioni 626.89 hadi tarehe 30 Juni 2023 kama **Jedwali Na. 43** linavyoonesha.

Kwa kiasi kikubwa, kesi hizi zimetokana na migogoro ya ardhi, madai ya wafanyakazi baada ya kustaafu, na ukiukwaji wa masharti ya mikataba.

**Jedwali Na. 43: Taasisi Zenye Madeni Tarajiwa**

Na.	Taasisi	Kiasi (Sh.)
1	Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa	562,952,633,000
2	Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi	16,540,000,000
3	Wakala wa Nishati Vijijini	15,784,715,000
4	Wakala wa Majengo Tanzania	6,761,962,512
5	Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania	6,097,487,009
6	Wizara ya Kilimo	5,923,266,075
7	Wakala wa Barabara Tanzania	4,262,154,961
8	Wizara ya Maliasili na Utalii	3,258,176,993
9	Idara ya Mhasibu Mkuu	1,446,126,162
10	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	810,893,523
11	Jeshi la Polisi Tanzania	653,488,612
12	Shirika la Mzinga	649,533,504
13	Kampuni Tanzu ya Mzinga	641,572,583
14	Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara	469,809,882
15	Taasisi ya Uhasibu Tanzania	404,866,000
16	Wizara ya Fedha - Huduma za Hazina	194,306,977
17	Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Afrika cha Nelson Mandela	45,500,000
	<b>Jumla</b>	<b>626,896,492,793</b>

**Chanzo:** Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti za mwaka 2022/23

Kwa maoni yangu, kama taasisi hizi zitashindwa katika mashauri haya, Serikali itapoteza fedha nyingi, na kama vyanzo vya mashauri havitashughulikiwa, vinaweza kusababisha kasoro hizi kujirudia.

**Ninapendekeza Serikali kutoa msaada wa kisheria kwa taasisi zilizopo katika mashauri ya kisheria yanayoendelea, na kutoa ushauri wa kisheria unaohitajika ili kuhakikisha uamuzi wenye manufaa au kutumia njia mbadala za utatuzi.**

# SURA YA TISA



## USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU, MISHAHARA, NA MAFAO YA WASTAAFU

### 9.1 Utangulizi

Katika sura hii, ninaelezea matokeo niliyoyabaini wakati wa ukaguzi yanayohusiana na usimamizi wa rasilimaliwatu, mishahara, na mafao ya wastaafu katika taasisi mbalimbali za Serikali.

### 9.2 Usimamizi wa Rasilimaliwatu

#### 9.2.1 Kutolipwa Sh. Bilioni 18.25 za Posho ya Mazingira Magumu

Kanuni ya 46(1) ya Kanuni za Utumishi wa Magereza ya Mwaka 1997 inawataka maafisa magereza wote wawe na haki ya kupata posho ya mazingira magumu, usafiri, na posho ya kazi za usiku.

Wakati wa ukaguzi wangu nilibaini kuwa Idara ya Jeshi la Magereza (Fungu 29) ilitenga bajeti ya Sh. bilioni 18.25 kwa ajili ya posho ya mazingira magumu, ambayo ni sawa na asilimia 15 ya mishahara. Hata hivyo, katika mwaka wa fedha 2022/23, maafisa wa magereza hawakulipwa posho zao za mazingira magumu kutokana na kutopewa fedha kutoka Hazina. Kutolipwa kwa posho za mazingira magumu kwa maafisa wa Magereza kunaweza kuathiri ari ya ufanyaji kazi na ustawi wao.

Ninapendekeza Serikali ifanye mapitio ya kina ya mgawanyo wa bajeti kwa ajili ya posho za mazingira magumu kwa maafisa wa Magereza na kuboeshwa bajeti kuhakikisha ustawi wa maafisa wa Magereza.

#### 9.2.2 Kutowasilisha Makato ya Mishahara Yenye Thamani ya Sh. Bilioni 1.06 katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Taasisi

Vifungu Na. 18 na 19 vya Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya Mwaka 2018 vinaelezea wajibu wa waajiri kukata asilimia 20 ya mishahara wa kila mwezi wa kila mfanyakazi na kuwasilisha kwenye mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Kushindwa

kuwasilisha kwa wakati makato hayo kutasababisha adhabu sawa na asilimia 1.5 ya kiasi ambacho mwajiri ameshindwa kuwasilisha kama inavyotakiwa na sheria. Vilevile, Kifungu Na. 8 cha Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ya Mwaka 1999 na Kifungu Na. 84 cha Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332 (iliyorekebisha mwaka 2019) vinataka taasisi kuwasilisha makato kila mwezi; na, kwamba, kushindwa kuwasilisha kwa wakati makato hayo kutasababisha adhabu kwa taasisi husika.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa taasisi 17 hazikuwasilisha makato ya kisheria ya kiasi cha Sh. bilioni 1.06 kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (PSSSF na NSSF), Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Kutowasilisha makato kunaathiri na kunaweza kuwakosesha watumishi haki na faida zinazotokana na kujiunga na mifuko ya jamii na afya. Pia, taasisi zilizoshindwa kuwasilisha makato kwa wakati zinaweza kupata adhabu hivyo kulipa malipo yasiyo na tija na kuathiri utekelezaji wa shughuli zingine zilizopangwa. **Jedwali Na. 44** linaonesha taasisi ambazo hazikuwasilisha makato ya mishahara ya wafanyakazi kwenye mifuko na mamlaka husika.

**Jedwali Na. 44: Taasisi ambazo Hazikuwasilisha Makato ya Mishahara**

Na.	Taasisi	Mlipwaji	Kiasi (Sh.)
1	Msajili wa Vyama vya Siasa	Mamlaka ya Mapato Tanzania (LIKU)	3,079,500
2	Shule ya Sekondari Kawawa	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii	37,375,740
3	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Bunda	Mamlaka ya Mapato Tanzania (LIKU)	55,773,267
		Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya	20,539,680
		Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma	65,074,001
4	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Busega	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma	20,874,560
5	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Ifakara	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma	890,500
6	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kasulu	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma	46,040,000
7	Wakala wa Vyu vya Mafunzo ya Mifugo	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma	7,847,105
8	Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Tanganyika	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii	3,155,000
9	Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini	Mfuko wa Fidia kwa Wafanyazi	2,436,890
		Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya	11,386,320
		Mamlaka ya Mapato Tanzania (LIKU)	18,543,328

Na.	Taasisi	Mlipwaji	Kiasi (Sh.)
		Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii	40,886,000
		Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu	4,848,000
10	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Wanging'ombe	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma	108,628,720
11	Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma	58,928,813
12	Mamlaka ya Mapato Tanzania - Matumizi	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma	88,442,137
13	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Tanga	Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya	35,408,970
		Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma	118,029,900
14	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Maswa	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma	232,247,793
15	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Makete	Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya	788,039
16	Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma	58,291,704
17	Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji (CBWSO)	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa watumishi wa Umma	21,523,000
	<b>Jumla</b>		<b>1,061,038,967</b>

Chanzo: Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti Mwaka 2022/2023

Ninapendekeza Serikali ifanye uhamasishaji ili kuwaelimisha waajiri kuhusu majukumu yao ya kuwasilisha makato ya kisheria na athari za kutofuata kanuni ili kuzuia kuendelea kujitokeza tena. Pia kuwasilisha makato hayo kwa taasisi husika bila kuchelewa zaidi.

### 9.3 Ukaguzi wa Awali wa Mafao

#### 9.3.1 Madhumuni ya Ukaguzi wa Awali

Ukaguzi wa awali wa mafao ya wastaafu unafanyika ili kubaini uhalali na usahihi wa malipo ya mafao ya wastaafu na utoshlevu wa taarifa zilizoambatishwa. Ukaguzi huu huwezesha kutambua makosa kabla ya malipo kufanyika. Kwa kuhakikisha usahihi na ukamilifu wa taarifa za malipo ya mafao ya wastaafu, zoezi la ukaguzi wa awali ni muhimu katika kupunguza upotevu wa fedha na kupunguza hatari ya matumizi mabaya ya fedha za Umma.



### 9.3.2 Mawanda ya Ukaguzi wa Awali

Ukaguzi wa awali wa mafao unahusisha watumishi wa umma ambao mafao yao yanalipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina. Mafao hayo yanajumuisha pensheni na kiinua-mgongo kwa watumishi wa umma wenye utumishi mchanganyiko; maafisa wa Jeshi la Wananchi Tanzania; maafisa wa Usalama wa Taifa; mafao kwa watumishi waliomaliza mikataba ya uongozi wa kisiasa; watumishi wasio raia wa Tanzania; wastaafu waliorejeshwa kwenye utumishi; raia walioajiriwa wakiwa na umri wa zaidi ya miaka 45 ambao ni watumishi wenye masharti ya mikataba; na mafao kwa watumishi wasio kwenye masharti ya pensheni.

### 9.3.3 Utekelezaji wa Ukaguzi wa Awali

Ukaguzi wangu ulianza na majalada 149 ikiwa ni bakaa kutoka mwaka wa fedha 2021/2022. Majalada 3,193 yaliwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 na kufanya jumla ya majalada 3,342 yaliyokuwapo kwa ukaguzi wa awali. Hali ya ukaguzi wa majalada ikilinganishwa na mwaka uliopita imeoneshwa katika Jedwali Na. 45.

**Jedwali Na. 45: Majalada ya Wastaafu Yaliyokaguliwa katika Mwaka 2022/23**

Maelezo	2022/23	2021/22
Majalada yaliyokuwapo tarehe 1 Julai 2022	149	137
Majalada yaliyopokelewa	3,193	3,095
Jumla ya majalada yaliyokuwapo kwa ukaguzi	3,342	3,232
Majalada yaliyokaguliwa na kuidhinishwa	2,873	2,867
Majalada yaliyokaguliwa na kurejeshwa kwa maafisa masuuli yakiwa na hoja	388	216
<b>Majalada yaliyosalia hadi tarehe 30 Juni 2023 (Yaliyo katika ukaguzi)</b>	<b>81</b>	<b>149</b>

Chanzo: Kitabu cha usajili wa majalada na "PPAMS"

## 9.4 Matokeo ya Ukaguzi wa Awali wa Majalada ya Mafao

Wakati wa ukaguzi wa awali wa mafao ya wastaafu kwa mwaka wa fedha 2022/2023, nilibaini masuala kadhaa kama yalivyofafanuliwa hapa chini:

### 9.4.1 Kukosewa kwa Ukokotoaji wa Mafao na Waajiri

Mapitio yangu ya majalada 2,873 yaliyoidhinishwa kwa malipo, yalibaini majalada 41 (1%) ya wastaafu yalilikotolewa kimakosa. Makosa hayo yalitokana na kutumia muda wa utumishi usio sahihi; kutumia mishahara isiyo sahihi; kutoa michango ya mwajiri isiyo sahihi; na makosa mbalimbali ya ukokotoaji wa

mafao. Hata hivyo, makosa hayo yalirekebisha na majalada hayo niliyaidhinisha kwa malipo.

Miongoni mwa majalada 41 ya mafao ya wastaafu yaliyokokotolewa kimakosa, majalada 23 (56%) yalidikotolewa zaidi ya kiwango stahiki kwa Sh. milioni 110.05 na majalada 18 (44%) yalidikotolewa kwa kiwango pungufu kwa Sh. milioni 138.78. Muhtasari wa idadi ya majalada na makosa yaliyobainika umeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 46**.

**Jedwali Na. 46: Majalada ya Mafao Yaliyokokotolewa Kimakosa**

Na.	Aina ya Kosa	Mafao Yaliyozidi		Mafao Yaliyopungua	
		Idadi ya Majalada	Kiasi (Sh.)	Idadi ya Majalada	Kiasi (Sh.)
1	Muda wa utumishi usio sahihi	17	72,471,601	11	64,101,972
2	Mishahara iliyokosewa	6	37,582,426	5	66,995,871
3	Makosa katika michango ya hifadhi ya jamii	0	0	1	88,064
4	Makosa mbalimbali katika ukokotoaji	0	0	1	7,600,000
	<b>Jumla</b>	<b>23</b>	<b>110,054,027</b>	<b>18</b>	<b>138,785,908</b>

**Chanzo:** Fomu za malipo ya mafao na uhakiki wa ukaguzi

Sababu zilizobainishwa zilikuwa upungufu katika kukokotoa mafao kutokana na makosa katika hesabu, tafsiri isiyo sahihi ya sera za mafao, dosari za ujazaji wa taarifa, na kutokuwapo kwa uhakiki wa kutosha wa uthibitishaji ili kutambua na kurekebisha makosa wakati wa mchakato wa ukokotoaji.

Bila ukaguzi wangu wa awali, Serikali ingeweza kupata hasara ya Sh. milioni 110.05 kutokana na ukokotozi uliozidi kiasi stahiki, na wastaafu wangepata mapunjo ya jumla ya Sh. milioni 138.78.

Upungufu uliobainishwa unaonesha kuwapo kwa thamani iliyoongezwa na ukaguzi wa awali wa mafao na malipo mengine yanayolipwa moja kwa moja kutoka kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina. Pia, unaonesha mapungufu ya udhibiti wa ndani hivyo kusababisha hasara kwa Serikali na mapunjo kwa wastaafu.

**Ninapendekeza Serikali iweke utaratibu mzuri wa kukokotoa mafao ya wastaafu, kabla ya kuwasilisha kwa ajili ya ukaguzi wa awali ili kuhakikisha wastaafu wanalipwa kwa wakati.**

### 9.4.2 Ucheleweshaji wa Uandaaji na Uwasilishwaji wa Taarifa za Mafao

Kanuni ya 88 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2022 inawataka waajiri na waajiriwa kutunza kumbukumbu za ajira kwa madhumuni ya marejeo wakati wa kukokotoa mafao ya kustaafu ya mwajiriwa.

Pia, Kanuni Na. F. 48 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za Mwaka 2009 ikisomwa pamoja na Kanuni ya 32(4) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2022 inamtaka mtumishi wa umma anayekaribia kustaafu kutoa taarifa kwa maandishi kuhusu nia yake ya kustaafu kwa mamlaka yake ya uteuzi kupitia njia za kawaida, angalau miezi sita kabla ya tarehe ya kustaafu.

Katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2022/2023, nilibaini waajiri waliochelewa kutayarisha na kuwasilisha majalada ya mafao ya wastaafu 414 (ambayo ni 13% ya majalada yote yaliyowasilishwa) kwa ajili ya ukaguzi wa awali kwa muda wa kuanzia mwaka mmoja hadi miaka 28. Kucheleweshwa kwa malipo ya wastaafu huathiri vibaya hali ya maisha ya wastaafu, kwani wengi wao hutegemea mafao ya kustaafu ili kukidhi mahitaji yao ya kila siku. **Jedwali Na. 47** linaonesha muhtasari wa idadi ya majalada ya mafao ya wastaafu na kiwango cha ucheleweshaji wao.

#### Jedwali Na. 47: Majalada Yaliyochelewa Kuandaliwa na Kuwasilishwa

Muda wa Ucheleweshwaji wa Majalada	Idadi ya Majalada
Hadi miaka 2	250
Hadi miaka 5	109
Hadi miaka 10	30
Hadi miaka 20	17
Hadi miaka 28	8
<b>Jumla</b>	<b>414</b>

Chanzo: Fomu za malipo ya mafao na uhakiki wa ukaguzi

Ninapendekeza Serikali ihakikishe uwasilishaji kwa wakati wa majalada kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na utekelezaji wa hatua za kushughulikia upungufu uliopo kwa kuanzisha utaratibu wa ufuatiliaji wa waajiri, ikiwa pamoja na kuanzisha mfumo wa ufuatiliaji kwa ajili ya uhakiki wa ufanisi na utatuzi kwa wakati wa upungufu.

### 9.4.3 Majalada Yenye Hoja a mbayo Hayakurejeshwa kwa Ukaguzi wa Awali

Kanuni ya 86 (2) ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za Mwaka 2009, Sura ya 47 inawataka maofisa masuuli kujibu hoja ya ukaguzi ndani ya siku 21 tangu siku ya kupokelewa.

Hadi tarehe 30 Juni 2023, kulikuwa na majalada 388 yenye kasoro ambayo hayakurejeshwa kwangu kutoka kwa waajiri. Majalada 41 kati ya hayo yalihatiji waajiri kuyarekebisha na kuyarejesha ofisini kwangu kwa ukaguzi na kuidhinishwa. Hata hivyo, hadi tarehe 30 Juni 2023, majalada hayo yalikuwa hayajarejeshwa. Kati ya majalada 41, majalada 31 (76%) yalikuwa yamekaa kwa muda wa kuanzia mwaka mmoja hadi miaka sita kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 48**. Majalada 347 yaliyobaki yanahusiana na wastaafu waliokuwa katika masharti ya kawaida ambao hawakustahili malipo ya kiinua mgongo kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina.

#### Jedwali Na. 48: Majalada yenye Hoja ambayo Hayakurejeshwa kwa Ukaguzi wa Awali

Na.	Muda wa Ucheleweshaji wa Majalada	Idadi ya Majalada
1	Mwaka 1	7
2	Kati ya Mwaka 1 mpaka miaka 3	11
3	Kati ya Miaka 3 mpaka miaka 6	13
<b>Jumla</b>		<b>31</b>

Chanzo: Kitabu cha usajili wa majalada na PPAMS

Ninapendekeza Serikali iweke kipaumbele katika kushughulikia kwa wakati hoja za ukaguzi, kuwezesha uidhinishaji wa malipo kwa wastaafu, na kuzuia ucheleweshaji wa kushughulikia mafao ya wastaafu.



## UFANISI KATIKA UTENDAJI

### 10.1 Utangulizi

Pamoja na ukaguzi wa kawaida unaohusisha ukaguzi wa kifedha na uzingatiaji wa sheria, pia nilipitia ufanisi katika uendeshaji wa shughuli za taasisi za serikali. Ukaguzi huu unalenga kutambua maeneo yanayohitaji maberesho ili kuongeza ufanisi kwenye utendaji wa shughuli za serikali. Ukaguzi huu unalenga kuangalia maeneo katika shughuli za serikali, ikiwa ni pamoja na udhibiti wa ndani, taratibu, na mifumo. Kwa kuchambua maeneo hayo, ukaguzi huu unatoa taswira kuhusiana na usimamizi wa rasilimali za serikali.

Sura hii inaainisha madhaifu yaliyobainika katika ukaguzi wa ufanisi wa utendaji katika taasisi za serikali, yanayohitaji maboresho. Taasisi hizi zinahusiana na shughuli za serikali za kiuchumi, kiutawala, na masuala ya kijamii.

### 10.2 Usimamizi wa Fedha

Ukaguzi niliufanya katika usimamizi wa fedha, ulibaini udhaifu katika wizara, idara na wakala za serikali kama yanayofafanuliwa hapa chini:

#### 10.2.1 Gharama za ziada Sh. Bilioni 13 katika Uboreshaji kwa Kiwango cha Lami wa Barabara ya Tanga - Pangani (kilomita 50)

Tarehe 31 Julai 2019, Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) iliingia mkataba na Kampuni ya M/S China Henan International Cooperation Group (TRD/HQ/1008/2019/2020) kwa ajili ya uboreshaji wa Barabara ya Bagamoyo (Makurunge) - Saadani - Pangani - Tanga yenye urefu wa kilomita 256 kwa kiwango cha lami, sehemu ya kwanza ya Pangani - Tanga (km 50), kwa mkataba wa Sh. bilioni 69 (bila kodi ya ongezeko la thamani). Hapo awali, muda wa mkataba uliisha tarehe 14 Novemba 2021 lakini uliongezwa hadi tarehe 5 Desemba 2022 na baadaye ukaongezwa hadi tarehe 21 Novemba 2023. Usimamizi wa mkataba ulikuwa chini ya mshauri elekezi Kampuni ya DOCHCH

Engineering and Management Consultancy ambaye alianza kazi tangu mradi ulipoanza.

- a) Nilibaini kuwa kazi za ujenzi wa mradi ilivuka muda wa kukamilika kwake tarehe 5 Disemba 2022 kutokana na sababu mbalimbali, ikiwemo ucheleweshaji wa malipo ya awali na hati za malipo ya muda (IPCs); mkandarasi kuchelewa kukabidhiwa eneo kwa sababu ya ucheleweshaji wa kulipa fidia kwa watu walioathiriwa na mradi; kuchelewa kuhamisha miundombinu ya huduma mbalimbali; na kuchelewa kupatiwa eneo la daraja la Kirare. Hivyo, mkandarasi aliomba kuongezewa muda ili kufidia ucheleweshaji huo na kusababisha gharama za ziada za Sh. bilioni 2.
- b) Aidha, mapitio yangu ya hati namba 13 ya malipo ya muda ya tarehe 2 Februari 2023 yalibaini makosa kwenye kiasi kilichoainishwa katika maelezo ya vipimo (BOQ), hususani katika kipengele cha uchimbaji na ujazaji kifusi kutoka vyanzo vingine. Maelezo ya vipimo awali yalitaja mita za ujazo 26,000 kwa kipengele cha uchimbaji, huku upimaji ukionesha kipimo halisi kilichohitajika ni mita za ujazo 502,875.58. Vilevile, maelezo ya vipimo ya awali yalionesha mita za ujazo 200 za kujaza kifusi kutoka vyanzo vya nje, ambapo kiasi halisi kilichopimwa wakati wa ukaguzi kilikuwa mita za ujazo 3,854.697. Tofauti hizi kati ya kiasi halisi kilichopimwa na maelezo ya vipimo ya awali zilisababisha ongezeko la gharama la Sh. bilioni 11.

Kutokana na hayo, jumla ya gharama za ziada za mradi zilifikia Sh. bilioni 13, ikiwa ni ongezeko la asilimia 17 kutoka gharama za awali kwenye mkataba. Nilibaini kuwa gharama za ziada zilichangiwa na usanifu na uhakiki usioridhisha ambao ulishindwa kuakisi vipimo halisi vilivyohitajika katika eneo la ujenzi. Ukiukaji huu unaweza kusababisha kuchelewa kukamilika kwa mradi na kusababisha usumbufu kwa watumiaji barabara. Pia, unaweza kuathiri bajeti ya serikali kwa kuhitaji fedha za ziada kugharamia kazi hizo zilizoongezeka.

**Ninapendekeza Serikali iimarisha mfumo wa usimamizi wa TANROADS ili kuzuia gharama za ziada katika miradi ya ujenzi wa barabara.**

### **10.2.2 Upungufu wa fedha Sh. bilioni 1.83 za Kugharamia shughuli za uendeshaji wa kivuko baada ya kukodi kivuko kutoka Kampuni ya Azam Marine LTD**

Tarehe 14 Juni 2022, Wakala wa Huduma za Umeme Tanzania (TEMESA) uliingia mkataba wa makubaliano (MoU) na Kampuni ya AZAM Marine Ltd ya kukodi na

kuendesha vivuko viwili vya baharini ‘Sea Taxi 1’, na ‘Sea Taxi 2’ kati ya Magogoni na Kigamboni. Mpango huu ulilenga kuongeza uwezo wa Wakala wa Huduma za Umeme Tanzania kuhudumia wateja kufuatia ukarabati mkubwa wa Kivuko cha MV Magogoni. Kila kivuko kilikuwa na uwezo wa kubeba abiria 250 kwa kila safari.

Kwa mujibu wa Kifungu Na. 5 cha Mkataba wa Makubaliano, mkodishwaji (Wakala wa Huduma za Umeme Tanzania), analazimika kuilipa Kampuni ya AZAM Marine Ltd ada ya huduma kila siku ya Sh. milioni 5 (pamoja na kodi ya ongezeko la thamani) pamoja na kodi ya zuio ya asilimia 5. Mkodishaji, Kampuni ya AZAM Marine Ltd itatoa ankara ya malipo kila mwezi inayoeleza idadi ya siku ambazo huduma ilitolewa kwa mkodishwaji katika mwezi husika.

Nilibaini kuwa kuanzia tarehe 1 Julai 2022 hadi tarehe 30 Juni 2023, Wakala wa Huduma za Umeme Tanzania ulikusanya jumla ya Sh. bilioni 5.76 za tozo za vivuko katika Kituo cha Magogoni - Kigamboni. Kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 1.83 (sawa na asilimia 31 ya makusanyo yote) zililipwa kwa Kampuni ya AZAM Marine Ltd kwa ajili ya uendeshaji wa vivuko viwili. Kutokana na hali hiyo, Wakala wa Huduma za Umeme Tanzania ulibakiwa na Sh. bilioni 3.93 (asilimia 69) ili kulipia gharama za uendeshaji kama vile mafuta ya vivuko, gharama za kazi, ukarabati na matengenezo, na gharama zinginezo. Hata hivyo, kiasi kilichobaki cha Sh. bilioni 3.93 kilikuwa hakitoshi kulipa gharama hizo, hivyo kusababisha Wakala wa Huduma za Umeme Tanzania kutumia fedha za vyanzo vingine kugharamia uendeshaji wa kituo cha Magogoni - Kigamboni.

Kwa maoni yangu, kuendelea kukodisha vivuko kutoka kwa kampuni ya AZAM Marine Ltd kunaathiri uendelevu wa huduma ya kivuko katika Kituo cha Magogoni - Kigamboni. Hali hii inasabisha Wakala kuendelea kutegemea ruzuku ya serikali kugharamia shughuli zake badala ya kujitegemea.

**Ninapendekeza TEMESA itathmini mikakati mbadala ya kupunguza utegemezi wa vivuko vya mwendokasi vilivyokodishwa, ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi ya vivuko ili kukabiliana na ongezeko la wateja.**

### **10.2.3 Malipo pungufu ya asilimia 3 ya tozo ya umeme kutoka Shirika la Umeme Tanzania kutokana na kutoripoti mauzo ya umeme Sh. Bilioni 9.05**

Kifungu cha 19(3)(c) cha Sheria ya Nishati Vijijini ya Mwaka 2005 kinautaka Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kukusanya tozo za hadi asilimia tano za

kuzalisha umeme wa kibiashara kwenye gridi ya taifa, ambazo zitatumwa kwenye Mfuko wa Nishati Vijijini ifikapo mwisho wa kila mwezi. Kwa mujibu wa kifungu hicho, tarehe 01 Agosti 2008, Waziri wa Nishati kupitia tangazo la Serikali Namba 118 lililochapishwa kwenye Gazeti la Serikali, alitoa agizo linalotamka kuwa tozo ya umeme itakuwa asilimia tatu kwenye mauzo ya umeme.

Wakala wa Nishati Vijijini inategemea kupata taarifa za mauzo ya umeme kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kupitia uwasilishaji wa majedwali ya mauzo ya umeme. Utaratibu huu unauwezesha Wakala wa Nishati Vijijini kuandaa ankara za kudai asilimia 3 ya mauzo ya umeme yanayokusanywa na Shirika la Umeme Tanzania.

Wakati wa mapitio yangu ya ripoti za usuluhishi uliofanyika mwezi Mei 2023, nilibaini kuwa Shirika la Umeme Tanzania lilifanya mauzo ya umeme ya Sh. trilioni 3.25 (bila kodi ya ongezeko la thamani) kuanzia tarehe 30 Julai 2021 hadi 30 Aprili 2023, hivyo kufanya madai ya asilimia 3 ya tozo ya umeme kwa Wakala wa Nishati Vijijini kuwa Sh. bilioni 97.73. Hata hivyo, nilibaini kuwa Shirika la Umeme Tanzania liliwasilisha jedwali la mchanganuo wa asilimia 3 ya tozo ya umeme lililoonesha tozo ya Sh. bilioni 88.68 tu kuanzia tarehe 1 Julai 2021 hadi 30 Aprili 2023 na kuulipa Wakala wa Nishati Vijijini kiasi hicho, hivyo kusababisha malipo pungufu ya tozo ya umeme kwa Sh. bilioni 9.05. Hali hiyo inaashiria kuwa Shirika la Umeme Tanzania liliwasilisha taarifa za mauzo pungufu ya umeme kwa Wakala wa Nishati Vijijini na kutumia tozo za umeme zilizokusanywa kwa niaba ya Wakala wa Nishati Vijijini hivyo kuathiri shughuli zake.

Zaidi ya hayo, ripoti ya usuluhishi ilibainisha kuwa sababu kuu ni kutokuwapo kwa muunganiko wa mfumo wa Shirika la Umeme Tanzania, yaani mfumo unaotumiwa kukusanya tozo za umeme na mfumo unaotumika kukokotoa na kuwasilisha malipo ya ankara za umeme kwa Wakala wa Nishati Vijijini.

**Kwa kuwa Mfumo wa Mita za Lipia Kabla ya Matumizi (LUKU) unatoa mchanganuo wa makusanyo ya ankara za umeme, ikiwa ni pamoja na tozo ya asilimia 3 ya umeme kwa REA, napendekeza REA, kwa kushirikiana na TANESCO, ipewe uwezo wa kuingia katika Mfumo wa LUKU ili kupata taarifa sahihi za kiasi cha tozo ya 3% ya umeme kilichokusanywa na TANESCO ili uandaaji ankara zinazoakisi uhalisia wa makusanyo hayo. Aidha, Serikali ihakikishe TANESCO inalipa kiasi hicho kilichobakia kwa REA kama inavyotakiwa na Sheria ya Nishati Vijijini.**



#### 10.2.4 Kutolipwa kwa fedha dola za Marekani 8,144,114.52 (Sh. Bilioni 18.94) za adhabu (demurrage) Zilizotokana na Kuchelewa Kushusha Mafuta kutoka kwenye Meli

Kifungu cha 18.1 cha mkataba kati ya wasambazaji wa mafuta<sup>10</sup> na kampuni za uuzaji wa mafuta<sup>11</sup> kinamtaka msambazaji wa mafuta awe na haki ya kutoza fedha za ucheleweshaji wa ushushaji wa mafuta isiyozidi dola za Marekani 22,000 kwa mafuta ya petroli na dola za Marekani 18,000 kwa mafuta ya dizeli kwa siku. Zaidi ya hayo, kifungu cha 18.9 kinabainisha kuwa, kampuni za uuzaji wa mafuta zitalipa gharama za tozo hizo ndani ya siku 14 baada ya kupokea ankara kutoka kwa msambazaji wa mafuta.

Fedha ya adhabu ni ada inayotozwa kwa mmiliki wa bidhaa au chombo kwa kuchelewa kupakia au kushusha mizigo zaidi ya muda uliopangwa kwenye mkataba. Ni adhabu iliyoundwa ili kuhimiza ushushaji wa haraka wa mizigo na kufidia gharama za mhusika wakati akisubiria mzigo.

Wakati wa ukaguzi wa Wakala wa Ununuzi wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA) niligundua kuwa wasambazaji wa mafuta walitoa ankara kwa kampuni za uuzaji mafuta zenye jumla ya dola za Marekani 8,144,114.52 (Sh. bilioni 18.94) kuanzia mwezi Februari 2019 hadi Agosti 2022 kama tozo za adhabu kwa kuchelewa kupakua mafuta kwenye meli, unaochangiwa na uhaba wa miundombinu ya upakuaji wa mafuta na mambo mengine yaliyosababishwa na kampuni za uuzaji mafuta. Hata hivyo, hadi wakati wa ukaguzi wangu mwezi Oktoba 2023, kampuni za uuzaji mafuta zilikuwa hazijalipa kiasi hicho kwa wasambazaji hao kwa zaidi ya mwaka mmoja, licha ya kukusanya tozo husika kwa watumiaji wa mwisho wa mafuta, kinyume na kifungu cha 18.9 cha Makubaliano ya Mkataba, ambacho kinataja malipo husika kufanywa ndani ya siku 14.

Maoni yangu ni kuwa malipo ya tozo za kuchelewa kushusha mafuta yalikuwa yamekusanywa kutoka kwa watumiaji wa mafuta na kampuni za uuzaji mafuta, lakini hayakulipwa kwa wasambazaji. Hivyo, kiasi hicho cha fedha kinaweza kuzinufaisha kibiashara kampuni za uuzaji wa mafuta kwa kutumia fedha hizo kwenye biashara zao. Hali hii inaathiri vibaya sekta ya mafuta ya ndani na kujenga taswira mbaya kutokana na kuchelewa kushusha mafuta na

<sup>10</sup> Wauzaji wa mafuta ni kampuni zinazohusika katika uchimbaji, uzalishaji, usafishaji, na usambazaji wa mafuta ghafi na bidhaa za petroli.

<sup>11</sup> Makampuni ya soko la mafuta yanazingatia shughuli za biashara ya kununua, kuuza na kufanya biashara ya mafuta kwa watumiaji wa mwisho.

kuchelewesha malipo ya tozo hizo. Pia, hali hii inaweza kusababisha wauzaji wa mafuta kuelekeza biashara zao nchi zingine, hivyo kusababisha usambazaji uhaba wa mafuta ikilinganishwa na mahitaji ya soko.

**Ninapendekeza PBPA ihakikishe makampuni ya mafuta yanawalipa wauzaji wa mafuta kwa wakati tozo zinazotokana na ucheleweshaji wa ushushaji wa mafuta.**

**10.2.5 Ukosefu wa dhamana za kifedha dola za Marekani 144,003,585 (Sh. Bilioni 335.16) kutoka kwa Kampuni za Madini kufuatia Kuidhinishwa Kufungwa kwa Migodi**

Kanuni ya 207(1)-(2) ya Kanuni za Uchimbaji (Usalama, Afya Kazini, na Ulinzi wa Mazingira) za Mwaka 2010 inawataka wamiliki wa leseni maalumu za uchimbaji madini wawasilishe dhamana ya ukarabati ili kufidia gharama za kufungwa kwa migodi ya uchimbaji madini kama ilivyoainishwa kwenye mpango wa kufunga migodi na Kamati ya Taifa ya Ufungaji Migodi. Zaidi ya hayo, Kanuni ya 207 (3) inabainisha kuwa dhamana hii ya fedha itaanzishwa kupitia makubaliano tofauti kati ya serikali na mwenye leseni.

Katika ukaguzi wa Wizara ya Madini, nilibaini kuwa Kamati ya Taifa ya Ufungaji Migodi ilipitisha mipango 6 ya kufungwa kwa migodi kuanzia mwezi Agosti 2022 hadi Mei 2023. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023, kampuni za uchimbaji madini zilikuwa hazijawasilisha dhamana za fedha zenye thamani ya dola za Marekani 144,003,585 (Sh. bilioni 335.16), kinyume na kanuni iliyotajwa hapo juu. **Jedwali Na. 49** linaonesha orodha ya migodi iliyoidhinishwa kufungwa ambayo dhamana zake za kifedha hazijawasilishwa.

**Jedwali Na. 49: Migodi Iliyoidhinishwa Kufungwa Inayosubiri Malipo ya Dhamana za Ukarabati**

Na.	Leseni	Tarehe ya Idhini	Kiasi cha Dhamana (Dola za Marekani)
1.	Williamson Diamond Ltd.	3/8/2022	11,094,000
2.	North Mara Gold Mine	7/10/2022	111,676,492
3.	Mbeya Cement Company Ltd.	4/11/2022	4,321,626
4.	Buckreef Gold Company Ltd.	1/12/2022	4,345,040
5.	Stamigold Company Ltd.	29/11/2022	10,446,048
6.	Twiga Cement	19/05/2023	2,120,379
	<b>Jumla</b>		<b>144,003,585</b>

**Chanzo:** Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti

Bila kuwa na dhamana za kifedha, ni hatari kwa serikali kwani kampuni za uchimbaji madini zinaweza kushindwa kushughulikia ipasavyo mahitaji ya ukarabati wa mazingira yaliyoharibiwa kutokana na shughuli za uchimbaji wa madini na kusababisha uharibifu wa mazingira na hatari zingine.

**Napendekeza Serikali ihakikishe kuwa makampuni ya madini yanazingatia kanuni ikiwa ni pamoja na kuwasilisha dhamana za fedha kwa ajili ya migodi iliyofungwa.**

### 10.2.6 Upotevu wa Mapato Sh. Bilioni 9.93 Kutokana na Maji yanayopotea

Upotevu wa mapato kutokana na maji yanayopotea (NRW) ni kiasi cha maji yanayozalishwa na mamlaka za maji safi na usafi wa mazingira kwa ajili ya kusambazwa lakini yanapotea kabla ya kuwafikia wateja waliokusudiwa. Kwa mujibu wa viwango vya Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), kiwango kinachokubalika cha upotevu wa maji kwa mamlaka za maji kinawekwa kulingana na madaraja ya mamlaka za maji na usafi wa mazingira.

Nilibaini kuwa kiwango cha upotevu wa mapato kutokana na maji yanayopotea kinavuka kiwango kinachokubalika kwa mujibu wa Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji kwa mamlaka za maji. Hali hii ilisababisha hasara ya Sh. bilioni 9.93 katika mamlaka 12 za maji, kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 50**. Sababu kubwa ya kiwango kikubwa cha upotevu wa maji ni uchakavu wa miundombinu ya maji.

**Jedwali Na. 50: Upotevu wa Mapato Unaotokana na Maji Yanayopotea**

Na.	Taasisi	Kiasi Kilichopotea (Mita za Ujazo)	Jumla (Sh.)
1.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Wanging'ombe	190,578	209,635,500
2.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Turiani	648,570	604,791,059
3.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kibondo	153,483	72,006,792
4.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Itumba-lsongole	156,778	50,012,182
5.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Lushoto	234,763	118,320,552
6.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Namanyere	30,496	21,591,130
7.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Rombo	5,806,329	5,063,118,888

Na.	Taasisi	Kiasi Kilichopotea (Mita za Ujazo)	Jumla (Sh.)
8.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Bunda	384,664	798,177,717
9.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Ifakara	80,735	91,507,471
10.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Handeni	964,551	2,151,235,340
11.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tunduru	69,172	86,603,344
12.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Maswa	-	666,079,452
	<b>Jumla</b>	<b>8,720,119</b>	<b>9,933,079,426</b>

Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi

Upotevu huo wa maji ulisababisha kukosekana kwa mapato ambayo yangeweza kukusanywa na kutumika kulipia gharama za uendeshaji wa mamlaka za maji na kupunguza utegemezi kwa serikali.

**Ninapendekeza Serikali ichukue hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kuboresha miundombinu ya maji ili kupunguza upotevu wa mapato yanayotokana na maji yanayopotea.**

### 10.2.7 Kuchelewa kwa Miaka Miwili Kusuluhisha Mgogoro wa kiasi cha Sh. Milioni 989.93 cha Tozo za Mrahaba na Huduma kwa Kampuni za Madini

Kanuni ya 12(1) ya Kanuni za Madini (Ukaguzi) za Mwaka 2018 inawataka wenye leseni za madini kujibu hoja za ukaguzi ndani ya siku 30 baada ya ukaguzi au uhakiki wa Tume ya Madini au ofisa aliyeidhinishwa. Kushindwa kutekeleza katika muda uliowekwa, kama ilivyoelezwa katika Kanuni ya 12(2), kunaweza kusababisha Tume ya Madini kumtaka mwenye leseni ya madini kujieleza kwa nini Tume isifute au kusimamisha leseni yake ya uchimbaji madini.

Wakati wa ukaguzi niliufanya katika Tume ya Madini kwa kampuni 27 za uchimbaji madini, kampuni 14 zilikuwa zimekiuka sheria, hivyo kutozwa jumla ya Sh. bilioni 6.05. Miongoni mwa tozo hizo ni pamoja na mrahaba na tozo za huduma za jumla ya Sh. bilioni 4.59 zinazodaiwa na Tume ya Madini katika mwaka wa fedha 2020/2021. Hata hivyo, ni Sh. bilioni 3.60 pekee ndizo zililipwa, huku kiasi cha Sh. milioni 989.93 zikipingwa na wamiliki watatu wa leseni za madini, Mundarara Ruby Mines Ltd., Salum Motors Transport Co. Ltd., na Hanil- Jiangsu Joint Venture Ltd.

Nina wasiwasi kuwa ucheleweshaji uliobainika wa kutatua migogoro ya kampuni za madini uliochukua muda wa miaka miwili tangu mwaka wa fedha 2020/2021 unaathiri uwezo wa Tume ya Madini kupata mapato na kutumia rasilimali-fedha kwa ufanisi. Pia, migogoro hii kuchukua muda mrefu kabla ya kusuluhishwa kunazorotesha uhusiano kati ya Tume ya Madini na kampuni za madini jambo ambalo linaweza kuondoa hali ya kuaminiana na kuzidisha mivutano.

**Napendekeza Serikali ihakikishe inatutua mgogoro huo ili kufikia muafaka wa kiasi stahiki kinachopaswa kulipwa ili kuboresha mahusiano kati ya Tume na makampuni ya madini.**

#### 10.2.8 Upotevu wa Mapato ya Sh. Bilioni 8.94 Uliotokana na Kukataliwa kwa Madai ya Huduma ya Bima ya Afya

Kifungu cha 27(2) cha Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ya Mwaka 1999 kinaeleza kuwa Mfuko unaweza kukataa au kupunguza malipo ya madai yasiyo sahihi au pale mdaiwa anaposhindwa kuzingatia sheria au kanuni za malipo ya madai yaliyotolewa chini ya sheria hii.

Ukaguzi wangu katika hospitali za rufaa za kanda na mikoa ulibaini jumla ya madai ya Sh. bilioni 8.94 kutoka hospitali 24 za rufaa za mikoa, za kanda, na hospitali maalumu yalikataliwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kutokana na ujazaji usio sahihi wa taarifa kwenye za fomu za madai zilizowasilishwa katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Kasoro hizo ni pamoja na uidhinishaji usio sahihi wa fomu, makosa ya kunakili namba rejea za ugonjwa, na kutozingatia Mwongozo wa Ubora wa Matibabu.

Nilibaini pia kuwa kati ya madai ya Sh. bilioni 71.21 yaliyowasilishwa katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, ni Sh. bilioni 62.27 (87%) pekee ndizo zilikubaliwa na kulipwa, huku Mfuko ukikataa madai ya thamani ya Sh. bilioni 8.94 (13%). Ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2021/2022, madai yaliyokataliwa mwaka 2022/2023 yameongezeka kwa Sh bilioni 1.14 kutoka Sh bilioni 7.8 hadi Sh bilioni 8.94. Hali hii inaonesha kuwa mapendekezo yangu hayakutekelezwa kikamilifu. **Kiambatisho Na. IX** ni orodha ya hospitali zilizokuwa na madai ya bima ya afya yaliyokataliwa.

**Ninapendekeza Serikali kupitia Wizara ya Afya iboreshe ukaguzi wa ndani, na kutoa mafunzo kuhusu namna ya kushughulikia madai ya bima ili kuboresha usahihi katika kukamilisha fomu za madai ya NHIF.**

### 10.2.9 Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kutolipa kwa wakati Madai ya Sh. Bilioni 12.52 ya Gharama za Matibabu kwa Hospitali Maalumu na za Rufaa

Kifungu cha 28 cha Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, Sura ya 395 (iliyorekebishwa mwaka 2015) kinataka madai yoyote ya fedha kwa watoa huduma za afya yalipwe ndani ya siku 60 tangu kuwasilishwa kwa madai hayo kwenye mfuko.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, nilifuatilia utaratibu wa ulipaji wa madai ya matibabu kutoka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa mujibu wa sheria na nilibaini kuwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulikuwa ukichelewesha malipo ya madai ya matibabu kwa hospitali maalumu, hospitali za rufaa za mikoa na za kanda. Ukaguzi ulibaini kuwa kiasi cha Sh. bilioni 12.52 zilichelewesha kulipwa katika muda wa kati ya siku 9 hadi 326 baada ya kumalizika kwa muda wa siku 60 uliowekwa kisheria kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 51.

Ucheleweshaji huu ulitokana na hospitali husika kutofuatilia kwa wakati madai ya gharama za matibabu, hivyo kusababisha Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kuchelewesha malipo zaidi ya siku 60.

#### Jedwali Na. 51: Kucheleweshwa kwa Malipo ya Madai ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa Hospitali Maalumu na za Rufaa za Mikoa

Na.	Jina la Hospitali Maalumu na Hospitali ya Rufaa ya Mikoa	Idadi ya Siku za Kuchelewesha Malipo	Kiasi (Sh.)
1.	Benjamin Mkapa	Siku 142	5,199,491,539
2.	Bukoba	Kutoka siku 11 hadi siku 67	537,995,975
3.	Hospitali ya Kanda, Chato	Kuanzia siku 7 hadi siku 55	334,875,785
4.	Dodoma	Kuanzia siku 30 hadi siku 135	2,989,741,133
5.	Geita	Kuanzia siku 38 hadi 64	262,808,275
6.	Mbeya	Kuanzia siku 72 hadi siku 87	423,059,315
7.	Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe	Kuanzia siku 35 hadi siku 113	512,072,359
8.	Musoma	Kuanzia siku 72 hadi siku 102	719,250,015
9.	Singida	Kuanzia siku 9 hadi siku 326	866,900,900
10.	Songea	Kuanzia siku 17 hadi siku 69	314,837,145
11.	Tabora	Kuanzia siku 30 hadi siku 90	368,516,495
Jumla			<b>12,529,548,936</b>

Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti Mwaka 2022/23

Ninapendekeza Serikali ihakikishe Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya inalipa madai ya Hospitali kwa wakati ili kurahisisha utoaji wa huduma za afya kwa umma. Zaidi ya hayo, Hospitali za rufaa ziboreshe usahihi kwenye ujazaji wa fomu za madai ili kupunguza makosa, pia uwasilishwaji wa fomu za madai kwa wakati ili kuzuia ucheleweshaji wa malipo kutoka NHIF.

### 10.2.10 Bohari Kuu ya Dawa kukaa na Fedha za Hospitali kiasi cha Sh. Bilioni 10.13 kwa zaidi ya mwaka mmoja bila kusambaza Dawa, Vifaatiba na Vitendanishi

Kanuni ya 140(3) na ya 141(3) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 zinaitaka Bohari Kuu ya Dawa kununua na kusambaza vifaatiba vya kwenye orodha na visivyo kwenye orodha ambavyo vinahitajika mara kwa mara kwa kipindi fulani.

Nilibaini hospitali za rufaa za mikoa 16 pamoja na Wizara ya afya ya Zanzibar zina jumla ya Sh. bilioni 10.13 zilizopo Bohari Kuu ya Dawa kwa ajili ya ununuzi na usambazaji wa dawa, vifaatiba, na vitendanishi. Hata hivyo, dawa, vifaatiba, na vitendanishi hivyo havikuwasilishwa kwenye hospitali husika kwa muda wa zaidi ya mwaka mmoja, kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 52**.

Niliripoti ucheleweshaji huo katika ripoti yangu ya mwaka wa fedha 2021/22 kuwa Sh. bilioni 20.66 zilikuwa zimehifadhiwa na Bohari Kuu ya Dawa bila kusambaza dawa, vifaatiba, na vitendanishi. Kuendelea kwa hali hii kunaashiria kuwa Serikali haitekelezi ipasavyo mapendekezo yangu.

Bohari Kuu ya Dawa kuendelea kushikilia fedha bila kutumika kwenye ununuzi na usambazaji wa dawa na vifaatiba kunapunguza upatikanaji wa dawa, vifaatiba, vitendanishi hivyo kuzorotesha utoaji wa huduma bora za matibabu katika hospitali maalumu na za rufaa za mikoa na kanda.

#### Jedwali Na. 52: Fedha Zinazoshikiliwa na Bohari Kuu ya Dawa bila Kusambaza Dawa na Vifaatiba

Na	Jina la Hospitali ya Rufaa na Wizara	Kiasi (Sh.)
1.	Bukoba	255,084,750
2.	Hospitali ya Kanda, Chato	2,980,250,938
3.	Dodoma	1,869,218,586
4.	Geita	1,029,343,009
5.	Kibong'oto	1,314,795,603
6.	Manyara	10,115,700
7.	Mawenzi	305,822,467
8.	Mbeya	984,799,635

Na	Jina la Hospitali ya Rufaa na Wizara	Kiasi (Sh.)
9.	Wizara ya Afya (Fungu 52)	36,300,000
10.	Mount Meru	10,591,300
11.	Mtwara	275,345,544
12.	Singida	11,945,920
13.	Sekou Toure	9,935,120
14.	Songea	8,843,220
15.	Songwe	4,660,420
16.	Temeke	799,174,978
17.	Wizara ya Afya Zanzibar	227,707,600
<b>Jumla</b>		<b>10,133,934,790</b>

Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi za Mwaka 2022/23

Ninarejea ushauri wangu kuwa Hospitali za rufaa za mikoa ziweke makubaliano ya kisheria na Bohari Kuu ya Dawa. Aidha, inapotokea Bohari kuu ya Dawa haina akiba ya dawa, irudishe fedha kwa hospitali husika.

#### 10.2.11 Gharama za ziada za Sh. Milioni 115.51 zilizotokana na Ununuzi wa Dawa na Vifaatiba kutoka kwa Wasambazaji Binafsi

Kanuni ya 130 (3) (4) na (5) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 (kama zilivyorekebisha) na Kanuni za Mwaka 2016 (Gazeti la Serikali Toleo Na.121 zilichopishwa tarehe 22 Aprili 2016) zinazitaka taasisi nunuzi kufanya ununuzi katika Bohari Kuu ya Dawa ndani ya siku moja ya kazi baada ya kufikia kiwango cha akiba. Kama bidhaa zilizoombwa hazipatikani, Bohari Kuu ya Dawa inalazimika itoe taarifa ya kutopatikana ndani ya siku moja ya kazi. Baada ya kupokea taarifa hiyo, taasisi nunuzi inaweza kuchagua mbinu mbadala ya ununuzi.

Katika mwaka wa fedha wa 2022/23, hospitali tatu za rufaa zilinunua vifaatiba mbalimbali vya thamani ya Sh. milioni 267.34 kutoka kwa wazabuni binafsi, ikilinganishwa na gharama ya Sh. milioni 151.83 endapo dawa na vifaatiba hivyo vingenunuliwa katika Bohari Kuu ya Dawa. Kutonunua vifaatiba katika Bohari Kuu ya Dawa kumesababisha kuingia gharama ya ziada ya Sh. milioni 115.51 kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 53.

#### Jedwali Na. 53: Gharama za Ziada Zilizotokana na Ununuzi wa Dawa na Vifaatiba kutoka kwa Wasambazaji Binafsi

Na	Jina la Hospitali ya Rufaa ya Mikoa	Kiasi cha Fedha Kilicholipwa kwa Wauzaji Binafsi (Sh.)	Gharama za Bohari Kuu (Sh.)	Gharama ya Ziada Iliyolipwa (Sh.)
1.	Katavi	90,575,500	61,164,432	29,411,068
2.	Maweni	81,455,375	38,652,911	42,802,464



Na	Jina la Hospitali ya Rufaa ya Mikoa	Kiasi cha Fedha Kilicholipwa kwa Wauzaji Binafsi (Sh.)	Gharama za Bohari Kuu (Sh.)	Gharama ya Ziada Iliyolipwa (Sh.)
3.	Tabora	95,318,720	52,017,304	43,301,416
<b>Jumla</b>		<b>267,349,595</b>	<b>151,834,647</b>	<b>115,514,948</b>

Chanzo: Taarifa za Ukaguzi za Mwaka 2022/23

Tatizo hili linasababishwa na upungufu wa mara kwa mara wa dawa na vifaatiba katika Bohari Kuu ya Dawa, hivyo hospitali kuamua kununua kutoka kwa wauzaji binafsi.

Ninapendekeza Serikali kupitia Wizara ya Afya iimarishie uwezo wa Bohari Kuu ya Dawa katika kushughulikia suala la upatikanaji wa dawa na vifaatiba ili kupunguza gharama za ziada zinazotokana na kununua Dawa na Vifaatiba kwa wauzaji binafsi, kitu kinachoweza kuathiri uwezo wa Hospitali kujiendesha.

#### 10.2.12 Vifaa vilivyo Nunuliwa na Hospitali za Rufaa lakini Havitumiki vyenye Thamani ya Sh. bilioni 3.47

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa vifaa mbalimbali vyenye thamani ya Sh. bilioni 3.47 vilinunuliwa kwaajili ya hospitali za rufaa za mikoa mitano vilikuwa bado havijaanza kutumika hadi wakati wa ukaguzi wangu. Vifaa hivyo ni kama vile mashine ya *CT-Scan*, mashine ya *X-Ray* ya kidijiti na mashine ya kusafisha damu kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na. X**.

Hali hii ni kinyume na Kanuni ya 87(1)(h) ya Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2001 inayohimiza matumizi ya vifaa pindi vinaponunuliwa. Ilielezwa kuwa sababu ya kasoro hii ni uhaba wa fedha na kutokamilika kwa miundombinu itakayotumika kwa ajili ya kufunga vifaa vilivyoununuliwa. Kutotumika kwa vifaa hivyo kunasababisha lengo la ununuzi wake lisifikiwe hivyo kuinyima jamii manufaa yake na kunaviweka vifaa hivyo katika hatari ya kuchakaa kabla ya matumizi.

Ninapendekeza Serikali itenge fedha za kutosha kwaajili ya kukamilisha miundombinu ili kuwezesha usakinishaji wa vifaa vilivyoununuliwa kuweza kutumika bila kuchelewa zaidi.

### 10.3 Masuala yanayohusu ukiukaji wa sheria, kanuni na miongozo

Wakati wa ukaguzi wangu, nilibaini ukiukaji wa kanuni, sheria na miongozo mbalimbali kwa taasisi za serikali kuu kama ilivyoelezwa hapa chini:

#### 10.3.1 Kutofanyika kwa ufuatiliaji na Tathmini ya Matumizi ya Fedha Sh. Bilioni 111.48 Zilizotolewa kwa Wakala Ziliotekeleza Miradi

Kanuni ya 15 ya Kanuni za Mfuko wa Taifa wa Maji za Mwaka 2019 inautaka Mfuko kufuatilia na kutathmini matumizi ya fedha zinazotolewa kwa wakala waliotekeleza miradi ya maji iliyopangwa, na kuhakikisha unazingatia muda, gharama, na masharti ya ubora wa miradi husika.

Hata hivyo, nilibaini kuwa Mfuko wa Taifa wa Maji haukufanya ufuatiliaji na tathmini ya matumizi ya Sh. bilioni 111.48 zilizotolewa kwa wakala 40 waliotekeleza miradi ya maji 367 iliyopangwa kufanyiwa tathmini. Udhaifu huu ulitokana na uhaba wa rasilimaliwatu na usimamizi usioridhisha wa ndani ya Mfuko. Bila ufuatiliaji wa ufanisi, kuna hatari ya fedha za Mfuko kutumika vibaya.

**Ninapendekeza Mfuko wa Taifa wa Maji ufanye ufuatiliaji na tathmini ya kutosha ya fedha zinazotolewa kwa wakala wa utekelezaji ili kupunguza hatari ya ubadhirifu wa fedha.**

#### 10.3.2 Utoaji wa hati za ugawaji wa maeneo ya vitalu vya uwindaji bila idhini ya waziri

Eneo Maalumu la Makubaliano ya Uwekezaji wa Wanyamapori (SWICA) ni eneo lililotengwa ndani ya hifadhi ya wanyamapori au pori la akiba ambapo mashirika au watu binafsi hupewa haki ya kuwekeza katika shughuli zinazohusiana na wanyamapori kama vile utalii, uwindaji au uhifadhi. Maeneo haya maalumu yalianzishwa ili kukuza usimamizi endelevu wa wanyamapori, kupata mapato kwa ajili ya juhudi za uhifadhi, kuchochea maendeleo ya kiuchumi katika maeneo ya vijijini, na kuhakikisha ulinzi wa viumbe hai na makazi asilia.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 3(1) ya Kanuni za Eneo Maalumu la Uwekezaji kwa Wanyamapori za Mwaka 2020, Waziri wa Maliasili na Utalii amepewa mamlaka, baada ya kupata mapendekezo ya Bodi ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), kuteua maeneo ya ardhi ndani ya mapori ya

akiba kuwa Maeneo Maalumu ya Makubaliano ya Uwekezaji wa Wanyamapori kwa madhumuni yaliyoainishwa katika Kanuni hizi.

Hata hivyo, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania ilitoa hati za ugawaji wa maeneo ya uwindaji (vyeti namba TAWA.0003, TAWA.0004 na TAWA.0005) kupitia makubaliano ya Eneo Maalumu la Uwekezaji kwa Wanyamapori kwa wawekezaji wawili kwenye jumla ya maeneo 13, ingawa maeneo hayo hayakupata idhini ya waziri kuwa vitalu vya uwindaji kama inavyotakiwa kisheria. Hali hii inaonesha kuwa, menejimenti ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania haikuzingatia majukumu ya Waziri wa Maliasili na Utalii kabla ya kutoa hati husika.

Ni maoni yangu kuwa, kutoa hati hizo kwa maeneo ambayo hayajapata idhini ya waziri ni kukiuka kwa kiasi kikubwa Kanuni za Eneo Maalumu la Makubaliano ya Uwekezaji wa Wanyamapori za Mwaka 2020 na kuleta shaka kuhusu uwazi na uadilifu wa mchakato wa ugawaji wa maeneo hayo.

**Napendekeza Serikali ihakikishe TAWA inazuia ugawaji wa maeneo maalumu ya uwekezaji kwa wanyamapori bila idhini ya Waziri.**

### 10.3.3 Kutochukuliwa kwa hatua dhidi ya taasisi zilizoachia majitaka zaidi ya viwango vilivyopendekezwa na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira na Shirika la Viwango la Tanzania

Kwa mujibu wa Kifungu cha 65(4) cha Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji ya Mwaka 2009, wenye vibali vya kuachia maji yaliyotumika wanalazimika kuzingatia ubora wa maji na viwango vilivyowekwa na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira au Shirika la Viwango Tanzania ili kuzuia uchafuzi wa maji.

Aidha, chini ya Kifungu cha 64(1)(a) na cha 64(4) cha Sheria hiyo, mtu yeyote anayeruhusu au kusababisha moja kwa moja taka au uchafu kuchafua vyanzo vya maji atakuwa anatenda kosa. Mtu huyo akitiwa hatiani, atawajibika kulipia gharama za kurekebisha uharibifu na kurejesha ubora wa maji au kutozwa faini ya angalau Sh. 300,000 au kifungu cha hadi mwaka mmoja, au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Nilipitia matokeo ya vipimo vya maji yaliyotumika viliyopimwa na Bodi ya Maji ya Bonde la Mto Pangani katika Kiwanda cha Saruji cha Tanga, Darsh Industries, na Sunflag Limited na nilibaini kutokidhi viwango vya maji yaliyotumika na viwango vya taka kwa mujibu wa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira na

Shirika la Viwango Tanzania. Nilibaini kuwa viwango vya pH vya maji hayo vilikuwa 6.0, ambavyo ni chini ya kiwango kinachohitajika cha 6.5 hadi 8.5. Zaidi ya hayo, viwango vya mahitaji ya oksijeni ya kibiokemikali (BOD) vilikuwa 70mg/l ambapo vilizidi kikomo kinachoruhusiwa cha 30mg/l, huku mahitaji ya oksijeni ya kemikali (COD) yalikuwa kati ya 156mg/l hadi 854.4mg/l, ambayo yalivuka kiwango kinachoruhusiwa cha 60mg/l.

Utofauti uliobainika wa viwango vya pH vinavyopendekezwa na viwango vya juu vya mahitaji ya oksijeni ya kibiokemikali na mahitaji ya kemikali ya oksijeni huleta hatari kubwa za kimazingira. Kiwango cha pH chini ya kiwango kinachohitajika cha 6.5 hadi 8.5 ni hatari kwa viumbe vya majini na vinaweza kutatiza usawa wa mfumo-ikolojia. Viwango vya juu vya mahitaji ya oksijeni ya kibiokemikali vinavyozidi kikomo kinachoruhusiwa cha 30mg/l, huashiria kuongezeka kwa vitu vya kikaboni kwenye maji, ambayo vinaweza kumaliza viwango vya oksijeni hivyo kusababisha hali ya hipoksiki na kuathiri vibaya maisha ya viumbe vya majini. Aidha, viwango vya juu vya mahitaji ya oksijeni ya kemikali kupita kiwango kinachoruhusiwa cha 60mg/l, huashiria viwango vya juu vya uchafuzi wa kaboni, ambavyo huweza kuharibu ubora wa maji, kuharibu makazi majini, na kusababisha hatari za kiafya kwa binadamu, wanyamapori, na viumbe hai wengine.

Licha ya ukiukaji huo, Bodi ya Maji ya Bonde la Mto Pangani haikuchukua hatua dhidi ya kampuni zilizohusika hadi kufikia mwezi Oktoba 2023. Hali hii ni kutokana na kutokuwapo kwa taratibu za ufuatiliaji na uchukuaji hatua katika Bodi ya Maji ya Bonde la Mto Pangani, hali iliyochangiwa na kukosekana utambuzi wa viashiria na uchukuzi wa hatua kwa wakati kwa ukiukaji wa sheria uliofanywa na viwanda husika.

**Ninapendekeza Bodi ya Maji ya Bonde la Pangani ichukue hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kutoza faini na adhabu, au kusitisha vibali vya utoaji maji taka kwa taasisi ambazo zitashindwa kufuata Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji ya mwaka 2009.**

#### 10.3.4 Mabwawa yenye Thamani ya Sh. Bilioni 5 Kujengwa bila Vibali

Kanuni ya 9(1) ya Kanuni za Usimamizi wa Rasilimali za Maji (Usalama wa Mabwawa) za Mwaka 2013 inamtaka mtu anayetarajia kujenga bwawa la maji kuomba kibali cha ujenzi kwa Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji wa Wizara ya Maji.

Nilibaini kuwa katika mwaka wa fedha 2022/23, Bodi ya Maji ya Bonde la Kati (IDBWB) ilitekeleza miradi 11 ya mabwawa yenye thamani ya Sh. bilioni 5. Hata hivyo, nilibaini kuwa IDBWB haikuomba vibali vya ujenzi kutoka Wizara ya Maji kinyume na Kanuni ya 9(1).

Sababu kuu iliyobainika ni mipango isiyoridhisha ya miradi ya mabwawa iliyosababisha kushindwa kupata vibali hivyo vya ujenzi. Udhaifu huo unaleta shaka kuhusu usalama na athari za kimazingira za mabwawa. Kibali cha Wizara ya Maji ni muhimu ili kuhakikisha kuwa ujenzi wa mabwawa unakidhi viwango vya usalama na mazingira.

**Ninapendekeza Bodi za Maji za Mabonde kuhakikisha kuwa miradi yote ya mabwawa inazingatia matakwa ya udhibiti kwa kupata vibali muhimu vya ujenzi ili kuhakikisha viwango na usalama wa mazingira.**

### 10.3.5 Vibali vya Matumizi ya Maji vyenye Thamani ya Sh. Bilioni 1.01 Vilivyoisha Muda wake

Kifungu cha 43 (1) cha Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji ya Mwaka 2009 kinamtaka mtu yeyote anayechukua maji kutoka vyanzo vya juu au chini ya ardhi, au kujenga au kudumisha kazi yoyote kwa madhumuni hayo, kuomba kibali cha matumizi ya maji kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

Katika ukaguzi wa bodi za maji za mabonde, nilibaini kuwa katika bodi tatu za maji za mabonde, vibali 1,200 vya matumizi ya maji vyenye thamani ya Sh. bilioni 1.01 vilikuwa vimekwisha muda wake. Licha ya vibali hivyo kuisha muda wake wa matumizi, wateja waliendelea kutumia maji kutoka katika vyanzo husika, hivyo kusababisha upotevu wa mapato hayo kama ada ya mwaka ya matumizi ya maji. **Jedwali Na. 54** linaonesha orodha ya bodi za mabonde ya maji, idadi ya vibali vilivyoisha muda wake, na kiasi cha fedha ambacho hakikusanywa.

**Jedwali Na. 54: Bodi, Idadi ya Vibali Vilivyoisha Muda Wake, na Kiasi cha Fedha ambacho Hakikusanywa**

Na.	Tasisi	Idadi	Ada Kiasi (Sh.)
1	Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Nyasa	319	338,245,421
2	Bodi ya Maji Bonde la Mto Wami - Ruvu	500	110,900,000
3	Bodi ya Maji ya Bonde la Mto Ruvuma na Pwani ya Kusini	381	569,363,524
	<b>Jumla</b>	<b>1,200</b>	<b>1,018,508,945</b>

**Chanzo:** Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti

Hasara hii inaathiri moja kwa moja uendelevu na uwezo wa kifedha wa uendeshaji wa bodi husika, hivyo kupunguza uwezo wao wa kufanya shughuli muhimu za usimamizi wa rasilimali za maji na matengenezo ya miundombinu. Pia, kuendelea kutumia maji licha ya vibali kwisha muda wake kunazua wasiwasi kuhusu usimamizi endelevu wa rasilimali za maji, jambo linaloweza kusababisha uharibifu wa mazingira.

**Ninapendekeza Bodi zinazohusika zifanye utaritibu wa uhakiki wa vibali vyote vya matumizi ya maji ili kubaini vibali vilivyokwisha muda wake au vinavyokaribia kuisha muda wa matumizi. Aidha, kuchukua hatua stahiki ili kuzuia utumiaji wa maji kwa vibali vilivyokwisha muda wake, ikiwa ni pamoja na adhabu kwa ukiukwaji wa sheria.**

### 10.3.6 Kushindwa Kutoa Huduma za Usafi wa Mazingira

Huduma za usafi wa maji na mazingira unamaanisha utoaji wa huduma, miundombinu na mifumo iliyowekwa ili kuhakikisha usafishaji na utoaji wa maji taka ili kuzuia kuenea kwa magonjwa na kulinda mazingira.

Kifungu cha 20 (a) cha Sheria ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2019 kinaainisha kazi za mamlaka ya maji safi na usafi wa mazingira kuwa ni pamoja na kutoa huduma za maji safi na usafi wa mazingira kama inavyotakiwa na Sheria hii au sheria nyingine yoyote iliyoandikwa inayohusu usimamizi wa rasilimali za maji, viwango vya ubora wa maji, na uhifadhi wa mazingira.

Kinyume na matakwa hayo, nilibaini kuwa mamlaka saba za usambazaji wa maji na usafi wa mazingira hazikutoa huduma za usafi wa mazingira kwa jamii. Sababu kuu ni ukosefu wa rasilimali muhimu, ikiwa pamoja na fedha, miundombinu, na utaalumu wa kuongeza huduma zao za usafi wa mazingira.

Kutokuwapo kwa huduma za usafi wa mazingira kunasababisha usimamizi usioridhisha wa taka na kuongeza hatari ya kuchafua vyanzo vya maji na uchafuzi wa mazingira, hivyo kuathiri mifumo ya ikolojia. Mamlaka za usafi wa mazingira zilizoshindwa kutoa huduma ya usafi wa mazingira ni pamoja na Biharamulo, Chato, Songe, Itumba-Isongole, Namanyere, Tunduru Mjini, na Maswa.

Napendekeza Serikali kutenga rasilimali za kutosha kwa Mamlaka za Maji kwa ajili ya ujenzi na matengenezo ya miundombinu ya usafi wa mazingira.

### 10.3.7 Biashara 49 Kufanywa bila Leseni Halali za Biashara

Kifungu cha 3(1) (a) cha Sheria ya Leseni za Biashara ya Mwaka 1972 kinaeleza kuwa hakuna mtu atakayefanya biashara nchini Tanzania, awe kampuni au wakala, isipokuwa kama ana leseni halali inayohusiana na biashara husika.

Hata hivyo, nimebaini wafanyabiashara 49 wa Iringa, Njombe na Arusha walikuwa wakifanya biashara bila leseni halali za biashara huku wakiwa bado hawajatambuliwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA). Udhaifu huu ulichangiwa na vibali vya wafanyabiashara 33 vilivyoisha muda wake kutohuishwa, na utumiaji wa leseni batili ya biashara ya daraja B inayotolewa na mamlaka za serikali za mitaa kwa wafanyabiashara 16.

Kushindwa kwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni kuchukua hatua kwa biashara zinazofanywa bila leseni halali kunaleta shaka kuhusu ufanisi wa usimamizi na udhibiti wa biashara hivyo kusababisha mianya kwa wafanyabiashara kufanya biashara bila kuzingatia sheria.

Ninapendekeza BRELA kufanya mapitio ya kina ya mfumo wake wa ufuatiliaji na uchukuaji wa hatua stahiki ili kubaini mapungufu ili kuhakikisha biashara zinafanywa zina vibali.

### 10.3.8 Usimamizi usioridhisha wa vyama vya ushirika wa akiba na mikopo (SACCOS)

Wakati wa ukaguzi wa Mfuko wa Usimamizi na Ukaguzi wa Ushirika, changamoto mbalimbali zilibainika kuhusu usimamizi wa vyama vya ushirika wa akiba na mikopo kama inavyofafanuliwa hapa chini.

#### a) Ukaguzi na usimamizi usioridhisha wa vyama vya ushirika wa akiba na mikopo

Kifungu cha 93(1) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika ya Mwaka 2013 kinasema kuwa, msajili wa vyama vya ushirika atafanya ukaguzi wa mara kwa mara wa shughuli na masuala ya fedha ya chama kilichosajiliwa.

Hata hivyo, nilibaini kuwa maafisa ushirika walifanya usimamizi nje na ndani ya maeneo yao kwenye vyama 623 (asilimia 30.4) tu kati ya vyama 2,046 ili

kutathmini uzingatiaji wa viwango vya ubora wa huduma. Aidha, nilibaini kuwa Tume ilikuwa na maafisa ushirika 186, ambao ni pungufu ya idadi inayotakiwa ya maafisa ushirika 677.

#### **b) Kuwapo kwa vyama 1,245 vya ushirika wa akiba na mikopo visivyo na leseni**

Kifungu cha 4 (1) cha Sheria ya Huduma Ndogo ndogo za Fedha mwaka 2019 inasema kuwa, chama cha ushirika wa akiba na mikopo hakitafanya shughuli yoyote ya fedha, isipokuwa kama chama hicho kimepewa leseni na benki au mamlaka Iliyokabidhiwa jukumu hili kwa mujibu wa masharti ya sheria.

Hata hivyo, mapitio yangu ya ripoti ya mwaka ya utendaji ya Mfuko wa Usimamizi na Ukaguzi wa Ushirika kwa mwaka wa fedha 2022/23 yalibaini kuwa kati ya vyama 2,046 vya ushirika wa akiba na mikopo vilivyosajiliwa, ni vyama 801 tu ndivyo vilikuwa na leseni, huku vyama 1,245 (sawa na asilimia 60.9) vikiendesha shughuli zake bila leseni.

Udhaifu huu unasababishwa na usimamizi usioridhisha wa Tume kwa vyama vya ushirika wa akiba na mikopo, na upungufu wa maafisa ushirika. Hali hii inaleta athari kama vile kutokidhi kwa mahitaji ya leseni hivyo kusababisha hatari za kiudhibiti na za kifedha.

**Napendekeza Serikali ihakikishe Mfuko wa Usimamizi na Ukaguzi wa Ushirika unakabiliana na mapungufu ya kiutawala ili kuimarisha uwajibikaji na uwazi katika vyama vya ushirika.**

#### **10.3.9 Wafanyabiashara wa Kemikali Wasiosajiliwa na wenye Leseni Zisizouhishwa**

Kifungu cha 61 cha Sheria za Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na za Watumiaji ya Mwaka 2020 kinataka mfanyabiashara anaokusudia kuhuisha usajili kutuma maombi kwa msajili miezi mitatu kabla ya kwisha kwa muda wake wa usajili. Endapo maombi ya uhuishaji wa usajili utafanyika kwa wakati, msajili atashughulikia maombi hayo kabla ya muda wa kumalizika kwa usajili wa awali.

Ukaguzi wangu niliufanya katika usajili wa wafanyabiashara wa kemikali katika Maabara ya Serikali ya Kemikali, Kanda ya Kaskazini ulibaini kuwa



wafanyabiashara 7 wa kemikali hawakusajiliwa. Pia, wafanyabiashara 23 wa kemikali hawakuhiisha usajili wao kinyume na kifungu tajwa hapo awali.

Upungufu huo unatokana na kutokamilika kwa ufuatiliaji ili kupata nyaraka za usajili kama vile tathmini ya athari kwa mazingira, mipango ya usimamizi wa mazingira, namba za utambulisho wa mlipakodi, leseni za biashara, na vyeti vya Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni kutoka mamlaka zingine za Serikali. Kutosajiliwa kwa wafanyabiashara wa kemikali kunazidisha hatari na vitendo vya udanganyifu ambavyo vinaweza kuwadhuru watumiaji.

**Ninapendekeza Serikali ichukue hatua stahiki kuhakikisha kuwa wafanyabiashara wa kemikali wanazingatia matakwa ya usajili, ili kupunguza hatari ya kemikali hatarishi kuwadhuru watumiaji.**

#### **10.3.10 Asasi zisizo za Kiserikali zilizosajiliwa Kutotayarisha na Kuwasilisha Ripoti za Ukaguzi, Ripoti za Shughuli za Kila Mwaka, na Mikataba yao na Wahisani**

Kifungu cha 29(1) cha Sheria ya Asasi Zisizo za Kiserikali ya Mwaka 2002 kinataka kila asasi isiyo ya kiserikali kuandaa na kuwasilisha taarifa za shughuli za mwaka, na taarifa za kikaguzi ambazo zinapaswa kuwekwa hadharani. Aidha, Kifungu cha 3.2 (xiv) cha Mwongozo wa Uratibu wa Asasi Zisizo za Kiserikali wa Mwezi Aprili Mwaka 2020 kinazitaka asasi zote zisizo za kiserikali zinazofanya kazi nchini kuwasilisha mikataba kati yao na wahisani wao.

Hata hivyo, nilibaini kuwa asasi 8,262 zisizo za kiserikali sawa na asilimia 87 ya asasi zote 9,453 hazikuwa zimeandaa na kuwasilisha taarifa za shughuli za mwaka na ripoti zilizokaguliwa, wala mikataba kati ya yao na wahisani.

Upungufu huo ulitokana na ufuatiliaji hafifu wa asasi zisizo za kiserikali na mamlaka husika, jambo linalopunguza uwazi kwa wadau kuhusu shughuli za asasi hizo nchini.

**Ninapendekeza Serikali ianzishe mifumo ya utekelezaji ili kuhakikisha kuwa asasi zisizo za kiserikali zinazingatia taratibu za kuwasilisha ripoti zao kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake, na Makundi Maalum.**

### 10.3.11 Tume ya Usuluhishi na Uamuzi Kutosuluhisha Migogoro ya Watumishi wa Sekta Binafsi kwa Zaidi ya Siku 30

Kifungu cha 86 (4)(5) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano ya Kazi (iliyorekebisha mwaka 2019) kinasema kwamba "kwa mujibu wa Kifungu cha 87, mpatanishi atatatua mgogoro ndani ya siku 30 tangu kuwasilishwa kwa rufaa. Hata hivyo, muda unaweza kuongezeka endapo pande zitakubaliana kwa maandishi".

Ukaguzi wangu wa Ripoti ya Mfumo wa Usimamizi wa Kesi Kieletroniki ya tarehe 30 Juni 2023 ulibaini kwamba kinyume na matakwa ya sheria, migogoro 172 ya watumishi wa umma iliyowasilishwa katika Tume ya Upatanishi na Usuluhishi ilikuwa haijatatuliwa kwa zaidi ya siku 30 hadi wakati wa ukaguzi huu mwezi Agosti 2023. Pia, nilibaini kutokuwapo kwa makubaliano ya maandishi kati ya pande mbili kuhusu ongezeko la muda wa upatanishi.

Upungufu huo unasababishwa na kutozingatiwa kwa ukomo wa muda uliopangwa wa usuluhishi na uamuzi. Hata hivyo, kutumia muda mrefu wa kutatuliwa migogoro kunachelewesha haki kwa wanaoitafuta.

**Ninapendekeza kwamba Serikali ihakikishe Tume ya Usuluhishi na Uamuzi inatatua migogoro ndani ya muda unaotakiwa ili kujengea umma imani na utendaji kazi wa Tume hiyo.**

### 10.3.12 Kutoteketezwa kwa Dawa Zilizokwisha Muda wake wa Matumizi

Kanuni ya 10 ya Sheria ya Tanzania ya Chakula, Dawa, na Vipodozi (Uainishaji wa Dawa) ya Mwaka 2015 inamtaka mkuu au mfamasia wa hospitali kuanzisha mchakato wa kuteketeza bidhaa zisizofaa kutokana na kwisha muda wake wa matumizi. Aidha, Kanunu ya 254 ya Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2001 inamtaka ofisa masuuli kuanzisha mchakato wa kuondosha magari, mitambo, na vifaa vyote vilivyoisha muda wake wa matumizi.

Mapitio ya rejista za dawa za matibabu zilizoisha muda wake wa matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yalibaini kuwa dawa mbalimbali zenye thamani ya Sh. bilioni 1.99 katika hospitali za rufaa za mikoa 10 zilikuwa zimeisha muda wake lakini hazikuteketezwa hadi wakati wa ukaguzi huu mwezi Disemba 2023. Aidha, dawa hizo zilikuwa zimepita muda wake kwa kipindi cha hadi miaka 18. **Jedwali Na. 55** linaonesha hospitali na thamani ya dawa ambazo muda wake wa matumizi ulikuwa umeisha lakini hakuteketezwa.

**Jedwali Na. 55: Hospitali na Thamani ya Dawa ambazo Muda Wake wa Matumizi Ulikuwa Umeisha lakini Hazikuteketezwa**

Na.	Jina la Hospitali za Rufaa	Thamani ya Dawa (Sh.)
1	Benjamini Mkapa	78,607,030.84
2	Bukoba	7,351,206.05
3	Hospitali ya Kanda, Chato	68,314,743.00
4	Mtwara	10,276,691.30
5	Musoma	22,177,528.00
6	Shinyanga	1,117,732,174.00
7	Simiyu	389,840,219.56
8	Songwe	2,468,964.03
9	Tabora	6,851,673.16
10	Tumbi	286,420,713.00
<b>Jumla</b>		<b>1,990,040,942.94</b>

Chanzo: Barua za Upungufu kwa Menejimenti za Mwaka 2022/23

Upungufu huo ulichangiwa na ufinyu wa bajeti kwa shughuli hiyo. Hata hivyo, kushindwa kuteketeza dawa zilizoisha muda wake kunaweza kusababisha hatari kadhaa kama vile watu wasio waaminifu kufungasha upya kisha kuzisambaza kwa matumizi hivyo kusababisha hatari kwa binadamu na mazingira. Pia, kuendelea kuhifadhi dawa zilikwishe muda wake si tu kunazidisha gharama za uhifadhi bali pia kunapunguza nafasi ya kuhifadhi dawa zingine zinazofaa kwa matumizi.

Ninapendekeza Serikali kuhakikisha kwamba hospitali za rufaa za mikoa zinateketeza dawa zilizokwisha muda wake wa matumizi kwa mujibu wa matakwa ya kisheria. Zaidi ya hayo, hospitali hizi zinapaswa kuepuka kupokea dawa zenye muda mfupi wa matumizi.

### 10.3.13 Upungufu katika Uendeshaji wa Vitengo vya Afya Mipakani na katika Viwanja vya Ndege

Kuanzishwa kwa vitengo vya afya mipakani kulilenga kutoa huduma za ukaguzi wa afya kwa abiria bandarini, viwanja vya ndege, na mipakani ili kuzingatia kanuni za afya za kimataifa za kuzuia kuenea kwa magonjwa ya kuambukiza na kutumika kama ulinzi wa kimsingi dhidi ya vihatarishi vya kiafya.

Tathmini yangu ya ufanisi katika utendaji kazi wa vitengo vitano vya afya katika viwanja vya ndege, na mipakani ilibaini kasoro kadhaa zinazohitaji kushughulikiwa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**(a) Mipaka ya Namanga na Tarakea**

Ukaguzi wangu katika mipaka hii ulibaini ubovu wa skana ya themo katika Kituo cha Mpaka cha Namanga kuanzia mwezi Julai 2022 hadi Juni 2023. Pia, nilibaini kuwepo kwa vifaa vya kupima maambukizi ya ugonjwa wa homa ya ini (Hepatitis B) vilivyokwisha muda wake. Katika mpaka wa Tarakea nilibaini kukosekana kwa gari la matumizi ya ofisi.

**(b) Mpaka wa Holili**

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa skana ya themo ilikuwa haitumiki kwa zaidi ya miaka mitatu kutokana na kutowasilishwa kwa baadhi ya vifaa vyake. Pia, hakukuwa na gari kwa matumizi ya ofisi.

**(c) Uwanja wa Ndege wa Arusha**

Ukaguzi wangu katika uwanja huu ulibaini uhaba wa vifaa muhimu vya kufanyia kazi kama vile magari (pamoja na gari la kubebea wagonjwa), pikipiki, na vifaatiba kama vile majokofu ya maabara, vipimo vya haraka vya magonjwa na vipimo vya kawaida vya magonjwa, na vifaa vya kukusanyia sampuli. Pia, kulikuwa na uhaba wa vitanda vya matibabu, vitanda kwa ajili ya uchunguzi, viti vya walemavu, vifaa vya kinga binafsi, vyumba kwa ajili ya kujitenga, simu za mkononi, orodha ya vifaa vya ofisi, kompyuta na seva, vifaa vya mawasiliano ya redio, mashine za faksi, mashine za kudurufu, skana za joto, tochi za mwanga wa UV, na kamera za kidijiti. Kukosekana kwa vifaa hivi kulikiuka Jedwali la Pili la Aya ya 1.6 ya Mwongozo wa Afya katika Uendeshaji wa Viwanja vya Ndege na Mipaka ya Nchi wa Mwezi Septemba 2022, ambao uliainisha mahitaji ya vifaa na zana muhimu zinazopaswa kuwapo.

Aidha, Uwanja wa Ndege wa Arusha haukuwa na huduma za chanjo kinyume na Aya ya 2.4 ya Mwongozo wa Uchangiaji Gharama wa Huduma za Afya Mipakani wa Mwaka 2022.

Upungufu uliobainika unaweza kusababisha kuchelewesha au kutofanikisha utoaji huduma za afya na huduma zingine kwenye viwanja vya ndege na mipakani.

**Ninapendekeza Serikali kupitia Wizara ya Afya iboreshe vitengo vya afya katika viwanja vya ndege na mipakani ili kutoa huduma za ukaguzi wa afya kikamilifu hivyo kuhakikisha usalama wa wasafiri na jamii.**

## 10.4 Usimamizi Usioridhisha wa Miundombinu

Ukaguzi wangu katika taasisi za serikali ulibaini upungufu katika usimamizi wa miundombinu ya umma, ambao unahitaji hatua za haraka za kuutatua. Upungufu uliobanika unafafanuliwa hapa chini.

### 10.4.1 Usimamizi usioridhisha wa uendeshaji wa vituo vya mizani ya kupima uzito wa magari

Agizo namba 3.6 (e) la Agizo la Wakala (Wakala wa Barabara Tanzania) (Uanzishwaji) (Marekebicho) la Mwala 2020 linaipa Wakala wa Barabara Tanzania mamlaka ya kuanzisha na kuendesha mizani na kudhibiti uzito uliozidi wa mizigo katika mtandao wa barabara ulio chini ya mamlaka yake. Wakati wa ukaguzi wa shughuli za mizani, nilibaini udhaifu kadhaa unaohitaji kuchuliwa hatua stahili, ambao ni pamoja na:

#### (a) Wasafirishaji 299 kutumia kibali kimoja cha mizigo maalumu kwa safari zaidi ya moja

Kanuni ya 15 (1) (a) ya Kanuni za Udhhibiti wa Uzidishaji wa Mizigo ya Magari ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (Mizigo Maalumu) ya Mwaka 2018 inaeleza kuwa mtu atakuwa ametenda kosa iwapo atasafirisha mizigo wowote maalumu bila kibali halali. Pia, Kifungu cha 9 (3) cha Sheria ya Udhhibiti wa Mizigo ya Magari ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2016 kinataka gari linalobeba mizigo yoyote iliyoainishwa katika kifungu kidogo cha (1) bila kibali maalumu kusimamishwa na kuzuiliwa na afisa aliyeidhinishwa.

Hata hivyo, mapitio yangu ya taarifa za kieletroniki za mizani katika vituo vya Nala (Dodoma), Himo (Kilimanjaro), Makuyuni (Arusha), na Vigwaza (Pwani) kuanzia tarehe 1 Julai 2022 hadi 30 Juni 2023, yalibaini matukio 299 ya wasafirishaji kutumia vibali vinavyofanana (kufanana kwa namba za kumbukumbu) kwa zaidi ya safari moja. Pia, nilibaini kuongezeka kwa idadi ya matukio hayo kutoka 153 yaliliyoripotiwa katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2021/2022 hadi 299 kwa mwaka wa fedha 2022/2023, jambo linaloonesha kutokuwapo kwa juhudi za makusudi kushughulikia suala hilo.

#### (b) Magari 93,622 kupita kwenye mizani bila kupimwa kutokana na mizani kufungwa mara kwa mara

Kifungu cha 8 (1) cha Sheria ya Udhhibiti wa Mizigo ya Magari ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2016 kinamtaka msafirishaji anayeendesha gari lenye uzito wa kilogramu 3,500 au zaidi kuhakikisha gari hilo limepimwa

katika kila kituo cha mizani kilichopo kwenye mtandao wa barabara ambao gari husika linapita.

Hata hivyo, nilibaini kuwa kuanzia tarehe 01 Julai 2022 hadi 30 Juni 2023, vituo 15 vya mizani vilifungwa mara kwa mara, hivyo kusababisha magari 93,622 yenye uzito wa zaidi ya kilogramu 3,500 kupita katika vituo hivyo vya mizani bila kupimwa.

**(c) Kutozuiliwa kusafirishwa mizigo hatarishi 330 bila vibali maalumu**

Kifungu cha 9 (3) cha Sheria ya Udhhibiti wa Mizigo ya Magari ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2016 kinataka gari linalobeba mizigo hatarishi bila kibali maalumu kusimamishwa na kuzuiliwa na afisa aliyeidhinishwa au kuelekezwa kwenda mahali panapofaa kwa kuzingatia afya au usalama. Msafirishaji wa gari hilo atawajibika kulipa faini au adhabu nyingine kadiri sheria za nchi mwanachama zinavyoelekeza.

Hata hivyo, katika ukaguzi wangu wa takwimu za mizani katika vituo 6 vya mizani vilivyopo Nala (Dodoma), Makuyuni (Arusha), Himo II (Kilimanjaro), Vigwaza (Pwani), Nangurukuru (Lindi), na Mpemba (Songwe) kuanzia tarehe 01 Julai 2022 hadi tarehe 30 Juni 2023, nilibaini kuwa magari 330 yalisafirisha mizigo hatarishi bila vibali maalumu lakini hayakuzuiliwa kwenye vituo vya mizani, kinyume na agizo lililoainishwa hapo juu. Udhaifu huo ulisababisha kutokusanywa kwa kiasi cha dola za Marekani 3,300.

Nilibaini kuwa udhaifu huu ulitokana na uendeshaji usioridhisha wa mizani pamoja na hitilafu katika vifaa vya kupimia uzito. Kuruhusu udhaifu huu kuendelea kunaweza kusababisha uharibifu mkubwa katika tabaka la lami la barabara na madaraja na kukosekana kwa mapato.

**Napendekeza Serikali ihakikishe TANROADS inafanya ufuatiliaji wa uhakika na kuchukua hatua madhubuti ili kukabiliana na dosari katika uendeshaji wa taratibu za mizani.**

**10.4.2 Kutofanya kazi kwa Vivuko**

Nilibaini kuwa vivuko tisa kati ya 35 (sawa na asilimia 26) vilikuwa havifanyi kazi kwa zaidi ya miezi 6. Vivuko hivyo ni MV Pangani II, MV Sabasaba, MV Kuchele, MV Tangazo, MV Lindi, MV SAR II, MV Ilagala, na MV Kilombero. Miongoni mwa vivuko hivyo ambavyo havifanyi kazi, sita vilikuwa vikisubiri kukaguliwa kwa ajili

ya ukarabati, huku vitatu vikionekana kuwa chakavu na hakutakuwa na tija iwapo vitakarabatiwa.

Sababu kubwa za vivuko hivyo kutofanya kazi ni pamoja na kuchelewa kwa michakato ya ukaguzi na ukarabati na uhaba wa fedha za ukarabati. Hali hii imesababisha kukosekana kwa huduma za vivuko, upotevu wa mapato kutokana na kupungua kwa uwezo wa vivuko kufanya kazi, na athari katika ufanisi wa shughuli za Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania.

**Ninapendekeza TEMESA ichukue hatua madhubuti ili kuharakisha mchakato wa ukaguzi na ukarabati wa vivuko visivyofanya kazi. Aidha, TEMESA inapaswa kufanya tathmini ya kina ya vivuko vilivyochakaa ili kubaini njia mbadala, kama vile kuviondoshwa au kubadilisha na vivuko vipya.**

#### 10.4.3 Kutokamilika kwa Ujenzi wa Nyumba 300 za Watumishi wa Umma Zenye Thamani ya Sh. Bilioni 20 katika Eneo la Nzuguni, Dodoma

Dhamira ya Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ni kutoa makazi bora na rafiki wa mazingira kwa serikali na watumishi wa umma kupitia biashara bora, huduma za ushauri, na usimamizi wa mali zisizohamishika.

Tarehe 25 Novemba 2021, Wakala wa Majengo Tanzania ilianza ujenzi wa nyumba 150 za watumishi wa umma (awamu ya kwanza) katika eneo la Nzuguni, Dodoma kwa makadirio ya gharama ya mradi ya Sh. bilioni 14. Mradi ulipangwa kukamilika ifikapo tarehe 31 Desemba 2022 lakini muda uliuhishwa hadi tarehe 30 Novemba 2023. Hata hivyo, katika ziara yangu ya tarehe 11 Januari 2024, nilibaini kuwa awamu ya kwanza ya mradi ilikuwa haijakamilika licha ya muda wa mradi kwisha tarehe 30 Novemba 2023. Pia, nilibaini kuwa nyumba 39 zilizojengwa katika awamu ya kwanza zilikuwa katika hatua za ukamilishaji, wakati nyumba 111 zilikuwa hazijafikia hatua za ukamilishaji.

Aidha, tarehe 1 Februari 2023, Wakala wa Majengo Tanzania ulianza ujenzi wa nyumba 150 za awamu ya pili kwa gharama ya Sh. bilioni 6. Awali mradi ulipangwa kukamilika ifikapo tarehe 31 Januari 2024, lakini tarehe ya kukamilika iliuhishwa hadi tarehe 30 Novemba 2024. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi huu, maendeleo ya mradi yalikuwa asilimia 15 tu licha ya muda wa mkataba kufikia asilimia 53.

Kutokamilika kwa miradi ya ujenzi wa awamu ya kwanza na pili yenye thamani ya Sh. bilioni 20 kulitokana na upungufu wa maji na upungufu wa fedha, hivyo

kukwamisha dhamira ya Wakala ya kutoa makazi kwa watumishi wa Serikali na Umma, hasa kwa kuzingatia ongezeko la watumishi wa umma wanaohamia Dodoma. Pia, ucheleweshaji huu unaweza kusababisha gharama za nyongeza kutokana na kupanda kwa bei ya vifaa vya ujenzi.

**Ninapendekeza Serikali ihakikishe TBA inaboresha usimamizi wa miradi ili kukamilisha miradi huo kwa wakati na kurekebisha dosari katika utekelezaji wa ujenzi.**

#### 10.4.4 Kuvamiwa kwa Hekta 717,671.58 za Hifadhi ya Misitū

Kifungu cha 26 (g) cha Sheria ya Misitu ya Mwaka 2002 kinatamka kuwa hakuna mtu atakayemiliki au kuishi katika ardhi yoyote ndani ya hifadhi ya misitu ya mamlaka ya kitaifa au ya mtaa isipokuwa kama ni mwenye kibali kinachotambulika ndani ya hifadhi hiyo, au ameingia makubaliano kwa mujibu wa masharti ya sheria.

Hata hivyo, wakati wa ukaguzi wangu katika Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), nilibaini masuala kadhaa ya uvamizi yanayoathiri jumla ya hekta 717,671.58 katika hifadhi mbalimbali za misitu, ikiwemo Hifadhi ya Msitu wa Nyantakara (Biharamulo - Kahama), Hifadhi ya Msitu wa Kyarano, Hifadhi ya Msitu wa Kyanyari, Hifadhi ya Msitu wa Ruiga, Hifadhi ya Msitu wa Mto Nikonga, Hifadhi ya Msitu wa Mlima Mkwani - Mlema Kiiga, na Hifadhi ya Msitu wa Shamba la Hisa la Malya. Licha ya idadi kubwa ya uvamizi na athari zake zinazoweza kujitokeza kwa maliasili zilizopo, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania ulikuwa haujatayarisha mikakati na sera ya kushughulikia, kutatua, na kupambana na uvamizi huo.

Uvamizi uliotambuliwa katika hifadhi nyingi za misitu yana athari kubwa kwa uharibifu wa mazingira, upotevu wa makazi ya wanyamapori, uharibifu wa rasilimali, na kuzuka kwa migogoro ya kisheria, mambo yanayoweza kuathiri uchumi wa nchi na jamii, na kuharibu jina la taasisi.

**Ninapendekeza TFS itengeneze mikakati na mipango ya ufuatiliaji ili kushughulikia masuala ya uvamizi yaliyobainika katika hifadhi nyingi za misitu.**



#### 10.4.5 Kuondolewa kwa Kamera za Kiotomatiki za Kudhibiti Mwendokasi wa Magari zenye Thamani ya Sh. Milioni 381.75 katika Maeneo ya Ubena Zomozi na Bwawani

Tarehe 16 Juni 2017, Wizara ya Ujenzi iliingia mkataba na Kampuni ya M/S Kamang Investment kwa ajili ya usambazaji, ufungaji, upimaji, na uanzishaji wa kamera za kiotomati za kudhibiti mwendokasi, kwa mkataba wa Sh. milioni 381.75. Mradi huo ulikamilika na kukabidhiwa na mshauri mwelekezi mwezi Januari 2019. Mradi huo ulilenga kuimarisha usalama barabarani kwa kufuatilia mwendokasi wa magari na kuhimiza uzuiaji wa mwendokasi zaidi ya unaohitajika katika maeneo ya Ubena Zomozi na Bwawani kando ya Barabara kuu ya TANZAM ili kupunguza ajali za barabani.

Nilibaini kuwa mwezi Agosti 2022, kamera hizo zilitolewa ili kuwezesha malori kusafirisha mizigo maalumu (urefu) kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanda cha Sukari cha Mbigiri. Hata hivyo, hadi kufikia muda wa ukaguzi wangu mwezi Novemba 2023, kamera hizo zilikuwa hazijarejeshwa.

Wizara ilinifahamisha kuwa kamera hazikufungwa tena kutokana na kutumia teknolojia iliyokwisha muda wake, ambayo inazuia upitishaji wa mizigo mingi maalumu katika barabara kuu ya TANZAM. Sababu nyingine ni kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iko kwenye mchakato wa kuweka teknolojia ya hali ya juu kwenye barabara kuu, hivyo kuzifanya kamera na mfumo huo wa awali kupitwa na wakati. Hata hivyo, kwa maoni yangu, udhaifu huu unaonesha mipango isiyoridhisha ya Wizara, hivyo kusababisha hasara ya Sh. milioni 381.75 ambazo ni gharama za kufunga kamera hizo.

Napendekeza Wizara ya Ujenzi iunganishe kamera zilizoondolewa pamoja na juhudi zinazoendelea kufanywa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili kupunguza hasara zinazotokana na kutotumika kwa kamera hizo na kuhakikisha kunakuwa na mipango ya kutosha ya matumizi bora ya fedha za walipa kodi.

#### 10.4.6 Kutokarabatiwa kwa Barabara na Miundombinu ya Viwanja vya Ndege yenye Thamani ya Sh. Milioni 545

Kifungu cha 3 cha Sheria ya Utalii ya Mwaka 2008 kinaeleza kuwa watu wote wanaotumia mamlaka au kutekeleza majukumu yoyote chini ya Sheria hii wajitahidi kukuza Sera ya Taifa ya Utalii, utalii wa kimazingira, utalii wa

kitamaduni, na aina zingine zozote za utalii zinazotoa uhusiano bora wa kisekta, kutengeneza ajira, na kuleta maendeleo endelevu.

Katika mapitio yangu katika Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania, nilibaini kulikuwa na miundombinu iliyotelekezwa yenye thamani ya Sh. milioni 545 katika Hifadhi ya Wanyama Maswa, Mkoa wa Simiyu ikiwa pamoja na kilomita 135 za barabara yenye thamani ya Sh. milioni 500 kutoka Butuli hadi Mbono - Makao iliyojengwa mwaka 2021. Sehemu nyingine iliyotelekezwa ni Uwanja Mdogo wa Ndege wa Butuli (kilomita 1.6) uliojengwa mwaka 2021 kwa thamani ya Sh. milioni 45 kwa lengo la kutangaza shughuli za utalii kwa kusaidia urahisi wa usafiri ili kuhamasisha watu wengi zaidi kutembelea eneo hilo. Hata hivyo, wakati wa ziara yangu ya tarehe 5 Septemba 2023, nilibaini kuwa, barabara na uwanja wa ndege haukufanyiwa ukarabati tangu mwaka 2022, hivyo miundombinu hii kutokuwa katika hali nzuri kwa matumizi.

Sababu kuu ya kutelekezwa kwa miundombinu hii ni uhaba wa fedha za ukarabati. Hali hii inaashiria upotevu wa rasilimali jambo linalodhoofisha utangazaji wa utalii.

**Napendekeza Serikali itoe fedha za kutosha kwa TAWA kwa ajili ya matengenezo ya viwanja vya Ndege na miundombinu ya barabara ili kukuza shughuli za utalii.**

#### 10.4.7 Usimamizi Usioridhisha wa Miundombinu ya Viwanja vya Ndege

Wakati wa ukaguzi katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania, nilibaini udhaifu katika usimamizi wa miundombinu ya viwanja vya ndege kama inavyofafanuliwa hapa chini.

##### a) **Kutelekezwa kwa taa 217 za uwanja wa ndege (AGL) zenye thamani ya dola za Marekani 334,986.05 katika Uwanja wa Ndege wa Dodoma**

Wakati wa ziara yangu kwenye Uwanja wa Ndege wa Dodoma, nilibaini kuwa taa 217 za uwanja wa ndege (AGL) zenye thamani ya dola za Marekani 334,986.05 zinazotumia nishati ya jua zilitelekezwa kwenye stoo ya uwanja huo baada ya kubadilishwa na uwanja kuanza kutumia taa zinazotumia nishati ya umeme. Aidha, nilibaini kuwa hapakuwa na mpango wa kuhamisha taa hizo zilizotelekezwa kwenye viwanja vya ndege vingine vyenye mahitaji makubwa, licha ya taa hizo kuwa katika hali nzuri. Nina wasiwasi hali ya taa hizo zilizotelekezwa inaweza kuwa mbaya kutokana

na mambo mbalimbali kama vile ukosefu wa matengenezo na uharibifu unaoweza kutokea kutokana na utunzaji usioridhisha.

**b) Matumizi ya simu za mkononi kwa ajili ya mawasiliano na mnara wa udhibiti katika Uwanja wa Ndege wa Bukoba**

Kanuni ya 259, 260 na 263 ya Kanuni za Usafiri wa Anga (Viwanja vya Ndege) za Mwaka 2017 zinamtaka mwongozaji wa ndege kuhakikisha kuwa vifaa vya uokoaji vinaendana na kiwango cha shughuli za ndege katika uwanja husika, ambapo magari ya uokoaji na zimamoto yanapaswa kuwa na uwezo wa kufika sehemu ya kila njia ya kurukia ndege ndani ya muda usiozidi dakika tatu. Pia, kanuni zinataka kuwa na mfumo wa mawasiliano bora unaounganisha kituo cha zimamoto, magari ya uokoaji, na mnara wa udhibiti kwenye uwanja wa ndege.

Hata hivyo, wakati wa ukaguzi wangu kwenye Uwanja wa Ndege wa Bukoba nilibaini kuwa wafanyakazi wa udhibiti wa ndege ardhini walikuwa wakitumia simu za mkononi kupokea taarifa za safari na kuwasiliana na Mnara wa Udhibiti wa Ndege uliopo Mwanza, kinyume cha sheria.

**c) Kukosekana kwa kamera za CCTV katika Viwanja vya Ndege vya Geita na Sumbawanga**

Kanuni ya 2 ya Kanuni za Usalama wa Usafiri wa Anga za Mwaka 2018 inataka kila mwendeshaji wa uwanja wa ndege unaohudumia usafiri wa anga kuwajibika kwa usalama wa vifaa ili kufikia malengo ya usalama wa anga. Hata hivyo, katika ziara yangu ya kutembelea Viwanja vya Ndege vya Geita na Sumbawanga, nilibaini kutokuwapo kwa kamera za CCTV kwenye majengo hayo, jambo ambalo ni kinyume cha kanuni.

**d) Kutokuwapo kwa mfumo wa maji wa kuzima moto katika Uwanja wa Ndege wa Mpanda**

Kwa mujibu wa Kiambatisho cha 14 cha Viwango na Mbinu Zinazopendekezwa (SARPs) za Usanifu na Uendeshaji wa Viwanja vya Ndege chini ya Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO), uwanja wa ndege unapaswa kuwa na hatua zinazofaa za usalama dhidi ya moto, ikiwa pamoja na mfumo wa zimamoto ili kuhakikisha usalama wa shughuli za ndege na abiria. Hata hivyo, ziara yangu ya mwezi Oktoba 2023 ilibaini ukosefu wa mfumo wa maji wa zimamoto katika Uwanja wa Ndege wa Mpanda, hivyo kuwa hatari kwa uwanja wa ndege endapo moto utatokea.

#### e) Eneo la msitu ndani ya maeneo ya Uwanja wa Ndege wa Mtwara

Katika ziara yangu ya kutembelea uwanja wa ndege wa Mtwara, nilibaini kuwapo kwa eneo la msitu ndani ya uwanja huo. Sehemu hii ya msitu haikuwa na usimamizi mzuri, hivyo kuzua wasiwasi kuhusu utendaji kazi na usalama wa uwanja wa ndege. Kuwapo kwa eneo la msitu ndani ya uwanja wa ndege kunaweza kuleta hatari za kiusalama kutokana na uwezekano wa kuishi wanyamapori, jambo ambalo linaweza kuhatarisha maisha ya wafanyakazi wa uwanja wa ndege, abiria, na ndege.

#### f) Hatari za kiusalama inayotokana na mnara usiotumika katika Uwanja wa Ndege wa Mtwara

Ukaguzi wangu katika Uwanja wa Ndege wa Mtwara ulibaini kuwapo kwa mnara uliotelekezwa na kutotumika ndani ya uwanja huo. Kuwapo kwa mnara huo kunaweza kusababisha hatari ya kiusalama kwa ndege wakati wa kutua na kuruka ikiwa mnara hautadhibitiwa ipasavyo.

Kwa maoni yangu, kuachwa kwa vifaa muhimu, matumizi ya simu kwa mawasiliano, ukosefu wa CCTV, kutokuwapo kwa mfumo wa maji ya zimamoto, na kuwapo kwa eneo la msitu na mnara usiotumika ndani ya uwanja wa ndege kunachangia hatari za kiusalama. Hatua za haraka zinahitajika ili kuimarisha usimamizi wa miundombinu, na kuzingatia kanuni na hatua za kiusalama ili kulinda wafanyakazi, abiria, ndege, na uendeshaji wa viwanja vya ndege.

**Ninapendekeza Serikali kuhakikisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania inaimarisha usimamizi wa miundombinu ya viwanja vya ndege, na kuzingatia kanuni na hatua za usalama ili kulinda usalama wa wafanyakazi, abiria na uendeshaji wa viwanja vya ndege.**

#### 10.4.8 Maji kutoka kwenye mabwawa yaliyojengwa kushindwa kukidhi viwango vya kimaabara

Kifungu cha 88(1)(a)(I) cha Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji ya Mwaka 2009 kinawataka wamiliki wa mabwawa kuomba kibali cha matumizi ya maji kwa Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji au afisa wa maji ya bonde, na kuwasilisha nyaraka muhimu ikiwa pamoja na taarifa ya ubora wa maji.

Mapitio yangu ya ripoti ya uchambuzi wa ubora wa maji kutoka Maabara ya Ubora wa Maji ya Singida iliyotolewa mwezi Agosti 2023 yalibaini kuwa mabwawa manne yaliyokamilika (Kambi ya Nyasa, Paranga, Hanet, na Kelema)

katika Wilaya za Chemba na Bahi, yalishindwa majaribio ya kolifomu na E. Koli. Viwango vya kolifomu vilikuwa kati ya asilimia 12 na 56, na viwango vya E. Koli vilikuwa kati ya asilimia 8 na 15, zaidi ya kiwango cha asilimia sifuri (0%) kinachotakiwa na Kiwango cha Taifa cha Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (TZS 789: 2018-EAS12:2018).

Ripoti ilionesha kuwa viwango vya tope kwa Mabwawa ya Kelema na Hanet vilikuwa 55 NTU na 60 NTU mtawalia, zaidi ya kiwango kinachotakiwa cha 25 NTU. Vilevile, viwango vya rangi ya maji kwa Mabwawa ya Kelema na Hanet vilikuwa TCU 55 na TCU 53 mtawalia, zaidi ya kiwango kilichopendekezwa na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira cha 50 TCU. Ripoti hiyo ilihitimisha kuwa, bila ya marekebisho maji hayo ya mabwawa hayafai kwa matumizi ya binadamu.

Sababu kuu ya kushindwa kwa majaribio ya ubora wa maji ni uchafu katika vyanzo vya maji vya nje, kama vile maji ya kilimo, taka za binadamu au wanyama, au utunzaji usiofaa wa vifaa vya ujenzi wakati wa ujenzi wa miradi ya mabwawa, pamoja na usimamizi usioridhisha. Kutokuwapo kwa ubora kwenye maji husababisha hatari kubwa za kiafya kwa jamii zinazotegemea mabwawa hayo kwa maji ya kunywa. Hatari hizo zinaweza kusababisha magonjwa yatokanayo na maji na madhara mengine ya kiafya. Uchafuzi huo pia unazua hofu kuhusu ufanisi na usalama wa miradi ya mabwawa, na kuathiri imani ya jamii na mafanikio ya juhudi za usimamizi wa rasilimali za maji.

**Ninapendekeza Bodi ya Maji Bonde la Ndani kuimarisha ufuatiliaji na utekelezaji wa viwango vya ubora wa maji, kuboresha taratibu za matengenezo ya mabwawa, na kuchukua hatua za kuzuia uchafuzi wa maji kutoka kwenye vyanzo vya nje. Zaidi ya hayo, kusimamisha matumizi ya maji kutoka kwenye mabwawa hadi maji hayo yatakapofanyiwa matibabu sahihi.**

#### **10.4.9 Kutokuwekwa kwa mita jumuiifu katika maeneo ya kuchukua maji kwenye vyanzo ili kufuatilia kiasi halisi cha maji kilichotumika**

Kanuni ya 4 (1) ya Kanuni za Usimamizi wa Rasilimali za Maji (Mpangilio wa Ada) za Mwaka 2019 inaitaka bodi ya maji ya bonde kuhakikisha inaweka mita jumuiifu katika eneo la chanzo cha maji kwa madhumuni ya kupima kiasi cha maji kinachotumiwa na mwenye kibali.

Mapitio yangu yalibainisha kuwa, katika bodi tano za maji za mabonde kutokuwekwa mita jumuiifu za maji kwa watumiaji wa maji 6,859 kwenye

vyanzo vya maji. Nina maoni kuwa, bila mfumo wa mita jumuifu, kuna hatari kubwa ya kupoteza maji kutokana na kuchukua maji kupita kiasi unaofanywa na watumiaji wa maji. Jambo hili linaweza kuzinyima mapato bodi za maji za mabonde na kuhatarisha uendeleu wa rasilimali za maji. **Jedwali Na. 56** linaonesha bodi za mabonde ambazo hazikuwekewa mita jumuifu.

**Jedwali Na. 56: Bodi za Mabonde ambazo Hazikuwekewa Mita Jumuifu**

Na.	Bonde la Maji	Idadi
1.	Bodi ya Maji Bonde la Pangani	1,922
2.	Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Nyasa	849
3.	Bodi ya Maji Bonde la Kati	1,264
4.	Bodi ya Maji Bonde la Wami Ruvu	2,766
5.	Bodi ya Maji Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini	58
	<b>Jumla</b>	<b>6,859</b>

Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi

Napendekeza Bodi za Maji za Mabonde kuhakikisha kuwa mita jumuifu za maji (cumulative flow meters) zinawekwa katika kila sehemu ya kuchukulia maji ili kudhibiti na kujua kiasi halisi cha maji yanayochukuliwa kutoka kwenye vyanzo vya maji ili kuhakikisha uendeleu wa rasilimali za maji.

#### 10.4.10 Mita za maji kutofungwa kwa wateja

Kifungu cha 21 (c) na (d) cha Sheria ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2019 kinaitaka mamlaka ya maji kufunga mita za maji kwa madhumuni ya kupima kiasi cha maji yanayotolewa kwa mtumiaji; na kutoza ada kwa kiwango halisi cha huduma zinazotolewa.

Katika mwaka wa fedha wa 2022/23, nilibaini kuwa mamlaka tano za maji zilikuwa na wateja 2,318 ambao hawakufungiwa mita za maji. **Jedwali Na. 57** linaonesha mamlaka za maji zilizokuwa na wateja ambao hawakufungiwa mita za maji. Udhaifu huu uliathiri uwezo wa mamlaka kuongeza mapato kwenye vyanzo vyake.

**Jedwali Na. 57: Mamlaka za Maji Zilizokuwa na Wateja ambao Hawakufungiwa Mita za Maji**

Na.	Jina la Taasisi	Idadi
1.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Rujewa	882
2.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Songe	45
3.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Itumba-Isongole	882
4.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Liwale	71
5.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mombo	438
	<b>Jumla</b>	<b>2,318</b>

**Chanzo:** Taarifa za Ukaguzi

Tathmini yangu imebaini kuwa, sababu ya msingi ya kuwa na idadi kubwa ya wateja wasiofungiwa mita za maji ni mamlaka za maji kutokuwa na vitendeakazi vya kufunga na kushindwa kutunza miundombinu ya mita, ikiwa pamoja na mita na vifaa vinavyohitajika. Bila kupima kwa usahihi matumizi ya maji, inakuwa vigumu kuwatoza wateja kulingana na matumizi yao halisi ya maji. Hali hii inaweza kusababisha upotevu wa mapato au makosa katika utozaji wa gharama za maji.

**Napendekeza mamlaka za maji kuweka vipaumbele vya kuweka mita kwa wateja wote ambao hawana mita. Hii itawezesha mamlaka kutoza wateja kulingana na matumizi yao halisi, na hivyo kuongeza ukusanyaji wa mapato.**

#### **10.4.11 Usimamizi Usioridhisha wa Ujenzi wa Miradi Saba ya Barabara Yenye Thamani ya Sh. Trilioni 3.75 Iliyofadhiliwa chini ya Njia ya Mkataba (EPC+F)**

Njia ya mkataba ya Uhandisi, Ununuzi, Ujenzi, na Ufadhili (EPC+F) ni makubaliano ya kina ambapo mkandarasi au muanzilishi wa mradi ana jukumu la kusimamia mzunguko mzima wa mradi, kuanzia usanifu na uhandisi hadi ununuzi, ujenzi na ufadhili.

Tarehe 16 Juni 2023, TANROADS ilisaini mikataba saba kwa Njia ya Uhandisi, Ununuzi, Ujenzi na Ufadhili (EPC+F) yenye thamani ya Sh. trilioni 3.75, kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 58**.

Wakati wa mapitio ya utekelezaji wa zabuni na mkataba husika, nilibaini madhaifu yanayohitaji utatuzi wa haraka, kama yalivyojadiliwa hapa chini:

##### **a) Kutojulikana kwa Mahitaji ya Serikali kuhusu Chanzo cha Ufadhili wa Miradi ya EPC+F**

Kwa mujibu wa Masharti ya Zabuni (ITT) katika nyaraka za zabuni za miradi ya EPC + F zilizochapishwa kwenye TANePS; wazabuni walitakiwa kuwasilisha angalau mapendekezo ya wafadhili wawili kwa zabuni husika. Wakati wa tathmini ya kiufundi na kifedha kwa wafadhili waliopendekezwa iliyofanywa kwa ushirikiano na Wizara ya Fedha, nilibaini kuwa masharti ya wafadhili hao yalibainika kutokua na maslahi kwa serikali hivyo serikali iliamua kutafuta njia mbadala ya kufadhili miradi hiyo.

Hata hivyo, mpaka muda wa ukaguzi mwezi Desemba 2023, serikali ilikuwa bado haijapata wafadhili wa miradi hiyo saba. Kwa maoni yangu, kushindwa kuweka mkakati wa kina wa ufadhili kumeifanya miradi hiyo kukosa chanzo cha fedha cha uhakika.

**b) Kuchelewa Kuanza kwa Kazi za Ujenzi wa Miradi**

Nilibaini kuwa kufikia Desemba 2023, kazi za ujenzi zilikuwa bado hazijaanza, ikionesha ucheleweshaji wa miezi sita tangu tarehe ya kusainiwa kwa mikataba.

Sababu kuu ya kuchelewa kuanza kwa mradi ni kutokana na wakandarasi kushindwa kuwasilisha dhamana ya benki ya utendaji kazi yenye thamani ya Sh. bilioni 375.51. Hii ni kinyume na Kifungu cha 14 cha mikataba, ambacho kinawataka wakandarasi kuwasilisha Dhamana ya Benki isiyo na Masharti sawa na asilimia 10 ya kiasi cha mkataba kilichokubaliwa, ili kumuwezesha mwajiri (TANROADS) kukabidhi wakandarasi maeneo ya ujenzi na hati ya kuanza kazi za ujenzi.

Kulingana na matokeo haya, nina mashaka kuwa bila ufadhili wa uhakika, miradi inaweza kukabiliwa na kuchelewa kwa utekelezaji, unaoweza kusababisha ongezeko la gharama (kutokana na riba ya ucheleweshaji malipo), na migogoro ya kisheria inayoweza kutokea na wakandarasi na wafadhili, na hivyo kuhatarisha mafanikio ya miradi husika.

**Jedwali Na. 58: Miradi ya Ujenzi wa Barabara Chini ya Mikataba ya EPC+F**

Na	Jina la Mradi	Nambari ya Mkataba	Jina la Mkandarasi	Gharama (Sh.)
1	Ujenzi wa Barabara ya Masasi-Nachungwea-Liwale (175Km) Kwa kiwango cha lami	TRD/HQ/1072/2022/23	M/s China Railways 15 Bureau Group Corporation	234,781,479,144
2	Ujenzi wa Barabara ya Karatu-Mbulu-Haydom-Sibiti River-Lalago-Maswa (339Km) kwa kiwango cha lami.	TRD/HQ/1073/2022/23	M/s China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC) Jv M/s China Railways 15 Bureau Group Corporation Ltd	553,493,783,684
3	Ukarabati wa Barabara za Igawa-	TRD/HQ/1071/2022/23	M/s China Civil Engineering	1,113,011,999,345



Na	Jina la Mradi	Nambari ya Mkataba	Jina la Mkandarasi	Gharama (Sh.)
	Uyole-Songwe-Tunduma (218Km) kwa kiwango cha lami (yaani, Barabara ya Njia Mbili ya Igawa-Uyole (Km 106) Sehemu ya Barabara Moja ya Barabara ya Mbeya (48.9Km) na Njia ya Njia Mbili IF8-KM (Tunduma)		Construction Corporation (CCECC)	
4	Ujenzi wa Barabara ya Arusha - Kibaya - Kongwa (453.42Km) kwa kiwango cha lami.	TRD/HQ/1075/2022/23	M/s China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC) Jv M/s China Railways 15 Bureau Group Corporation Ltd	546,294,711,452
5	Ujenzi wa Barabara ya Handeni-Kiberashi-Kijingu-Njaro-Olboroti Mrijo-Dalai-Chambalo-Chemba-Kwa Mtoro-Singida (460Km) kwa Kiwango cha Lami.	TRD/HQ/1066/2022/23	M/s CRCEG-COVEC-CREC4	432,542,372,881
6	Ujenzi wa Barabara za Mafinga-Mtwango- Mgololo (81Km) kwa kiwango cha Lami	TRD/HQ/1070/2022/23	M/s Sinohydro Corporation Ltd	110,580,728,375
7.	Ujenzi wa Barabara ya Kidatu-Ifakara-Lupiro-Malinyi-Kilosa kwa Mpepo-Londo-Lumecha/Songea (512Km) kwa Viwango vya Lami.	TRD/HQ/1074/2022/23	M/s China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC) Jv M/s China Railways 15 Bureau Group Corporation Ltd	764,437,076,827
		<b>Jumla</b>		<b>3,755,142,151,708</b>

Chanzo: Taarifa ya Mapungufu

Napendekeza Serikali kuhakikisha TANROADS inaharakisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya EPC - F ili kusaidia ukamilishaji wa miradi kwa wakati na kuepuka ongezeko la gharama. Aidha, katika siku zijazo, wakala ihakikishe inabaini chanzo endelevu cha fedha za miradi kabla ya kuanza kwa miradi.

#### 10.4.12 Kutofungwa kwa Mtambo wa Gesi ya Oksijeni katika Hospitali ya Rufaa Songwe

Wizara ya Afya ilisaini mkataba wenye kumbukumbu namba MOHCDGEC/2020-2021/G/04 tarehe 22 Oktoba 2020 kwa ajili ya kusambaza, kufunga, na kuwasha mitambo 12 ya oksijeni katika hospitali za rufaa katika mikoa ya Kigoma, Lindi, Morogoro, Mara, Njombe, Tabora, Shinyanga, Simiyu, Mara, Mwanza, Songwe na Katavi chini ya ufadhili wa Mfuko wa Dunia wa *Kupambana na UVIKO 19 (C19-RM)*. Gharama ya mkataba ilikuwa dola za Marekani 3,125,208 sawa na Sh. bilioni 7.18. Kwa mujibu wa makubaliano, mkataba ulipaswa ukamilike ndani ya miezi miwili, ila muda wa kukamilika uliongezwa hadi kufikia tarehe 30 Novemba 2021 kutoka tarehe 22 Disemba 2020. Hata hivyo mpaka kufikia tarehe 30 Novemba 2021 Mkandarasi alikuwa amesha lipwa jumla ya Sh. 6.43 billion

Ukaguzi pamoja na ziara niliyofanya tarehe 18 Septemba 2023 katika Hospitali ya Rufaa Songwe nilibaini kuwa mtambo wa kusambaza oksijeni ulikuwa haujafungwa kutokana na kutokamilika kwa uwasilishaji wa baadhi ya vifaa vya mtambo huo. Ilibainika pia kuwa baadhi ya vifaa vilipokelewa tarehe 9 Januari 2023 na vingine vilikuwa havijawasilishwa hadi kipindi ninakamilisha ukaguzi wangu mwezi Disemba 2023.

Hofu yangu ni kuwa muda mrefu umepita lakini ufungaji wa mtambo huo haujakamilika, jambo ambalo si tu linakwamisha kupata thamani ya fedha bali pia inakwamisha manufaa yaliyokusudiwa kwa jamii kwa utumiaji wa mtambo huo.

Ninapendekeza Wizara ya Afya kuhakikisha kuwa inamsimamia kwa karibu Mkandarasi ili kuhakikisha anafikisha vifaa vilivyobaki na kukamilisha ufungaji wa mtambo wa oksijeni.

#### 10.5 Kutofikiwa kwa Malengo ya Kimkakati

Nilibaini kutofikiwa kwa malengo ya kimkakati katika taaasisi za serikali kama ifuatavyo:

### 10.5.1 Upungufu wa uzalishaji wa mbegu tani za metriki 117,557.62 ikilinganishwa na mahitaji

Aya ya 3.2.1 (ii) ya Majukumu na Muundo wa Wizara ya Kilimo ulioidhinishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 04 Julai 2022 unaeleza kuwa idara ya uzalishaji wa mazao itaimarisha matumizi ya teknolojia ili kuongeza uzalishaji wa mazao.

Katika ukaguzi wangu katika Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2022/23, nilibaini kuwa mahitaji ya mbegu nchini yalifikia tani za metriki 187,197. Hata hivyo, wazalishaji wa mbegu walifanikiwa kuzalisha tani za metriki 69,639.38 tu za mbegu, hivyo kutokidhi mahitaji ya mbegu ya tani za metriki 117,557.62 (63% ya mahitaji yote ya mbegu).

Nilibaini zaidi kuwa uzalishaji mdogo wa mbegu ulichangiwa na uhaba wa miundombinu ya kuhifadhi na kusambaza mbegu, hivyo kuathiri upatikanaji wa mbegu bora. Kwa maoni yangu, ukosefu wa mbegu za kutosha unachangia kupungua kwa uzalishaji wa jumla wa bidhaa za chakula na kuathiri usambazaji wa mazao.

**Napendekeza Serikali kupitia Wizara ya Kilimo kuwa na mkakati wa kina unaohusisha uboreshaji wa kanuni za kilimo, miundombinu, sera, na uendelezaji wa aina ya mazao unaostahimili changamoto za kimazingira, hivyo kukidhi mahitaji ya mbegu.**

### 10.5.2 Utegemezi mkubwa wa mbolea kutoka nje ya nchi kwa tani za metriki 824,085

Aya ya 3.2.1 (ii) ya Majukumu na Muundo wa Wizara ya Kilimo ulioidhinishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 04 Julai 2022 inaagiza Kitengo cha Pembejeo za Kilimo kuchochea uwekezaji katika utengenezaji wa pembejeo za kilimo nchini.

Hata hivyo, katika mwaka wa fedha wa 2022/2023, jumla ya mahitaji ya mbolea nchini ilifikia tani 908,731, huku uzalishaji wa ndani ukichangia tani 84,646 tu, na tani 824,085 zilizobaki (sawa na asilimia 91) ziliagizwa kutoka nje. Ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliopita 2021/2022, mbolea iliyoagizwa kutoka nje ilikuwa tani 379,927, sawa na asilimia 85 ya jumla ya mbolea yote tani 442,651. Hali hii inaonesha ongezeko la utegemezi wa mbolea kutoka nje kutoka asilimia 85 hadi 91.

Sababu kuu ya hali hii ni kutokuwapo kwa uzalishaji wa ndani wa mbolea muhimu ambazo ni mbolea ya fosfeti (SA), mbolea ya sulfeti ya amonia (CAN), Mbolea ya urea, na michanganyiko mbalimbali ya NPK kutokana na uhaba wa malighafi na ukosefu wa wawekezaji wanaotengeneza mbolea. Utegemezi mkubwa wa uagizaji wa mbolea kutoka nje huleta hatari za kiuchumi kutokana na kuongezeka kwa bei, kutokuwa na uhakika wa ugavi, na kubadilika kwa viwango vya ubadilishaji wa sarafu katika masoko ya kimataifa.

**Ninapendekeza Wizara ya Kilimo ishirikiane na washirika wa maendeleo katika kuongeza na kuimarisha usambazaji wa mbolea kupitia mipango ya uzalishaji wa ndani, juhudi za utafiti na maendeleo katika teknolojia ya mbolea, na sera saidizi.**

### 10.5.3 Kushindwa kununua metriki tani 79,990 za nafaka na uwezo mdogo wa kuhifadhi nafaka

Kwa mujibu wa mpango wake wa biashara, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), ilipanga kununua tani za metriki 100,000 za nafaka katika mwaka wa fedha 2022/2023. Hata hivyo, Wakala ulifanikiwa kununua tani 20,010 tu za nafaka, hivyo kuacha jumla ya tani za metriki 79,990 za nafaka ambazo hazikununuliwa, sawa na asilimia 80 ya mpango. Kati ya tani 20,010 za nafaka zilizonunuliwa, tani za metriki 18,463.581 ni mahindi (92%), tani za metriki 1,036.457 ni mtama (5%), na tani za metriki 509.962 ni mchele (3%). Hali hii inaonesha utegemezi mkubwa kwa mahindi kuliko mazao mengine ya nafaka. Udhaifu huu unahitaji mikakati zaidi ya kuzingatia katika ununuzi wa mazao mengine ya nafaka kuliko kuendelea na utegemezi mkubwa katika mahindi.

Aidha, mpango wa uwekezaji wa miaka 10 wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula wa kuanzia tarehe 2014/2015 hadi 2023/2024 unaonesha kuwa Wakala ulilenga kuongeza uwezo wa kuhifadhi chakula kwa tani za metriki 255,000, kutoka tani za metriki 251,000 zilizopo hadi tani za metriki 506,000, ikiwa pamoja na ujenzi wa silo zenye ujazo wa tani za metriki 190,000 na maghala yenye ujazo wa tani za metriki 65,000. Hata hivyo, hadi tarehe 30 Juni 2023, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula ulifanikiwa kuongeza uwezo wa kuhifadhi nafaka kwa tani za metriki 85,000 pekee (kutoka tani za metriki 251,000 hadi tani za metriki 336,000), kiwango ambacho ni chini ya lengo la kuongeza tani za metriki 170,000 (67%).

Ni maoni yangu kuwa hali hii imesababishwa na mifumo isiyoridhisha ya ufuatiliaji, uhaba wa rasilimali-fedha, na ucheleweshaji wa miradi ya ujenzi. Sababu hizi kwa pamoja zilizuia uwezo wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula kununua kiasi kilichopangwa cha nafaka na kuongeza uwezo wa kuhifadhi nafaka kama ilivyokusudiwa hapo awali. Changamoto hii isiposhughulikiwa, kutakuwa na hofu kutokuwa na uhakika wa chakula nchini.

**Ninapendekeza NFRA iwe na mifumo thabiti ya ufuatiliaji ili kufuatilia shughuli za manunuzi, na miradi ya uongezaji wa uwezo wa kuhifadhi, kuhakikisha utambuzi na utatuzi kwa wakati juu ya hitilafu zozote au ucheleweshaji. Pia, kuomba rasilimali fedha za kutosha kusaidia juhudi za ununuzi wa nafaka na kuharakisha mipango ya miradi ya ujenzi ya kuongeza uwezo wa uhifadhi.**

#### **10.5.4 Changamoto za uendeshaji kutokana na kusitishwa kwa fedha kutoka Wizara ya Kilimo**

Mfuko wa Uchocheaji wa Kilimo Tanzania unalenga kuleta mabadiliko makubwa katika sekta ya kilimo nchini kwa kusaidia mipango inayoboresha tija, uendeleu, na ustahimilivu. Mfuko pia unalenga kukusanya rasilimali, kukuza ushirikiano, na kuwekeza katika miradi inayohimiza uvumbuzi, teknolojia, na kujenga uwezo kwa wakulima wadogowadogo.

Tarehe 12 Mei 2023, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Uchocheaji wa Kilimo Tanzania (TACT) aliarifiwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo kuhusu kusitishwa kwa utoaji wa fedha. Katika mwaka 2022/2023, jumla ya Sh. milioni 460 zilisitishwa kupelekwa kwenye Mfuko huo kati ya Sh. bilioni 1.5 zilizoidhinishwa.

Kutokana na usitishaji huo, nilibaini upungufu huo wa kifedha ulisababisha matatizo makubwa ya fedha na kuathiri uendeshaji wa taasisi. Pia, nilibaini kuwa wafanyakazi wote waliondolewa kazini mnamo tarehe 15 Mei 2023 na hivyo kuathiri zaidi uendeshaji wa taasisi.

Wizara ya Kilimo kusitisha utoaji wa fedha kulikwamisha uwezo wa Mfuko wa Uchocheaji wa Kilimo Tanzania wa kuchochea mabadiliko katika sekta ya kilimo nchini kwa kuzuia uwezo wake wa kusaidia mipango inayolenga kuongeza tija, uendeleu, na ustahimilivu katika kilimo.

**Ninapendekeza Serikali kutatua masuala yaliyopelekea kusitishwa kwa ufadhili ili kuhakikisha ufadhili endelevu kwa mipango ya kilimo.**

### 10.5.5 Uwezo mdogo wa uzalishaji wa maji ikilinganishwa na mahitaji ya wateja

Kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2019 kinaitaka mamlaka ya maji kufanya kila njia ili kutoa huduma ya maji safi na usafi wa mazingira katika eneo lililo chini ya mamlaka yake.

Nilibaini kuwa mahitaji ya maji katika mamlaka 10 za maji kwa mwaka 2022/2023 yalikuwa mita za ujazo 11,096,159. Hata hivyo, mamlaka husika za maji zilikuwa na uwezo wa kuzalisha kwa mwaka mita za ujazo 3,092,238 tu. Hali hii ilisababisha upungufu wa mita za ujazo 8,003,921 (lita bilioni 8), sawa na upungufu wa asilimia 72. Upungufu kwa baadhi ya mamlaka za maji ulikuwa mkubwa, kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 59** hapa chini.

**Jedwali Na. 59: Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira Zilizokuwa na Uwezo Mdogo wa Kukidhi Mahitaji ya Maji**

Na.	Jina	Mahitaji ya Mwaka (m <sup>3</sup> )	Uzalishaji kwa Mwaka (m <sup>3</sup> /)	Upungufu (m <sup>3</sup> )
1	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kilindoni	889,140	124,830	764,310
2	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Rujewa	2,835,840	744,965	2,090,875
3	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kilwa Masoko	985,500	547,500	438,000
4	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Liwale	855,560	204,035	651,525
5	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Ludewa	709,704	399,331	310,373
6	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mombo	634,005	337,625	296,380
7	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Namanyere	1,074,925	88,651	986,274
8	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Utete	401,500	179,945	221,555
9	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Makete	803,000	319,740	483,260
10	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tunduru	1,906,985	145,616	1,761,369
	<b>Jumla</b>	<b>11,096,159</b>	<b>3,092,238</b>	<b>8,003,921</b>

**Chanzo:** Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti

Nilibaini kuwa chanzo kikuu cha upungufu wa maji ni uvujaji wa miundombinu ya maji kutokana na kuchakaa na uhaba wa miundombinu ya maji. Hali hii

ilisababisha uhaba wa maji, unaoweza kuathiri wananchi, biashara, na shughuli za kilimo.

**Napendekeza Serikali itoe kipaumbele kwa uboreshaji wa miundombinu katika mamlaka za maji ili kukidhi mahitaji ya maji.**

#### 10.5.6 Upungufu wa Wataalamu wa Afya na Vifaatiba katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Hospitali za Kanda, na Hospitali Maalumu

Aya ya 2.4 ya Mwongozo wa Uendeshaji uliotolewa na Wizara ya Afya mwezi Juni 2019 inataka hospitali za rufaa za mikoa, hospitali za kanda, na hospitali maalumu kuwa na wataalamu wa afya, dawa, na vifaatiba vya kutosha.

Ukaguzi wangu kwenye hospitali za rufaa za mikoa, hospitali za kanda, na hospitali maalumu katika mwaka wa fedha 2022/2023 ulibaini kuwa hospitali 17 za rufaa za mikoa, za kanda, na maalumu zilikuwa na upungufu wa wataalamu 217 wa afya; na hospitali 8 zilikuwa na upungufu wa vifaatiba 179 kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. XI**.

Ilibainika kuwa upungufu huu ulisababishwa na ufinyu wa bajeti ya kuajiri idadi ya kutosha ya wataalamu wa afya na kununua vifaatiba. Tatizo hili linazuia hospitali za hospitali za rufaa za mikoa, hospitali za kanda, na hospitali maalumu kutotoa huduma za rufaa za kutosheleza hivyo kusababisha hospitali hizi kutoa rufaa nyingi kwa wagonjwa kwenda hospitali za rufaa za juu.

**Ninapendekeza Serikali iweke kipaumbele katika mgao wa fedha za kutosha kwa sekta ya afya ili kuweza kuajiri wataalamu wa afya na kuhakikisha upatikanaji wa Vifaatiba hivyo kuboresha huduma za afya.**

#### 10.6 Usimamizi wa Vyombo Vya Kijamii Vya Utoaji Wa Huduma Za Maji (CBWSO)

Sehemu hii inawasilisha muhtasari wa ukaguzi wa jumla wa vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji. Inaelezea changamoto za kiuendeshaji na kiutawala wa vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji katika kutimiza majukumu yao kwa mujibu wa sheria iliyowekwa.

Vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji vimeanzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 32(1) cha Sheria ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2019. Kifungu hichi kinaeleza kuwa wanajamii lazima waidhinisha uundwaji wa kila CBWSO.

Vyombo hivi zinasajiliwa chini ya Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Msajili wa vyombo hivi ni meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini wa wilaya husika au mtu yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini kufanya kazi za usajili katika eneo ambalo halina meneja wa wilaya wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini.

Hivyo, Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini ina jukumu la kusimamia utendaji kazi wa vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji. Pia, ina jukumu la kuidhinisha katiba au makubaliano yaliyowasilishwa kwa CBWSO iliyopendekezwa; kuweka kumbukumbu na taarifa za vyombo hivyo; na kuchunguza jambo lolote linalohusu utekelezaji wa shughuli za vyombo hivyo.

Kifungu cha 33(1) cha Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2019 kimeainisha majukumu ya vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji ikiwemo kumiliki mali zinazohamishika na zisizohamishika zikiwemo vifaa vya kusambazia maji na miundombinu ya maji, kutoza ada ya kwa huduma ya maji iliyotolewa kwa wateja kupitia vituo vya umma au miundombinu ya maji; kutumia mita za maji kupima viwango vya maji vilivyotolewa kutoka kwenye vyanzo au kwa mteja; na kushiriki katika mashauriano na ushirikiano na mabaraza ya vijiji au taasisi zozote zinazosimamia matumizi ya ardhi.

Nilifanya ukaguzi wa vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji katika mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo nilikagua vyombo 136 kati ya vyombo 1,975 vilivyosajiliwa hadi tarehe 30 Juni 2023. Wakati wa ukaguzi wangu nilibaini masuala mbalimbali ambayo yanahitaji kuchuliwa hatua muhimu kama ilivyoelezwa hapo chini

#### 10.6.1 Mapato yasiyokusanywa ya thamani ya Sh. bilioni 1.14 yatokanayo na ankara za maji

Kifungu cha 35 (5) cha Sheria ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2019 kinaeleza kuwa, kuanzia tarehe ya kusajiliwa kwa chombo cha watoa huduma ya maji, watumiaji wa maji wanaopata huduma kutoka kwenye chombo hicho husika watalazimika kulipia huduma hiyo kwa kutumia kiwango kitakachotozwa na chombo husika.



Kifungu cha 38 (a) cha Sheria hiyohiyo, chanzo kikuu cha fedha kwa vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji ni gharama za maji zinazolipwa na kila mtumiaji anayepata huduma za maji kutoka chombo husika.

Nilifanya ukaguzi wa vitabu vya fedha vya vyombo 136 na kubaini kuwa mapato ya Sh. bilioni 1.14 hayakukusanywa kutoka kwa ankara za maji zilizotolewa kwa wateja waliopata huduma za maji kutoka vyombo 50. katika **Kiambatisho Na. XII** ni orodha ya vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji.

Kutokusanya mapato ni changamoto kuu kwa vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji, ambayo inaathiri uwezo wake wa kutoa huduma za maji kwani fedha zinabaki mikononi mwa wateja wakati wanaendelea kutumia maji bila malipo.

**Ninapendekeza Serikali, kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini kama msimamizi wa vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji, iweke mikakati na mbinu madhubuti za kukusanya mapato zitakazohakikisha wateja wanaopatiwa huduma za maji na vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji wanalipa ankara zao ili mapato hayo yasaidie kuboresha miundombinu ya maji na kufanya huduma za maji ziwe endelevu.**

#### 10.6.2 Vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji kutofikia lengo la kutoa huduma za maji kwa jamii

Kanuni ya 24(1) & (2) ya Kanuni za Maji Safi na Usafi wa Mazingira (Usajili na Uendeshaji wa Vyombo vya Kijamii vya Utoaji wa Huduma za Maji) za Mwaka 2019 inatoa wajibu kwa kila chombo cha watoa huduma ya maji kuwafikia wanufaika wake wote ndani ya eneo la huduma kama ilivyoainishwa kwenye cheti cha usajili wa chombo husika. Cheti cha usajili hueleza vijiji na mitaa ambayo chombo kinapaswa kuhudumia.

Vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji vinapewa mamlaka ya kutoa huduma ya maji safi na usafi wa mazingira kwenye eneo la huduma lililo chini ya mamlaka yake.

Wakati wa ukaguzi wangu nilipitia usajili wa vyombo 136 vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji na kuhakiki maeneo yaliyofikiwa na huduma za maji na nilibaini kuwa vyombo 7 vilikuwa na vijiji 77 vilivyosajiliwa chini yake kwa madhumuni ya kusambaza huduma ya maji safi lakini ni vijiji 24 tu sawa na asilimia 32 ndivyo vilikuwa vimefikiwa na huduma za maji, huku vijiji 53 sawa

na asilimia 68 vikiwa havina huduma za maji safi. **Kiambatisho Na. XIII** ni orodha ya vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji vilivyoshindwa kufikisha huduma za maji katika maeneo yake kama ilivyopangwa.

Ukosefu wa huduma za kutosha za maji umesababishwa na uchache na uchakavu wa mitandao ya maji, hivyo kuathiri sehemu kubwa ya wakazi wa vijiji husika. Hali hii ni kikwazo katika upatikanaji wa maji safi na salama na inahatarisha afya za wananchi, mifugo, shughuli za kilimo, na maendeleo ya jamii kwa ujumla.

**Ninapendekeza Serikali, kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, iweke mikakati madhubuti ya usimamizi ili kuhakikisha upatikanaji wa kuridhisha wa maji katika maeneo ambayo vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji yaliyopangiwa vimepangiwa kutoa huduma za maji hivyo kufikia malengo ya kitaifa ya kufikisha huduma za maji na usafi wa mazingira kwa wananchi wote.**

### 10.6.3 Mita za maji kutohakikiwa na Wakala wa Vipimo

Kifungu cha 19 (2) cha Sheria ya Vipimo, Sura ya 340 kinataka kila chombo cha kupima kipimo chochote kuhakikiwa na hatimaye kuthibitishwa na msimamizi anayetambulika kwenye sheria hiyo, ambaye ni Wakala wa Vipimo. Pia, Kifungu cha 21 (1) cha Sheria ya Vipimo, Sura ya 340 kinataka kila uzito, kipimo, chombo cha kupimia kinachotumika au kinachokusudiwa kutumika katika biashara kugongwa alama ya uhakiki iliyoainishwa ili kuzuia ulaghai.

Hata hivyo, katika ukaguzi wangu nilibaini mita za maji 15,827 za vyombo 32 vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji hazikuhakikiwa na kuthibitishwa na Wakala wa Vipimo. **Kiambatisho Na. XIV** ni orodha ya vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji ambavyo mita zake hazikuhakikiwa na kuthibitishwa.

Kushindwa kuhakiki mita za maji kunaweza kusababisha wateja kutozwa ankara zisizo sahihi, ambazo ama ni zaidi au pungufu ya kiasi halisi cha maji walichotumia. Hali hii inaweza kusababisha upotevu wa mapato hivyo kuharibu taswira ya vyombo hivyo.

**Ninapendekeza Serikali, kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, izingatie Sheria ya Vipimo (Sura ya 340) kwa kuwasiliana na Wakala wa Vipimo ili mita zote za maji zinazotumiwa na vyombo vya kijamii vya**

utoaji wa huduma za maji zihakikiwe na kuthibitishwa ili kuwa na uhakika na kiwango cha maji kinachouzwa kwa wateja.

#### 10.6.4 Muundo usiofaa wa utendaji kazi katika vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji

Kifungu cha 41 cha Sheria ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2019 kinaupa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini jukumu la kufuatilia utendaji wa vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji.

Ukaguzi wangu wa CBWSO 136 kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023, uligundua hatarishi katika mfumo wa wafanyakazi na ripoti kwa vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji. Kwa kuzingatia vyeti vya usajili wa CBWSO, mamlaka ya juu ya usimamizi ni Kamati ya maji ya chombo cha watoa huduma ya maji, ambayo inatakiwa kukutana mara mbili kwa mwaka kulingana na Jedwali la Pili la Sheria ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya 2019.

Kifungu cha 34(4) cha Sheria kinaweka jukumu la utendaji kazi za kila siku na uendeshaji wa vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji chini ya uongozi wa vyombo hivyo. Ukaguzi wangu wa vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji ulibaini kuwa hakukuwa na mwongozo maalumu wa malipo kwa watumishi wa vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji. Matokeo yake, wafanyakazi wa vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji wameajiriwa na vyombo husika kwa masharti na viwango vya malipo tofauti. Pia, baadhi ya wafanyakazi wa vyombo hivyo hawakuwa na mikataba ya ajira. Hali hii husababisha wafanyakazi kuacha kazi mara kwa mara. Hivyo, ni maoni yangu kuwa ni vema wafanyakazi wa vyombo hivi wakaajiriwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini badala ya kuajiriwa na wenyeviti wa kamati za maji za vijiji.

Pia, baadhi ya wafanyakazi hawana makubaliano ya kimkataba na uwepo wao katika CBWSO sio wa uhakika hivyo kuathiri ufanisi wa vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji. Hali iliyopo isiporekebishwa, kuna hatari ya miradi ya maji vijijini kutokuwa endelevu.

**Ninapendekeza Serikali, kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, ifanyie marekebisho sheria zinazohusu vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji na uendeshaji wa huduma za maji vijijini ili Wakala uchukue jukumu la uendeshaji na utoaji huduma za maji vijijini ikiwemo kuajiri watumishi wa vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za**

maji wenye sifa watakaosimamia na kuendesha miradi ya maji ili iwe endelevu.

#### 10.6.5 Changamoto zingine zinazoathiri uendeleu wa miradi ya maji inayosimamiwa na vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji

Kwa mujibu wa Kifungu cha 32(1) cha Sheria ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2019, vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji vimeundwa na kupewa jukumu la kutoa huduma za maji kwenye eneo ambalo chombo husika kimesajiliwa kuhudumu.

Katika mapitio yangu ya vyombo 136 vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji kwa mwaka wa fedha 2022/2023, nilibaini mambo yanayohatarisha uendeleu wa miradi na huduma za maji kwa ujumla kama ninavyofafanuliwa hapa chini.

##### (a) Ukusanyaji wa mapato kutofikia malengo kwa Sh. bilioni 1.64

Kifungu cha 38 (a) cha Kanuni za Usambazaji wa Maji Usafi na Usimamizi wa Mazingira (Usajili na Uendeshaji wa Vyombo vya Kijamii vya Utoaji wa Huduma za Maji) za Mwaka 2019 kinataja chanzo kimoja cha fedha kwa vyombo hivyo kuwa ni tozo ya matumizi ya maji zinazolipwa na wateja.

Katika mapitio yangu, nilibaini kuwa vyombo 47 kati ya 136 vilipanga kukusanya Sh. bilioni 4.54 lakini vilifanikiwa kukusanya Sh. bilioni 2.90 (63%) tu, ambapo Sh. Bilioni 1.64 (36%) hazikukusanywa.

Kutokusanya mapato kunachangia kushuka kwa utendaji kazi wa vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji hivyo kuathiri utoaji wa huduma endelevu kwa jamii. **Kiambatisho Na. XV** ni orodha ya vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji vilivyokuwa na makusanyo chini ya bajeti.

##### (b) Ukosefu wa watumishi wenye sifa muhimu za kitaaluma

Kifungu cha 34(4) cha Sheria ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2019 kinaitaka timu ya usimamizi wa maji ya vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji kuwa chombo cha utendaji kinachohusika na shughuli za kila siku za vyombo hivyo. Timu hiyo itafanya kazi zote kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 33 (1) cha mkataba wa makubaliano ya chombo cha watoa huduma ya maji.

Katika ukaguzi wangu, nilibaini vyombo 50 kati ya 136 vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji havikuwa na watumishi wenye sifa muhimu za taaluma wakiwemo wahasibu, watunza fedha, mafundi bomba, mafundi mitambo, wagavi, na wataalamu wa bajeti. Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini umekuwa ukikabidhi kwa vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji miradi ya maji yenye thamani kubwa kutokana na gharama na mitambo na miundombinu ya maji. Hata hivyo, vyombo hivyo zimeshindwa kuajiri watumishi wenye sifa za kitaaluma katika fani mbalimbali kutokana na uhaba wa rasilimali-fedha. Hivyo, kukosekana kwa watumishi wenye sifa za kitaaluma katika fani za ufundi bomba na ufundi mitambo kunahatarisha miundombinu ya maji kwani inaweza kuharibika na kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi kutokana na kutotunzwa na kuhudumiwa vizuri. Halikadhalika, kukosekana kwa watumishi mahiri kwa fani za uhasibu, fedha, ugavi, na bajeti kunaathiri mifumo ya udhibiti wa ndani hivyo kuzorotesha uwajibikaji wa mapato na matumizi na taarifa za fedha kwa ujumla. **Kiambatisho Na. XV** ni orodha ya vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji vilivyokuwa na ukosefu wa watumishi wenye sifa muhimu za kitaaluma.

Kukosekana kwa watumishi wenye sifa muhimu za kitaaluma kwenye fani muhimu kumesababisha changamoto zifuatazo kwa vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji:

- a) Kutoandaliwa kwa mipango ya ununuzi ya mwaka kinyume na Kanuni ya 69 (7) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013;
- b) Utayarishaji wa bajeti bila vifungu vya akaunti kinyume na Kanuni ya 115 ya Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2001;
- c) Risiti za vocha za mapokezi ya fedha kutoorodheshwa kwenye rejista kinyume na Kanuni ya 65 (1) ya Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2001;
- d) Malipo kukosa viambatisho vinavyohibitisha matumizi kinyume na Kanuni ya 95 (4) ya Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2001;
- e) Mapokezi ya bidhaa bila kukaguliwa kinyume na Kanuni ya 244(1) na ya 245 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013;
- f) Ununuzi uliofanywa bila hati ya kuagiza ununuzi husika kinyume na Kanuni ya 164(2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013;
- g) Daftari la mali za kudumu kukosa taarifa muhimu kinyume na Aya ya 6.2 (ii) ya Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Umma wa Mwaka 2019; na
- h) Kutotayarisha daftari la mali za kudumu kinyume na Aya ya 12 ya Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Umma wa Mwaka 2019.

Ninapendekeza Serikali, kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, ihakikishe mapato yote ya vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji yanakusanywa kama yalivyoidhinishwa kwenye bajeti; michango ya watumishi na waajiri inawasilishwa kwenye mfuko wa hifadhi ya jamii; inapitia na inaboresha sheria zinazohusu vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji ili watumishi wenye sifa za kitaaluma waajiriwe kuendesha shughuli zote za vyombo hivyo hali itakayosaidia kuboresha mifumo ya udhibiti wa ndani, kuimarisha huduma za maji vijijini, na kufanya huduma hizo ziwe endelevu.

## 10.7 Masuala ya Diplomasia ya Uchumi

Ukaguzi wangu pia ulijumuisha maeneo ya diplomasia ya uchumi na nilibaini mapungufu yafuatayo:

### 10.7.1 Kutotekelezwa kwa Diplomasia ya Uchumi kwa Nchi Zilizoidhinishwa

Kifungu cha 26 cha Sera Mpya ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001 kinalenga kukuza na kulinda maslahi ya Tanzania kupitia diplomasia ya uchumi na kuwianisha uhusiano na mataifa mengine na taasisi za kimataifa zenye maslahi ya kiuchumi. Ubalози wa Tanzania, Kairo uliidhinishwa kutoa huduma za kibalozi kwa nchi 6 ambazo ni Libya, Lebanoni, Jodani, Siria, Iraki, na Palestina. Kinyume na matakwa ya kifungu hicho, mapitio yangu yalibaini kutotekelezwa kwa diplomasia ya uchumi katika nchi hizo zilizoidhinishwa kutokana na Ubalози wa Tanzania Kairo kushindwa kuwasilisha nyaraka zilizoidhinishwa ambazo zinatoa mamlaka ya kisheria kwa ubalozi huo kutekeleza diplomasia ya uchumi na usalama katika nchi husika.

Upungufu huu ulisababishwa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kutopeleka nyaraka za utambulisho katika nchi husika kutokana na kuwapo kwa machafuko ya kisiasa kwenye baadhi ya nchi hizo. Ni maoni yangu kwamba fursa zinazohusiana na uwekezaji na utalii hazikupatikana.

Ninapendekeza Serikali, kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ihakikishe nyaraka za utambulisho wa mabalozi wa nchi zikamilishwa na zinawasilishwa kwenye nchi za Libya, Lebanoni, Jodani, Siria, Iraki, na Palestina ili kuimarisha diplomasia ya uchumi na uhusiano wa kidiplomasia baina ya Tanzania na nchi hizi.

### 10.7.2 Kutohuishwa kwa Mkataba wa Balozi wa Heshima katika Jamhuri ya Angola

Kifungu cha 45 cha Sera Mpya ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001 kinaipa mamlaka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuratibu sera na kuhakikisha kuwa kanuni na malengo ya sera yanatekelezwa na kufanya kazi. Ili kufikia malengo ya sera, ofisi za ubalozi zinapaswa kupewa rasilimali za kutosha na mazingira mazuri ya kufanyia kazi. Kwa kufanya hivyo, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki inaweza kuboresha ufanisi wa ofisi za ubalozi katika kutoa huduma za kibalozi na kukuza biashara, uwekezaji, na maslahi ya kiuchumi.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa na uhusiano wa kidiplomasia na Jamhuri ya Angola tangu mwaka 1975 wakati Angola ilipopata uhuru. Hata hivyo, Ubalози wa Tanzania nchini Angola ulifungwa mwaka 1993 kutokana na changamoto za kiuchumi na kisiasa nchini Angola. Tangu kufungwa kwa ubalozi, Tanzania iliendeleza uhusiano wa kibalozi nchini Angola kupitia mwakilishi wa heshima anayeendesha shughuli chini ya makubaliano na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kusimamiwa na Ubalози wa Tanzania, Lusaka.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na mwakilishi wa heshima jijini Angola yalikuwisha muda wake tarehe 25 Januari 2022. Hata hivyo, nilibaini pia kuwa mwakilishi huyo wa heshima anaendelea kutekeleza majukumu yake bila makubaliano mapya licha ya juhudi za Ofisi ya Ubalози, Lusaka kuwasiliana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuomba kuhuishwa kwa makubaliano hayo.

Upungufu huu ulitokana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuchelewa kushughulikia uhuishaji wa makubaliano hayo. Ni maoni yangu kwamba mwakilishi wa heshima kuendelea kutekeleza majukumu yake bila makubaliano halali kunaiweka Serikali ya Tanzania katika hatari ya kutokutekeleza masuala ya kidiplomasia kwa ufanisi kati yake na Angola.

**Ninapendekeza Serikali, kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ihakikishe mkataba kati ya Serikali ya Tanzania na mwakilishi wa heshima nchini Angola unahuishwa haraka au uwakilishi nchini Angola unasitishwa.**

### 10.7.3 Serikali Kuchelewa Kutoa Mrejesho wa Fursa za Uwekezaji Zilizozanzishwa na Ofisi za Balozi

Kifungu cha 26 cha Sera Mpya ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001 kinalenga kukuza na kulinda maslahi ya kisiasa, kiuchumi, kijamii, na kitamaduni ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia diplomasia ya uchumi iliyo thabiti na kuhakikisha kuwa uhusiano kati ya Serikali ya Tanzania, mataifa mengine, na taasisi za kimataifa yanazingatia maslahi ya kiuchumi.

Ofisi ya Ubalozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Addis Ababa imeidhinishwa kutoa huduma za kibalozu katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Ethiopia, Jamhuri ya Kiarabu ya Yemeni, na Jamhuri ya Jibuti. Ubalozu pia umeidhinishwa kutoa huduma za kibalozu kwa Umoja wa Afrika na Tume ya Uchumi ya Umoja wa Mataifa kwa Afrika. Ukaguzi wangu ulibaini kuwa Serikali ya Tanzania ilishindwa kutoa mrejesho juu ya mapendekezo 15 ya miradi ya uwekezaji yaliyotolewa na Ofisi ya Ubalozu wa Tanzania, Adis Ababa.

Ukaguzi zaidi katika Ubalozu wa Tanzania, Kuala Lumpur ulibaini kuwa tangu mwaka 2017, wawekezaji watatu kutoka Malaysia walionesha nia ya kuwekeza katika kilimo cha michikichi na kujenga kiwanda cha kutengeneza vichwa vya treni na mabehewa nchini katika eneo la Kibaha. Hata hivyo, Serikali ya Tanzania haijatao mrejesho tangu kuwasilishwa kwa mapendekezo hayo ya uwekezaji.

Zaidi ya hayo, nilibaini jitihada zilizofanywa na Ubalozu wa Tanzania, Stockholm Swideni, ambapo wawekezaji wawili walikuwa na nia ya kuwekeza katika shule ya soka na katika sekta ya afya ili kuifanya Tanzania moja ya maeneo muhimu kwa utalii wa matibabu barani Afrika. Hata hivyo, taasisi husika za Serikali hazijatoa mrejesho tangu uwasilishawaji wa mapendekezo hayo mwezi Juni 2023.

Aidha, nilibaini kuwa Serikali ya Tanzania haikutoa mrejesho wa mapendekezo matano ya uwekezaji yaliyoanzishwa na Ubalozu wa Tanzania, Washington DC katika nyakati tofauti kati ya tarehe 16 Februari na 30 Juni 2023 hivyo kuchelewesha utekelezaji wake na kusababisha malengo ya miradi hii kutofikiwa.

Upungufu huu unasababishwa na mawasiliano hafifu kati ya taasisi za Serikali nchini na ofisi za ubalozu nje ya nchi kutokana na kukosekana kwa ofisa mteule anayefuatilia na kuchambua mapendekezo ya uwekezaji kutoka kwa



wawekezaji mbalimbali duniani kupitia balozi zetu. Ni maoni yangu kwamba, kuchelewa kutoa mrejesho wa mapendekezo ya uwekezaji nchini kunakatisha tamaa wawekezaji tarajiwa. Aidha, hali hii inazorotesha ushirikiano kati ya ofisi za ubalozi na taasisi za Serikali nchini. Vilevile, hali hii inaathiri juhudi za waheshimiwa mabalozi kuendelea kutafuta wawekezaji katika muktadha wa utekelezaji wa diplomasia ya uchumi, hivyo kuhatarisha ushirikiano na kuzuia maendeleo na malengo ya pamoja.

**Ninapendekeza Serikali, kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ihakikishe inateua Afisa atakayesimamia mawasiliano na kufuatilia na kuchambua mapendekezo ya uwekezaji yanayotolewa na ofisi za ubalozi nje ya nchi.**

#### 10.7.4 Kuchelewa kwa Uimarishaji wa Mpaka wa Tanzania na Kenya

Waraka wa Umoja wa Mataifa wa Mwaka 2017 unaamuru kukamilika kwa zoezi la kimataifa la kuimarisha mipaka katika nchi za Afrika kufikia mwaka 2021. Mchakato huu unajumuisha kupitia upya na kuthibitisha mipaka ya kimataifa kwa ajili ya uwazi na kudumisha amani na uwazi. Unasisitiza umuhimu wa kuzingatia muda uliowekwa wa zoezi hili la kutambua mipaka ya nchi.

Ukaguzi wangu ulibaini kwamba Tanzania na Kenya zimefanikiwa kutambua mipaka kwa umbali wa kilomita 458 kati ya jumla ya ardhi iliyopo ya kilomita 758, huku kilomita 300 za ardhi zikiwa hazijatambuliwa, hususani katika maeneo yenye miamba. Aidha, uhakiki wa mipaka katika ukanda wa ziwa haujaanza ukisubiri mchakato wa kuthibitisha upya kilomita 300 zilizobaki.

Upungufu huu ambao ulichangiwa na uhaba wa fedha unaweza kusababisha mipaka ya nchi na umiliki wa rasilimali kutofahamika kisheria. Pia, unaweza kuathiri shughuli za kiuchumi, maamuzi ya uwekezaji, na uhusiano wa kidiplomasia. Pia, unaweza kusababisha mizozo ya mpaka na migogoro baina ya nchi hizi mbili.

**Ninapendekeza Serikali, kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ihakikishe mchakato wa kuthibitisha mipaka baina ya Tanzania na Kenya unafanywa kwa haraka kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi ya Tanzania.**

## 10.8 Vyama vya Siasa

Sehemu hii inawasilisha muhtasari wa masuala muhimu yaliyobainika wakati wa ukaguzi wangu wa vyama vya siasa. Ukaguzi huu ulifanyika kwa mujibu wa Kifungu cha 18A (2) (a) cha Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258 (iliyorejewa mwaka 2019). Sheria hii inataka kila chama cha siasa kilichosajiliwa kuandaa na kuwasilisha taarifa za fedha kwa ajili ya ukaguzi.

Katika ukaguzi wa vyama vya siasa 19 kwa mwaka wa fedha 2022/23, nilibaini masuala muhimu yanayohitaji kuchukuliwa hatua. Masuala haya yameelezwa kwa undani katika sehemu hii, na ninapendekeza kwamba Msajili wa Vyama vya Siasa achukue hatua kuyashughulikia haraka.

### 10.8.1 Kuchelewa Kuwasilisha Taarifa za Fedha kwa Ajili ya Ukaguzi

Kifungu cha 18A (2) (a) cha Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258 (iliyorejewa mwaka 2019) kinataka vyama vyote vya siasa vilivyosajiliwa kuwasilisha taarifa zao za fedha kwa ajili ya ukaguzi ifikapo tarehe 30 Septemba ya kila mwaka.

Hata hivyo, ukaguzi wangu ulibaini kuwa vyama vitano vya siasa, yaani National Reconstruction Alliance (NRA), Tanzania Labor Party (TLP), Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Civic United Front (CUF), na Democratic Party (DP) vilikabidhi taarifa zao za kifedha baada ya tarehe 30 Septemba 2023.

Kucheleweshwa kuwasilisha taarifa za fedha kulikadiriwa kuwa kati ya siku 9 hadi 52. Uongozi wa vyama hivyo vya siasa ulieleza kuwa ucheleweshaji huo ulichangiwa na kukosekana kwa fedha na miongozo inayovitaka vyama vya siasa kuajiri wahasibu wenye ujuzi, ambao wangeweza kuandaa kwa wakati taarifa za kifedha. Nina wasiwasi kwamba muda wa ukaguzi wangu wa taarifa za fedha haukutekelezwa ipasavyo kulingana na kalenda ya ukaguzi.

Ninapendekeza Msajili wa Vyama vya Siasa, kuvitaka vyama vya siasa NRA, TPL, CHADEMA, CUF, na DP kuajiri wahasibu wenye ujuzi watakaofanikisha uandaaji wa taarifa za fedha kwa wakati ifikapo tarehe 30 Septemba kila mwaka.

### 10.8.2 Michango ya Wanachama yenye Thamani ya Sh. milioni 104.08 Kutowasilishwa katika Akaunti za Benki za Vyama vya Siasa

Kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258 (iliyorekebisha mwaka 2019) kinataka kila chama cha siasa, ambacho kimesajiliwa kisheria kufungua akaunti ya benki ya chama, ambayo mapato yote yanayopatikana kutokana na ada za uanachama, michango ya hiari, misaada, ruzuku, au mapato ya uwekezaji yanapaswa kuwasilishwa benki.

Hata hivyo, ukaguzi wangu ulibaini kwamba katika mwaka wa fedha 2022/2023, vyama vitano vya siasa, yaani Chama cha Kijamii (CCK), National League for Democracy (NLD), NCCR Mageuzi, Chama cha Muungano wa Kidemokrasia wa Afrika (ADA TADEA), na Chama cha Umoja kwa Demokrasia ya Vyama Vingi (UMD) vilikusanya michango kutoka kwa wanachama mbalimbali jumla ya Sh. milioni 104.08 bila kuwasilisha katika akaunti za benki za vyama husika. **Jedwali Na. 60** ni orodha ya vyama vya siasa ambavyo havikuwasilisha kwenye akaunti za benki michango ya wanachama wake.

#### Jedwali Na. 60: Vyama vya Siasa ambavyo Havikuwasilisha kwenye Akaunti za Benki Michango ya Wanachama Wake

Na.	Chama cha Siasa	Kiasi Kisichowasilishwa Benki (Sh.)
1.	Chama cha Kijamii (CCK)	6,401,200
2.	National League for Democracy (NLD)	1,100,000
3.	NCCR Mageuzi	90,499,000
4.	Chama cha Muungano wa Kidemokrasia wa Afrika (ADA TADEA)	2,886,100
5.	Chama cha Umoja kwa Demokrasia ya Vyama Vingi (UMD)	3,200,000
<b>Jumla</b>		<b>104,086,300</b>

**Chanzo:** Vitabu vya Fedha na Taarifa za Benki

Hali hii ilitokana na hulka ya muda mrefu ya kuepuka gharama za uendeshaji wa akaunti za benki hivyo kusababisha akaunti za benki kutotumika. Kuhusu chama cha NLD, akaunti ya benki ilikuwa haifanyi kazi kutokana na kutotumika kwa muda mrefu. Kushindwa kuwashilisha fedha za makusanyo ya michango ya wanachama katika akaunti za benki kunavutia matumizi mabaya ya fedha, huku ikileta uwezekano wa kutofautiana kwa kumbukumbu za kihasibu na inaondoa uwazi katika utendaji.

Ninapendekeza Msajili wa Vyama vya Siasa kuhakikisha makusanyo ya fedha yanawasilishwa kwa wakati katika akaunti za benki za vyama vya siasa na Chama cha NLD kifungue akaunti ya benki ya chama.

### 10.8.3 Vyama 15 vya Siasa Kushindwa Kukusanya Mapato ya Sh. bilioni 2.51 Kulingana na Bajeti

Kifungu cha 58(b) cha Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015 inataka mtu aliye na mamlaka ya ukusanyaji wa mapato ya umma awajibike kikamilifu na ukusanyaji, uhasibu, na utoaji wa taarifa ya makusanyo kulingana na sheria inayotumika na kuchukua tahadhari ili kuzuia upotezaji wa mapato.

Ukaguzi wangu wa bajeti za vyama vya siasa ulibaini kuwa vyama 15 vya siasa vilipanga kukusanya jumla ya Sh. bilioni 2.87. Kati ya hizo, Sh. milioni 358.66 zilikusanywa sawa na asilimia 12 na kushindwa kukusanya kiasi cha Sh. bilioni 2.51 (asilimia 88). Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa vyama viwili vya siasa, yaani Chama cha Alliance for Democratic Change na Chama cha United Democratic Party vilikuwa na bajeti zisizo na uhalisia kwani ukusanyaji ulikuwa asilimia 2 tu ya bajeti. **Jedwali Na. 61** linaonesha vyama vya vyama vya siasa, ambavyo havikukusanya mapato kulingana na bajeti zao.

**Jedwali Na. 61: Vyama vya Siasa Vilivyoshindwa Kukusanya Mapato**

Na.	Chama cha Siasa	Bajeti (Sh.)	Halisi (Sh.)	Upungufu (Sh.)	Asilimia ya Kutofikia Ukusanyaji (Sh.)
1	Democratic Party (DP)	10,000,000	1,811,109	8,188,891	82
2	Alliance for Democratic Change (ADC)	1,078,506,000	21,391,000	1,057,115,000	98
3	Alliance for Africa Farmers Party (AAFP)	9,824,000	1,435,300	8,388,700	85
4	Civic United Front (CUF)	335,700,000	196,001,842	139,698,158	42
5	National Reconstruction Alliance (NRA)	29,250,000	6,030,000	23,220,000	79
6	Tanzania Labour Party (TLP)	8,500,000	300,000	8,200,000	96
7	United Peoples Democratic Party (UPDP)	5,000,000	3,765,000	1,235,000	25
8	Union for Multi-party Democracy (UMD)	12,360,000	3,200,000	9,160,000	74

Na.	Chama cha Siasa	Bajeti (Sh.)	Halisi (Sh.)	Upungufu (Sh.)	Asilimia ya Kutofikia Ukusanyaji (Sh.)
9	Chama cha Kijamii (CCK)	103,982,800	6,401,200	97,581,600	94
10	Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMA)	6,000,000	1,857,000	4,143,000	69
11	National League for Democracy (NLD)	8,840,000	1,100,000	7,740,000	88
12	National Convention for Construction and Reform (NCCR-Mageuzi)	219,697,546	88,503,446	131,194,100	60
13	Demokrasia Makini (DM)	17,440,000	7,410,000	10,030,000	58
14	Sauti ya Umma (SAU)	5,800,000	1,407,500	4,392,500	76
15	United Democratic Party (UDP)	1,020,000,000	18,048,800	1,001,951,200	98
<b>Jumla</b>		<b>2,870,900,346</b>	<b>358,662,197</b>	<b>2,512,238,149</b>	<b>88</b>

**Chanzo:** Hesabu za Fedha kwa Mwaka 2022/2023

Hali hii ilitokana na wanachama wa vyama vya siasa kushindwa kulipa ada zao za usajili za kila mwezi na ufuatiliaji usioridhisha wa ukusanyaji wa mapato kutokana na kutohuishwa kwa taarifa za wanachama kwenye rejista. Kwa upande mwingine, bajeti zilizoandaliwa za Vyama vya Siasa vya ADC na UDP zilikuwa za juu na hazikuwa na uhalisia hivyo kusababisha kuwa na makusanyo chini ya bajeti. Ni maoni yangu kuwa kushindwa kukusanya mapato kwa mujibu wa bajeti kunavikwamisha vyama vya siasa kutimiza shughuli zao zilizopangwa na kufikia malengo yao ya kisiasa.

**Ninapendekeza Msajili wa Vyama vya Siasa ahakikishe maandalizi ya bajeti za vyama vya siasa yawe na uhalisia na kuhuisha taarifa za wanachama kwenye rejista kwa ajili ya usimamizi bora.**

#### 10.8.4 Vyama 5 vya Siasa Havikuwasilisha Tamko la kila Mwaka la Mali kwa Msajili wa Vyama vya Siasa

Kifungu cha 14 (1) (b) (ii) cha Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258 (iliyorejewa mwaka 2019) kinataka vyama vya siasa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Kisiasa tamko la mali zote zinazomilikiwa na chama husika mwishoni mwa kila mwaka wa fedha.

Hata hivyo, ukaguzi wangu ulibaini kuwa vyama vinne vya siasa ambavyo ni Chama cha Wakulima wa Afrika (AAFP), Chama cha Demokrasia Makini (DM), Chama cha Muungano wa Ujenzi wa Kitaifa (NRA), na Chama cha Kitaifa cha Kidemokrasia (NLD) vilishindwa kuwasilisha tamko la orodha ya mali zote kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kwa mwaka uliomalizika tarehe 30 Juni 2023. Hata hivyo Msajili wa Vyama vvyaa Siasa hakuweza kutoza faini, kuvisimamisha, au kufuta usajili wa vyama hivi kama sheria inavyotaka. Kutowasilisha matamko ya orodha ya mali kunadhoofisha uwazi na uwajibikaji, hivyo kuondoa imani ya wananchi kwa vyama vya siasa na uongozi wake.

Ni maoni yangu kwamba kutowasilisha uthibitisho kwa tamko la kila mwaka la mali zinazomilikiwa na vyama vya siasa kunaweza kusababisha faini, kusimamishwa, au kufutwa kwa usajili kwa mujibu wa matakwa ya kifungu cha 21D (2) cha Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258 (iliyorejewa mwaka 2019). Zaidi ya hayo, hali hii inazuia uwezo wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Kisiasa kutimiza majukumu yake, kwa mujibu wa kifungu cha 14 cha Sheria ya Vyama vya Siasa. Katika hali yoyote ile, inaweza kuleta utata katika umiliki, na Msajili hataweza kurekebisha hali hiyo.

**Ninapendekeza Msajili wa Vyama vya Siasa atoe adhabu, ikiwa pamoja na faini, na kusimamisha au kufuta usajili wa vyama vinavyoshindwa kuwasilisha tamko la mali kila mwaka kama inavyotakiwa na sheria.**

# SURA YA KUMI NA MOJA



## UTAWALA, UDHIBITI WA MIFUMO YA NDANI, NA USIMAMIZI WA VIHATARISHI

### 11.1 Utangulizi

Utawala wenye ufanisi, udhibiti thabiti wa mifumo ya ndani, na usimamizi wa vihatarishi ni misingi muhimu katika utawala bora wa umma. Misingi hii hutumiwa kama nyenzo za shughuli za taasisi za Serikali katika kuhakikisha uwazi, uwajibikaji, na matumizi sahihi ya rasilimali. Kwa kuzingatia kanuni za utawala bora, Serikali inaweza kujenga imani kwa umma, kuboresha mchakato wa maamuzi, na kuongeza ufanisi katika taasisi za umma.

Katika Sura hii, ninawasilisha matokeo ya ukaguzi wa utawala bora, udhibiti wa mifumo ya ndani, na usimamizi wa vihatarishi katika taasisi za Serikali kuu. Ukaguzi ulilenga kufanya tathmini ya ufanisi wake, kuinisha maeneo ya kuboresha, na kutoa mapendekezo kwa ajili ya maboresho.

### 11.2 Mapitio ya Utawala Bora katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, na Wakala za Serikali

Mwongozo wa Kuimarisha Mifumo ya Udhibiti wa Ndani katika Taasisi za Umma unasisitiza kwamba bodi za usimamizi katika taasisi za umma au mabaraza ya madiwani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, zina jukumu kubwa la kuhakikisha kuwapo kwa mazingira yanayofaa ya udhibiti wa mifumo ya ndani. Hii ni pamoja na kusimamia muundo wa taasisi na utekelezaji wa mfumo mzuri wa udhibiti wa ndani. Bodi za uongozi au mabaraza yanaweza kukasimisha jukumu hili kwa kamati maalumu kama vile kamati za dedha na mipango, na kamati za ukaguzi. Tathmini yangu ya utawala bora katika wizara, idara, na wakala za serikali ilibaini yafuatayo:

### 11.2.1 Kutounda na Kuendeleza Bodi za Uongozi Zenye Ufanisi

Shughuli za bodi za uongozi, bodi za wadhamini na bodi za ushauri za wizara zinasimamiwa na sheria husika za uanzishaji wake. Kwa wakala za serikali, bodi za ushauri za wizara hufanya kazi chini ya Kifungu cha 6(1) cha Sheria ya Wakala za Serikali ya Mwaka 1997 (T.S. Na. 83 la Mwaka 2003). Bodi za hospitali za rufaa za mikoa hufanya kazi chini ya Mwongozo wa Bodi za Ushauri za Hospitali za Rufaa za Mkoa, na bodi za ushauri na usimamizi za taasisi zingine hufanya kazi chini ya sheria za uanzishaji wake.

Baada ya kufanya tathmini ya kuwapo kwa utendaji kazi wa bodi za uongozi za wizara, idara zinazojitegemea na Wakala za Serikali, nilibaini kuwa taasisi 15 zilikuwa zinaendeshwa bila kuwa na bodi za uongozi. Aidha, bodi za taasisi sita zilikuwa hazijatimiza idadi ya vikao vinavyotakiwa kisheria katika kutekeleza majukumu yake, kama ilivyooneshwa katika Jedwali Na. 62.

#### Jedwali Na. 62: Taasisi zenye Bodi za Uongozi zenye Mapungufu

Na.	Taasisi	Maelezo
<b>A.</b>	<b>Taasisi ambazo Hazikuwa na Bodi za Uongozi</b>	
1.	Bodi ya Mfuko wa Barabara	Bodi ilimaliza muda wake tangu mwezi Novemba mwaka 2022.
2.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Loliondo	Haina Bodi ya ushauri.
3.	Hospitali Maalumu ya Magonjwa Ambukizi, Kibong'oto	Bodi ya wadhamini bado haijaanzishwa.
4.	Hospitali ya Rufaa ya Kanda, Mbeya	Bodi ya ushauri ilimaliza muda wake tangu mwezi Julai mwaka 2022.
5.	Baraza la Wataalamu wa Afya ya Mazingira	Baraza lilimaliza muda wake tangu mwezi Februari mwaka 2023.
6.	Baraza la Famasia	Bodi ilimaliza muda wake tangu mwezi Oktoba mwaka 2021.
7.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Singida	Bodi ya ushauri ilimaliza muda wake tangu mwezi Septemba mwaka 2022.
8.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Katavi	Bodi ya ushauri ilimaliza muda wake tangu mwezi Oktoba mwaka 2022.
9.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Songea	Bodi ya ushauri ilimaliza muda wake tangu mwezi Machi mwaka 2022.
10.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Sokoine	Bodi ya ushauri ilimaliza muda wake tangu mwezi Februari mwaka 2023.
11.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Mwananyamala	Bodi ya ushauri ilimaliza muda wake tangu mwezi Agosti mwaka 2022.
12.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Mtwara	Bodi ya ushauri bado haijaanzishwa.
13.	Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya	Bodi ya ushauri ilimaliza muda wake tangu mwezi Julai mwaka 2022.



Na.	Taasisi	Maelezo
14.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Ligula	Bodi ya ushauri ilimaliza muda wake tangu mwezi Mei mwaka 2023.
15.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Dodoma	Bodi ya ushauri ilimaliza muda wake mwezi Septemba mwaka 2022.
<b>B.</b>	<b>Taasisi ambazo Bodi Zake Zilishindwa Kufanya Vikao vya Bodi</b>	
1.	Chuo cha Sheria Tanzania	Baraza lilifanya vikao viwili tu badala ya vinne
2.	Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa	Kamati ya uongozi ilifanya vikao viwili tu badala ya vinne
3.	Mamlaka ya Maji Safi wa Usafi wa Mazingira, Kilindoni	Kamati ya ushauri haikufanya kikao chochote.
4.	Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Tanganyika	Baraza lilifanya kikao kimoja tu badala ya vinne.
5.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Njombe	Baraza la ushauri la Hospitali lilifanya vikao viwili tu badala ya vinne.
6.	Baraza la Madaktari la Tanganyika	Baraza lilifanya vikao viwili tu badala ya vinne.

**Chanzo:** Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti

Ninahusisha udhaifu huu na kucheleweshwa kwa uteuzi wa wajumbe wa bodi, hivyo kusababisha ugumu katika kufikia akidi ya vikao, pamoja na upungufu wa rasilimali-fedha kwa ajili ya kugharamia vikao.

Kwa maoni yangu, kutokuwapo kwa bodi zilizo hai kunazorotesha utoaji wa maamuzi na usimamizi, hivyo kuathiri mwelekeo na utendaji chanya wa taasisi. Pia, kutekelezwa kwa majukumu haya na bodi ambazo muda wake umekwisha kunaweza kusababisha ugumu katika kuwawajibisha kwa maamuzi yao.

**Ninapendekeza kwamba, Serikali ihakikishe kuwa taasisi zinazohusika zinaanzisha na kudumisha bodi zilizo hai, kuteua wajumbe kabla ya muda wao kumalizika. Pia, kuhakikisha kwamba bodi hizo zinafanya vikao vinavyohitajika ikiwa ni sehemu ya majukumu yao.**

### 11.2.2 Upungufu katika utendaji wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya

Sheria ya Mahakama (Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi) ya Mwaka 2002, Sura ya 2 inaitaka Wizara ya Ardhi kuanzisha, kusimamia, na kuendeleza mabaraza ya ardhi na nyumba ya wilaya kwa ajili ya kutatua migogoro ya ardhi katika ngazi ya wilaya.

Ukaguzi wangu wa mchakato wa kutatua migogoro ya ardhi ulibaini kwamba hadi tarehe 30 Juni 2023, mabaraza haya yalikuwa na jumla ya migogoro 15,480 iliyokuwa ikisubiri utatuzi. Katika kutathmini utendaji wa mabaraza haya katika kutatua migogoro hii, nilibaini yafuatayo:

- a) Kutokuwapo kwa mabaraza katika wilaya 46: Kinyume na Kifungu cha 22(1) cha Sheria ya Mahakama (Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi) ya Mwaka 2002, ambacho kinataka Waziri mwenye dhamana ya ardhi kuanzisha baraza la ardhi na nyumba katika kila wilaya, ni mabaraza 93 tu kati ya 139 yanayohitajika ndio yalikuwa yameanzishwa, huku mabaraza 46 yakiwa hayajaanzishwa.
- b) Kutokuwapo kwa wenyeviti katika mabaraza 41: Kinyume na Kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Mahakama (Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi) ya Mwaka 2002, kinachotaka kila baraza kuwa na mwenyekiti mmoja na si chini ya wapatanishi wawili, mabaraza 41 hayakuwa na wenyeviti.

Udhaifu huu unaotokana na upungufu wa rasilimaliwatu na rasilimali-fedha, unaweza kuathiri uwezo wa mabaraza katika kutatua kwa ufanisi migogoro ya ardhi na kutimiza majukumu yao yaliyokusudiwa.

**Ninapendekeza kwamba Serikali, kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ichukue hatua za kuwezesha uteuzi na uundaji wa mabaraza ya ardhi na makazi ya wilaya ili kuboresha na kurahisisha utatuzi wa migogoro ya ardhi katika ngazi ya wilaya.**

### **11.2.3 Kutokuwapo kwa Kanuni za Kusimamia Ukusanyaji wa Ada za Leseni za Kila Mwaka kutoka kwa Kampuni za Mafuta na Gesi**

Kifungu Na. 114 cha Sheria ya Petroli ya Mwaka [Sura ya 21] kinataka wakandarasi (Kampuni za Mafuta na Gesi) kulipa ada za kila mwaka kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kwa ajili ya leseni. Ada hizi za kila mwaka ni pamoja na kodi ya eneo, ada za mafunzo na utafiti, na mapato yaliyokusanywa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania chini ya kifungu hiki.

Hata hivyo, ukaguzi wangu katika Wizara ya Nishati kupitia Mkataba wa Mgawanyo wa Uzalishaji wa Nishati, ulibaini kuwa, tangu kuanzishwa kwa Sheria hiyo mwaka 2015, hakuna kanuni zilizowekwa kusimamia ukusanyaji na usimamizi wa ada hizi. Kufuatia hali hiyo, kumekuwapo na utamaduni wa muda mrefu wa Wizara ya Nishati kugawana na Shirika la Maendeleo ya Petroli

Tanzania kwa usawa ada za mafunzo ya kila mwaka zinazolipwa na kampuni za mafuta na gesi bila kutumia kanuni za mgawanyo wala makubaliano baina yao. Aidha, nilibaini kuwa kwa mwaka wa fedha 2022/23, Wizara ya Nishati kupitia Mkataba wa Mgawanyo wa Uzalishaji wa Nishati ilipaswa kupokea 50% ya dola za Marekani 1,070,000, ambazo zilipaswa kukusanywa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania, yaani, Dola za Marekani 535,000, sawa na Sh. bilioni 1.24 kwa kiwango cha ubadilishaji fedha tarehe 30 Juni 2023. Hata hivyo, Wizara ya Nishati kupitia Mkataba wa Mgawanyo wa Uzalishaji wa Nishati ilipokea kiasi cha Dola za Marekani 166,751.57 pekee. Ukaguzi wangu unahusisha hali hii na ufuatiliaji hafifu wa kutunga na kuweka kanuni hizo.

Kwa mtazamo wangu, kutokuwapo kwa kanuni hizi kunaweza kuchangia katika upungufu wa ufanisi ambao ungeepukika, endapo kanuni hizi zingekuwepo.

**Ninapendekeza kwamba Serikali, kupitia Wizara ya Nishati, iwezeshe kuundwa kwa kanuni za kusimamia ukusanyaji na matumizi ya ada za leseni za kila mwaka kutoka kwa makampuni ya mafuta na gesi, ili kuhakikisha uwazi na ufanisi katika ukusanyaji na usimamizi wa ada hizo.**

#### 11.2.4 Upungufu katika Utendaji wa Kamati za Ukaguzi

Kwa mujibu wa Kanuni ya 30 ya Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2001, ni jukumu la taasisi za umma kuunda kamati za ukaguzi na kufuatia muundo na majukumu yaliyoelezwa katika Kanuni ya 31 na ya 32. Pia, kwa mujibu wa Kifungu cha 5.3 cha Mwongozo wa Udhhibiti wa Mifumo ya Ndani wa Mwezi Desemba 2014, kamati ya ukaguzi ina jukumu kuu la kuhakikisha ufanisi wa mifumo ya udhibiti wa ndani wa taasisi. Hali hii ni pamoja na mapitio ya mfumo wa udhibiti wa ndani, kufuatilia mapendekezo ya ukaguzi wa ndani na wa nje, na kusimamia majibu ya menejimenti.

Kamati za ukaguzi zinatakiwa kuandaa vikao vya kila robo mwaka kwa ajili ya kupitia mipango ya ukaguzi, ripoti za utendaji, usimamizi wa vihatarishi, na udhibiti wa mifumo ya ndani. Hata hivyo, ukaguzi wangu ulibaini upungufu ufuatao unaojirudia: taasisi 7 hazikuwa na kamati za ukaguzi, na kamati za ukaguzi za taasisi 15 hazikutimiza majukumu yao ipasavyo ya kupitia taarifa za kifedha, kutathmini michakato ya usimamizi wa vihatarishi, kufanya vikao vinavyohitajika, kujifanyia tathmini binafsi, na kuandaa ripoti ya utendaji ya kila mwaka. Muhtasari wa upungufu kwa kila taasisi umeoneshwa katika **Kiambatisho Na. XVII.**

Upungufu huo unatokana na kuchelewesha uteuzi wa wajumbe wa kamati na upungufu wa rasilimali-fedha kwa ajili ya shughuli zao, hivyo kuathiri utendaji kazi wa kamati za ukaguzi katika kutekeleza majukumu yao.

Ninapendekeza kwamba Serikali, kupitia taasisi husika, ihakikishe kuwa taasisi hizo zinaanzisha kamati za ukaguzi na kutenga rasilimali za kutosha kuziwezesha kutekeleza majukumu yao kwa ukamilifu.

### 11.2.5 Kutoanzisha na Utendaji Usioridhisha wa Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani

Kwa mujibu wa Kanuni ya 28(1) ya Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2001, maafisa masuuli wanapaswa kuunda vitengo vya ukaguzi wa ndani vyenye ufanisi ili kuhakikisha ufanisi wa udhibiti wa mifumo ya ndani ya taasisi. Aidha, Mwongozo wa Udhibiti wa Mifumo ya Ndani wa Mwenzi Desemba 2014 unaeleza kwamba vitengo vya ukaguzi wa ndani vinapaswa kutoa uhakikisho na ushauri wa kitaalamu kuhusu ufanisi wa mifumo ya udhibiti wa ndani wa taasisi za serikali.

Ukaguzi wangu umebaini upungufu katika utendaji wa vitengo vya ukaguzi wa ndani katika taasisi 16, ambapo taasisi 10 hazikuwa na vitengo vya ukaguzi wa ndani, na taasisi sita zilikuwa na utendaji usioridhisha na uhaba wa rasilimali za kutimiza majukumu. **Jedwali Na. 63** na **Jedwali Na. 64.** yanaonesha orodha ya taasisi ambazo ama hazikuwa na vitengo vya ukaguzi wa ndani au vitengo vya ukaguzi havikuwa vikitimiza ipasavyo majukumu yake. Upungufu huu ambao ulibainika pia katika ukaguzi wangu uliopita, unaendelea kutokea, ambapo mwaka jana taasisi 22 zilibainika kuwa na kasoro hizi. Hali hii inaonesha upungufu katika uwezo wa taasisi hizi kuunda vitengo vya ukaguzi wa ndani vyenye ufanisi na kuhakikisha vinafanya kazi kikamilifu.

#### Jedwali Na. 63: Taasisi ambazo Hazikuwa na Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani

Na.	Taasisi	Kundi	Sekta
1.	Shirika la Uzalishaji Mali la Polisi	Taasisi nyingine	Utawala
2.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Busega	Taasisi nyingine	Uchumi
3.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Orkesumet	Taasisi nyingine	Uchumi
4.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbulu	Taasisi nyingine	Uchumi
5.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbinga	Taasisi nyingine	Uchumi

Na.	Taasisi	Kundi	Sekta
6.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kibondo	Taasisi nyingine	Uchumi
7.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kibaya	Taasisi nyingine	Uchumi
8.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kasulu	Taasisi nyingine	Uchumi
9.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Liwale	Taasisi nyingine	Uchumi
10.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kilwa Masoko	Taasisi nyingine	Uchumi

**Chanzo:** Taarifa za Ukaguzi ya 2022/23 kwa Menejimenti

**Jedwali Na. 64: Taasisi ambazo Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani Vilikuwa na Upungufu**

Na	Taasisi	Kundi	Sekta	Maelezo
1.	Ubalozi wa Tanzania Berlin, Ujerumani	Taasisi nyingine	Utawala	Ukaguzi wa ndani haukufanyika kwa mwaka 2022/23.
2.	Ubalozi wa Tanzania Algiers, Algeria	Taasisi nyingine	Utawala	Ukaguzi wa ndani haukufanyika kwa mwaka 2022/23.
3.	SUMA JKT Makao Makuu	Taasisi nyingine	Utawala	Ukosefu wa mafunzo kwa watumishi wa kitengo, na upungufu rasilimaliwatu and rasilimali-fedha.
4.	Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania	Taasisi nyingine	Uchumi	Ukaguzi wa ndani haukufanyika kwa mwaka 2022/23.
5.	Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma	Fungu 67	Uchumi	Hakukuwa na mafunzo kwa wafanyakazi wa ukaguzi wa ndani
6.	Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi	Taasisi nyingine	Uchumi	Kutokuwapo kwa watumishi wa kitengo cha ukaguzi wa ndani

**Chanzo:** Taarifa ya Ukaguzi ya 2022/23 kwa Menejimenti

Kutokuwapo kwa vitengo vya ukaguzi wa ndani kunasababisha taasisi kukosa fursa ya awali ya kubaini kasoro na upungufu katika mifumo ya udhibiti wa ndani.

Ninapendekeza kwamba Serikali, kupitia taasisi husika, ihakikishe kuwa taasisi hizo zinaanzisha vitengo vya ukaguzi wa ndani na kutenga rasilimali za kutosha kuviwezesha kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

### 11.3 Upungufu katika Udhhibiti wa Mifumo ya Ndani katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, na Wakala za Serikali

Kwa mujibu wa Mwongozo wa Wizara ya Fedha wa Maboresho ya Mifumo ya Udhhibiti wa Ndani katika Taasisi za Umma wa Mwezi Desemba 2014, udhhibiti wa mifumo ya ndani ni mchakato wa kibunifu ulioundwa na uongozi na wafanyakazi wa taasisi. Lengo lake ni kusimamia vihatarishi na kutoa uhakikisho wa kutosha kwamba shughuli za taasisi zinazingatia kanuni na taratibu, maadili, na ni za ufanisi. Udhhibiti imara wa mifumo ya ndani, pamoja na usimamizi bora wa vihatarishi na utawala bora, hufungua njia kuelekea uwazi katika utendaji, ubora katika utoaji wa huduma, matumizi bora ya rasilimali, na ufanisi wa shughuli za Serikali. Katika kutathmini ufanisi wa udhhibiti wa mifumo ya ndani katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, na Wakala za Serikali, nilibaini yafuatayo:

#### 11.3.1 Vitabu 9,319 vya Vibali vya Kusafirisha Mifugo na Bidhaa za Mifugo Havikurejeshwa kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Mifugo) kwa ajili ya Uhakikii

Kanuni ya 2 ya Kanuni za Udhhibiti wa Magonjwa ya Mifugo (Udhhibiti wa Usafirishaji wa Mifugo na Bidhaa za Mifugo) (Marekebisho ya Mwaka 2020) inahitaji kupata kibali maalumu kutoka kwa mkaguzi kabla ya kusafirisha mifugo au bidhaa za mifugo ndani au nje ya wilaya, pamoja na kulipa ada inayotakiwa.

Tathmini yangu ya mifumo ya udhhibiti wa utoaji wa vibali vya usafirishaji wa mifugo na bidhaa za mifugo pamoja na ukusanyaji wa ada za vibali katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Mifugo), ilibaini kwamba vitabu 9,319 vya vibali vilisambazwa kwenye vituo vya mifugo vya kanda na mamlaka za serikali za mitaa. Vitabu hivi vya vibali hutumika kutoa vibali vya usafirishaji wa mifugo na bidhaa za mifugo pamoja na kukusanya ada zinazohusika. Hata hivyo, kinyume na Kifungu cha 79 cha Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2001 kinachotaka maafisa masuuli kuhakikisha utunzaji wa kumbukumbu sahihi kwa kuchunguza na kuthibitisha miamala kila siku katika vitabu vya fedha na vitabu vya mapato, nakala za vitabu hivi hazikurudishwa kwa Wizara ya Mifugo kwa ajili ya ukaguzi na uhakiki baada ya matumizi yake.

Ninahusisha upungufu huu na ufuatiliaji na uangalizi hafifu wa Wizara wa vitabu vilivyosambazwa, jambo linaloweza kuhatarisha uwezo wa Wizara kuthibitisha vibali vilivyotolewa na mapato yaliyokusanywa.

Ninapendekeza Serikali, kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, iweke mfumo imara wa ufuatiliaji ili kuhakikisha kuwa vitabu vya vibali vinarejeshwa kwa wakati wizarani kwa ajili ya uhakiki baada ya kutumika, hivyo kuongeza uwajibikaji na uwazi katika utoaji wa vibali na ukusanyaji wa mapato.

### 11.3.2 Ripoti za mapato katika masoko 233 ya mifugo sawa na asilimia 46 hazikuwasilishwa wizarani

Kifungu cha 79 cha Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2001 kinataka maafisa masuuli kuhakikisha uwekaji wa kumbukumbu sahihi kwa kuhakiki na kuthibitisha miamala kila siku katika vitabu vya fedha, vitabu vya mapato, na akaunti zingine. Baada ya ukaguzi, nilibaini upungufu ufuatao katika usimamizi wa fedha na taarifa katika masoko ya mifugo:

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa, katika mwaka wa fedha wa 2022/23, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Mifugo) ilikusanya jumla ya Sh. bilioni 7 kutoka kwenye masoko ya mifugo. Mapitio ya taarifa za masoko haya katika Wizara yalibaini kuwapo kwa masoko 504 ya mifugo yaliyopo katika tawala za mikoa, na mamlaka za serikali za mitaa. Kati ya hayo, ni masoko 271 tu ya mifugo (54%) ndio yaliwasilisha ripoti za mapato yaliyokusanywa kupitia ada za vibali vya usafirishaji wa mifugo, huku masoko 233 (46%) yakiwa hayakuwasilisha ripoti za ukusanyaji wa mapato yao.

Hii imechangiwa na kutokuwapo kwa udhibiti wa kutosha wa makusanyo ya fedha katika masoko ya mifugo, jambo ambalo linaweza kuibua hatari ya ubadhirifu wa fedha za umma.

Ninapendekeza kwamba Serikali, kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ianzishe mifumo thabiti ya udhibiti katika ukusanyaji wa mapato katika masoko ya mifugo ili kuhakikisha taarifa sahihi za mapato kutoka masoko hayo, na hivyo kupunguza hatari ya matumizi mabaya ya fedha za umma.

### 11.3.3 Upungufu katika Usimamizi wa Kanzidata ya Akaunti za Benki za Serikali katika Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali

Mhasibu Mkuu wa Serikali amepewa jukumu la kusimamia uendeshaji wa akaunti za benki ya serikali kwa mujibu wa Kanuni ya 155 ya Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2001. Mhasibu Mkuu wa Serikali, kupitia kitengo cha usimamizi wa fedha, hufanya ukaguzi wa maombi ya kufungua na kufunga akaunti kutoka kwa taasisi za serikali na kutoa maelekezo stahiki. Hata hivyo, ukaguzi wangu

ulibaini kuwa, Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali haikuweka mfumo thabiti wa kusimamia kanzidata ya akaunti za benki za serikali, ambayo ilionesha kuwa na jumla ya akaunti 78,762 hadi tarehe 30 Juni 2023.

Ukaguzi wangu ulibaini zaidi kuwa hakukuwa na kumbukumbu zinazoonisha kwamba ukaguzi ulikuwa unafanywa kwa maombi ya ufunguzi wa akaunti za benki ili kuhakikisha taratibu na malengo ya serikali yanazingatiwa. Hali hii inadhoofisha ufanisi na uwajibikaji katika mchakato wa kufungua akaunti za serikali. Zaidi ya hayo, kanzidata ya Mhasibu Mkuu wa Serikali haikuwa sahihi, kwani haikuendana na idadi halisi ya akaunti zilizokuwa zinamilikiwa na baadhi ya taasisi za serikali. Kwa mfano, Wakala wa Barabara Tanzania ilithibitisha kumiliki akaunti 138 tu, lakini kanzidata ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ilionesha kuwa Wakala huo ulikuwa unamiliki jumla ya akaunti 250. Tofauti hii ya akaunti 112 inaonesha kukosekana kwa udhibiti katika usimamizi wa taarifa za benki za serikali hivyo kusababisha uwezekano wa kuendesha akaunti za Serikali bila idhini au kusababisha mianya ya ubadhirifu.

Upungufu huu unaiweka Serikali katika hatari ya kupata hasara za kifedha, ufanisi duni, na matumizi mabaya ya fedha za Serikali kutokana na kuwapo kwa kanzidata isiyo sahihi kwa udhibiti wa usimamizi.

**Ninapendekeza kwamba Serikali, kupitia Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, iweke udhibiti imara katika usimamizi wa akaunti za benki za Serikali na kanzidata yake ili kuhakikisha usahihi na kufuata malengo ya Serikali, hivyo kupunguza hatari ya hasara za fedha na matumizi mabaya ya fedha za umma.**

#### 11.3.4 Kuwapo kwa Akaunti za Benki Zisizotumika kwa Muda Mrefu

Kifungu cha 154 cha Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2001 kinaelezea taratibu za kusimamia akaunti za benki za serikali. Kifungu hicho pia kinampa jukumu Mhasibu Mkuu wa Serikali kuidhinisha ufunguzi wa akaunti za benki. Katika kutekeleza jukumu hilo, kwa mujibu wa maelekezo ya waziri mwenye dhamana ya fedha, Mhasibu Mkuu anaweza kuchagua benki moja au zaidi za Kitanzania kuwa benki ya Serikali itakayoshughulikia fedha za umma na majukumu rasmi ya benki.

Ukaguzi wangu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania ulibaini kwamba mamlaka ilikuwa inamiliki akaunti tatu za benki ambazo hazikutumika kwa zaidi ya mwaka mmoja. Kufikia tarehe 30 Juni 2023, akaunti hizi zilikuwa na kiasi cha dola za Marekani 209 pamoja na Sh. milioni 170.14. Aidha, nilibaini kuwa Wakala



wa Majengo Tanzania alikuwa na jumla ya akaunti dumavu 33 za benki ambazo hazikuwa zinatumiwa tangu mwezi Oktoba 2020. Kati ya akaunti hizo, saba zilikuwa na kiasi cha Sh. milioni 12.48 hadi tarehe 30 Juni 2023.

Kwa maoni yangu, upungufu huu unadhihirisha usimamizi mdogo wa akaunti za benki, hali ambayo, kwa upande mwingine, inaweza kuiweka Serikali katika hatari ya kupata hasara za kifedha, matumizi mabaya ya fedha za umma, na kuruhusu mianya ya ubadhirifu.

**Ninapendekeza kwamba Serikali, kwa kushirikiana na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na Wakala wa Majengo Tanzania, pamoja na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, ifunge akaunti zote zisizotumiwa ili kupunguza hatari ya hasara za fedha, matumizi mabaya ya fedha za umma, na hatari ya shughuli za udanganyifu.**

### 11.3.5 Kutosomana kwa Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato wa Tume ya Madini na Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato wa Serikali (GePG)

Kifungu cha 4.2(3) cha Mwongozo wa Usimamizi wa Mfumo wa Serikali wa Ukusanyaji wa Mapato kinaziruhusu taasisi zisizo na mfumo wa ukusanyaji wa mapato kutumia moduli ya ankara iliyomo katika Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali kama suluhisho la muda wakati zinatafuta suluhisho la kudumu la mfumo wa makusanyo. Ukaguzi wangu ulibaini kuwa Tume ya Madini ilikuwa inatumia Mfumo wa Usimamizi wa Uuzaji wa Madini (MIMS) kwa ukusanyaji wa mapato ya mauzo ya madini na Mfumo wa Huduma za Leseni kwa Njia ya Mtandao (MCIMS) kwa utoaji na usimamizi wa leseni.

Hata hivyo, baada ya kukagua matumizi yake, nilibaini kuwa mchakato wa ukusanyaji wa mapato kwa wachimbaji na mawakala ulitegemea moduli ya ankara ya Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali ambayo ni ya muda. Hali hii ililazimu kuingiza taarifa kwa njia isiyo ya kiotomatiki kutoka mifumo ya Tume kwenda Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali wakati wa kutoa ankara kutokana na kutosomana kwa mifumo hiyo. Kutosomana kwa mifumo hiyo kulitokana na Tume kukosa umiliki kamili wa Mfumo huo hivyo kutokuwa na uwezo unaohitajika wa kuwezesha kuunganishwa na Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali.

Kutosomana kwa mifumo hii kunaweza kuathiri ufanisi katika utendaji kazi na ukusanyaji wa mapato.

Ninapendekeza kwamba Serikali, kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao, itoe msaada kwa Tume ya Madini ili kuunganisha mifumo yake ya ukusanyaji mapato na GePG, ili kuongeza ufanisi katika utendaji na kuimarisha ukusanyaji wa mapato.

### 11.3.6 Kutotumika kwa Mfumo wa Ulipaji Serikalini (MUSE) katika uhasibu na uandaaji wa taarifa

Waraka wa Hazina Namba 5 wa Mwaka 2019 na agizo la Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango ya Mwezi Aprili 2020 kwa pamoja linaisitiza umuhimu wa kutumia Mfumo wa Ulipaji Serikalini (MUSE) ndani ya taasisi za serikali. Hata hivyo, baada ya kukagua utekelezaji wa waraka na agizo hilo katika taasisi za serikali, nilibaini kuwa si taasisi zote zilikuwa zinatumia kikamilifu MUSE. Nilibaini kuwa, taasisi 26 zilizo rodheshwa katika **Jedwali Na. 65** hazikuwa zinatumia MUSE katika kuandaa taarifa zao za kifedha, nyingi zikitoa sababu za changamoto za mfumo na hitaji la mafunzo. Badala yake, taasisi hizi zilichagua kutumia njia za kizamani kuandaa taarifa zao za kifedha.

#### Jedwali Na. 65: Taasisi ambazo Hazikutumia Mfumo MUSE

Na	Taasisi
1.	Mfuko wa Taifa wa Mambokale
2.	Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania
3.	Ubalozi wa Tanzania Jakarta Indonesia
4.	Ubalozi wa Tanzania Hague, Uholanzi
5.	Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Nyasa
6.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Rujewa
7.	Baraza la Mifugo Tanzania
8.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Busega
9.	Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji
10.	Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Nyasa
11.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Rujewa
12.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Orkesumet
13.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbulu
